Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Ishirini na Nane - Tarehe 21 Julai, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## DUA

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Kabla hatujaanza, ninawafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba, leo kwenye *Gallery* kuna mgeni ambaye ni Mheshimiwa Balozi wa China nchini Tanzania, pamoja na Maafisa wake. *(Makofi)*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:**

Hotuba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo katika mwaka uliopita pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 269

### Walimu Kufuata Mishahara Yao Makao Mkuu ya Wilaya

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA** aliuliza:-

Kwa kuwa walimu hupoteza siku nyingi kwa mwaka kwa ajili ya kufuata mishahara yao kwenye Makao Makuu ya Wilaya; na kwa kuwa kwa kufanya hivyo hufundisha siku 139 tu badala ya siku 194 kwa mwaka; na kwa kuwa sehemu kubwa ya mishahara wanayoifuata hupotea kwa ajili ya nauli, malazi na chakula, hali inayopunguza sana kipato chao:-

(a) Je, Serikali italitatua lini tatizo hilo ili badala ya kuifuata mishahara yao kwenye Makao Makuu ya Wilaya, wapelekewe mishahara yao mahali pa kazi?

(b) Kama Serikali haiwezi kuwafikishia walimu mishahara yao kwenye sehemu zao za kazi; je, isingekuwa vyema kuwarudishia gharama zote wanazozitumia kwa shughuli hiyo?

(c) Je, kama mwalimu hatafundisha kwa siku 194 Serikali inafikiri elimu itaboreshwa vipi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, yenye jumla ya shule za msingi 266 imewahi miaka ya nyuma kuwalipa watumishi wote wakiwemo walimu mishahara yao katika vituo vyao vya kazi ambapo iliichukua Halmashauri hiyo takriban siku 30 kukamilisha kuwalipa. Hata hivyo, Halmashauri ilisitisha zoezi hili kwa sababu zifuatazo:-

(i) Jiografia ya Wilaya ya Mbinga ni yenye milima na mabonde mengi na ugumu wa mawasiliano hasa wakati wa masika.

(ii) Gharama kubwa ya posho za Maafisa, walinzi na dreva pamoja na mafuta wakati wa kutembelea maeneo hayo.

(iii) Usalama wa fedha na watumishi husika kutokana na matukio mbalimbali ya ujambazi. Kwa mfano, tarehe 3 Septemba, 1997 watumishi wa Kampuni ya *DORMAN* walivamiwa na majambazi waliotaka kupora Sh. 60 milioni za ununuzi wa kahawa katika Kijiji cha Luwaita. Aidha, mwaka 1998/99 watumishi wa Kampuni hiyo hiyo ya *DORMAN* waliokoa tena jumla ya Sh. 60 milioni walipovamiwa na majambazi katika eneo la Kiteleha. Vile vile, tarehe 15 Novemba, 2000 fedha na vocha za pembejeo zenye thamani ya Sh. 4,667,000/= zikiwa ni mali ya wakulima walioiuzia Kampuni ya Kukoboa Kahawa Mbinga, ziliporwa katika eneo la Ndengo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia matukio haya mbalimbali, Baraza la Halmashauri lilijadili suala hili katika vikao vyake vya tarehe 21 Desemba, 2001 na tarehe 27 Septemba, 2002 na kuamua kuendelea kutotumia utaratibu wa kuwapelekea watumishi mishahara kutokana na sababu hizo. Kwa bahati mbaya hali hii iko katika sehemu nyingi hapa nchini. Hivyo basi, katika mazingira ya namna hii, Serikali inasita kutumia utaratibu unaoshauriwa na Mheshimiwa Mbunge. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuzishauri Halmashauri kuanzisha vituo vya kulipia mishahara katika Wilaya ambapo vinafikika kwa urahisi na kuna usalama na uwezo wa fedha wa kufanya hivyo kama ilivyofanya Halmashauri ya Bunda.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina utaratibu wa kuwarejeshea watumishi fedha zao wanazotumia wakati wanapofuata mishahara yao katika vituo vya malipo Wilayani. Aidha, Serikali inaona kuwa ingekuwa vizuri sana kuwarudishia gharama zao kibinadamu ili kuwamotisha zaidi. Hata hivyo, uwezo wake wa kutekeleza azma hiyo kwa sasa ni mdogo hasa ikizingatia idadi kubwa ya walimu ambao wanakabiliwa na tatizo hilo.

(c) Mheshimiwa Spika, hatuna uhakika namna Mheshimiwa Mbunge, alivyofikia takwimu ya idadi ya siku 139. Lakini ninakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa mwalimu kuweza kutumia siku zote 194 kufundisha darasani, ni moja ya jambo la muhimu sana katika kuboresha elimu. Ndiyo maana nimesema kuwa tutaendelea kuzishauri Halmashauri zetu pale inapowezekana kuanzisha vituo ambavyo vitakuwa karibu na watumishi. Hata hivyo, utaratibu huo utakuwa ni wa muda tu kwa kuwa Serikali inakamilisha taratibu za watumishi wote kulipwa mishahara yao kupitia Benki.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa wanafunzi wa Vijijini hawafundishwi siku 194 zilizopagwa na Wizara; na kwa kuwa katika hali hiyo wanafunzi hao hawapati programu iliyopangwa kikamilifu; je, isingekuwa vema kuwa mitihani ya wanafunzi ya Kitaifa kungekuwa na viwango viwili kwa wanafunzi wa Vijijini na wanafunzi wa Mijini ili ushindani uwe sawa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, swali alilouliza Mheshimiwa Mbunge ni suala la kisera na kwa kweli linapaswa kujibiwa vizuri

sana na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni. Kwa hiyo, tutakachofanya ni kuliwasilisha kwake ili pengine atalitafakari na kuona kama hilo linawezekana.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika maeneo yaliyokuwa na matatizo ya milima na mabonde kama ya Mbinga na katika Mto Rufiji kule katika *Delta* kuna matatizo ya mitumbwi; je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba kuna haja sasa ya kuwapelekea walimu mishahara yao mapema kabisa ili waweze kuchukua siku chache kwenda na kurudi katika vituo vyao ukilinganisha na maeneo mengine ambayo hayana matatizo Tanzania?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, suala la kuwahisha mishahara kwa baadhi ya maeneo ambayo yanakabiliwa na matatizo ya mawasiliano si jambo jepesi sana kwa sababu upo utaratibu wa namna mishahara inavyolipwa. Kuna tarehe ambazo Hazina wanazizingatia na ndiyo maana maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwa walimu kulipwa mishahara ni tarehe 25. Sasa kutegemea kwamba zinaweza zikalipwa labda mapema tarehe 10 au tarehe 11, inawezekana lisiwe jambo jepesi sana. Lakini hata hivyo, tutakachofanya ni kwamba tutajaribu na sisi kuliwasilisha jambo hili kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tuone atalipa mtazamo gani.

Na. 270

***Net Group* Kuboresha *TANESCO***

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliingia Mkataba wa uendeshaji wa *TANESCO* na *Net Group Company* kwa lengo la kuboresha uendeshaji na ukusanyaji mapato ya *TANESCO*; je, Serikali inaweza kueleza uboreshaji wa *TANESCO* uliofikiwa tangu *Net Group* ianze kazi?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Kampuni ya *Net Group Solution* ilianza kazi mwezi Mei, 2002 na hadi sasa wastani wa makusanyo ya *TANESCO* kwa mwezi yameongezeka kutoka Sh. 10 bilioni hadi kufikia Sh. 15 bilioni. Kwa sasa hali ya kifedha ya *TANESCO* ni bora zaidi kuliko ilivyokuwa awali na hivyo kuiwezesha *TANESCO* kununua vifaa vya kurekebisha mifumo ya umeme iliyochakaa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati najibu swali Na. 233 tarehe 15 Julai, 2003 katika mkutano huu, Wizara yangu ikishirikiana na *TANESCO* imefanya mambo yafuatayo:-

- *TANESCO* chini ya *Net Group Solution* imeandaa utaratibu wa kufanya matengenezo muhimu katika mifumo ya umeme ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme;

- Kununua vifaa muhimu kwa ajili ya kukarabati mifumo ya kusambaza umeme na tayari shilingi karibu bilioni 7.0 zimetengwa na wazabuni wameteuliwa kwa ajili ya kuleta vifaa muhimu vya kukarabati mifumo;

- Matengenezo muhimu yamefanyika katika mifumo ya umeme ikiwa ni pamoja na kubadilisha nguzo zilizooza, vikombe vichakavu, *transforma* zilizozidiwa na mzigo na nyaya chakavu;
- Kwa sasa hivi kuna mradi mkubwa unaoendelea kutekelezwa wa kukarabati vituo vyote vya *Grid* ya Taifa katika Mikoa yote;

- Menejimenti imeanza kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ikiwa ni pamoja na kutangaza tenda za kununua vifaa kwa uwazi zaidi ili kuleta ushindani na kununua vifaa kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotajwa hapo juu zinapofanyika, matangazo hutolewa kwenye vyombo vya habari. Matatizo ambayo hayatangazwi *(unplanned),* ni yale yanayotokana na hali halisi ya uchakavu wa mifumo hiyo, jambo ambalo linasababisha hitilafu.

Matatizo ya kukatika umeme mara kwa mara yatapungua kutokana na matengenezo ya dharura ya kukarabati mifumo na vituo vya umeme inayoendelea kufanyika katika Mikoa yote. Tatizo hili litapata ufumbuzi wa kudumu mara baada ya kupata fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati wa mifumo ya umeme.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika kujibu swali la msingi amekiri kwamba kumekuwa na ongezeko la makusanyo kutoka shilingi bilioni 10 na kufikia shilingi bilioni 15 tangu *Net Group Solution* iingie katika mkataba; na kwa kuwa wananchi wengi wa Vijijini wamekuwa wakiona nyaya za umeme zinapita juu lakini hawawezi kupata umeme, jambo ambalo lilikuwepo kabla *Net Group Solution* haijaja; je, kwa kipindi hiki Mheshimiwa Waziri ataweza kuniambia kwamba sasa wataweza kuboresha mfumo wa umeme kwa kuwapatia umeme wananchi wa Vijijini?

(ii) Pili, kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi ya wananchi kubambikiziwa bili kubwa za umeme; na kwa kipindi hicho hicho kumekuwa na malalamiko mengi kwamba *Net Group Solution* wanajilimbikizia mishahara mikubwa na malipo mbalimbali; je, inaweza kuwa na mahusiano gani hii kwamba inawezakana kuongeza bili huko kwa wananchi kusikokuwa kwa kawaida, pengine ndiyo kunakowafanya wao wajilipe; je, Mheshimiwa Waziri ana maelezo gani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa sababu fedha zimeongezeka, makusanyo yameongezeka kutoka shilingi bilioni 10 hadi shilingi bilioni 15 kwa mwezi; je, umeme utafika Vijijini? Jibu lake ni kwamba, ni kweli kwa sababu uwezo wa kukusanya unaongezeka na ndiyo wameanza tu, ndiyo wanamaliza mwaka mmoja na uwezo huo unazidi kuongezeka jinsi muda unavyopita. Ongezeko hilo litatumika kukarabati miundombinu yote na kusambaza umeme na kuwaunganishia wananchi umeme Mijini na Vijijini. Kwa hiyo, jibu ni kwamba, ndiyo uwezo wetu umeongezeka na tutaongeza kasi yetu ya kupeleka umeme Vijijini.

Mheshimiwa Spika, pili, anahisi bili zinabambikizwa na labda mapato yao mazuri pamoja na mishahara mikubwa mikubwa ya wafanyakazi wa *Net Group Solution* vina uhusiano. Ukweli ni kwamba wafanyakazi wa *Net Group Solution* wanalipwa kutokana na fedha zilizopo kwenye ule mkataba ambao umewaleta hapa, hazitokani na mapato ya *TANESCO* ya kila siku, huo ndiyo ukweli. Kwa hiyo, fedha zinazopatikana kutokana na bili zote zinaingia katika mapato, ndiyo zile shilingi bilioni 15 ambazo zimepanda.

Mheshimiwa Spika, tatizo mojawapo ambalo linafanywa na *TANESCO* sasa, ni kuhakikisha kwamba bili zinakuwa za uhakika na mita zinakuwa nzuri na kama ni LUKU zinakuwa zinafanya kazi vizuri ili kuondokana na hilo tatizo la bili ambazo zinaonekana kama zimebambikizwa na wananchi wanaumia. Tatizo hilo la bili zisizo na uhakika linapungua hivi sasa.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa *Net Group Solution* imepewa kazi ya kusambaza umeme nchi nzima na uko umeme wa kutoka Uganda uliokusudiwa kwa sababu ya Mkoa wa Kagera ambao unatumika kwa kilovoti tano tu kati ya kilovoti nane ambazo zilitegemewa kwamba zingetosheleza Mkoa mzima; ni kwa vipi Wizara haijaielekeza *Net Group Solution* kusambaza umeme huo katika Mkoa mzima? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunanunua umeme kutoka Uganda ambao unaweza kufika nadhani ni megawati nane ambazo tunaweza kununua wakati wowote ule. Sasa usambazaji unategemea na ile *infrastructure,* ile gridi iliyopo kwamba; je, kuna waya mahali fulani ili uweze kupeleka ule

umeme kutoka Uganda kule. Kama hujaweka hiyo gridi kutoka pale ilipo sasa mpaka Vijiji vipya au Vijiji ambavyo havijapata, basi zile megawati za umeme ambazo zipo na tunaweza kuzinunua, haziwezi kufika kwenye Vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, uwezo ambao tumeupata sasa unatuwezesha kusambaza umeme kwenye Vijiji vya sehemu hizo za Tanzania ambapo umeme haujafika na ikiwa ni pamoja na umeme ambao unatoka Uganda. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika hotuba yangu ya Bajeti, siku ya Alhamisi, nitazungumzia umeme kufika Biharamulo na Ngara ambako ni sehemu anayotoka. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali mengine yasubiri hotuba ya Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko)*

Na. 271

**Mradi wa Kupeleka Maji ya Ziwa Victoria Kahama**

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa sasa Serikali inatekeleza mradi kamambe wa muda wa kati wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria kwenye Miji ya Kahama na Shinyanga:-

(a) Je, ni hatua gani imefikiwa hadi sasa katika utekelezaji wa mradi huo?

(b) Kwa kuwa Serikali imekubali kutekeleza mradi wa dharura wa kuupatia maji Mji wa Kahama, ambao unakadiriwa kuwa na wakazi wapatao 120,000 lakini takriban asilimia 98 ya wakazi hao sasa hivi wanapata maji yasiyoaminika ya visima na kwa njia ya madumu yanayosambazwa kwa mikokoteni; je, Serikali itakubali kupokea shukrani za dhati kutoka kwa wananchi wa Kahama?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raphael M. Mlolwa, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kutekeleza mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria hadi Miji ya Kahama na Shinyanga, pamoja na Vijiji ambako bomba linapitia, baada ya kutambua matatizo ya upungufu wa maji kwenye Mkoa wa Shinyanga. Aidha, mradi huo utatoa huduma ya maji kwa baadhi ya Vijiji vya Mkoa wa Mwanza katika Wilaya ya Misungwi vikiwemo Vijiji vya Tarafa ya Mwamashimba.

Utekelezaji wa mradi huu umeanza rasmi mwaka 2002/2003, ambapo Mhandisi Mshauri *GIBB (Eastern Africa) Limited* kutoka Kenya, akishirikiana na Makampuni mawili ya Tanzania ya *Don Consult Limited* na *NETWAS Limited,* ambayo yalichaguliwa kwa njia ya zabuni. Makampuni hayo yanafanya upembuzi yakinifu, usanifu, pamoja na kutayarisha makabrasha ya zabuni ya ujenzi. Mradi huu umepangwa kutekelezwa katika awamu mbili kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2002/2003 hadi 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Mhandisi Mshauri kwa sasa anaendelea na upimaji wa chanzo cha maji, sehemu ya chujio la maji, matanki ya maji pamoja na njia kuu za bomba. Aidha, shughuli za uchunguzi wa udongo katika maeneo mbalimbali ya mradi zinaendelea ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa takwimu za kiuchumi na kijamii katika eneo la mradi.

Mheshimiwa Spika, Mhandisi Mshauri anatarajiwa kuwasilisha usanifu na makabrasha ya zabuni kwa ajili ya awamu ya kwanza ya mradi ifikapo Jumatano wiki hii, tarehe 23 Julai, 2003. Baada ya hapo Mkandarasi wa kujenga mradi kwa awamu hii atatafutwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubali kupokea shukrani za dhati kutoka kwa wananchi wa Kahama na Mkoa wa Shinyanga kwa ujumla. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Raphael Mlolwa, kwa kutambua juhudi za Serikali katika kuondoa kero ya maji kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga.

Mradi huu ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na unatekelezwa kwa fedha zetu wenyewe. *(Makofi)*

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. Naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa washauri wa Mradi huu, Wahandisi wa Kampuni ya *GIBB* katika utafiti wao wamegundua kwamba kasi ya ongezeko la Mji wa Kahama ni zaidi ya asilimia 10 kwa mwaka na kwamba ifikapo mwaka 2024 watafikia zaidi ya laki sita; je, Serikali imetambua hilo na inalizingatia kikamilifu katika kutekeleza huu Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua hilo na Wahandisi au Kampuni ya *GIBB (Eastern Africa)* wameshaliona hilo kama alivyolieleza Mheshimiwa Mbunge. Lakini pia lazima uelewe kwamba, *projection* zetu za huu mradi ni kukidhi maji kwenye maeneo husika kwa miaka 20. Lakini hata hivyo, ningependa kumweleza Mheshimiwa Raphael Mlolwa kwamba, ile *rate* ya kukua kwa Mji wa Kahama iko hivyo ikichangiwa kwa kiwango kikubwa na *Informal Mining* kwenye maeneo hayo. Jinsi tutakavyoendelea ku-*formalize* hii *mining,* yaani uchimbaji wa madini kwa mpangilio mzuri, nina hakika kwamba, kukua kwa Mji wa Kahama na maeneo hayo unaweza ukarudi kwenye kiwango kinachoweza kukidhi mahitaji na kuweza kutuwezesha kukidhi maji katika maeneo husika. Kwa hiyo, ninamshukuru sana Mheshimiwa Raphael Mlolwa, kwa kuliona hilo na aelewe kwamba Serikali pia imeshaliona.

Na. 272

**Mabwawa Yaliyotelekezwa**

**MHE. LUCAS L. SELELII (k.n.y. MHE. STEPHEN M. KAHUMBI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mabwawa yaliyojengwa zamani na Idara ya Maji kama lile la Malolo na Mihama Wilayani Nzega yametelekezwa na hayakukamilishwa ili kupeleka maji yalikotazamiwa kwenda japokuwa matanki yalijengwa yote. Je, Wizara ina mpango gani kuhusu mabwawa haya na mengine ya aina yake nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen M. Kahumbi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Maji ya Malolo na Mihama ni miongoni mwa miradi mingi hapa nchini iliyobuniwa na kuanza kujengwa na Serikali miaka ya 70, kwa lengo la kutumia mabwawa kama vyanzo vya maji hasa maeneo kame. Pamoja na kutokamilika kwa wakati huo, miradi hiyo imeendelea kuzeeka na kuchakaa kutokana na kutotunzwa na wananchi. Kuibiwa mashine ya kusukuma maji ya Mradi wa Malolo mwaka 1988, pamoja na kuharibiwa mabomba ni mfano mmojawapo.

Kama ilivyobainishwa kwenye Sera ya Maji ya mwaka 2002, hali hii ya uharibifu wa mifumo ya maji na wizi wa vifaa mbalimbali vya miradi ya maji, inatokana na kutoshirikishwa wananchi katika ubunifu, upangaji, ujenzi, uendeshaji na kumiliki miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba, 2002, Wizara yangu ilituma wataalam kwenda Nzega kufanya tathmini ya hali halisi ya mabwawa hayo ikiwa ni pamoja na kupata gharama za kuendeleza kazi. Kazi hiyo imefanyika na sasa Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, inatafuta fedha itakayowezesha kuendeleza kazi ya ujenzi wa mabwawa hayo. Hata hivyo, pamoja na juhudi hizi, wananchi wanatakiwa kuonyesha nia ya kuhitaji huduma hiyo ya maji kwa kuanza kuchangia fedha kwa ajili ya mradi wanaotaka uendelezwe. Naomba Mheshimiwa Mbunge, asaidie kuhamasisha wananchi kuchangia fedha kwa ajili ya miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maeneo mengine nchini ambayo ni kame, Wizara yangu imeandaa mkakati wa ujenzi na ukarabati wa mabwawa ikiwa ni pamoja na ukarabati na ununuzi wa matingatinga ambayo yatatumika katika kazi hiyo. Aidha, Serikali itawahusisha wananchi na wadau mbalimbali katika kutekeleza mkakati huu.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Malambo haya mawili ya Malolo na Mihama yalilenga kuwapatia maji safi na salama wananchi wa Bukene na wa Tarafa ya Puge lakini kwa bahati mbaya yalikabidhiwa kabla hayajakamilika; je, Serikali ipo tayari kulipa angalau gharama ile ambayo ilikusudiwa ili yakamilike na kufanya malengo yaliyowekwa yaweze kufikiwa?

Pili, kwa kuwa maeneo ambayo yalikuwa yamelengwa ya Tarafa ya Bukene na Puge bado hayajapata maji na kwa jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri anasema hakuna uwezo; je, Serikali ipo tayari kutoa visima badala ya kutumia mtandao ambao ni wa gharama kubwa zaidi huu wa mabwawa, malambo haya ya Malolo na Mihama?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi ni kwamba, tunashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega katika kutatua tatizo hilo. Lakini tukianza kudaiana sasa hivi na sisi tunaweza kudai warudishiwe vifaa vilivyoibiwa kwenye mradi. Lakini hilo sidhani kana kwamba ni wakati wake huu. Kwa hiyo, tutashirikiana na Halmashauri ya Wilaya, tukishirikiana na Mheshimiwa Mbunge, ili tuweze kutatua matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, pili, visima katika maeneo aliyoyataja ambayo yako karibu na Puge na Bukene, vinachimbwa, *World Division* sasa hivi wanachimba visima vingi sana lakini licha ya hilo Serikali katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita, tumesaidia katika kutatua baadhi ya matatizo lakini siyo yote. Vivyo hivyo tutaendelea kusaidia kutatua matatizo ili wananchi wa Wilaya ya Nzega waweze kupungukiwa na matatizo haya ya maji.

Na. 273

**Usafiri kwa Shule za Sekondari Wilaya ya Mbulu**

**MHE. PHILIP S. MARMO** aliuliza:-

Kwa kuwa Shule za Sekondari za Maghang, Maretadu, Haydom na Tumati katika Wilaya ya Mbulu ziko mbali na Makao Makuu ya Wilaya (kama Haydom ambayo iko zaidi ya kilomita 100 toka Makao Makuu ya Wilaya). Je, ni lini Serikali itazipatia shule hizo angalau gari moja ili walimu na watumishi wa shule hizo wapate huduma hasa ya kufuata mishahara kwa urahisi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philip S. Marmo, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli shule inapokuwa na usafiri wa kuaminika inasaidia sana katika kutekeleza mambo mengi shuleni pamoja na kuhudumia walimu na wanafunzi katika shida mbalimbali. Shule za Sekondari za Maghang, Maretadu, Haydom na Tumati, zilizoko katika Wilaya ya Mbulu, ni miongoni mwa shule 644 za sekondari za Serikali zinazosimamiwa na Wizara yangu. Kati ya shule hizo 644 ni shule 82 tu ndizo zenye magari mazima. Shule zilizotajwa ni kati ya shule ambazo hazina magari kama alivyobainisha Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swali Na. 88 lililoulizwa na Mheshimiwa Paul Ntwina, Mbunge wa Songwe, katika Mkutano wa Bunge la Bajeti 2002/2003. Wizara yangu inaendelea na jitihada ya kupata fedha za kununulia magari kwa ajili ya shule zake zenye matatizo ya usafiri. Mathalani, katika mwaka wa fedha 2001/2002, Wizara ilinunua magari sita na kuyagawa katika shule za sekondari za wasichana Kibondo, Mtwara na Songea na katika shule nyingine za Mangaka, Morogoro na Sarwatt iliyoko Wilaya ya Mbulu. Magari hayo yatatumiwa sio tu na shule ambazo zimekabidhiwa bali pia na shule za jirani kwa shughuli za kikazi. Serikali kwa Bajeti yake ya ndani, haina uwezo wa kuzipatia shule zake zote vyombo vya usafiri kwa wakati mmoja. Wizara itaendelea kutafuta fedha ili iweze kununua magari ya kutosha kupunguza matatizo ya usafiri katika shule na Vyuo vya Ualimu na shida hii itazingatiwa katika wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari 2004 - 2009, ambao unakamilishwa kwa ushirikiano na wabia wetu katika maendeleo ya elimu.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu swali la msingi kwa umakini kabisa. Nadhani nitamwonea na kumyanyasa nikimwuliza swali gumu. Lakini hata hivyo, atakubali kuwakumbusha wahusika katika Wizara ya Elimu na Utamaduni kuhusu ombi letu la kuzipa shule mbili za sekondari za Mule na Kenamu, ambazo ziko katika mazingira magumu ya Milima, ambazo hazifikiki hasa wakati wa masika ili wapewe pikipiki na tupate jibu haraka iwezekanavyo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nitafikisha ombi hilo kwa Mheshimiwa Waziri anayehusika. Lakini ni vyema vilevile nikaendelea kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba, shule 644 ni nyingi mno na kila shule ina matatizo ya aina yake, matatizo yanaweza kuwa yanatofautiana kati ya shule na shule, lakini kwa kweli bila ya kuwa na usafiri ni matatizo makubwa.

Kwa hiyo, ningeomba tuvute subira ili itakapofikia kutekelezwa kwa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, Mpango ambao unaanzishwa katika mwaka 2004 - 2009, ili tuweze kupata vyombo hivyo kwa wakati mmoja na kupunguza tatizo hilo kwa shule zetu za Sekondari na Vyuo vya Ualimu. *(Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa shule zetu za sekondari nyingi ziko vijijini; na kwa kuwa uwezo wa Serikali ni mdogo na inatoa magari kwa uchache; je, Serikali itaweza kuzingatia utaratibu wa kuweka angalau gari moja katika kila Makao Makuu ya Wilaya ilipo shule ya sekondari ili liweze kuhudumia shule nyingine zilizoko katika Wilaya ile?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, Serikali ingependa siyo kuweka gari moja tu kila Makao Makuu ya Wilaya, ingependa pengine kuweka gari kwa kila Tarafa au Kata, lakini tatizo ni uwezo wetu mdogo kwa hivi sasa kuweza kufanya ununuzi wa magari hayo. Ndiyo maana tuliamua kuweka Mradi Maalum, ambao utajumuisha na tatizo la usafiri ili kuacha kule kujidanganya kwamba unapeleka magari mawili katika Wilaya.

Tukifikiria kwamba yanatosha, hilo siyo jambo la kweli sasa hivi tunalazimisha tu kwamba shule za jirani zisaidiane na shule nyingine katika kutumia usafiri huo mmoja. Kwa hiyo, bado narudia kutoa ombi kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi tuvute subira tufikie katika ule Mpango wa Maaendeleo ya Elimu ya Sekondari ili ukianza kutekelezwa, tatizo hili tutalisahau kama tunavyoyasahau matatizo mengine sasa hivi katika Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi. *(Makofi)*

Na. 274

**Uboreshaji wa Nyumba za Walimu**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa mpango wa kuboresha Elimu ya Msingi nchini umezingatia tu ujenzi wa madarasa na siyo nyumba za walimu; na kwa kuwa nyumba za walimu ziko kwenye hali mbaya na duni sana na Halmashauri nyingi nchini ikiwemo Halmashauri ya Liwale hazina uwezo wa kujenga nyumba bora kwa ajili ya walimu wote:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha nyumba za walimu ili ziende sambamba na mpango mzima wa kuboresha madarasa?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kwa kutokuboresha nyumba za walimu hasa wa vijijini kunaathiri uboreshaji wa Elimu ya Msingi kwa ujumla wake kwani walimu watakosa ari ya kufundisha vizuri kutokana na hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) 2002 - 2006, ina malengo mbalimbali ya kuboresha Elimu ya Msingi ikiwa ni pamoja na kuboresha na kujenga aina zote za majengo ya shule kama vile madarasa, nyumba za walimu, ofisi na maliwato, pamoja na kununua aina zote za samani za shule, yakiwemo madawati, meza, viti na kabati. Anayeamua ni Halmashauri ya Wilaya, Mji, Manispaa na Jiji, wakati wa kuandaa mpango wake wa mwaka kwa kuzingatia hali halisi ya mahitaji.

Mheshimiwa Spika, malengo ya ujenzi wa nyumba za walimu kwa muda wa miaka mitano 2002 - 2006 ya (MMEM) Kitaifa ni kama ifuatavyo:-

| Mwaka | Nyumba |
|---|---|
| 2002 | 8,000 |
| 2003 | 7,732 |
| 2004 | 8,197 |
| 2005 | 3,921 |
| 2006 | 3,266 |

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kwamba, Serikali hutoa Ruzuku ya Maendeleo *(Development Grant),* kwa kila jengo lililopangwa kujengwa shuleni. Kwa hiyo, fedha za Ruzuku ya Maendeleo zinazotolewa hazilengi kujenga madarasa tu, bali kulingana na mpango wa ujenzi wa shule husika, fedha hizo zinaweza kutumika katika kujenga aina zote za majengo ya shule, pamoja na kununua samani za shule kwa lengo la kufikia katika kila Wilaya vile vigezo vinne vya ujenzi na uendeshaji wa shule ambavyo ni:-

(i) Umri wa wanafunzi darasani uwe sawa au karibu sawa ili wafundishwe vizuri kwa kasi moja;

(ii) Wingi wa wanafunzi darasani wasiwe zaidi ya wanafunzi 40;

(iii) Ukubwa wa shule ya msingi kwa wingi wa wanafunzi (a) vijijini usizidi mikondo miwili (40x2x7) jumla wanafunzi 560; na (b) Mijini usizidi mikondo mitatu yaani 40x3x7 sawa na wanafunzi 840; na

(iv) Viwango vya Ubora kwa majengo ya shule yakiwemo madarasa nyumba za walimu na maliwato.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

La kwanza, itakumbukwa kwamba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni alisitisha ziara yake kwa Mkoa wa Lindi; je, sasa lini atafanya tena ziara hiyo ili aweze kujionea mwenyewe hali halisi ya walimu na madarasa hayo yanayojengwa katika Mkoa wa Lindi hususan Wilaya ya Liwale?

Pili, kwa vile walimu wengi hasa vijijini wamekuwa na matatizo mengi sana wakati wanapewa uhamisho na kutokupewa posho zao zinazostahili, hali hii imefikia kwamba Wilaya zote pamoja na Wilaya yangu ya Liwale walimu wanadai zaidi ya shilingi milioni 59. Sasa Lini Wizara itafanya mkakati wa kuweza kulipa malimbikizo haya ya madai ya walimu wa shule za msingi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni aliahirisha ziara kwa Mkoa Lindi, lakini aliahirisha kwa sababu kubwa mbili. Moja, alikuwa anahitaji maelezo ya kutosha kuhusu Mkoa huo ili anapokwenda awe na majibu. Kwa mfano, tunajua kule Liwale tuliwapa shilingi 30,173,758.59 kama Ruzuku ya Maendeleo na tumepanga vilevile kupeleka fedha zaidi baadaye mwaka huu shilingi 28,461,291.86 kwa ajili ya kupunguza matatizo. Kwa sababu tunajua Liwale sasa hivi kuna nyumba za walimu 58 na mahitaji yao halisi ni nyumba 313. Kwa hiyo, tuna upungufu wa nyumba walimu za walimu 255. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, ingawa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, aliahirisha ziara ile, hakuifuta alitaka hizi

kumbukumbu na ndiyo maana anatanguliza na hizi fedha nyingine shilingi milioni 28 ili akienda matatizo ya Liwale yaweze kutatuliwa kwa urahisi zaidi na hii ni kwa kila Wilaya katika Mkoa wa Lindi.

Kuhusu swali lake la pili, halihusiani na swali la msingi juu ya madai ya walimu. Lakini napenda kumthitibishia kwamba, Wizara ya Elimu na Utamaduni, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, inafanya kila jitihada iwezekanayo ili shilingi milioni 59 wanazodaiwa katika Wilaya ya Liwale na katika Wilaya nyingine, ziweze kulipwa taratibu kama shughuli yenyewe ya ulipaji kwa walimu wote ilivyokuwa tayari imeshaanza.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa vile katika swali la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri, amejibu kabisa kwamba, MMEM inaboresha au ina nia ya kuboresha mazingira ya elimu ya msingi kwa ujumla, nyumba, madawati, maliwato na vinginevyo. Napenda kuuliza kwamba kwa vile watu wenye ulemavu ni sehemu ya jamii, je, ni lini Serikali itatoa michoro ya nyumba za walimu na madarasa yanayokidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu kwa mfano, wasioona, wale wanaoenda na *wheel-chair* kusudi iwe ni rahisi kwenda darasani? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Margareth Mkanga, tumekuwa naye katika Ofisi yetu ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kuhusu sera ya walemavu na alifurahishwa vilevile na hatua ambayo Serikali imeanza kuchukua katika Vyuo vya *VETA,* kutengeneza mazingira ambayo yataruhusu na walemavu nao kuweza kufanya shughuli zao bila matatizo. Kwa kweli hiyo ni sera ya Serikali kwa jumla. Lakini lazima tuwe na mahali pa kuanzia na mahali pa kuanzia ni sera hiyo ya walemavu ambayo anaifahamu Mheshimiwa Mkanga kwamba, iko katika hatua za mwisho mwisho kabla ya kupelekwa kwenye Baraza la Mawaziri na kuletwa Bungeni kama sheria.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika majibu ya swali la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba, Wizara katika kuboresha Elimu ya Msingi inapunguza uwiano wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 40. Lakini mikakati hiyo haikujibu swali la shule yenye wanafunzi 90, lakini madarasa yote kutoka darasa la kwanza mpaka darasa la saba kwa uwiano kwamba sasa shule kama hiyo itakuwa na walimu wawili wasioweza kumudu madarasa saba. Je, anasema nini? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza uamuzi huu wa kuweka uwiano wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 40 ni uamuzi ambao ulitokana na Mawaziri wa Elimu wa Afrika ambao walikutana mwezi Desemba, 2002 pale Dar es Salaam na kuamua kwamba, waweke uwiano unaofanana kwa nchi zote za Afrika kwamba wanafunzi sasa tubadilishe kutoka 1 kwa 45 iwe 1 kwa 40. Kwa hiyo ni uamuzi wa Afrika na inawezekana tukapata matatizo katika utekelezaji wake. Lakini hayo matatizo ndiyo njia ya kutusaidia kurekebisha humo njiani na kufikia mwisho wake. Hata hivyo, tatizo la upungufu wa walimu kama nimemuelewa vizuri, ni tatizo ambalo linafahamika, lakini tunafanya jitihada kubwa sana. Kwa mfano, tumejitahidi kuajiri walimu 20,000 na hawa walimu tarajali watakapokuwa wamemaliza muda wao mwakani, tutakuwa tumezidi lengo la walimu wa shule za msingi kwa walimu karibu 4,000. Kwa hiyo, tunakwenda taratibu matatizo haya yatakuwa yanatoweka tu kwa sababu tumeanza. *(Makofi)*

Na. 275

**Ukarabati wa Sehemu za Barabara ya Songwe -Tunduma**

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkandarasi aliyepewa kazi ya kukarabati sehemu ya barabara ya Songwe - Tunduma inaelekea kwamba ameshindwa kazi hiyo kutokana na ukweli kwamba vifaa anavyotumia ni vibovu na kwamba tangu aanze kazi kwenye barabara hiyo yenye urefu wa km. 75 bado kazi yake hairidhishi kwa maana kwamba hajaweza hata kukamilisha km.5 kati ya hizo 75; na kwa kuwa wakati wote vifaa vya matengenezo kama vile magari, greda na mitambo mingine vinakuwa kwenye matengenezo ya mara kwa mara:-

(a) Je, ni vigezo gani vilivyotumika kumpata Mkandarasi ambaye hana ujuzi wa kutosha na badala yake anajifunzia kazi kwenye barabara hiyo ya Kimataifa?

(b) Je, Serikali ina habari kwamba hivi sasa kazi haiendelei na kwamba kwa msingi huo barabara hiyo haitaweza kukamilika kama ilivyopangwa na hivyo kulikosesha Taifa letu fedha kutokana na kutoweza kutumika kwa barabara hiyo na wenzetu wa nchi jirani?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Vigezo vilivyotumika kumpata Mkandarasi huyu ni kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za Zabuni za *General Regulation for the Procurement of Works Services and Supplies Under IRP 1991.*

- Tangazo la kuwakaribisha Makandarasi mbalimbali kuomba kuwekwa kwenye orodha ya wazabuni walio na sifa lilitangazwa na Bodi ya Taifa ya Zabuni katika kikao chake cha 17 Julai, 2000 ambapo Makandarasi 17 wenye sifa za kutosha kushindania zabuni hiyo walichaguliwa.

- Mchujo wa wazabuni hao 17 walioteuliwa na Bodi ya Zabuni, ulifanywa na Mhandisi Mshauri, *M/S Norconsult International AS,* kutoka Norway, ambapo Makandarasi sita waliokuwa na sifa za juu kuliko wenzao waliruhusiwa kununua nyaraka za zabuni.

- Zabuni zilizonunuliwa na Makandarasi hao sita wenye sifa za juu, zilifunguliwa tarehe 10 Julai, 2001 na Bodi ya Taifa ya Zabuni. Baada ya ufunguzi, zabuni hizo zilitumwa Wizara ya Ujenzi na baadaye zilipelekwa kwa Mhandisi Mshauri, *M/S Norconsult,* kufanya uchambuzi wa kina na baada ya uchambuzi, Mkandarasi *China Road and Bridge Corporation* alipendekezwa kupewa kazi ya ukarabati.

- Wakati wa uteuzi wa Mkandarasi huyu, Wizara ilitegemea kuwa atafanya kazi yake bila matatizo yoyote kwa vile alikuwa na sifa zote ambazo zilihitajika.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kazi ilikuwa haiendelei vizuri hapo awali na hadi kufikia mwezi Juni 2003, Mkandarasi alikuwa amekamilisha asilimia 25 ya kazi ikilinganishwa na asilimia 40 iliyokusudiwa kimkataba. Jitihada mbalimbali zimefanyika kumhimiza Mkandarasi huyo aongeze uzalishaji na kuanzia mwezi Juni, 2003, Mkandarasi ameanza kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi kwa kiwango kinachoridhisha. Jitihada zilizofanyika ni pamoja na kufanya kikao tarehe 22 Agosti, 2002 kilichotathmini maendeleo ya mradi na kiliwahusisha Mkandarasi, Mwajiri (*TANROADS* na Wizara), Mfadhili, Ubalozi wa China na Mhandisi Mshauri. Katika kikao hicho Mkandarasi alielezwa wazi kwamba, kama hakutakuwa na mabadiliko kwenye kazi, hatua za kimkataba zitachukuliwa dhidi yake. Aidha, Mkandarasi aliagizwa afanye yafuatavyo:-

(i) Abadilishe wataaalm walioonekana kuwa na mapungufu; na

(ii) Aongeze baadhi ya mitambo na kubadilisha mitambo ambayo ilikuwa na uzalishali mdogo, hususan katika kupasua miamba ya mawe na kusaga mawe.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu ulikuwa nyuma kwa muda wa miezi miwili hadi kufikia mwezi Juni, 2003 na iwapo Mkandarasi hatakamilika mradi katika muda uliopangwa, Serikali itachukua hatua sawa na masharti ya Mkataba.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Kwa kuwa sasa amekubali kwamba Mkandarasi alikuwa hana uwezo wa kufanya kazi kwa *speed* waliyokubaliana na baada ya vikao vyao ndiyo wanasema watamuangalia tena baadaye kama anakwenda sawasawa. Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba huyo Mkandarasi atalipualipua kazi tu kama wanavyolipua barabara zingine tunazoziona sasa hivi zinajengwa, lakini inaonekana wanakwenda kwa *speed* ili kukidhi miezi ile halafu barabara zinabomoka baada ya muda mfupi, haoni kwamba huyo Mkandarasi bado hakuwa na sifa nzuri?

(b) Kwa kwa barabara hiyo hiyo ndiyo inayokwenda Sumbawanga na Mheshimiwa Waziri alishatoa taarifa hapa Bungeni kuhusu mpango wa miaka miwili, mitatu, iliyopita kwamba barabara hiyo itatengenezwa kwa

kiwango cha lami kutoka Tunduma kuelekea Sumbawanga. Lakini kilomita 52 za kwanza kwenda Ndaramba toka Tunduma. Je, baada ya yule kumaliza kufika Tunduma ni vyema basi aendeleze kile kipande kingine ambacho wameshatoa kuelekea Sumbawanga?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Eliachim Simpasa, kwa jinsi anavyofuatilia bararabara hii kwa karibu sana na ndiye hasa alisababisha Mheshimiwa Waziri anitume mimi niende nikaiangalie barabara hiyo. Sasa ni kwamba, huyu Mkandarasi sababu mojawapo ya kuchelewa kazi kwa muda wa miezi miwili ni kwa sababu ya kusimamiwa kwa karibu sana. Tunaye *Resident Engineer* wetu, tunaye *Consultant Engineer,* ambaye ameteuliwa na *European Union,* wote wanamsimamia huyo Mkandarasi. Kwa hiyo, hatalipua hiyo barabara kwa mantiki ya kufidia muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, je, itawezekana sasa huyu akishafika mpakani aendelee na zile kilomita 50 kutoka Tunduma kuelekea Sumbawanga? Kiutaratibu haitawezekana hata kidogo. Kwa sababu hii, itatangazwa *tender* mpya na yeye kama akiomba na akafanikiwa atapewa. Lakini kama hakufanikiwa ni mtu yeyote ambaye atakuwa na sifa na akafanikiwa ndiye atakayepewa.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa majibu ya msingi yamedhihirisha kwamba inawezekana mapungufu ambayo yanapelekea kutokea matatizo kama haya ni kwa sababu Makandarasi wanakuwa hawafahamiki. Kwanza, uwezo na ujuzi kwa maana ya vifaa pamoja na wataalam. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana na mimi kwamba sasa ni bora *CRB* ikaweka mojawapo ya vigezo kwamba hawa Wakandarasi wawe na *websites* ambazo zita-*declare openly* uwezo wao wa vifaa pamoja na utaalam na vile vile na kazi ambazo wanakuwa wanazifanya kwa wakati huo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Wakandarasi hawa 6 ambao walichujwa na *Norconsult* ni Wakandarasi waliokuwa na sifa ambazo zinatosheleza kupewa *tender*. Kwa hiyo, taarifa zao zote zilikuwa zinajulikana na *CRB* wanazifahamu na ziko wazi kwao. Kwa hiyo, ni Mkandarasi ambaye sifa zake zinajulikana na kazi alizofanya zinajulikana. Lakini inawezekana amekwama tu kwa sababu ya utaalam na mapungufu yale ambayo nimeyataja kwenye jibu la msingi kwamba alikuwa na wataalam ambao hawakuwa na sifa na tulimlazimisha awaondoe wataalam hao.

Na. 276

**Barabara ya Ikoma *Gate* - Makutano**

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Ikoma *Gate* hadi Makutano ni muhimu sana kwa ajili ya kukuza shughuli za Utalii Mkoani Mara; na kwa kuwa barabara hiyo ni ya Udongo haipitiki nyakati za mvua na masika na hivyo kuwa kero kwa watalii na wananchi:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya hali ya barabara hiyo?

(b) Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami au changarawe kama inavyofanya sasa katika barabara ya Makuyuni hadi *Ngorongoro Gate*?

(c) Je, Serikali itakubali na kukiri kwamba kutoifanyia matengenezo barabara hiyo kumezorotesha shughuli za Utalii Mkoani Mara na hivyo kuathiri uchumi wake?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Mkoa wa Mara na Taifa hili kwa ujumla na kwa kuzingatia gharama kubwa ya ujenzi kwa kiwango

cha lami, Serikali imebadili mwelekeo wa barabara hiyo kwa nia ya kupunguza urefu wa kujengwa kwa lami na hivyo kupunguza gharama za ujenzi.

Kwa kuwa tayari barabara ya kutoka Makutano hadi Kyabakari ina lami, tumeamua kuanza kujenga barabara ya lami kutoka Kyabakari hadi Butiama (kilometa 12) badala ya Makutano hadi Butiama (kilometa 24) na baadaye tutaendelea hadi *Fort Ikoma* kupitia Nyamuswa kadri uwezo wa kifedha utakavyoruhusu. Awamu ya kwanza ya sehemu ya Kyabakari - Butiama ya kuweka Makalvati, pamoja na kunyanyua tuta sehemu yalipojengwa makalvati kwa gharama ya shilingi milioni 714, imekamilika mwaka wa fedha 2002/2003. Maandalizi ya awamu ya pili ya sehemu ya Kyabakari - Butiama yameanza kwa utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kuitisha zabuni ya kujenga tuta lote na kuweka tabaka la lami. Kazi ya ujenzi itaanza mwaka wa fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya barabara hii ya Makutano-Butiama - Nyamuswa na kufika hadi *Ikoma Gate* inapitika kwa sasa kwani inafanyiwa matengenezo ya kawaida ya mara kwa mara wakati juhudi za kutafuta wafadhili kwa ajili ya ujenzi kufikia kiwango cha lami, sehemu iliyobakia inaendelea. Katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, jumla ya shilingi milioni 120/= zilitumika kwenye matengenezo ya sehemu korofi. Aidha, tarehe 19 Juni, 2003 Mkataba umesainiwa wa jumla ya shilingi milioni 450 kwa ajili ya ukarabati wa barabara hii.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anakumbuka kwamba kwa maslahi ya Taifa, Mkoa wa Mara ulikubali kwamba mpaka wa Porongoja ufungwe na hivyo kufanya watalii kupitia Arusha kutoka Mwasaimara kwenda Arusha na kurudi. Lakini ahadi ilikuwa kwamba barabara hiyo ya Sirari - Makutano mpaka *Ikoma Gate* itatengenezwa. Angalau anasema kwamba inapitika, hiyo barabara ni mbaya sana hadi sasa. Je, kwa sababu sasa sisi watu wa Mkoa wa Mara tunakosa watalii, kwa sababu ya kuwa na barabara mbaya, Serikali inaweza kukiri na kusema kwamba itatu-*compensate in one way or another?*

(b) Je, Mheshimiwa Waziri kwa sababu hajatembelea barabara zetu za Mkoa wa Mara, anaweza kuja na kuziona hasa katika Wilaya ya Serengeti kuona kwamba ni mbaya sana zinawekewa tu viraka badala ya kutengenezwa kikamilifu ili aje kujionea mwenyewe kwani kuona ni kuamini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba, barabara za kule ni mbovu na ndiyo maana Serikali tunajitahidi sana sasa hivi kuitengeneza barabara hii iwe kwa kiwango cha lami mpaka *Ikoma Gate* ili watalii waweze kupita kutoka Musoma wakipitia Butiama na kufika kule.

Kwa hiyo, ni jitihada ya Serikali kabisa kuhakikisha kwamba, barabara hizo za Mkoa wa Mara zinakuwa nzuri. Tutajitahidi kwa uwezo wetu wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu la pili, kwa kweli ilikuwa nifike katika Mkoa wa Mara kabla ya kipindi hiki cha Bunge, lakini nilikwama kwa shughuli za dharura kidogo ilibidi badala ya kwenda Mkoa wa Mara niende Sumbawanga mara ya pili. Kwa hiyo, ninatumaini kwamba, safari hii itafika huko.

Na. 277

Hifadhi ya Misitu ya Milima ya Usambara

**MHE. CHARLES H. KAGONJI (k.n.y. MHE. HENRY D. SHEKIFFU)** aliuliza:-

Kwa kuwa Shirika la *TANAPA* linafanya kazi nzuri ya hifadhi ya misitu ya Milima ya Usambara ambazo zimo katika hatari ya kutoweka na kwamba kuna misitu na mimea hususan miti ambayo haikulindwa kikamilifu na uoto wa asili unaelekea kutoweka kabisa kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira:-

(a) Je, ni utaratibu na vigezo gani vinavyotumika ili kulifanya eneo fulani kutangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa?

(b) Kwa kuwa ni dhahiri kwamba maeneo mengi ya Hifadhi ya Misitu ya Milima ya Usambara Magharibi yameharibika sana kutokana na uchomaji moto na ukataji wa mbao ovyo kwa njia za wizi ambao Serikali imeshindwa kuudhibiti kupitia Idara ya Misitu; na kwa kuwa *TANAPA* imeonyesha uwezo mkubwa wa kulinda maliasili adimu kama zile za Hifadhi za Milima ya Udzungwa, Mahale na kadhalika; Je, ni kwa nini *TANAPA* isipewe jukumu la kulinda na kuhifadhi maeneo nyeti katika Milima ya Usambara ambayo ni chanzo muhimu cha maji yanayotumika kuzalisha umeme kwenye vituo vya Hale na Pangani?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Henry Daffa Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa vigezo vinavyotumika kutenga eneo fulani kuwa Hifadhi ya Taifa ni kama ifuatavyo:-

- Wananchi kutokana na kuchukia uharibifu wa mazingira au kuona vivutio vilivyopo ni bora viendelezwe kwa shughuli za utalii, hutoa pendekezo kwenye Halmashauri za Wilaya husika.

- Halmashauri ya Wilaya husika hutafakari na kukubali mapendekezo ya wananchi na kwa kupitia vikao halali huwasilisha mapendekezo hayo katika Wilaya yangu.

- Shirika la Hifadhi za Taifa, kwa kufuata vigezo vilivyowekwa na ambavyo nitavitaja punde hutoa uamuzi wake.

- *TANAPA* wakifuatana na Uongozi wa Wilaya hupita katika eneo husika na kuelezea kazi zake na manufaa yatakayopatikana kwa wananchi endapo eneo litatangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa.

- Wataalam wa kupima mipaka ya *TANAPA* huandaa rasimu ya eneo na kuiwasilisha Wizarani kukamilisha taratibu za kisheria.

Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotumika katika kulitangaza eneo fulani kuwa Hifadhi ya Taifa vimebainishwa katika Sera ya Hifadhi za Taifa ya 1994. Vigezo hivyo ni:-

- Eneo liwe na maliasili au amali *(resources)* za kitamaduni zenye umuhimu Kitaifa, kwa mfano, maliasili za kipekee, Kimataifa, ubora wa thamani ya kipekee inayodhihirisha urithi wa Tanzania, kulinda vyanzo vya maji na ardhi inayodumisha uwiano wa kiikolojia na kusaidia kuikimu jamii nje ya eneo husika, ubora wa kunufaisha au kuburudisha au kwa ajili ya utafiti wa kisayansi na mfano halisi wa maliasili ambayo haijaharibiwa.
- Eneo liwe ni nyongeza inayofaa na inayowezekana katika mfumo wa hifadhi kwa kuwa na ukubwa wa kutosha wenye kuzingatia mifumo ya kiasili ili kudumisha uhifadhi wa maliasili.

- Eneo lisimamiwe na Shirika la Hifadhi za Taifa moja kwa moja badala ya kusimamiwa na chombo kingine kinachomiliki ardhi au Sekta binafsi.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Misitu ya Milima ya Usambara Magharibi ambayo ni sehemu ya Milima ya Safu ya Ukanda wa Mashariki yenye utajiri wa mimea na viumbe adimu, imekuwa inaharibiwa kutokana na uchomaji moto, uvunaji usiodhibitiwa na uvamizi kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imechukua hatua mbalimbali za kudhibiti uharibifu huu ikiwa ni pamoja na kufanya doria na kuwafikisha Mahakamani wahalifu wanaokamatwa, kuwashirikisha wananchi na jamii zinazozunguka misitu hiyo katika kusimamia, kuiendeleza na kuitumia misitu kwa uendelevu. Ushiriki wa wananchi katika kutunza, kuendeleza na kuilinda misitu hiyo umeonyesha mafanikio yafuatayo:-

(i) Vijiji vitano vinavyozunguka misitu ya Shagayu na Gologolo, kila kimoja kimeweza kuanzisha Kamati ya Mazingira ambayo inahusika na masuala ya uhifadhi na ulinzi wa misitu kikamilifu; na

(ii) Katika maeneo ambayo wananchi wanashirikishwa, ushiriki wao umewezesha kuwafichua wahalifu na kupunguza matukio makubwa ya uhalifu kutoka 30 mwaka 1999 hadi matukio matatu mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hatua zinazochukuliwa za kuhifadhi misitu hiyo muhimu na kuzingatia madhumuni ya msingi ya uhifadhi, misitu hiyo itaendelea kusimamiwa kwa utaratibu uliopo.

**SPIKA:** Kwa kuwa mwuliza swali la msingi hayupo, naomba Mheshimiwa Kagonji, uruhusu muda uliobaki tuutumie kujibu swali linalofuata la Mheshimiwa Ngwatura.

Na. 278

**Raslimali ya Meno ya Tembo**

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati biashara ya meno ya Tembo ilipozuiliwa, Tanzania ilikuwa na tani nyingi za meno ya Tembo, mali ambayo ilikuwa iuzwe na kuliingizia Taifa mapato:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha na raslimali nyingine zinatumika katika kulinda na kuhifadhi raslimali hiyo?

(b) Kwa kuwa nchi za Botswana, Zimbabwe, Namibia na Afrika Kusini zimeruhusiwa kuuza shehena zao baada ya kutimiza masharti ya kimenejimenti na kiuhifadhi wa Tembo, je, ni sababu zipi zinaifanya Tanzania isiruhusiwe kuuza meno ya Tembo ambayo yamerundikana tangu mwaka 1989?

**WAZIRI WA MALISILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ireneus Ndunguru Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Gharama ya kulinda meno ya tembo inajumuisha mishahara ya watumishi, kazi ya kuhesabu (kuhakiki) na kupanga meno ya tembo stoo, matengenezo ya mara kwa mara ya mashelfu ya kutunzia meno na uhakika wa utunzaji wa nyaraka/kumbukumbu.

Makadirio ya jumla ya gharama hizo kwa mwaka ni takriban shilingi milioni 28. Gharama hizi zinajumuisha ulinzi wa Ofisi zote pamoja na vitendea kazi mbalimbali vilivyoko katika eneo la *Ivory Room.*

(b) Mheshimiwa Spika, ili nchi mwanachama wa Mkataba wa *CITES* iweze kuruhusiwa kufanya biashara ya meno ya tembo, pamoja na bidhaa nyingine zitokanazo na tembo, inapaswa iwe imetimiza masharti yafuatayo:-

- Kuwepo na uthitibisho wa kuonyesha kuwa kuna idadi ya kutosha ya tembo katika mazingira yao ya asili, kuonyesha kiwango cha kuongezeka, kuonyesha hali ya uvunaji haramu na takwimu za vifo vya asili.

- Nchi ionyeshe kuwa imeweka mkakati wa muda mrefu na namna inavyoutekeleza ili kuhakikisha kizazi cha tembo kinaendelezwa bila kuathiriwa ki-ikolojia.

- Nchi ionyeshe jinsi inavyotekeleza Mpango wa kufuatilia mwenendo wa Uwinadji wa Tembo, yaani *Monitoring of Illegal Killing of Elephants (MIKE),* kwa kutoa taarifa na takwimu zinazohusu uvunaji haramu wa tembo katika nchi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kuwepo kwa masharti yaliyotajwa na kwa kuwa bado hatujaweza kutekeleza masharti hayo kikamilifu, Tanzania haijafikia hatua ya kuomba kufanya biashara ya meno ya tembo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu, kuwa Tanzania imeanza kutekeleza mpango wa muda mrefu wa kudhibiti ujangili, hususan uanzishaji wa maeneo ya Jumuia ya Uhifadhi wa Wanyamapori *(Wildlife Management Areas)*. Aidha, mikakati mingine ni ya kutenga fedha za kutosha, kwa kutumia mpango wa Serikali wa *Retention* na Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori Tanzania *(TWPF).* Pamekuwepo na matokeo mazuri katika suala zima la uhifadhi wa tembo, kwa mfano, tembo wameongezeka nchini kutoka 52,000 mwaka 1989 hadi 83,000 mwaka 2002. Mara mpango huu mahsusi wa kudhibiti ujangili utakapokuwa umefanikiwa, tathmini itafanyika mara moja na hatua ya kuondoa kutumia mazao ya tembo kwa maana ya meno, itachukuliwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Tunaendelea na shughuli nyingine, baada ya matangazo yafuatayo:-

Vikao vya leo ni kama ifuatavyo: Kuna kikao cha Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. William Shija, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje wakutane katika chumba Na. 56 saa 5.00 asubuhi hii.

Kikao kingine ni cha Waheshimiwa Wabunge Wanawake *(TWPG).* Mwenyekiti wake Mheshimiwa Anne Makinda anaomba Wabunge Wanawake wakutane leo kuanzia saa 7.00 katika chumba Na. 58, vyumba vya Kamati. Mheshimiwa Dr. James Nsekela, alishawatangazia wanachama wa *TAPAC* kuwa kutakuwa na semina katika makundi mbalimbali ya wanachama 40, 40. Sasa nataka niwakumbushe wale waliopangwa katika kundi la kwanza kwamba semina yao itakuwa leo hii kuanzia saa 7.00 na itafanyika katika chumba Na. 81, hiyo ni *TAPAC.*

Baada ya hapo napenda kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge, mabadiliko madogo katika ratiba ya jinsi Wizara zitakavyowasilisha makadirio yake hapa Bungeni. Kutokana na msiba uliompata Mheshimiwa George Kahama, ameomba na amekubaliwa apangiwe siku nyingine ya kuwasilisha makadirio yake. Alikuwa awasilishe Jumatatu ijayo tarehe 28 Julai, 2003 sasa wamekubaliana na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto wabadilishane tu. Kwa hiyo, tarehe hiyo ya 28 Julai, 2003 itakuwa ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ambayo ilipangiwa tarehe 31 Julai, 2003. Kwa hiyo, tarehe 31 Julai, 2003 ndiyo atakuja Waziri wa Ushirika na Masoko, Mheshimiwa Kahama.

Mwisho wa matangazo. Tuendelee na *Order Paper.*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2003/2004**
**Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo**

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kisekta ya Ardhi na Kilimo, likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kwasilisha hotuba yangu, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya, waliochaguliwa katika Chaguzi ndogondogo zilizofanyika mwezi Mei, 2003. Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa pamoja na Majimbo yao ni hawa wafutato: Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga (CCM - Kilombero), Mheshimiwa Ali Said Juma (*CUF* - Kojani), Mheshimiwa Ali Said Salim (*CUF* - Ziwani), Mheshimiwa Bakar Shamis Faki (*CUF* - Ole), Mheshimiwa Edward Ndeka Nziriye (CCM - Kigoma Kusini), Mheshimiwa Khamis Ali Salehe (*CUF* - Mgogoni), Mheshimiwa Karim *Said Othman* (CUF - Chambani), Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa (*CUF* - Mtambwe) na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa (*CUF* - Gando).

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim (*CUF* - Mtambile), Mheshimiwa Mchande Salim Mchande (*CUF* - Konde), Mheshimiwa Mohammed Ali Said (*CUF* - Wingwi), Mheshimiwa

Mohamed Juma Khatib (*CUF* - Chonga), Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha (*CUF* - Utaani), Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi (CCM - Bukoba Vijijini), Mheshimiwa Omari Juma Omary (*CUF* - Pandani), Mheshimiwa Salim Omar Ali (*CUF* - Tumbe), Mheshimiwa Shoka Khamis Juma (*CUF* - Micheweni) na Mheshimiwa Sumri Abdallah Salum Mohamed (CCM - Mpanda Magharibi).

Pia, nachukua fursa hii kuwapongeza wananchi wa Majimbo hayo kwa kupata wawakilishi katika Bunge hili Tukufu. Nawapongeza pia wale waliorejeshwa na Mahakama. Nachukua fursa hii kuwapongeza wananchi wa Majimbo hayo kwa kupata uwakilishi katika Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri Mkuu, Mbunge wa Hanang, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mbunge wa Handeni, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda na Waziri wa Fedha, Mbunge wa Rombo, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, kwa hotuba zao nzuri zilizoweka mwelekeo wa Bajeti ya Serikali katika mwaka huu wa fedha wa 2003/2004. Malengo, maelekezo na vigezo vilivyomo kwenye hotuba hizo vimezingatiwa kikamilifu katika kuandaa Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2003/2004. Pia nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote walionitangulia kwa hotuba zao nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Juni, 2003, Kamati ya Bunge ya Ardhi na Kilimo, chini ya Mwenyekiti wake, Mbunge maarufu sana Mbunge wa Mbozi Magharibi, Mheshimiwa Joachim Simpassa, ilipitia na kuchambua Taarifa ya Kazi na Malengo ya Serikali yaliyotekelezwa na Wizara yangu kwa mwaka 2002/2003 na Mapendekezo ya Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2003/2004. Napenda kuchukua fursa hii, kuishukuru Kamati hiyo kwa kupitia kwa kina, Bajeti ya Wizara yangu. Naushauri maoni, mapendekezo na maelekezo waliyoyatoa, ambayo yatasaidia kuboresha huduma zitolewazo na Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inazingatia kwa makini maelekezo yaliyomo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2000 katika kutekeleza majukumu ya Sekta ya Maji na Mifugo. Kwa kifupi, Ilani inasisitiza juu ya ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji, kufufua na kujenga mabwawa ya maji, kushirikisha wananchi katika ujenzi na uendeshaji wa miradi yao ya maji, kuvuna maji ya mvua na utunzaji wa vyanzo vya maji. Aidha, Ilani inatilia mkazo ushirikishaji wa Halmashauri za Wilaya katika kuweka miundombinu ya mifugo na uboreshaji wa ufugaji ili utoke ule wa kijadi na kuwa ufugaji wa kisasa unaozingatia ubora wa mifugo kuliko wingi. Pia, Ilani inaelekeza kuweka mkakati wa Kitaifa wa kuwaandalia wafugaji mazingira mazuri yatakayowahakikishia upatikanaji wa maji, malisho na majosho ili hatua kwa hatua waondokane na maisha ya kuhamahama. Maelezo kuhusu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM na Malengo ya Serikali kwa mwaka 2002/2003, yameelezwa kwa kina katika aya zifuatazo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, katika Wizara yangu, kumekuwa na mikutano na matukio muhimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mwaka 2002 Serikali ilipitisha Sera ya Maji baada ya Wizara yangu kukamilisha mapitio na marekebisho ya sera ya mwaka 1991 kwa kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi na kijamii. Sera ilizunduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, tarehe 16 Machi, 2003 wakati akizindua Maadhimisho ya Wiki ya Maji Mjini Shinyanga.

Aidha, Sera inalenga katika kuweka mazingira mazuri yatakayowawezesha wananchi, sekta binafsi, Taasisi za Kitaifa na Kimataifa, pamoja na wadau wengine, kuchangia katika kuleta ufanisi wa huduma ya maji nchini. Wizara yangu ina jukumu la kuhakikisha kuwa, Sera inatekelezwa kikamilifu kulingana na taratibu na sheria zilizopo. Kwa sasa, Wizara inaendelea kuandaa Mkakati shirikishi wa kutekeleza sera hii pamoja na kuboresha Sheria za Maji ili ziendane na sera. Nia ya Wizara ni kueneza na kuisambaza Sera ya Maji, kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na vipindi vya redio, televisheni, magazeti, vijarida, vipeperushi na mafunzo kwa vikundi vya watumia maji na watalamu katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, kila mwaka kati ya tarehe 16 na 22 Machi, Wizara yangu huandaa Maadhimisho Kitaifa ya Wiki ya Maji kwa madhumuni ya kutoa nafasi kwa wadau wa Sekta ya Maji, kutathmini hali halisi ya maendeleo ya utoaji huduma ya maji nchini. Maadhimisho haya hufikia kilele tarehe 22 Machi kila mwaka, sambamba na maadhimisho ya siku iliyochaguliwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kuwa Siku ya Maji Duniani *(World Water Day),* kufuatana na Azimio lake la mwaka 1993.

Kwa mwaka 2003, maadhimisho hayo ya Wiki ya Maji, ambayo maudhui yake yalikuwa "Hifadhi Maji kwa Vizazi Vijavyo", Kitaifa yalifanyika Mkoani Shinyanga ambapo yalifunguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Pamoja na mambo mengine Mheshimiwa Rais, alizindua Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kwa Mkoa wa Shinyanga, ambayo inatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali yetu na Serikali ya Uholanzi na maonyesho ya vifaa na Teknolojia za Maji.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kukubali kuzindua maadhimisho hayo ya Wiki ya Maji. Kushiriki kwa Mheshimiwa Rais katika maadhimisho haya kumetoa msukumo mkubwa, faraja kwa wananchi na changamoto katika juhudi za Serikali za kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika uendelezaji wa miradi ya maji. Aidha, napenda kuwashukuru wananchi wote wa Mkoa wa Shinyanga, wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Abubakar Mgumia, pamoja na viongozi wengine kwa kushiriki kikamilifu katika maadhimisho hayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeweka utaratibu wa kufanya kongamano kila mwaka, kuwakutanisha wataalam wa maji kutoka nchini kote. Madhumuni ya Kongamano hilo ni kubadilishana uzoefu na kujifunza mambo mapya yanayojitokeza katika Sekta ya Maji. Katika mwaka 2002/2003, Kongamano la *AWEC* lilifanyika kuanzia tarehe 25 hadi 29 Novemba, 2002 Mjini Arusha. Maudhui ya kongamano hilo yalikuwa Mchango wa Teknolojia ya Mawasiliano Katika Kuendeleza Sekta ya Maji. Kongamano liliazimia yafuatayo:-

(a) Upokeaji na utunzaji wa taarifa za maji kwa kutumia njia bora za mawasiliano;

(b) Kuimarisha na kuboresha mitandao ya kuweka na kupokea taarifa za maji;
(c) Ushirikishaji wa Sekta Binafsi; na

(d) Kuimarisha na kujenga uwezo wa kupata na kutumia nyenzo za kisasa za mawasiliano na kuhifadhia taarifa katika ngazi ya Wilaya.

Wizara yangu inayafanyia kazi maazimio haya ili kuboresha utoaji huduma ya maji nchini.

Mheshimiwa Spika, mkutano wa mwaka wa Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini ulifanyika Mjini Moshi kati ya Tarehe 3 - 4 Machi, 2003. Madhumuni ya mkutano huu ni kupima maendeleo ya utendaji kazi wa mamlaka hizo pamoja na kupitia taarifa za hesabu za mwaka. Maudhui ya mkutano huu yalikuwa uondoaji umaskini na huduma ya majisafi na uondoaji majitaka kwa wateja wenye kipato cha chini. Mkutano huo ambao ulifunguliwa na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, ulifungwa kwa kutoa maazimio ambayo yatatekelezwa katika kipindi cha mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maazimio ya mkutano huo, kuanzia mwaka huu wa fedha, mamlaka za majisafi na majitaka mijini katika Miji Mikuu ya Mikoa, itaanzisha utaratibu wa kuwapatia wananchi wasiojiweza huduma ya maji kwa bei nafuu. Kila familia isiyojiweza itapatiwa lita 5,000 za maji bure kila mwezi, sawa na ndoo nane za maji kila siku. Hata hivyo, matumizi ya maji yatakayozidi kiwango hiki, yatalipwa kwa bei ya kawaida ya maji ya majumbani. Utaratibu mzuri wa kuwatambua wasiojiweza, utawekwa na kila mamlaka kwa kuzingatia mazingira ya mji husika.

Matumizi ya dira ni muhimu sana katika kudhibiti matumizi ya maji yasiyokuwa ya lazima, pamoja na upotevu wa maji. Taratibu za kutoa huduma ya maji mijini zinaelekeza kuwa kila mteja aliyefungiwa dira ya maji, hana budi kuilipia dira hiyo kila mwezi *(Meter Rent).* Ni dhahiri kuwa ulipiaji huu una makusudi mazuri ya kurudisha gharama ya ununuzi wa dira hiyo ili pindi zitakapoharibika au kuchakaa, nyingine mpya ziweze kununuliwa na kufungwa. Hata hivyo, si busara kuendelea kumlipisha mteja fedha hizi kila mwezi hata pale ambapo gharama ya ununuzi wa dira imekwisha lipwa yote. Kwa mantiki hii, kuanzia mwaka huu wa fedha gharama za kuilipia dira kila mwezi zitasitishwa mara baada ya makato hayo kufikia gharama ya ununuzi wa dira husika.

Nachukua nafasi hii kuwaomba wateja wa maji kuzilinda na kuzitunza dira za maji ili zidumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Kimataifa wa Maendeleo Endelevu ulifanyika kuanzia tarehe 26 Agosti 4 - Septemba, 2002 Mjini Johannesburg Afrika ya Kusini. Wakuu wa nchi na viongozi wa Mashirika mbalimbali ya Kimataifa walikubaliana mambo muhimu matatu kuhusu Sekta ya Maji:-

(i) Kupunguza idadi ya watu duniani wasio na huduma ya majisafi na salama kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2015;

(ii) Kupunguza idadi ya watu wasio na huduma ya uondoaji majitaka na usafi wa mazingira kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2015; na

(iii) Kila nchi ianzishe na kutekeleza mfumo shirikishi wa usimamizi wa raslimali za maji ifikapo mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa makubaliano ya mkutano wa Johannesburg, kuanzia tarehe 18 - 22 Machi, 2003 kulifanyika Kongamano la Tatu la Maji Duniani huko Kyoto Japan. Katika kongamano hilo, Mawaziri wanaoshughulikia Sekta ya Maji Duniani, walikubaliana pamoja na mambo mengine kuwa kila nchi iandae Mkakati wa namna ya kufikia malengo yaliyokubaliwa katika mkutano huo. Wizara yangu inaandaa mkakati wa namna ya kutekeleza makubaliano hayo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na tatizo la kusambaa kwa magonjwa ya mifugo takriban katika Mikoa yote nchini, hali ambayo inachangia kurudisha nyuma juhudi za Serikali za kuendeleza sekta ya mifugo. Tatizo hili linatokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoandaliwa kikamilifu kwa sekta binafsi kutoa huduma za afya ya mifugo baada ya Serikali kujitoa, sheria za udhibiti wa ueneaji wa magonjwa ya mifugo zilizopitwa na wakati, kutokuwepo na mtiririko wa utoaji wa taarifa za magonjwa ya mifugo, usafirishaji holela wa mifugo, kutokuwepo na mikakati na mipango ya pamoja na nchi jirani katika kudhibiti magonjwa ya mifugo na magonjwa yanayoambukiza mifugo kutoka kwa wanyamapori.

Ili kuondokana na hali hii, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alitoa Waraka Namba 1 wa mwaka 2002, kuhusu hatua za kuchukua ili kudhibiti ueneaji wa magonjwa ya mifugo nchini. Waraka huu unaagiza mambo muhimu yafuatayo:-

(a) Kuanzia sasa kila Asasi iwe na mipango shirikishi ya kudhibiti magonjwa ya mifugo katika bajeti zake;

(b) Kila Halmashauri ya Wilaya ifungue mfuko wa kuendeleza sekta ya mifugo kwa kutenga asilimia isiyopungua 15 ya mapato yote yatokanayo na mifugo na kutoa taarifa za mapato na matumizi ya mfuko huu kwenye vikao vya Halmashauri;

(c) Kila Halmashauri za Wilaya ziwe na mipango ya kuelimisha sekta binafsi juu ya wajibu wao wa kusambaza madawa na kutoa matibabu ya mifugo;

(d) Halmashauri za Wilaya zitunge sheria ndogo za kuimarisha usimamizi wa minada na usafirishaji wa mifugo;

(e) Kuanzia sasa utaratibu wa kuswaga mifugo kwenye maeneo yenye reli, barabara za lami au njia za maji uachwe mara moja na Wakuu wa Wilaya wasaidie kufanikisha hili;

(f) Halmashauri za Wilaya zihakikishe kwamba, taarifa za magonjwa ya mifugo ziwe zinatumwa kwenye vituo vya kuchunguza magonjwa ya mifugo *(Veterinary Investigation Center)* kabla ya tarehe 5 ya kila mwezi na ndani ya saa 24 baada ya kupata tukio lolote la ugonjwa wa mlipuko;

(g) Halmashauri zote nchini ziwe na mipango ya kufufua majosho na au kujenga mengine mapya kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000; na

(h) Wafugaji wahimizwe kukaa kwa utaratibu wa kudumu kwenye maeneo walipo na walinganishe idadi ya mifugo yao na uwezo wa malisho uliopo ili ufugaji uendeshwe kwa faida.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kutoa Waraka huu ambao unalenga kutekeleza mikakati ya kupunguza umaskini nchini kwa njia ya kukuza Pato la Taifa litokanalo na sekta hii. Waraka huu tayari umesambazwa kwenye Wizara mbalimbali, Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Asasi zisizo za Kiserikali, sekta binafsi na kwa wadau wengine. Wizara inaendelea kutekeleza Waraka huu ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha wafugaji kuhusu njia za kukabiliana na magonjwa ya mifugo. Aidha, sheria mpya ya kudhibiti magonjwa ya mifugo inaandaliwa na inategemewa kuwasilishwa Bungeni mwezi Oktoba, 2003.

heshimiwa Spika, kila mwaka tarehe 8 Agosti huwa tunaadhimisha Siku ya Wakulima na Wafugaji nchini (Nane Nane). Lengo la maonyesho haya ni kutathmini mafanikio na matatizo ya sekta ya mifugo, pia kuwawezesha wafugaji na wadau wengine kujifunza mbinu bora za uzalishaji, usindikaji, hifadhi ya mazao yatokanayo na mifugo, pamoja na huduma za ushauri. Katika mwaka 2002/2003, Wizara ilishiriki katika maadhimisho hayo ambayo Kitaifa yalifanyika Mjini Morogoro na yalifunguliwa na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Pius Msekwa. Kauli mbiu ya maadhimisho haya ilikuwa ondoa umaskini kwa kuendeleza kilimo, ufugaji na ushirika. Kilele kilihitimishwa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye. Napenda kuchukua nafasi hii, kuwashukuru Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kukubali kufungua na kuhitimisha maonyesho hayo. Pia nawashukuru viongozi wengine pamoja na wananchi na wadau wote wa sekta ya mifugo kwa kushiriki kikamilifu katika maonyesho hayo.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuboresha na kuendeleza ufugaji nchini, kwa mara ya kwanza, kongamano la pamoja la Madaktari wa Mifugo, *Tanzania Veterinary Association (TVA)* na Maafisa wa Mifugo, *Tanzania Society of Animal Production (TSAP)* wa hapa nchini na nchi za jirani, lilifanyika Mjini Arusha kuanzia tarehe 3 - 5 Desemba, 2002. Madhumuni ya kongamano hilo yalikuwa kubadilishana uzoefu na kujifunza mambo mapya yanayojitokeza katika maendeleo ya sekta ya mifugo. Maudhui ya kongamano yalikuwa ni kuboresha maisha ya wananchi vijijini kwa kuendeleza ufugaji.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa huduma endelevu ni kigezo na kichocheo muhimu katika kufanikisha jitihada za Serikali za kupunguza umaskini nchini. Maji huhitajika kukidhi mahitaji mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukuza sekta za uzalishaji umeme, kilimo cha umwagiliaji, uvuvi, viwanda, pamoja na mahitaji ya binadamu, mifugo na wanyamapori. Maji pia huhitajika katika shughuli nyingine ambazo hutoa ajira na kuongeza kipato miongoni mwa wananchi hususan wenye kipato kidogo. Mathalani, upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo utawapunguzia wafugaji tatizo la kuhamahama hivyo kuwawezesha kupata huduma za kiuchumi na kijamii kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, sekta ya mifugo ni muhimu katika kutekeleza mkakati wa Taifa wa kuondoa umaskini hususan kwa wafugaji ambao kwao mifugo ni raslimali muhimu inayoweza kutumika haraka wakati wa dharura na kuwahakikishia kuwepo kwa chakula hasa wakati wa ukame. Mifugo hutoa mchango mkubwa katika kuendeleza kilimo kwa kuchangia nguvukazi, samadi, nishati na ajira kwa wafugaji. Inakadiriwa kuwa asilimia 80 ya Watanzania huishi vijijini kwa kutegemea ufugaji na kilimo. Kati ya kaya milioni 3.8 za wakulima zilizopo nchini, kaya milioni 1.4 au asilimia 37 zinafuga na kulima na kaya 119,000 au asilimia 3 zinafuga tu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitoe taarifa ya hali halisi ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2002/2003 na mapendekezo ya mpango wa mwaka 2003/2004 kwa sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kuboresha utoaji wa huduma ya majisafi na salama vijijini na mijini. Jitihada hizi zinaelekezwa zaidi katika kukarabati na kukamilisha miradi ya zamani na hatimaye kukabidhi kwa wananchi ili waitunze na kuiendesha wao wenyewe. Juhudi hizo zimeanza kuonyesha mafanikio ambapo takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba karibu asilimia 53 ya wananchi waishio vijijini na asilimia 73 ya wakazi waishio vijijini wanapata huduma ya majisafi na salama. Hata hivyo, ipo haja ya kufanya jitihada zaidi za kuwawezesha wananchi wetu kupata huduma bora na endelevu. Aidha, uwezo wa Serikali peke yake wa kuwapatia wananchi huduma ya maji karibu na maeneo wanayoishi katika kipindi kifupi ni mdogo. Ili kuongeza kasi ya utoaji huduma ya maji, wananchi na sekta binafsi zinashirikishwa kikamilifu kwa lengo la kuwapatia wananchi huduma ya maji safi na salama katika kipindi kifupi iwezekanavyo.

Wizara yangu itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukarabati miradi ya maji vijijini na mijini, kuchimba visima virefu na vifupi, hususan katika Wilaya kame, ujenzi wa mabwawa madogo na

makubwa na uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia teknolojia rahisi. Lengo ni kuhakikisha kuwa maji yanapatikana kwa wingi na ubora unaotakiwa kulingana na mahitaji ya sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii ili ziweze kuchangia zaidi katika Pato la Taifa. Kwa upande wa uondoaji wa majitaka, huduma hii imeboreshwa na kufikia asilimia 17 ya wakazi wote mijini kutokana na kukamilika kwa mradi mkubwa wa ukarabati wa miundombinu ya uondoaji majitaka katika miji 7 yenye mifumo hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina jukumu la kuweka mfumo endelevu wa kukusanya, kuchambua na kuhifadhi takwimu kuhusu raslimali za maji nchini. Takwimu hizi hutumika katika kutathmini raslimali za maji, kuboresha usanifu wa miradi ya maji na kuwezesha kupanga kwa usahihi matumizi endelevu ya rasilimali za maji kulingana na mahitaji ya sekta mbalimbali. Katika mwaka 2002/2003, Wizara yangu iliendelea kukarabati na kujenga vituo vipya vya kukusanyia takwimu ili kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za maji juu ya ardhi. Vituo 71 vya kupima wingi wa maji kwenye mito vimekarabatiwa katika mabonde ya maji ya Pangani na Rufiji na vituo 19 vya hali ya hewa vimekarabatiwa katika mabonde hayo kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itakarabati vituo 25 vya ukusanyaji wa takwimu za maji juu ya ardhi katika mabonde ya Mto Ruvuma na Ziwa Nyasa, Tanganyika, Rukwa na Bonde la Kati ambalo linajumuisha Maziwa ya Manyara, Eyasi na Natron. Aidha, chini ya Mradi wa Ukodishaji wa *DAWASA*, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* imetoa mkopo wa fedha Dola za Kimarekani milioni moja kwa ajili ya kukarabati vituo 35 vya kupima uwingi wa maji juu ya ardhi katika Bonde la Mto Ruvu/Wami, ambalo ndilo chanzo kikuu cha maji kwa Jiji la Dar es Salaam. Pia, vituo 9 vya kupima hali ya hewa vitajengwa chini ya programu hii.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Wizara yangu iliendelea kutafuta maeneo nchini yanayofaa kuchimba visima vya maji kwa matumizi mbalimbali. Maeneo 534 yalipimwa katika Mikoa yote, kati ya hayo, maeneo 280 yalipimwa na Wizara wakati maeneo 254 yalipimwa na Wakala wa Uchumbaji wa Visima kwa ajili ya kuchimba visima vya watu binafsi, Mashirika, Taasisi na Asasi mbalimbali. Aidha, visima 428 vilichimbwa katika Mikoa yote kupitia Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na Makampuni binafsi. Wakala ilichimba visima 349 na makampuni binafsi visima 79. Wizara yangu ilisimamia uchimbaji wa visima hivi ili kuhakikisha kuwa taratibu za kitaalam zinafuatwa na takwimu za visima hivyo zinapatikana ili kurahisisha uratibu wa matumizi ya maji chini ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi ya kutafuta maeneo ya kuchimba visima, Wizara yangu kwa mwaka 2002/2003, ilifanya tathmini ya raslimali za maji chini ya ardhi katika Miji ya Lindi, Masasi, Nachingwea, Kahama, Same na Manispaa ya Arusha ili kutatua matatizo ya maji yaliyojitokeza katika miji hiyo. Mapendekezo ya kitaalam ya kuongeza vyanzo vya maji kwa Miji ya Masasi, Nachingwea, Kahama na Same yametolewa. Aidha, mradi wa kufuatilia mwenendo wa wingi na ubora wa maji chini ya ardhi kwa Manispaa ya Arusha umetayarishwa na kuwasilishwa *UNDP, JICA* na *GTZ,* ambao wameonyesha nia ya kusaidia. Ufuatiliaji wa mwenendo wa maji chini ya ardhi umefanyika katika mabonde ya Kititimo - Singida, Mwawaza - Shinyanga na Mtawanya - Mtwara, kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa maji.

Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itafanya utafiti wa maji chini ya ardhi kwenye maeneo 700 nchini ili kutambua yale yanayofaa kuchimbwa visima vya maji. Pia, Wizara itaendelea na usimamizi wa uchumbaji visima vya maji pamoja na ukaguzi wa Makampuni binafsi ya uchimbaji visima.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki, Wizara yangu iliendelea na utekelezaji wa mradi wa Kutathmini Raslimali za Maji Chini ya Ardhi kwenye Bonde la Mto Ruvu. Takwimu za ubora wa maji toka kwenye vyanzo vya mito, visima, chemichemi na mabwawa, zimekusanywa kwa kutumia teknolojia ya uhakika zaidi ya *isotopes*. Aidha, utafiti wa raslimali za maji kwa kutumia teknolojia hii umeanza katika Ziwa Victoria ili kubaini mizani ya maji *(Water Balance)* ya Ziwa hilo. Mradi huu unapata msaada kutoka Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki na unashirikisha nchi sita zilizomo kwenye Bonde la Mto Nile ambazo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Ethiopia, Sudan na Misri. Katika mwaka wa 2002/2004, utafiti katika Bonde la Mto Ruvu/Wami na Ziwa Victoria utaendelea.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea na kazi za kulinda na kuhifadhi Bonde la Makutupora dhidi ya uchafuzi, ambalo ni chanzo kikuu cha maji cha Manispaa ya Dodoma. Katika mwaka 2002/2003, Serikali imewalipa fidia wakazi wote waliostahili kulipwa na sasa wameanza kuhama. Nachukua fursa hii kuwashukuru viongozi wa Mkoa wa Dodoma na Wilaya ya Dodoma Vijijini, kwa kusimamia kikamilifu na kufanikisha

utekelezaji wa kazi hii muhimu. Aidha, mtandao wa ukusanyaji wa takwimu mbalimbali za Rasilimali za Maji Chini ya Ardhi katika Bonde hilo, umeendelea kuimarishwa kwa kuchimba visima viwili vya ufuatiliaji wa mwenendo wa maji na kukarabati vingine vitatu. Katika mwaka 2003/2004, uimarishaji wa mtandao wa Raslimali za Maji Chini ya Ardhi utaendelea kwa kufunga vifaa vya kisasa vya kukusanyia takwimu *(Data Loggers)*. Aidha, maeneo yaliyoathirika kutokana na shughuli za binadamu ambako wanavijiji wamehamishwa yatapandwa miti. Pia, eneo la hifadhi ya Bonde litawekewa mipaka ya barabara na vibao ili lisiingiliwe tena.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kushirikiana na nchi ambazo tunachangia matumizi ya maji katika mabonde ya maji shiriki *(Transboundary Waters)*. Maji ya Bonde la Mto Nile ni mojawapo ya raslimali kubwa duniani, yenye kutegemewa na zaidi ya wakazi milioni 300 kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi. Nchi za Bonde la Mto Nile ni Burundi, Ethiopia, Eritrea, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kenya, Misri, Rwanda, Sudan na Uganda.

Ili kuhakikisha kwamba, raslimali hii ya maji shiriki inatumika kwa manufaa ya kila nchi katika Bonde, nchi zote kwa pamoja zinachukua hatua ya kihistoria ya kuanzisha chombo cha kudumu cha usimamizi wa raslimali hii. Chombo kitakachoundwa kitakuwa badala ya taasisi ya mpito iliyopo sasa ya *Nile Basin Initiative* iliyoanzishwa kwa lengo la kutayarisha na kuratibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya matumizi ya raslimali za maji katika Bonde hilo. Mpaka sasa kila nchi imeteua wataalamu wawili kuunda Kamati *(Negotiating Committee)* ya nchi zilizo katika Bonde ili kujadili rasimu ya chombo mbadala. Madhumuni ya hatua zinazochukuliwa ni kuendeleza nchi hizi kiuchumi na kijamii kwa kugawana na kutumia raslimali za maji kwa haki na usawa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeshiriki katika maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya Mto Mara na Mto Kagera chini ya *Nile Equitorial Lakes Subsidiary Action Program (NELSAP)*. Miradi hii inazihusisha nchi za Burundi, Rwanda, Kenya, Uganda na Tanzania. Kwa upande wa Bonde-dogo la Mto Mara, Serikali ya Tanzania, kwa kushirikiana na Serikali ya Kenya, imeunda Kamati *(Regional Project Steering Committee)*, kwa ajili ya kuratibu Mradi wa Bonde-dogo la Mto Mara. Mradi huo unalengo la kuendeleza rasilimali za maji ya Bonde hilo. Mtaalam Mashauri *WSP International* ya Sweden tayari ameteuliwa kufanya upembuzi yakinifu wa mradi huo. Kwa upande wa Bonde-dogo la Mto Kagera, Kamati ya Uendeshaji inayohusisha nchi za Uganda, Burundi, Rwanda na Tanzania tayari imeundwa.

Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itaendelea kushiriki katika kuandaa utekelezaji wa miradi iliyobuniwa chini ya programu ya *Nile Basin Shared Vision.* Aidha, Kamati iliyoundwa *(Negotiating Committee),* itaendelea na majadiliano kuhusu rasimu ya chombo cha kudumu cha kusimamia matumizi ya raslimali za maji katika bonde hilo na kutekeleza miradi iliyobuniwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeanza majadiliano ya kupata miradi ya ushirikiano kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wizara inasimamia na kuratibu utayarishaji wa Dira na Mkakati wa Kuendeleza Bonde la Ziwa Victoria kwa ajili ya uwekezaji wenye lengo la kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika Bonde hilo. Zoezi la utayarishaji wa Dira na Mkakati limefanyika kwa wakati mmoja kwa nchi zote tatu za Afrika ya Mashariki, kwa kuhusisha wadau wote. Katika mwaka 2003/2004, kazi ya kuainisha taarifa za kila nchi na kutengeneza dira na mkakati mmoja wa kuendeleza Bonde la Ziwa Victoria itafanyika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Wizara yangu iliendelea kudumisha uhusiano mzuri uliopo kati yetu na Jmuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* katika kuendeleza na kusimamia matumizi bora ya raslimali za maji kwenye mabonde ambayo tunachangia matumizi ya maji. Wizara yangu ilishiriki katika maandalizi ya utekelezaji wa Mpango/mkakati wa Jumuiya hiyo *(SADC Regional Strategic Action Plan),* unaojumuisha miradi mbalimbali ya matumizi endelevu ya raslimali za maji katika nchi za Jumuiya. Miradi hii inalenga kuboresha upatikanaji wa takwimu na taarifa zitakazowezesha kufanya tathmini ya raslimali za maji, kuimarisha uwezo wa taasisi za maji katika nchi za jumuiya.

Hatua za awali za utekelezaji wa miradi iliyopo chini ya mpango huu zimeanza kufanyika baada ya wafadhili kuonyesha nia ya kusaidia miradi hiyo. Serikali ya Sweden inasaidia juhudi za Tanzania, Msumbiji na Malawi, kuanzisha ushirikiano wa uendelezaji na usimamizi wa raslimali za maji kwenye Bonde la Ziwa Nyasa na Mto Shire *(Integrated Water Resources Management for Lake Nyasa* na *Shire Sub-basin)*. Rasimu za awali za Mkataba wa Makubaliano, muundo wa uendeshaji wa Asasi itakayoundwa, gharama za ukarabati na uboreshaji wa

mtandao wa ukusanyaji wa takwimu za raslimali za maji katika Bonde zimeandaliwa ili zipitiwe na kuridhiwa na nchi shiriki.

Mheshimiwa Spika, Mto Songwe ambao ni sehemu ya mpaka kati yaTanzania na Malawi, unahamahama na kusababisha kumegwa kwa ardhi ya nchi hizi na hivyo kuleta utata wa mpaka. Kama nilivyolielezea Bunge lako Tukufu mwaka 2002 kuwa, Serikali yetu na Serikali ya Malawi zinaendelea kufanya upembuzi yakinifu kwa lengo la kupata njia sahihi ya kutatua tatizo hili. Kazi hii inatarajiwa kukamilika Novemba, 2003.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kusimamia matumizi bora ya raslimali za maji kwa kutoa hati za kutumia maji. Lengo ni kuimarisha matumizi endelevu ya raslimali hii ili kujenga mazingira ya kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Jumla ya viwanda 22 katika Bonde la Pangani, Ziwa Victoria na Mto Wami/Ruvu vilikaguliwa ili kuhakiki kama vinafuata maelekezo ya kusafisha majitaka kufikia kiwango kilichowekwa. Aidha, viwanda 15 katika Bonde la Ziwa Victoria, Bonde la Wami/Ruvu na Bonde la Mto Pangani vimetuma maombi ya kutupa majitaka *(Discharge Permit),* baada ya kutimiza masharti na hati hizo zitatolewa mwaka huu kulingana na Sheria ya Maji.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sera ya Maji, Wizara yangu inazipitia upya sheria zinazohusu matumizi ya maji ili ziendane na hali halisi ikiwa ni pamoja na kuangalia upya viwango vipya vya ada za matumizi ya maji. Vile vile, Wizara inaendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa wananchi na viongozi katika ngazi mbalimbali, juu ya sheria ya usimamizi wa raslimali za maji ikiwa ni pamoja na umuhimu wa hati ya kutumia maji, utaratibu wa kuomba hati na ulipaji wa ada za matumizi ya maji. Katika kipindi cha mwaka 2002/2003, kutokana na uhamasishaji uliofanyika, Wizara yangu ilipokea jumla ya maombi 349 kutoka sehemu mbalimbali nchini. Kati ya maombi hayo 111 yamekwishapitishwa na hati za kutumia maji kwa wahusika zitatolewa katika vikao vya Bodi mwaka huu. Aidha, visima 91 vya Dar es Salaam vilikaguliwa na kuagizwa kuomba hati za kutumia maji na kati ya hivyo 8 vimekwishapewa hati hizo.

Mheshimiwa Spika, ni jukumu la Wizara yangu kufanya uchunguzi wa usafi na ubora wa maji katika vyanzo mbalimbali nchini. Kazi hizi zinalenga kulinda afya za wananchi na viumbe viishivyo majini. Katika mwaka 2002/2003, Maabara za Sumbawanga, Shinyanga, Iringa, Singida na Mbeya, zilipatiwa vifaa na madawa. Aidha, Wizara yangu ilihakiki ubora wa madawa yanayoletwa hapa nchini kwa ajili ya kusafisha na kutibu maji.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba, maji yasambazwayo na Mamlaka za Maji Mijini ni safi na salama, Maabara za maji katika Mikoa ya Arusha, Tanga, Mwanza, Mtwara, Mara, Shinyanga, Rukwa, Ruvuma, Morogoro, Kagera, Kigoma, Singida, Iringa, Mbeya na Dar es Salaam, zimeendelea kuratibu ubora wa maji yanayosambazwa mijini. Pale ilipojitokeza kwamba hali si salama, hatua zilichukuliwa kurekebisha hali hiyo kwa kutoa ushauri. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itaendelea na uchunguzi wa usafi na ubora wa maji katika vyanzo mbalimbali nchini na kuwahusisha wananchi katika juhudi za kudhibiti uchafuzi wa vyanzo hivyo. Vile vile, Wizara itaendelea kuziimarisha Maabara za maji zilizopo nchini kwa kuzipatia vifaa, madawa, usafiri na kutoa mafunzo kwa watumishi ili kuzijengea uwezo.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi uliofanywa na wataalam wa ubora wa maji na mfumo ikolojia, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, umethibitisha kwamba, uchafuzi wa Ziwa Victoria hutokana na shughuli mbalimbali za binadamu kwenye bonde ikiwa ni pamoja na viwandani na mijini, siyo tishio kwa Ziwa. Hata hivyo, uchafuzi kutokana na shughuli hizo unaleta kasi kubwa ya uoto na uchafu kwenye maeneo karibu na ufukwe. Ili kupunguza tatizo hili, Wizara yangu imekamilisha ukarabati wa mfumo wa kusafisha majitaka katika Jiji la Mwanza. Upembuzi yakinifu wa mfumo rahisi na shirikishi jamii wa majitaka katika Kata ya Igogo Jijini Mwanza na mabwawa ya takatope katika Mji wa Bukoba umefanyika. Wizara yangu pia, imehamasisha uzalishaji bora viwandani, matumizi ya teknolojia rahisi ya maeneo chepechepe katika usafishaji wa majitaka kutoka viwandani na mijini.

Katika mwaka 2003/2004, Wizara itaendelea na ushirikiano kati yetu na nchi jirani za Kenya na Uganda katika utekelezaji wa Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria, kwa kuimarisha na kuboresha mtandao wa kuchunguza ubora wa maji na mfumo ikolojia. Pia, Wizara itaendelea kuelimisha, kuhamasisha na kushirikisha jamii katika kuhifadhi mazingira ya Ziwa Victoria.

Baada ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mijini mwaka 1998, kumekuwa na ongezeko la wingi na ubora wa maji pamoja na muda wa upatikanaji wa maji katika miji yote mikuu ya Mikoa. Ongezeko hili limewezesha upatikanaji wa maji kwa wakazi wa mijini kufikia asilimia 73 mwaka 2002, ikilinganishwa na asilimia

68 mwaka 1995. Uzalishaji wa majisafi kwa Mamlaka zote 18 uliongezeka kutoka lita bilioni 91 mwaka 1997/98 na kufikia lita bilioni 102 mwaka 2002/2003.

Makusanyo ya maduhuli pia yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 4.4 mwaka 1997/98 na kufikia shilingi bilioni 13.2 mwaka 2002/2003. Katika kuhakikisha kwamba wateja wa maji mijini wanalipa gharama halisi kulingana na matumizi yao, jitihada zilielekezwa katika ufungaji wa dira za maji. Hadi sasa, ufungaji wa dira kwa mamlaka zote za maji mijini umefikia asilimia 50 ya wateja wote.

Mwaka 2003/2004, Wizara imepanga kununua dira za maji zenye thamani ya shilingi milioni 136 kwa ajili ya Mamlaka za Mbeya, Mtwara, Tabora, Musoma, Sumbawanga, Songea, Singida, Iringa, Shinyanga na Bukoba. Mamlaka zote 18 nazo zimetenga jumla ya shilingi milioni 556 kutokana na maduhuli yao kwa ajili ya ununuzi wa dira.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Wizara yangu kwa kushirikiana na wahisani mbalimbali, iliendelea kuimarisha huduma za majisafi na uondoaji majitaka mijini kwa kufanya ukarabati na upanuzi wa mifumo ya majisafi na majitaka. Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, ilikamilisha mradi wa upanuzi wa mfumo wa majisafi katika Manispaa ya Dodoma kwa gharama ya shilingi bilioni 4. Mradi huu umeongeza uwezo wa uzalishaji maji kutoka lita milioni 24 hadi milioni 40 kwa siku, sawa na ongezeko la asilimia 67 ambapo kwa Manispaa hii inapata maji ya kutosha. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lake la Benki ya Maendeleo *(KfW),* ilitekeleza awamu ya pili ya mradi wa kuimarisha miundombinu ya majisafi katika Miji ya Arusha, Moshi na Tanga kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 46.2 ambapo uwezo wa uzalishaji maji umeongezeka kutoka lita milioni 81 hadi lita milioni 101.4 kwa siku, sawa na ongezeko la asilimia 25.

Vilevile, katika mwaka 2002/2003, jitihada za kuimarisha huduma ya majisafi katika Jiji la Mwanza na Manispaa za Iringa na Mbeya zimeendelezwa. Wiara yangu kwa kushirikiana na Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU)* na *KfW*, ilifanya mapitio ya usanifu wa mradi wa majisafi kwa Jiji la Mwanza, kwa lengo la kukidhi mahitaji ya maji ya muda mrefu. Aidha, usanifu wa miradi ya majisafi katika Manispaa za Iringa na Mbeya unaendelea. Hatua hizi za usanifu zitakapokamilika, utekelezaji wa miradi hii utagharamiwa na *EU* na *KfW* kwa pamoja kwa gharama ya *Euro* milioni 90.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani kupitia *KfW*, imekamilisha uchunguzi na usanifu wa miradi ya majisafi na majitaka kwa Mji wa Songea. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara itaanza kazi ya ukarabati na upanuzi wa mfumo wa majisafi Mjini Songea kwa gharama ya *Euro* milioni 6.38.

Kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la Maendeleo *(AfD),* Wizara itafanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya mifumo ya majisafi na majitaka katika Miji ya Musoma, Misungwi na Bukoba kwa gharama ya *Euro* 166,000. Serikali ya Ufaransa imeonyesha nia ya kugharamia ujenzi wa miradi ya maji katika miji hii usanifu utakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi, 2003 Wizara yangu ilikamilisha upembuzi yakinifu wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwa ajili ya miji ya Kahama na Shinyanga, pamoja na vijiji litakapopita bomba kuu kwa gharama ya shilingi milioni 546. Taarifa ya awali ya mradi ilijadiliwa na wadau wa mradi huo ambao ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa eneo husika mwezi Aprili, 2003. Katika mwaka 2003/2004, kazi ya ujenzi wa awamu ya kwanza ya mradi itaanza ambapo shilingi bilioni 3.4 zimetengwa. Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia fedha zetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2002/2003, Wizara yangu iliendelea kufanya uchunguzi na usanifu wa mifumo ya majisafi na majitaka kwa Miji ya Dodoma, Tabora na Morogoro kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia chini ya Mradi wa *Urban Sector Rehabilitation Project (USRP).* Lengo la uchunguzi huu ambao utakamilika Oktoba, 2003, ni kutafuta vyanzo vipya vya maji katika miji husika ili kukidhi mahitaji ya baadaye ya ukuaji wa miji hiyo, pamoja na kuainisha mahitaji ya mifumo ya usambazaji majisafi na uondoaji majitaka.

Vilevile katika mwaka 2002/2003, Wizara yangu imekamilisha taratibu na kuingia mkataba na Benki ya Maendeleo ya Kiarabu kwa Afrika *(BADEA),* pamoja na *OPEC,* ili kupata Dola za Kimarekani milioni 12.7 za kugharamia ukarabati na upanuzi wa mfumo wa majisafi kwa ajili ya Mji wa Singida. Kwa mwaka 2003/2004, kazi

za kukamilisha usanifu na kuteua mkandarasi wa ukarabati na ujenzi wa mradi wa majisafi, pamoja na kumpata mshauri wa upembuzi yakinifu wa mfumo wa majitaka katika mji huo zitaanza.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Wizara yangu ilifanya ukarabati na upanuzi wa mifumo ya majisafi katika Miji ya Songea, Kigoma, Musoma, Bukoba, Sumbawanga, Shinyanga na Mtwara. Mitambo minne ya kusukumia maji imenunuliwa kwa ajili ya Mji wa Mtwara, mitatu kwa ajili ya mji wa Kigoma na minne kwa ajili ya Mji wa Lindi. Mabomba na viungio vyake yalinunuliwa kwa ajili ya Miji ya Sumbawanga, Shinyanga na Mtwara. Aidha, mradi wa dharura wa Maji Mjini Lindi ulianza kutekelezwa Oktoba, 2002 baada ya chanzo cha awali kukauka. Jitihada zilizofanyika kunusuru hali hiyo ni kutafuta vyanzo vipya vya maji kwa kuchimba visima virefu 10 na hivyo kuongeza kiwango cha uzalishaji maji kutoka lita 850,000 na kufikia lita 4,200,00 kwa siku. Katika mwaka 2002/2004, Wizara itaendelea kuzisaidia Mamlaka za Majisafi na Majitaka katika miji hiyo ili kuimarisha mitandao ya majisafi kwa kuboresha uzalishaji na usambazaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, jitihada za kuboresha huduma ya majisafi kwa Jiji la Dar es Salaam ziliendelea. Katika mwaka 2002/2003, Wizara yangu ilifanya ukarabati wa mabomba makuu ya maji yanayopeleka maji Jijini kutoka vyanzo vya maji vya Ruvu Juu na Ruvu Chini. Upanuzi wa mtandao wa maji katika maeneo ya Kitunda (Ukonga), Mwananyamala Kisiwani na Kunduchi ulikamilika. Pia visima virefu 9 vyenye uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 2,270 kwa siku vilikamilishwa na baadhi viliunganishwa kwenye mtandao wa majisafi katika maeneo ya Mbagala Kibonde Maji, Machinjioni, Nzasa, Kiburugwa, Yombo na Kipawa Miembeni.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma ya uondoaji majitaka mijini, Wizara yangu iliendelea kushirikiana na wahisani katika kutekeleza miradi mbalimbali. Hadi sasa, ni miji tisa tu ambayo inatoa huduma hiyo ikiwa ni pamoja na Jiji la Dar es Salaam na Mwanza, Manispaa za Arusha, Moshi, Tanga, Morogoro, Dodoma, Iringa naTabora. Kwa sasa ni asilimia 17 ya wakazi wa mijini ndio wanaohudumiwa na mitandao ya majitaka. Kiwango hiki kimepanda kutoka asilimia 10 mwaka 2001/2002, kutokana na jitihada za Serikali za kukarabati na kupanua miundombinu ya majitaka katika miji kwa lengo la kuwawezesha wakazi wengi zaidi wa mijini kuunganishwa kwenye mtandao. Mwaka 2003/2004 Wizara itaendelea na juhudi za ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya majitaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Wizara kwa kushirikiana na Jumuiya ya Ulaya *(EU)*, ilikamilisha mradi mkubwa wa ukarabati wa mfumo wa majitaka Jijini Mwanza kwa gharama ya *Euro* milioni 5.5. Kukamilika kwa mradi huu kumepunguza tatizo la uchafuzi wa maji ya Ziwa Victoria, ambapo lita milioni 2.2. za majitaka kwa siku zilizokuwa zinaingia ziwani, sasa zinasafishwa kabla ya kurudishwa ziwani. Katika mwaka 2003/2004, ukarabati wa mabomba ya ukusanyaji majitaka utafanyika pamoja na uunganishwaji wa wateja katika mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 nililieleza Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imekusudia kukodisha Miundombinu ya utoaji wa huduma ya maji kwa Jiji la Dar es Salaam. Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam *(DAWASA)*, ndiyo yenye jukumu la kutoa huduma ya majisafi na uondoaji majitaka katika Jiji, Miji ya Kibaha na Bagamoyo na Vijiji yanakopita mabomba makuu ya maji. Katika mwaka 2002/2003, Wizara yangu ilikamilisha zoezi la kukodisha miundombinu ya majisafi na uondoaji majitaka ya *DAWASA* baada ya taratibu zote za zabuni kukamilika. Mwendeshaji binafsi aliyeshinda zabuni ni Kampuni ya *Biwater International* ya Uingereza ikishirikiana na Kampuni ya *Gauff Ingenieure* ya Ujerumani. Mkataba wa kukodisha miundombinu ya *DAWASA* kwa muda wa miaka kumi, umesainiwa Februari, 2003 na mkodishaji ataanza kazi rasmi mwezi huu. Chini ya mkataba huo, miundombinu ya *DAWASA* itaendelea kumilikiwa na Serikali. Tayari chombo binafsi kitakachotoa huduma ya majisafi na majitaka Jijini kimeshaundwa na kinaitwa *City Water Service Company Ltd.*

Mheshimiwa Spika, sambamba na ukodishaji wa *DAWASA*, mradi mkubwa wa kuboresha huduma ya majisafi na uondoaji majitaka katika eneo linalohudumiwa na *DAWASA* utatekelezwa. Mradi huu utahusu ukarabati wa miundombinu kwa kuboresha uzalishaji na usambazaji wa maji, kufunga dira kwa wateja na kufanya tafiti mbalimbali ili kuwezeshwa upanuzi wa baadaye. Mradi huu utakaotekelezwa kwa muda wa miaka mitano, utagharimu Dola za Kimarekani milioni 164.6 zitakazotolewa kwa pamoja na Benki ya Raslimali ya Nchi za Jumuiya ya Ulaya, Kampuni ya *City Water Service Ltd.* na Serikali.

Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu kupitia mwendeshaji huyo binafsi, itatekeleza kazi za dharura ikiwa ni pamoja na ufungaji wa dira 60,000 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.3. Lengo ni kudhibiti matumizi ya maji na kuboresha ukusanyaji wa mapato. Aidha, matengenezo ya mitambo ya maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini yatafanyika kwa gharama ya shilingi bilioni 1.6 kwa lengo la kuimarisha uzalishaji wa maji katika mitambo hiyo.

Hatua hii itafuatiwa na kazi ya ukarabati mkubwa wa vituo vya maji vya Mtoni, Ruvu Juu na Ruvu Chini na mabomba makuu yanayosafirisha maji kutoka mitambo hiyo. Katika hatua hii, shilingi bilioni 11.6 zitatumika. Lengo ni kuongeza ubora na uwingi wa maji na kupunguza upotevu wa maji katika mabomba hayo. Aidha, ukarabati wa mfumo wa majitaka utafanyika kwa gharama ya shilingi bilioni 2.7, lengo likiwa ni kuboresha mfumo wa ukusanyaji majitaka jijini.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa huduma ya maji inawafikia wakazi wenye kipato kidogo na katika maeneo ambako awamu ya kwanza ya mradi mkubwa haitaweza kuyafikia, Serikali imeandaa utaratibu maalum wa kutoa huduma hiyo. Maeneo yatakayohusika ni yale yaliyo kandokando ya mabomba makuu na maeneo yaliyo pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo. Kwa kushirikisha Asasi zisizo za Kiserikali, Wizara yangu itaanza utekelezaji wa programu ya usambazaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira *(Community Water Supply and Sanitation Programme)* kwenye maeneo hayo kwa gharama ya shilingi bilioni 1.2.

Katika mwaka 2003/2004, Wizara itaendelea kuratibu shughuli za mwekezaji aliyekodishiwa miundombinu ya *DAWASA* kwa nia ya kuhakikisha kuwa huduma ya majisafi na uondoaji majitaka imeboreshwa katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, hali ya utoaji wa huduma ya maji Vijijini imeendelea kuimarika japokuwa juhudi zaidi zinahitajika ili kuongeza kiwango cha upatikanaji maji na kuimarisha huduma hiyo ili iwe endelevu pale inapotolewa. Takwimu zinaonyesha kuwa idadi ya wananchi wanaoishi Vijijini wanaopata huduma ya majisafi na salama karibu na makazi yao imefikia asilimia 53. Mafanikio yametokana na juhudi za makusudi za Serikali katika maeneo yafuatayo:-

(a) Sera ya Maji imetoa nafasi ya kushirikisha wadau katika kuendeleza na kusimamia utoaji wa huduma za maji Vijijini tofauti na siku za nyuma ambapo Serikali pekee ndiyo ilikuwa na jukumu hilo. Kushiriki kwa wadau wengine kumeongeza raslimali na utaalam katika Sekta ndogo ya maji Vijijini.

(b) Serikali imeelekeza raslimali zaidi katika sekta ndogo ya maji Vijijini hususan kuanzia mwaka 2000/2001, kutokana na mchango mkubwa wa huduma ya maji katika kuondoa umaskini. Wahisani nao sasa wanavutika kuwekeza kwenye huduma za maji Vijijini kutokana na sera nzuri iliyopo.

(c) Ushirikiano na Halmashauri za Wilaya katika kutekeleza na kusimamia maendeleo ya huduma ya maji Vijijini umeimarika. Halmshauri za Wilaya zinapatiwa uwezo zaidi na zimekuwa na uhusiano wa karibu na wananchi katika kupanga na kusimamia maendeleo Vijijini.

(d) Kuimairisha na kuanzisha Kisheria vyombo vya watumiaji maji Vijijini ili viweze kumiliki, kuendeleza na kusimamia utoaji wa huduma ya maji. Vyombo vya watumiaji vinahakikisha kuwa wananchi wanagharamia huduma na hivyo kuwa endelevu. Hatua hii inaipunguzia Serikali gharama za uendeshaji wa huduma za maji Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika jitihada za kuboresha huduma ya maji Vijijini ilianza zoezi la kubaini miradi ambayo haitoi huduma ya maji kikamilifu, ikiwa ni pamoja na ile ambayo ujenzi wake ulianza lakini haikukamilishwa kutokana na matatizo mbalimbali. Aidha, ipo miradi ambayo ilikamilika lakini haitoi huduma kama ilivyokusudiwa kutokana na uharibifu, uchakavu kwa kuwa imejengwa muda mrefu au kukosa matunzo. Lengo la zoezi hili lilikuwa kubainisha miradi hiyo, kutambua matatizo yanayoikabili, gharama na vifaa vinavyohitajika kuifanyia ukarabati na kuikamilisha. Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, imekamilisha tathmini ya miradi ya aina hiyo katika Mikoa yote. Tathmini hii imebaini jumla ya miradi 794 ambayo inahitaji kufanyiwa ukarabati na kukamilishwa. Makisio ya awali ya gharama za kukarabati na kukamilisha miradi hiyo ni shilingi bilioni 43. Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Wahisani na Asasi zisizo za Kiserikali, itaendelea kuifanyia ukarabati na kuimalizia miradi hiyo kwa awamu ili hatua kwa hatua wananchi wengi zaidi Vijijini wanufaike na huduma hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia inasimamia uendeshaji wa miradi mitano mikubwa ya maji ya Kitaifa ya *Handeni Trunk Main (HTM),* Makonde, Mugango/Kyabakari, Maswa na Wanging'ombe. Gharama za uendeshaji wa miradi hii zinachukua sehemu kubwa ya Bajeti ya Wizara na hivyo kupunguza uwezo wa kupanua huduma ya maji katika maeneo mengine hapa nchini. Serikali inachukua hatua za kuimarisha miradi hii ili ikabidhiwe kwa vyombo vya watumiaji maji vitakavyoratibiwa na Halmashauri za Wilaya. Aidha, Sera ya Maji inataka wananchi wagharamie kikamilifu uendeshaji na usimamizi miradi yao ya maji. Katika mwaka 2002/2003, Wizara imekamilisha maandalizi ya makabidhiano ya mradi wa Wanging'ombe kwa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Maandalizi ya kukabidhi miradi mingine yatafanyika katika kipindi cha mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Wahisani na Taasisi mbalimbali za ndani na nje, imeendelea kuimarisha na kuboresha huduma ya maji Vijijini kwa kufanya ukarabati na ujenzi wa miradi mipya ya maji. Katika mwaka 2002/2003, Wizara yangu iliendelea na jitihada za kujenga na kupanua miradi ya maji ya Nachingwea Mjini, Maswa, Masasi Mjini, Lushoto na Makuyuni. Miradi mingine ni Chalinze unaogharamiwa kwa pamoja kati ya Serikali yetu ya Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na Mradi wa Hanang', Singida Vijijini, Manyoni na Igunga, unaotekelezwa kwa msaada wa Serikali ya Japan. Awamu ya Kwanza ya mradi huu ilikamilika katika Wilaya mbili za Hanang' na Igunga na kuzinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein, mwezi Mei, 2003. Utekelezaji wa miradi mingine uko katika hatua mbalimbali.

Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Uholanzi, imeendelea na utekelezaji wa programu ya miaka minne ya maji Vijijini katika Mkoa wa Shinyanga inayohusisha Wilaya zote za Mkoa huo. Programu hii ambayo imeanza kutekelezwa kuanzia Julai, 2002 inahusisha uchimbaji wa visima, ujenzi wa miradi ya maji ya bomba na uchimbaji wa mabwawa. Mradi huo unashirikisha kikamilifu wananchi katika hatua zote kuanzia kubuni, kutayarisha, kujenga na kuendesha miradi ya maji ili hatimaye waimiliki wenyewe. Serikali ya Uholanzi imetenga jumla ya *Euro* 9.2 kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii ikiwa ni pamoja na gharama za msaada wa kiufundi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara itaendelea na ujenzi wa miradi ya maji Vijijini na Miji midogo, ikiwa ni pamoja na Kazilankanda na Nyakagomba Mkoani Mwanza, Chalinze na Mzenga Mkoani Pwani, Rondo, Kitomanga na Nachingwea Mjini Mkoani Lindi, Maswa Mkoani Shinyanga, Nanganga Mkoani Mtwara, Losinyai na Magugu Mkoani Manyara. Pia Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani itaendelea na utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi wa maji katika Wilaya ya Hai. Awamu ya pili ya mradi wa maji katika Wilaya ya Hanang', Singida Vijijini, Manyoni na Igunga inayotekelezwa kwa msaada wa Serikali ya Japan itakamilishwa. Aidha, miradi ya usambazaji maji katika Miji ya Mwanhuzi, Bariadi na Bukombe itaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imegharamia upembuzi yakinifu wa miradi ya maji katika Miji midogo ya Kiomboi na Shelui, Katesh, Namanyere, Tukuyu, Kilolo, Kipatimu - Kilwa, Same, Kayanga, Simanjiro, Sikonge na Kiponzelo. Tathmini ya hali ya upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Biharamulo pia imefanyika. Vile vile mwaka 2002/2003 Wizara yangu ilikamilisha usanifu na utayarishaji wa zabuni za mradi wa maji na usafi wa mazingira wa Wilaya ya Monduli utakaonufaisha Vijiji 20 ikijumuisha Miji Midogo ya Monduli, Namanga na Mto wa Mbu. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuanza baada ya kupata fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara itafanya upembuzi yakinifu kwa Miji ya Karatu, Serengeti, Tunduru, Urambo, Biharamulo, Geita na Kibondo, kwa lengo la kutambua gharama na mahitaji ya vifaa kwa ajili ya ujenzi wa miradi mipya. Pia utafiti wa kina na usanifu utaendelea kufanyika katika baadhi ya Vijiji vya Mikoa ya Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Wizara yangu ilifanya ukarabati wa baadhi ya miradi hapa nchini kwa lengo la kuongeza kiwango cha utoaji wa huduma ya maji Vijijini. Miradi inayohusika ni pamoja na Dumila, Iramba Vijijini, Kiponzelo, Mwamapuli/Ulenya, Uchira, Mugango-Kyabakari, Lupaso na Umbwe Onana. Miradi mingine ni Same Mjini, Njombe Mjini, Tandahimba, Mpanda Mjini, Kazilankanda, Nyakagomba, Magu Mjini, Ruangwa, Manyoni Mjini, Malya na Mwanga Mjini. Mingine ni Kibondo, Kisarawe Mjini, Korogwe Mjini, Kilombero, Ibadakuli (Shinyanga), Pangani, Wanging'ombe na Lembeni. Ukarabati wa miradi hiyo uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2003/2004, Wizara itakarabati miradi ya Mahenge, Migori, Kiponzelo, Lumeya, Misasi, Malya na Kilulu. Miradi mingine ni Singida Vijijini, Mwamapuli/Bulenya, Mugango/Kyabakari, Bunda, Magugu, Korogwe, Nassa, Sikonge, Urambo, Iwindi, Mto wa Mbu-Esilalei, Chato, Kabila, Tarime, Hedaru, Lotima na Gabimori. Wizara pia imepanga kufanya ukarabati wa pampu za maji katika miradi ya Kisarawe, Kibondo, Kilombero, Rungwe, Tunduru, Mafinga na Biharamulo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na jitihada za kujenga miradi mipya ya maji na kukarabati miradi ya maji kwa lengo la kuongeza kasi ya utoaji huduma za maji Vijijini, Wizara yangu iliendelea na uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa ikiwa ni jitihada za kupata vyanzo vipya vya maji katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Katika mwaka 2002/2003, Wizara iligharamia uchimbaji wa visima katika Mji wa Tunduma, Ngara, Mugumu, Nzega, Songwe, Simanjiro, Chato, Namanyere na Igombe. Maandalizi na uchimbaji wa visima katika maeneo hayo upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Ujenzi wa Bwawa la Mwanyahina ulikamilika kwa kuimarisha utoro wa maji ili kuzuia uwezekano wa maji kujaa kupita kiasi. Katika mwaka 2003/2004, uchimbaji wa visima virefu utafanywa katika maeneo ya Dang'aida, Serengeti na Nachingwea na ujenzi wa Bwawa la Magumu utaanza. Vile vile, Wizara itaendelea kusaidia kuimarisha vyombo vilivyoundwa na wananchi wenyewe kwa ajili ya kusimamia na kuendesha miradi yao ya maji Vijijini ikiwa ni pamoja na chombo cha Mwisanga/Ntomoko.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka 2002/2003, nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu imeanza kutekeleza mradi mkubwa wa maji Vijijini kwa kutumia mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia. Mradi huu umeendelea kutekelezwa kwa kujenga mifumo ya maji na usafi wa mazingira Vijijini katika Wilaya ya Rufiji, Kilosa na Mpwapwa. Wilaya hizo zinashirikisha wananchi, sekta binafsi na asasi zisizo za Kiserikali katika kubuni, kujenga na kusimamia miradi ya maji Vijijini. Maandalizi ya ujenzi wa miradi yanaendelea kwa Wilaya nyingine tisa za Morogoro Vijijini, Handeni, Kiteto, Kondoa, Kongwa, Manyoni, Singida Vijijini, Iramba na Igunga. Utekelezaji unatarajiwa kuanza mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, chini ya mradi huu, Halmashauri za Wilaya zinapewa mafunzo na nyenzo za kufanyia kazi ili ziweze kusimamia utekelezaji. Kwa kuwa mradi huu unasisitiza mipango shirikishi, miradi itakayogharamiwa ni ile ambayo wananchi wenyewe watashiriki kupanga na kusimamia. Wilaya ambazo zitahamasisha zaidi wananchi ndizo zitakazopata fedha zaidi na kugharamia miradi. Wizara pia itaendelea na usambazaji wa teknolojia ya uvunaji maji ya mvua kwa kutoa elimu kwa umma na vikundi, kujenga miradi ya mfano katika Wilaya za Manyoni na Sikonge. Kwa kuwa teknolojia hii inaweza kutekelezwa katika ngazi ya familia, Wizara itaendelea kuhamasisha Halmashauri za Wilaya na Miji kuweka sheria ndogondogo kuwataka wanaojenga nyumba kulazimika kuvuna maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia katika kipindi cha mwaka 2002/2003, kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la *AfD*, iliendelea na majadiliano kuhusu taratibu za kutekeleza mradi wa maji na usafi wa mazingira unaohusu ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji pamoja na kutoa elimu ya usafi wa mazingira katika Miji Midogo ya Kilosa, Gairo, Turiani, Mvomero, Mpwapwa, Kibaigwa, Utete, Kibiti na Ikwiriri. Mradi huu utachukua miaka minne kukamilika. Wizara iliendelea na taratibu za kupata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu wa mradi. Kwa kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara itaendelea na usanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni za miradi ya maji katika Miji hiyo midogo tisa.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuhakikisha huduma ya maji Vijijini na katika Miji ya Wilaya zinakuwa endelevu, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya iliendelea na juhudi za kuimarisha huduma za maji katika Miji Midogo ikiwa ni pamoja na Makao Makuu ya Wilaya kwa kuunda Bodi za Maji na Kuanzisha Mamlaka za Maji za Miji ya Wilaya. Hadi sasa Miji Mikuu ya Wilaya 37 imeshatangaza kwenye Gazeti la Serikai kama Mamlaka za Maji za Miji ya Wilaya na kati ya hiyo, Miji ya Wilaya 17 imeanzisha Bodi za Maji. Miji hiyo ni Magu, Ngudu, Igunga, Mafinga, Nzega, Kilosa, Njombe, Mahenge, Mbinga, Mugumu, Masasi, Mpwapwa, Maswa, Sengerema, Mpanda, Bunda na Chunya. Miji mingine 12 ya Tukuyu, Korogwe, Same, Mwanga, Ngara, Kibondo, Kyela, Makete, Tarime, Kasulu, Makambako na Manyoni, iko kwenye hatua mbalimbali za kuunda Bodi. Aidha, Miji minane ya Bariadi, Kahama, Muheza, Lushoto, Sikonge, Utete, Karagwe na Geita, inaendelea na taratibu za kuwasilisha mapendekezo yao ya kuunda Bodi za Maji. Nia ya Wizara yangu ni kuanzisha Mamlaka za Maji kwenye Miji Mikuu ya Wilaya kote nchini ikiwa ni pamoja na Miji mingine midogo huko Wilayani. Zoezi hili litaendelea katika kipindi cha mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wiaya, imetoa miongozo na kusajili vyombo huru vya watumiaji maji katika ngazi za Vijiji na Kata. Hadi sasa jumla ya vyombo vya watumiaji

maji vilivyosajiliwa Vijijini ni kama ifuatavyo: Jumuiya za watumiaji maji 22, Makampuni ya maji 22, vyombo vya Udhamini viwili na vikundi vya watumiaji maji Vijijini 1,186. Katika mwaka 2003/2004, Wizara inatarajia kusajili vyombo zaidi vya watumiaji maji katika maeneo mbalimbali yatakayokuwa tayari.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuchimba visima na kujenga mabwawa, Wizara iliendelea kuimarisha Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa *(DDCA).* Katika mwaka 2002/2003, mitambo mitatu ya ujenzi wa mabwawa 15 ya uchimbaji wa visima na mitambo saba ya shindilia hewa *(compressor)* ilikarabatiwa. Kutokana na uwezo kuongezeka, visima virefu 428 vilichimbwa, 110 vimefanyiwa ukarabati, mabwawa 12 yalipimwa na usanifu ulifanyika kwenye maeneo mbalimbali. Pia kwa kutumia mitambo na mafundi wake, Wakala imekamilisha ujenzi wa mabwawa madogo matatu ya Ndomoni - Nachingwea, Nditi - Masasi na Mayembe Juu - Mtwara Vijijini. Vile vile malambo matatu kwa ajili ya kunyweshea mifugo yamejengwa na kukamilika Buyuni, Mbala - Chamakweza na Gumba Wilayani Kibaha. Jitihada za kuimarisha Wakala zitaendelezwa katika mwaka 2003/2004, kwa kuikarabati mitambo na kununua mtambo mmoja mpya. Aidha, wakala unatarajia kuchimba visima 400 kote nchini kwa fedha za Serikali, Halmashauri za Wilaya, Makampuni Binafsi, Mashirika ya Dini na wateja wengine.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Chuo cha Maji cha Rwegarulila, kiliendelea kutoa mafunzo katika fani za ufundi mchundo na ufundi sadifu, ambayo yanahitajika katika utekelezaji wa programu za maji nchini. Jumla ya wanafunzi 31 walihitimu katika fani mbalimbali za ufundi mchundo na wanafunzi 102 walihitimu katika fani za ufundi sadifu. Aidha, awamu ya kwanza ya kazi ya ukarabati wa mabweni ya wanafunzi na ufungaji umeme katika karakana ilikamilika na ununuzi wa kompyuta kwa ajili ya mafunzo ulifanyika. Pia Chuo kilianza kuufanyia mapitio mtaala wa sasa wa mafundi mchundo ili uende sambamba na matakwa ya Sera ya Maji ya mwaka 2002, ambayo inatoa nafasi kwa wadau wa sekta kushiriki kikamilifu katika kutoa huduma ya maji.

Katika mwaka 2003/2004, Chuo kitafanya upembuzi yakinifu wa kuanzisha mafunzo ya Stashahada ya Juu ya Taaluma ya Raslimali za Maji *(Advanced Diploma in Water Resources)*. Chuo kitaanzisha utaratibu wa kupeleka mafunzo ya kujenga uwezo wa watendaji wa sekta ya maji katika Halmashauri za Wilaya kwa kushirikiana na Waratibu wa Mafunzo wa sekta ya maji, ambao tayari wameteuliwa na Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya husika. Mpango huu utaimarisha uwezo wa Wilaya kuhudumia miradi ya maji na hivyo kuifanya miradi hiyo kuwa endelevu. Aidha, utekelezaji wa awamu ya pili ya ukarabati wa majengo ya Chuo utaanza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea hali ya utekelezaji na mpango katika sekta ya maji, kwa ruhusa yako naomba sasa nielezee hali ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2002/2003 na mapendekezo ya mpango wa mwaka 2003/2004 kwa sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inayo raslimali kubwa ya mifugo ambayo kwa sasa inatosheleza mahitaji muhimu ya ulaji wa mazao ya mifugo nchini. Kulingana na takwimu za mwaka 2002, nchi yetu inakadiriwa kuwa na ng'ombe milioni 17.7, mbuzi milioni 12.5 kondoo milioni 3.5, nguruwe 880,000 na kuku milioni 47. Hali hii inaonyesha kwamba, kumekuwa na ongezeko la asilimia 1.6 kwa ng'ombe, asilimia 1.5 kwa mbuzi na asilimia mbili kwa nguruwe kwa mwaka. Hata hivyo, bado kuna haja ya kufanya sensa ya mifugo ili kuwa na takwimu sahihi za mifugo nchini.

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwa na idadi hii kubwa ya mifugo, mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa ni mdogo kutokana na kuwepo na matatizo mbalimbali hasa katika uzalishaji. Hii ikiwa ni pamoja na matumizi duni ya ardhi, uhaba wa maji na malisho, tija ndogo kutokana na aina ya mifugo na mifumo ya uzalishaji iliyopo, kuwepo magonjwa mengi ya mifugo, ukosefu wa viwanda vya kusindika mazao ya mifugo, ukosefu wa masoko, ukosefu wa mikopo, uwekezaji mdogo katika sekta na elimu duni kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa na raslimali kubwa ya mifugo, viwango vya ulaji wa mazao ya mifugo kama nyama, mayai na unywaji wa maziwa bado viko chini kulingana na viwango vya Kimataifa. Mathalan, hivi sasa kwa wastani kila Mtanzania anakunywa lita 30 za maziwa kwa mwaka wakati Uganda ni lita 40, Kenya lita 80, Sweden lita 157 na Ireland lita 190. Kiwango kinachopendekezwa na Shirika la Kilimo na Chakula Duniani *(FAO)* ni lita 200 za maziwa kwa mwaka. Katika nchi yetu, lengo hili ni pamoja na kampeni ya wiki ya uhamasishaji wa unywaji wa maziwa ambako kila mwanafunzi anatakiwa kupewa glasi moja ya maziwa kila siku. Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha imeanza kuwapa wanafunzi maziwa katika baadhi ya shule. Nachukua nafasi hii kuiomba Mikoa mingine iige mfano huo kwani mafanikio yake, licha ya kuongeza afya, hufanya mahudhurio shuleni kuwa mazuri na wanafunzi hujengewa msingi wa kupenda maziwa.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada ya kusambaza mifugo bora nchini, Wizara yangu iliendelea kuboresha mashamba ya uzalishaji mitamba nchini ambapo katika mwaka 2002/2003, jumla ya mitamba 4,494 ilizalishwa na kusambazwa kwa wafugaji wadogo. Kati ya hiyo, mitamba 614 ilizalishwa katika mashamba sita ya Wizara ya Mabuki, *Sao Hill,* Nangaramo, Kibaha, Kitulo na Ngerengere na mitamba 3,880 ilizalishwa na kusambazwa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuongeza kasi ya uendelezaji mifugo katika Mikoa ya Kusini hususan Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma, Wizara ilipeleka jumla ya ng'ombe 125 kwa kupitia Shirika la *Heifer Project Tanzania* na mitamba 45 kutoka Shamba la Mitamba Nangaramo. Mitamba hiyo ilisambazwa kufuatana na mpango wa Kopa ng'ombe lipa ng'ombe ambao unamwezesha mwananchi asiyekuwa na mtaji kuweza kumpata ng'ombe au mbuzi wa maziwa. Wizara yangu pia iliendelea na juhudi za kuendeleza sekta ndogo ya mbuzi wa maziwa nchini kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ambapo mbuzi 783 walisambazwa. Katika mwaka 2003/2004, mitamba 700 itasambazwa kutoka mashamba ya Serikali na mitamba 4,000 kutoka katika Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Aidha, Wizara itaagiza mbuzi wa maziwa 140 na madume bora ya mbegu 10 aina ya *Boer* kutoka Afrika ya Kusini kwa ajili ya kuwazalisha ili kuwasambaza kwa wafugaji wadogo. Vile vile Wizara itaendelea na mpango wake wa kuendeleza mifugo Mikoa ya Kusini kwa kupeleka mitamba 100.

Mheshimiwa Spika, mazao yatokanayo na mifugo ni pamoja na maziwa, nyama, mayai na ngozi. Uzalishaji wa maziwa nchini uliongezeka kutoka lita milioni 900 katika mwaka 2001/2002 hadi kufikia lita milioni 980 mwaka 2002/2003, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia tisa. Lengo la mwaka 2003/2004 ni kuzalisha lita bilioni 1.2 za maziwa. Uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutokana na ongezeko la ng'ombe wa kisasa wa maziwa na wa kienyeji na ongezeko la tija kwa ng'ombe wa kisasa wa maziwa na wa kienyeji na imechukua hatua mbalimbali za kuwasaidia wazalishaji nchini ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za kuendeleza sekta ndogo ya maziwa, ikiwa ni pamoja na kuondoa kidogo kwa vifungashio vyote vya maziwa, kuweka kodi ya maziwa toka nje ya asilimia 20, kodi ya *VAT* asilimia 20 na pia kodi ya kuyaingiza nchini ya asilimia 15.

Aidha, katika kupanua soko la ndani la unywaji wa maziwa na utumiaji wa mazao yatokanayo na maziwa, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, huadhimisha Wiki ya Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa mwezi Juni kila mwaka. Maadhimisho haya kwa mwaka 2002/2003 yalifanyika Kitaifa Mkoani Iringa, ambapo ujumbe ulikuwa Glasi moja ya maziwa kila siku ni haki ya mtoto. Katika mwaka 2003/2004 sherehe za wiki ya uhamasishaji unywaji maziwa zitafanyika Kanda ya Ziwa katika Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa nyama uliongezeka kwa asilimia 2.4 kutoka tani 333,000 mwaka 2001/2002 hadi tani 341,500 mwaka 2002/2003. Ongezeko hili limetokana na kuwepo malisho mengi ya kutosheleza mifugo kwa kipindi kirefu cha mwaka pamoja na kupanuka kwa soko la ndani na mbinu za usindikaji. Lengo la mwaka 2003/2004 ni kuzalisha tani 348,800 za nyama. Aidha, uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai milioni 650 mwaka 2001/2002 hadi mayai milioni 790 mwaka 2002/2003, sawa na ongezeko la asilimia 21 na hivyo kuongeza wastani wa ulaji wa mayai kwa kila Mtanzania kwa mwaka kufikia mayai 23. Ongezeko la uzalishaji limetokana na wananchi wengi kuanza kutumia chanjo mpya ya ugonjwa wa mdondo na pia wananchi wengi kuingia katika ufugaji wa kuku.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inalo pia jukumu la kuratibu na kuhamasisha usindikaji wa mazao ya mifugo. Kwa upande wa maziwa, vipo viwanda 15 ambavyo vina uwezo wa kusindika lita 500,000 kwa siku. Hata hivyo, viwanda hivi vinasindika lita 150,000 tu kwa siku au asilimia 30 ya uwezo kutokana na gharama kubwa ya uzalishaji. Baada ya Serikali kuondoa kodi za vifungashio katika mwaka huu wa fedha ni mategemeo yangu kwamba usindikaji utaongezeka. Aidha, juhudi zinazoendelea za uhamasishaji unywaji maziwa zitakuwa kichocheo cha kungeza usindikaji nchini. Kwa upande wa usindikaji nyama, viwanda vya kusindika nyama bado ni vichache na vinatoa aina chache za mazao kama *sausages*. Hivyo, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika eneo hili hususan katika ujenzi wa viwanda vya kusindika nyama na machinjio ya kisasa. Machinjio nyingi zilizopo hapa nchini ama zinamilikiwa na Halmashauri za Wilaya au na watu binafsi na zipo katika hali mbaya. Kutokana na hali hii ya kutoridhisha, Wizara yangu inaandaa utaratibu wa kuweka viwango vya ujenzi wa machinjio ili hatua kwa hatua tuwe na machinjio za kisasa zinazokidhi matakwa ya Kimataifa ili kuongeza uuzaji wa mazao yatokanayo na mifugo.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa ngozi katika mwaka 2002/2003, uliongezeka kwa asilimia 8.6 na kufikia vipande milioni 2.66 vyenye thamani ya shilingi bilioni 5.5 ukilinganisha na mwaka uliopita. Ukusanyaji huu ni sawa na asilimia 60 tu ya idadi ya ngozi zinazozalishwa hapa nchini. Hali hii inatokana na ngozi nyingi kuharibika kutokana na utayarishaji mbaya na pia nyingi kuuzwa nje kwa magendo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, vipande milioni 2.2 vyenye thamani ya shilingi bilioni 4.6 viliuzwa nje, ikiwa ni ongezeko la asilimia 17 ikilinganishwa na mwaka uliopita. Ongezeko hili limetokana na ukusanyaji mzuri na ubora wa ngozi kutokana na mafunzo yaliyotolewa kwa wakaguzi na wafanyabiashara wa ngozi. Kwa upande wa usindikaji ngozi, ni viwanda viwili tu vya Mbagala na Kibaha,, kati ya vitano ndivyo vinavyofanya kazi *(Semi-processing)*. Ili kuboresha sekta ya mifugo, Serikali imeanzisha Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo *(Livestock Development Fund).* Fedha za Mfuko huo zitatokana na ushuru wa asilimia 20 utakaotozwa ngozi ghafi zitakazouzwa nje. Fedha hizo zitatumika kuendeleza sekta ya mifugo kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuelimisha na kuhamasisha wadau wa sekta ya mifugo;

(b) Kuboresha uchinjaji;

(c) Kuendeleza ugani na utafiti; na

(d) Kudhibiti magonjwa yanayoathiri ubora wa mifugo na mazao yake.

Mheshimiwa Spika, lengo katika mwaka 2003/2004 ni kukusanya vipande milioni 3.2 vya ngozi vyenye thamani ya shilingi bilioni sita. Aidha, wakaguzi 500 wa nyama na ngozi watapatiwa mafunzo juu ya uchinjaji na utayarishaji wa ngozi.

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti utoaji na uingizaji wa mifugo, mazao na pembejeo za mifugo, Wizara katika kipindi cha mwaka 2002/2003, ilianza mpango wa kuimarisha vituo vya ukaguzi *(Zoosanitary Check Points)* vya mipakani vya Kasesya, Isongole na Sirari na vituo vingine 30 vimepatiwa vitendea kazi. Aidha, wakaguzi 399 wa vituo walipatiwa mafunzo. Katika mwaka 2003/2004 vituo vitaendelea kuimarishwa na mafunzo yataendelea kutolewa kwa wakaguzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Kituo cha Madume cha Kuzalisha Mbegu Bora na Ng'ombe cha *NAIC* kilichopo *Usa River* Mkoani Arusha, kiliendelea kuimarishwa kwa kukarabati miundombinu. Ili kuongeza uzalishaji wa mbegu, madume bora matatu yaliyohakikiwa ubora *(Progeny Tested)* yalinunuliwa kutoka Afrika ya Kusini na mengine nane kutoka Kenya. Jumla ya dozi 41,250 za mbegu zilizalishwa ikilinganishwa na dozi 37,852 za mwaka 2001/2002 sawa na ongezeko la asilimia tisa. Aidha, jumla ya ng'ombe 38,560 walihamilishwa ikilinganishwa na ng'ombe 28,950 mwaka uliopita, sawa na ongezeko la asilimia 33. Ongezeko hili limetokana na mashamba ya *NARCO* kuanza kutumia teknolojia ya uhamilishaji katika kuzalisha mitamba ya ng'ombe wa maziwa. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, dozi 58,500 za mbegu bora zitazalishwa na ng'ombe 52,600 wanatarajiwa kuhamilishwa.

Mheshimiwa Spika, ufugaji wa kuku umeendelea kuwa chanzo cha chakula na mapato kwa wafugaji wadogo wengi walioko Vijijini na Mijini. Hata hivyo, ufugaji huu umeendelea kuathirika kutokana na ugonjwa wa mdondo ambao husababisha vifo vya kuku wengi kwa wakati mmoja. Jitihada za kudhibiti ugonjwa huu kwa kutumia chanjo ambayo haihitaji kuhifadhiwa kwenye jokofu zinaendelea. Jumla ya kuku milioni 6.2 walichanjwa katika Vijiji 145. Tathmini ya awali inaonyesha vifo vya kuku katika Vijiji hivyo vimepungua toka asilimia 80 hadi 20. Katika mwaka 2003/2004, dozi milioni 10 za dawa hiyo zitatengenezwa na kusambazwa nchini kote. Waheshimiwa Wabunge wanashauriwa kuwahamasisha wafugaji kutumia chanjo hiyo ili kuutokomeza ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, aidha, hali ya uzalishaji vifaranga nchini haikidhi mahitaji na hivyo kufanya nchi yetu kuendelea kuagiza vifaranga na mayai ya kuanguliwa kutoka nje. Kwa sasa, vipo vituo 11 vya kuangulia mayao vyenye uwezo wa kuangua vifaranga milioni 40 kwa mwaka. Uwezo huu hautumiki kikamilifu kutokana na gharama kubwa za uzalishaji. Katika mwaka 2002/2003 vifaranga milioni 17.5 vilizalishwa nchini na vifaranga milioni tano na mayai ya kuangaliwa milioni saba yaliagizwa toka nje. Kwa lengo la kuboresha ufugaji wa kuku wa

kienyeji, majogoo ya kisasa yamesambazwa kwa wafugaji. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004 lengo ni kuzalisha vifaranga milioni 34 ikilinganishwa na mahitaji ya vifaranga yanayokadiriwa kufikia milioni 39.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa nyanda za malisho unajumuisha kuzitambua, kutenga maeneo ya malisho, kutambua uwezo wake, kuondoa ndorobo na kuweka miundombinu. Uhaba wa ardhi katika baadhi ya maeneo, uhaba wa maji na malisho umeendelea kuathiri shughuli za uzalishaji mifugo pamoja na kuchochea migogoro kati ya wafugaji na wakulima. Aidha, wafugaji wameendelea kuhamahama, hali ambayo imesababisha usambazaji wa magonjwa na uharibifu wa mazingira. Ili kuondokana na hali hii, Wizara yangu iliendelea kuzihamasisha Halmashauri za Wilaya kutenga maeneo ya kulisha mifugo na kuishauri wafugaji wamilikishwe na kuyaendeleza ili kuwe na mipango endelevu ya ufugaji wa kisasa. Sambamba na hili, Wizara yangu iliendesha warsha mbili katika ngazi ya kanda za wadau wa sekta ya mifugo katika Wilaya 34 ili kuandaa programu shirikishi ya uendelezaji na matumizi endelevu ya nyanda za malisho.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi mojawapo inayoshiriki katika Mpango wa kutokomeza mbung'o na ugonjwa na Nagana Barani Afrika yaani *Pan African Tsetse and Trypanosomosis Eradication Campaign (PATTEC)*. Mpango huu upo chini ya uratibu wa Umoja wa Nchi za Afrika chini ya Taasisi ya Raslimali za Wanyama, *African Union Inter African Bureau of Animal Resources (AU/IBAR).* Aidha, nchi yetu inatekeleza Mradi wa *Farming in Tsetse Controlled Areas (FICTA)* unaofadhiliwa na Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU),* kwa lengo la kuondoa mbung'o na ugonjwa wa Nagana kwa kuwashirikisha wanavijiji. Mradi utatekelezwa kwa kipindi cha miaka minne kwa gharama ya *Euro* 800,000. Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya za Karagwe, Bukoba Vijijini, Pangani na Handeni kwa kushirikiana na wataalamu wa Halmashauri za Wilaya na sekta binafsi. Katika mwaka 2002/2003, utekelezaji wa mradi umegharimu shilingi milioni 249 wakati mpango wa mwaka 2003/2004 utagharimu shilingi milioni 240.

Katika jitihada za kupunguza ueneaji wa mbung'o nchini, uchunguzi wa ueneaji wa mbung'o na utayarishaji wa ramani, umefanywa kwa Wilaya zote za Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara na Wilaya za Lushoto na Kondoa ili kujua hali halisi. Aidha, elimu ya mbinu shirikishi ya uzuiaji wa mbung'o imetolewa kwa maafisa 20 wa Mikoa ambayo imeathirika zaidi ya Kigoma, Mara, Tabora, Tanga na Morogoro. Kwa mwaka 2003/2004, shughuli za uzuiaji mbung'o na ugonjwa wa Nagana kwa kutumia mbinu shirikishi na endelevu zitaendelezwa kwenye Wilaya nyingine zenye matatizo ya mbung'o.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuchangia uchimbaji na ukarabati wa malambo ili kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa mifugo na pia kama njia ya kudhibiti uhamaji wa wafugaji kutokana na ukosefu wa maji. Katika mwaka 2002/2003, Wizara yangu ilichangia jumla ya shilingi milioni 489 kuchimba na kukarabati malambo 163. Hadi Juni, 2003 jumla ya malambo 31 yamekamilika na mengine 132 yaliyobaki yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara yangu itachangia uchimbaji wa malambo 180. Ili kufanikisha kazi hii tunahitaji ushirikiano mkubwa wa Waheshimiwa Wabunge, kuwahamasisha wananchi na Halmashauri zao waweze kuchangia uchimbaji wa malambo kulingana na mahitaji ya Wilaya zao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, mashamba ya kuzalisha mbegu bora za malisho ya Langwira (Mbeya), Vikuge (Pwani) na Taasisi ya Utafiti na Uzalishaji Mifugo Mpwapa ziliendelea kuimarishwa ili kuzalisha mbegu bora za nyasi na jamii ya mikunde. Uzalishaji wa mbegu hizi pia umeendelea katika Vituo vya *Sao Hill*, Tengeru, Buhuri na Uyole, pamoja na watu binafsi. Jumla ya tani 5.3 za mbegu bora za malisho na marobota 61,000 ya hei yalizalishwa. Katika mwaka 2003/2004, mashamba haya yataendelea kuimarishwa kwa lengo la kuzalisha tani saba za mbegu bora za malisho na marobota 96,000 hei.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya biashara ya mifugo katika nchi yetu ilikuwa inafanyika kwa njia isiyo rasmi kutokana na kukosekana kwa miundombinu muhimu ya biashara ya mifugo pamoja na mazao yake. Tatizo hili limeanza kupungua baada ya Wizara yangu kukarabati baadhi ya miundombinu ya biashara ya mifugo. Katika mwaka 2002/2003, Wizara ilikarabati vituo 35 vya kupumzikia mifugo, vituo vitatu vya karantini, vituo vitano vya ukaguzi wa mifugo, minada minne, vituo vitatu vya kupakilia na mabehewa 10 ya kusafirishia mifugo kwa gharama ya shilingi milioni 580. Ujenzi na ukarabati wa miundombinu hiyo umekuwa ukitekelezwa Kaskazini mwa Reli ya Kati kwenye Mikoa 12 kwa mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Pia kwa kutumia mkopo huo,

Wizara iliendelea na ujenzi wa machinjio ya kisasa na Chuo cha Taaluma ya Ukataji Nyama Mjini Dodoma, ambao umefikia asilimia 60 na ujenzi unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2004. Aidha, kuanzia Novemba, 2002 Tanzania imeanza kuuza mifugo nje na tumeuza nchini Comoro ng'ombe 1,093 wenye thamani ya shilingi milioni 280 na mbuzi 430 wenye thamani ya shilingi milioni 12.5. Jitihada hizi zilizoanza zitaendelea kukuzwa kwa kushirikiana na sekta binafsi ili tuweze kuingia kwenye masoko ya nchi jirani na nchi za Uarabuni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara itaanza kujenga na kukarabati miundombinu ya mifugo katika Mikoa ya Kusini mwa Reli ya Kati kwenye Mikoa ya Iringa, Rukwa, Mbeya, Lindi na Mtwara kwa kutumia fedha za ndani ambapo shilingi milioni 200 zimetengwa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa ikikumbwa na magonjwa mbalimbali ya mifugo ambayo huleta hasara kubwa kwa wafugaji. Wizara yangu inachukua hatua mbalimbali za kudhibiti hali hiyo. Katika mwaka 2002/2003 Wizara iliendelea kutekeleza mikakati ya kuzuia na kudhibiti ueneaji wa magonjwa ya mifugo hasa ya milipuko chini ya Mradi wa Kudhibiti Milipuko ya Magonjwa ya Mifugo - *Pan African Programme for the Control of Epizootics (PACE)* unaofadhiliwa na Jumuiya ya Nchi za Ulaya na kusimamiwa na Umoja wa Nchi za Afrika chini ya Taasisi ya Rasilimali za Wanyama. Jumla ya shilingi bilioni 1.13 zilitumika chini ya mradi huo. Uchunguzi wa ugonjwa wa sotoka na ufuatiliaji wa dalili zinazofanana na ugonjwa huo ulifanyika katika Wilaya 10 za mpakani mwa nchi yetu na Kenya na pia katika maeneo ya mbuga za wanyama. Huu ni mwaka wa sita tangu ugonjwa huu ulipotokea mara ya mwisho na kufuatiwa na chanjo mwaka 1997. Nchi yetu ipo katika hatua ya mwisho ya kuutokomeza kufuatana na viwango vilivyowekwa kwa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003 vituo sita vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo pamoja na taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Mifugo *(ADRI - Temeke),* viliendelea na uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ya mifugo. Vituo vinne vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo vya Mpwapwa, Mtwara, Tabora na Arusha vilifanyiwa ukarabati, kununuliwa vifaa vya maabara, vitendea kazi na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi. Katika mwaka 2003/2004 shilingi milioni 985 zimetengwa kwa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kupambana na ugonjwa wa Homa ya Mapafu ambao umeendelea kuenea na kuwa tishio kwa maendeleo ya sekta ya mifugo na kuathiri uuzaji nje wa mifugo na bidhaa zake. Kwa sasa ugonjwa huu umeenea katika Mikoa yote ya Tanzania Bara isipokuwa Mkoa wa Kilimanjaro. Katika mwaka 2002/2003 dozi milioni 6.4 zilisambazwa katika Wilaya 60 kwenye Mikoa 12.

Mheshimiwa Spika, juhudi zinazochukuliwa na Serikali kudhibiti ugonjwa huo zinaonyesha mafanikio kiasi hasa kutokana na kupungua kwa kasi ya maambukizi mapya pamoja na vifo vinavyotokana na ugonjwa huo. Mwaka 2001 matukio 3,904 ya ugonjwa yaliripotiwa na idadi ya ng'ombe waliokufa ni 3,275 wakati mwaka 2002 matukio ni 3,263 yaliripotiwa na ng'ombe 1,354 walikufa. Kwa mwaka 2003 kuanzia Januari hadi Juni ni Wilaya mbili tu za Songea na Lindi ndizo zilitoa taarifa mpya za ugonjwa huu. Kwa ujumla, Mikoa ambayo hali ya ugonjwa ni mbaya ni Tabora, Singida, Kigoma na Rukwa. Wizara imeagiza dawa za chanjo dozi milioni saba ambazo zitasambazwa katika Wilaya 60 na jumla ya ng'ombe milioni 6.5 watapatiwa chanjo hiyo. Juhudi za kukabiliana na ugonjwa huo pia zitaelekezwa katika kudhibiti usafirishaji holela wa mifugo. Katika kipindi cha 2003/2004, jumla ya dozi milioni sita zitanunuliwa ili kuendelea na chanjo ya kudhibiti ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, magonjwa yatokanayo na kupe yameendelea kuwa chanzo cha vifo vingi vya mifugo nchini. Katika mwaka 2002/2003, ugonjwa wa Ndigana Kali uliongozwa kwa kusababisha vifo vya ng'ombe 1,385. Magonjwa mengine yaenezwayo na kupe yalisababisha vifo kama ifuatavyo: Ugonjwa wa Ndigana Baridi vifo 500, ugonjwa wa maji kwenye moyo vifo 132 na ugonjwa wa kukojoa damu uliua ng'ombe 100. Hali hii imetokana na majosho mengi kutofanya kazi kutokana na gharama kubwa za matengenezo na bei kubwa ya dawa za kuogesha. Kati ya majosho 2,050 yaliyopo nchini ni majosho 476 tu sawa na asilimia 23 ndiyo yanayofanya kazi.

Katika mwaka 2002/2003, Wizara iliendelea kuhimiza ukarabati wa majosho, uogeshaji wa mifugo pamoja na kuchanja ng'ombe dhidi ya Ndigana Kali ili kuzuia vifo vya mifugo. Jumla ya ng'ombe 20,278 walipatiwa chanjo ya Ndigana Kali. Aidha, ugonjwa wa *Ormillo (Cerebral Theileriosis),* ambao huletwa na kupe, ulisababisha jumla ya vifo 105,000 vya ng'ombe wenye thamani ya shilingi bilioni 10.5 katika Wilaya za Mikoa ya Arusha, Manyara na Morogoro. Uchunguzi wa kitaalam uliendelea kufanyika kwa msaada wa Serikali ya Uingereza kupitia Shirika lake la *DFID* ili kujua kiwango cha usambaaji, madhara yatokanayo na ugonjwa huo pamoja na kujua aina za kupe wanaoeneza. Kwa mwaka 2003/2004, lengo ni kuihusisha sekta binafsi kupanua wigo wa kuchanja mifugo

dhidi ya ugonjwa wa Ndigana Kali kupitia msaada wa *FAO* na kufuatilia ugonjwa wa *Ormillo* ili kudhibiti kuenea kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa miguu na midomo *(FMD)* umeendelea kuathiri biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi ambapo matukio 53 yalitolewa taarifa. Udhibiti wa ugonjwa huu unahusisha uzuiaji wa uingizaji na usafirishaji wa mifugo na bidhaa za mifugo kutoka kwenye maeneo yenye ugonjwa pamoja na kutoa chanjo. Katika mwaka 2002/2003, Wizara imeandaa mkakati wa kudhibiti ugonjwa huu na tayari umewasilishwa katika Jumuiya ya Nchi zilizo Kusini mwa Afrika *(SADC)* na Jumuiya ya Afrika Mashariki, ili kuandaa mkakati wa pamoja wa kutokomeza ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa Nagana unaosambazwa na mbung'o kwa wanyama umeendelea kuwa ni tatizo kubwa katika uzalishaji wa ng'ombe wa asili kwani maeneo mengi hayawezi kutumika kwa shughuli za ufugaji. Katika mwaka 2002/2003, ng'ombe 13,073 wenye thamani ya shilingi bilioni 1.3 walikufa kati ya ng'ombe 352,836 walioambukizwa ugonjwa huo. Aidha, watu wapatao 232 katika Wilaya za Kasulu, Kibondo, Kigoma Vijijini na Urambo waliambukizwa ugonjwa wa Malale. Katika jitihada za kudhibiti ugonjwa huo kwa mifugo na binadamu, mbinu shirikishi za kutumia mitego na vitambaa vyenye sumu ya kuua mbung'o zilihamasishwa katika vijiji vya Wilaya za Kigoma Vijijini, Kibondo, Kasulu, Serengeti, Tarime, Bunda na Musoma Vijijini. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa wataalamu 20 toka katika Wilaya 20 zenye ndorobo kuhusu mbinu shirikishi na endelevu za kuzuia ndorobo katika Wilaya zao. Mwaka 2003/2004, Wizara itaendelea na mafunzo haya katika maeneo mengine yenye matatizo ya mbung'o na ugonjwa wa ndorobo.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa kichaa cha mbwa bado ni tishio kwa wanyama na binadamu hapa nchini. Katika mwaka 2002/2003, kumekuwa na matukio 527 ya watu walioumwa na mbwa. Katika jitihada za kukabiliana na ugonjwa huu, Wizara imenunua dozi za chanjo 60,000 na kusambazwa katika Wilaya 30 zilizotoa taarifa ya matukio ya ugonjwa huo. Vile vile, viperurushi 3,000 viliandaliwa na kusambazwa kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu athari za ugonjwa wa kichaa cha mbwa kwa wananchi. Katika mwaka 2003/2004, Wizara itanunua dozi 50,000 na kutoa elimu kwa umma kuhusu athari za ugonjwa huu. Wizara inazishauri Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa, kuhimiza utekelezaji wa Sheria ndogo ndogo za ufugaji wa mbwa katika maeneo yao ili kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo kwa binadamu.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa maadili ya Huduma za Afya ya Mifugo, kutokana na mabadiliko ya majukumu ya Wizara, sehemu kubwa ya shughuli za utoaji wa huduma za afya ya mifugo hutolewa na sekta binafsi. Ili kudhibiti na kusimamia vyema mienendo ya utoaji huduma ya mifugo, Wizara imeendelea kuimarisha Bodi ya Madaktari wa Mifugo. Katika mwaka 2002/2003, Bodi ilisajili Madaktari wapya 26 na kufanya jumla ya Madaktari waliosajiliwa nchini kufikia 654. Hata hivyo, ni Madaktari wa mifugo 446 tu wanaotoa huduma kisheria, wengine wameondolewa katika rejesta kwa sababu mbalimbali. Asilimia 55 ya Madaktari hao wameajiriwa Serikalini na Mashirika ya Umma wakati asilimia 45 wanatoa huduma katika sekta binafsi. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itawatambua na kuwaandikisha kisheria wataalam wengine wote wanaotoa huduma ya afya ya mifugo nchini.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma za ushauri kwa wafugaji ni njia mojawapo ya kuwapatia wafugaji teknolojia sahihi na mbinu za ufugaji bora. Katika mwaka 2002/2003, kwa kushirikiana na TAMISEMI, Wizara yangu iliendelea kutoa ushauri wa kitaalam pamoja na miongozo ya utekelezaji wa shughuli za mifugo. Utoaji huduma za ushauri kwa wafugaji uliendelea kutekelezwa chini ya Halmashauri za Wilaya. Aidha, Wizara yangu ilitoa mafunzo ya kuimarisha vikundi vya wafugaji ambapo jumla ya viongozi 102 kutoka vikundi vya wafugaji 43 walipatiwa mafunzo ya uongozi. Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO),* imetumia dhana ya mbinu shirikishi kuanzisha vikundi na kutoa mafunzo kwa wafugaji katika Wilaya sita za Morogoro Vijijini, Kongwa, Kilombero, Biharamulo, Kondoa na Kilosa. Dhana hii itaendelezwa katika sehemu nyingine ili kuendeleza ufugaji bora hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kuwahamasisha wananchi kwa njia mbalimbali kuhusu ufugaji bora ikiwa ni pamoja na kuandaa na kusambaza vijitabu na vipeperushi na kurusha vipindi vya redio, pamoja na kufanya maonyesho ya mifugo. Zaidi ya nakala 15,000 za vipeperushi kuhusu ugonjwa wa Kideri, Homa ya Mapafu, Maadili ya Madaktari wa Mifugo na majarida ya Afya ya mifugo vilichapishwa na kusambazwa. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itaendelea kuandaa na kusambaza vijitabu vya ufugaji bora, vipindi vya redio na televisheni kuhusu ufugaji bora na wa kibiashara.

Aidha, Wizara yangu ilishiriki katika kuadhimisha Siku ya Chakula Duniani, ambayo ilifanyika Kitaifa Mkoani Mbeya. Maadhamisho hayo hufanyika duniani kote tarehe 16 Oktoba kila mwaka kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuzalisha chakula cha kutosha na chenye lishe bora. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Shirika hilo katika kuandaa maadhimisho hayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kufanya utafiti wa mifugo ili kuboresha ufugaji pamoja na kutatua matatizo yanayowakabili wafugaji nchini. Shughuli za utafiti zinalenga katika maeneo yafuatayo: Magonjwa ya mifugo, namna ya kuongeza uzalishaji wa maziwa na nyama, uendelezaji wanyama wadogo pamoja na malisho bora na nyanda za malisho.

Katika mwaka 2002/2003, Wizara yangu ilinunua mitamba 200 ya ng'ombe aina ya *Boran* kwa ajili ya kuendeleza uzalishaji wa ng'ombe aina ya Mpwapwa. Jumla ya ng'ombe 98 aina ya Mpwapwa walisambazwa kwa wafugaji katika vijiji vya Mtumba (Dodoma), Chipogoro (Mpwapwa), Ititi (Singida), Longido, Kiteto na Ngorongoro (Arusha) kwa majaribio. Mbuzi chotara *(Blended Goats)* 550 waliosambazwa Mkoani Dodoma mwaka 2001/2002, wameonyesha kustahimili na tayari mbuzi 776 wamezaliwa. Katika mwaka 2003/2004, utafiti wa ng'ombe aina ya Mpwapwa utaendelea kufanyika pamoja na kusambaza madume bora ya mbuzi na kutoa ushauri kwa wafugaji kwa kushirikiana na Halmashauri husika. Mkazo utatolewa katika kuainisha koo mbalimbali za mifugo ya asili na kuitathmini ili kupata sifa zao kwa ajili ya kuiendeleza.

Mheshimiwa Spika, kituo cha Utafiti wa Mifugo cha Tanga kinachohudumia Kanda ya Mashariki ya Mikoa ya Morogoro, Pwani, Tanga na Dar es Salaam, kilisambaza majogoo chotara 1,131 kwa wafugaji katika mwaka 2002/2003. Aidha, kuanzia mwaka 2000 kwa kutumia madume 22 ya ng'ombe chotara *(F1-Bulls)* waliopelekwa Vijijini kutoka katika kituo hicho cha utafiti, ndama 180 walizaliwa katika Wilaya za Bagamoyo na Handeni. Madume ya mbuzi wa maziwa 15 yalisambazwa katika Vijiji vya Mavovo (Muheza) na Misima (Handeni) ili kuboresha mbuzi wa asili katika maeneo hayo. Katika mwaka 2003/2004, usambazaji wa ng'ombe wa maziwa utaendelea katika Wilaya nyingine za Kanda ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa msaada wa *USAID* na *FAO*, Wizara imeendelea na utafiti juu ya athari za maafa dhidi ya mifugo hasa wakati wa kiangazi kwa kuainisha kumbukumbu za hali ya hewa na malisho *(Livestock Early Warning System)* na kutoa ramani zanye kuainisha malisho kwa kipindi cha miezi miwili mbele katika Kanda mbili za Kati na Kaskazini zenye Mikoa ya Singida, Dodoma, Arusha, Kilimanjaro na Manyara. Aidha, jitihada zitafanyika kusambaza Teknolojia hii katika maeneo mengine hapa nchini kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea na utafiti juu ya kudhibiti magonjwa ya mifugo katika kituo cha *ADRI - Temeke.* Utafiti unafanyika wa kutengeneza chanjo ya majaribio ya ugonjwa wa homa ya mapafu ya ng'ombe, ugonjwa wa kutupa mimba *(Brucellosis)*, Kimeta *(Anthrax)* na Chambavu *(Blackquarter)*. Aidha, utafiti unafanyika ili kupata njia rahisi za kugundua ugonjwa wa mapafu. Matokeo ya awali yanaonyesha uwezekano wa kupata na kutengeneza chanjo hizi hapa nchini na juhudi hizo za utafiti zitaendelea katika mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea na utafiti wa kutokomeza mbung'o kwa kutumia Teknolojia ya kuhasi madume ya mbung'o katika Taasisi ya Utafiti wa Ndorobo na Malale iliyopo Tanga. Upembuzi wa awali umefanyika katika maeneo ya Kondoa, Simanjiro, Same na Tanga ili kuainisha aina mbalimbali za mbung'o. Aidha, Taasisi ilipata msaada wa jumla ya Dola za Kimarekani 236,000 kutoka Marekani kwa ajili ya kukarabati Maabara na Dola 454,000 kutoka *International Atomic Energy Agency (IAEA),* kwa ajili ya kununulia vifaa vya Maabara na kufuga madume ya mbung'o yaliyohasiwa kwa ajili ya kuwapeleka Ethiopia na Botswana na kufuga wengine kama tahadhari ya kinga kwa Zanzibar. Taasisi hii ndiyo pekee Barani Afrika yenye uwezo wa kuzalisha madume ya mbung'o yaliyohasiwa ambayo hutumika kutokomeza ndorobo. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itaendelea kuimarisha Taasisi hiyo ili kuiongezea uwezo wa kuzalisha mbung'o na kufanya tafiti za magonjwa hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha miundombinu ya vituo vya Utafiti wa Mifugo, Wizara yangu ilikarabati kituo cha utafiti wa uzalishaji wa mifugo Mpwapwa na Tanga. Aidha, kazi ya ujenzi wa Maabara kwa ajili ya utafiti wa ugonjwa wa Miguu na Midomo, yaani *Foot and Mouth Disease (FMD)* imeendelea. Vifaa kwa ajili ya kuimarisha Maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Mgonjwa ya Wanyama Temeke vimeagizwa. Katika mwaka

2003/2004, Wizara itaendelea na ukarabati wa Vituo na Taasisi za Utafiti wa Mifugo ili kuweka mazingira mazuri ya utendaji mzuri.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaandaa Sera ya Uzalishaji wa Mifugo *(National Livestock Breeding Policy)* ili kuweka mwongozo wa namna ya kuboresha mifugo iliyopo nchini. Uamuzi huu unatokana na mkutano wa Wadau wa Mifugo uliofanyika Arusha Aprili, 2001 ambao ulibainisha kuwa, mifugo duni nchini ni mojawapo ya vikwazo vikubwa katika uzalishaji wa mifugo.

Aidha, kwa kuwa Taifa letu ni sehemu ya mpango wa Umoja wa Mataifa wa kusimamia utunzaji wa viumbe hai *(United Nations Convention on Biological Diversity),* tunawajibika kuwa na Sera ya Utunzaji, Uboreshaji na uzalishaji endelevu wa mifugo iliyopo.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu vituo vya mafunzo ya mifugo viliachwa bila kufanyiwa matengenezo kutokana na uhaba wa fedha na hivyo kuathiri mazingira ya vyuo hivyo. Katika mwaka 2002/2003, Wizara yangu ilianza kuvikarabati vyuo hivyo ili kuboresha mazingira. Sambamba na Uboreshaji huo, idadi ya wanachuo wanaogharamiwa na Wizara imeongezeka kutoka wanachuo 480 mwaka 2000/2001 hadi kufikia 629 mwaka 2002/2003. Aidha, idadi ya wanachuo wanaochangia gharama za mafunzo yao kutoka ndani na nje imeongezeka kutoka wanachuo 185 hadi 210 mwaka 2002/2003. Vile vile, Wizara yangu kwa kushirikiana na asasi mbalimbali, iliendesha mafunzo kwa wafugaji 1,557 kutoka sehemu mbalimbali nchini.

Kazi nyingine zilizotekelezwa ni kuhuisha muhtasari wa Stashahada ya Utunzaji wa Nyanda za Malisho na Udhibiti wa Ndorobo ili kukidhi mahitaji ya walengwa. Aidha, vitabu vya kiada na rejea katika fani ya uzalishaji wa kuku na nguruwe viko katika hatua za uchapishaji. Utayarishaji vitabu vya kiada na rejea vya uzashaji wa wanyama, uhamilishaji, mazao ya mifugo na ubora wake umefanyika. Utayarishaji wa kozi za utotoaji wa vifaranga, ufugaji wa ng’ombe na mbuzi wa maziwa, ufugaji wa nguruwe, usindikaji wa maziwa na tiba ya mifugo pia umefanyika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itaendelea kuboresha na kuimarisha mazingira katika vyuo vya mifugo. Aidha, Wizara yangu itafadhili wanachuo 220 na kutoa mafunzo kwa wafugaji 1,800 kwa kushirikiana na asasi mbalimbali. Vile vile, itahuisha muhtasari wa stashahada ya uzalishaji wa mifugo na stashahada ya Ufundi Mchundo wa Maabara na kukamilisha uandikaji wa vitabu vya kiada na rejea katika fani mbalimbali za mifugo.

Mheshimiwa Spika, vyakula vya ziada vyenye virutubisho ni muhimu katika kuongeza uzalishaji wa tija ya mifugo hususan ng’ombe na mbuzi wa maziwa, kuku na nguruwe. Ukosefu wa vyakula hivyo, uhafifu wake na bei kubwa bado ni tatizo linaloathiri uzalishaji na ukuaji wa wanyama hao kwa muda unaotakiwa. Katika mwaka 2002/2003, Wizara yangu imeendelea kuratibu, kudhibiti na kuhamasisha sekta binafsi ili kuongeza uzalishaji na kuboresha viwango vya vyakula hivyo. Kwa sasa, vipo viwanda 82 vyenye uwezo wa kutengeneza tani 700,000 za vyakula mbalimbali vya mifugo. Hata hivyo, uzalishaji kwa mwaka 2002/2003, ulifikia tani 491,000 ukilinganisha na mahitaji ya tani 650,000 zinazotakiwa kwa mwaka. Katika mwaka 2003/2004, kiasi cha tani 495,000 kinatarajiwa kuzalishwa.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Sera ya Chama cha Mapinduzi, “Dhana ya uwezeshaji maana yake ni kuunda mazingira muafaka yanayowapatia Watanzania fursa ya kumiliki na kuendesha uchumi wa nchi yao.... Wananchi wahimizwe na wawezeshwe kuingia kwenye ufugaji wa kati na mkubwa wa kibiashara”. Ili kufikia azma hii, Serikali imetoa nafasi kwa Wananchi kumiliki na kushiriki katika shughuli za ufugaji katika mashamba ya Dakawa, Nkundi na Nachingwea.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu mwaka 2002, Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO),* itaendelea kumiliki eneo la hekta 20,000 kwenye Ranchi za *Kikulula Complex* (hekta 76,940), Kitengule (hekta 41,700), *West Kilimanjaro* (hekta 30,000), Kalambo (hekta 64,650), Mkata (hekta 71,970), Mzeri (hekta 41,246) na Misenyi (hekta 60,851), ili yawe mashamba ya mfano katika shughuli za kuzalisha mifugo. Maeneo yatakayobaki katika ranchi hizo yatagawanywa kwenye ranchi ndogo ndogo za ukubwa wa hekta 4,000 na kumilikishwa kwa Wananchi ili waendeshe shughuli za ufugaji kibiashara.

Katika mwaka wa 2002/2003, *NARCO* ilizalisha ndama 10,400 wa nyama na maziwa kutokana na ng'ombe 42,500. Pia, katika kipindi hicho ng'ombe 9,000 wa nyama waliuzwa ikiwa ni pamoja na mitamba wa maziwa 1,290. Uzalishaji wa mitamba wa maziwa umekuwa kichocheo kikubwa katika kuendeleza ufugaji wa ng'ombe wa maziwa hasa kwa wafugaji wadogo na kwa hiyo kusaidia katika jitihada za kuondoa umaskini.

- Katika mwaka wa 2003/2004, *NARCO* inategemea kuzalisha ndama 11,000 na kati ya hawa ndama 7,600 watakuwa wamezalishwa kwa njia ya uhamilishaji.

Aidha, ng'ombe 10,300 wa nyama na mitamba 1,320 wa maziwa wanatarajiwa kuuzwa. Kiasi kikubwa cha mitamba wa maziwa kitauziwa wafugaji wadogo kwenye Mikoa ya Kagera, Tanga, Pwani, Rukwa na Dodoma. Aidha, inatarajiwa kuwa ng'ombe 5,000 watanunuliwa kutoka kwa wafugaji wadogo na kunenepeshwa kwa ajili ya kuuzwa.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wanaweza kutatua matatizo yanayowakabili kwa ufanisi zaidi endapo watajiunga katika vikundi. Katika mwaka 2002/2003, Wizara iliendelea na juhudi za kuwahamasisha wafugaji na wadau wengine wa Sekta ya Mifugo, kuunda vikundi ili kuwa na nguvu ya pamoja katika kutatua matatizo yao ya ufugaji na kutafuta masoko. Vikundi ambavyo vimeshaanzishwa vimeendelea kuimarishwa. Aidha, vikundi 193, vya wafugaji wa ng'ombe wa asili vimeanzishwa. Kati ya hivyo, 23 vimesajiliwa na vinajishughulisha na uendelezaji wa majosho, uuzaji mifugo na usimamizi wa matumizi ya maji kwenye malambo. Lengo la kuhamasisha uundwaji wa vikundi hivi ni kuviwezesha hapo baadaye kuunda, kusimamia na kuendesha Bodi mbalimbali za mazao yatokanayo na mifugo kwa manufaa yao.

Katika mwaka 2003/2004, Wizara itaandaa mikakati madhubuti inayohusu matumizi ya teknolojia rahisi kwenye maeneo ya wafugaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kukusanya takwimu za maji na usafi wa mazingira katika Mikoa mbalimbali nchini. Takwimu hizo zinahitajika katika kuratibu na kutathmini maendeleo ya Sekta ya Maji na Mifugo. Vile vile, juhudi za kukusanya takwimu kwa ajili ya Sekta ya Mifugo zimeimarishwa. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha Kitengo cha Benki ya Takwimu kwa kukipatia vifaa vya kisasa ili kuongeza ubora, upatikanaji na uchambuzi wa takwimu na taarifa za kitaalam. Watumishi kutoka kitengo hicho wamehudhuria mafunzo ya namna ya kukusanya, kuchambua na kuhifadhi takwimu. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itaendelea kukiimarisha Kitengo hicho pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi husika.

Mheshimiwa Spika, katika kupiga vita kuenea kwa janga la UKIMWI mahali pa kazi, Wizara imeendesha semina 3 kwa watendaji wakuu na watumishi wote wa Wizara, ambapo mbinu mbalimbali za kujikinga na janga hilo zilielezwa na kutolewa ufafanuzi. Ni matumaini yangu kuwa maelezo ya kitaalam kuhusu namna ya kujikinga na gonjwa hili yatazingatiwa ili kupunguza kasi ya kuenea. Vile vile, Wizara iliendelea kupiga vita rushwa ya aina yoyote ile mahali pa kazi. Waratibu wanaoshughulikia masuala ya UKIMWI, jinsia na rushwa, wameteuliwa ili kuyapa msukumo unaostahili majukumu haya. Katika mwaka 2003/2004, Wizara itatoa msukumo katika masuala ya jinsia, hifadhi ya mazingira na kupambana na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, watumishi wengi wa Wizara yangu ambao wanafanya kazi katika ngazi mbalimbali, watakuwa wanastaafu kazi muda si mrefu. Hivyo suala la ajira mpya na kujenga uwezo ni muhimu sana. Katika mwaka 2002/2003, watumishi 57 waliajiriwa, 221 walithibitishwa kazini, 3,601 walipandishwa vyeo. Kati ya hao watumishi 330 ni wa Sekta ya Maji na 3,271 ni wa Sekta ya Mifugo. Pia, watumishi 401 wa Sekta ya Mifugo. Pia, watumishi 401 wa Sekta ya Maji wameombewa kibali cha kuwapandishwa vyeo kwa mserereko kutoka Idara Kuu ya Utumishi. Aidha, watumishi 110 wamepata mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi kwa kuzingatia mahitaji ya kazi zao. Vile vile, Wizara yangu ilizindua Mkataba wa Huduma kwa Mteja *(Client Service Charter)* na inaendelea kupokea maoni na kutoa elimu ya uhamasishaji kwa wadau na watumishi wake.

Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu inatarajia kuwapandisha vyeo watumishi 3,000. Aidha, katika kutekeleza mpango wa uboreshaji wa utumishi wa umma, Wizara yangu itashirikisha Sekta binafsi katika kutoa baadhi ya huduma kwa kuanzia katika maeneo ya ulinzi, usafi na mapokezi. Vile vile, katika kutekeleza Sera ya Menejimenti na Ajira, Wizara yangu itakamilisha mpango wa mafunzo ambao utaweka utaratibu wa kila mtumishi kupata mafunzo ya kujiendeleza katika fani yake.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka uliopita yametokana na ushirikiano na misaada mikubwa ya kifedha na kiufundi toka kwa nchi wahisani, Mashirika mbalimbali ya misaada, Taasisi za hiari zisizokuwa za Kiserikali, Mashirika ya Kidini na Taasisi mbalimbali za Fedha, bila kusahau hamasa na ushiriki wa Wananchi wakiongozwa na wawakilishi wao Waheshimiwa Wabunge na Madiwani.

Napenda kuzishukuru Serikali za nchi ya Ujerumani, Japan, Ufaransa, Jamhuri ya Watu wa China, Uholanzi, Denmark, Sweden, Marekani, Canada, Uswisi, Ireland, Ubelgiji na Uingereza. Aidha, napenda kutoa shukrani kwa Taasisi za Fedha za Kimataifa, yaani Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA), European Investment Bank (EIB)*, Umoja wa Nchi zinazouza Mafuta Duniani *(OPEC)*, pamoja na Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU),* Umoja wa Nchi za *NORDIC* na Mashirika ya Umoja wa Mataifa, yaani *UNDP, UNICEF,* Shirika la Chakula la Umoja wa Mataifa *(FAO), UNIDO, IFAD, AU/AIBAR, Global Environmental Facility (GEF)* na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki *(IAEA),* kwa misaada na michango yao ya utaalamu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Aidha, nachukua nafasi hii kuyashukuru Mashirika ya Kidini ya *World Islamic League,* Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Kanisa la Kilutheri la Ujerumani na Kanisa Katoliki Tanzania, pamoja na Taasisi nyingine za hiari za *Water Aid, Vet Aid* na *OXFAM* za Uingereza, *Austro-Project, Heifer Project International (HPI), World Vision, USAID* na wote wale ambao kwa njia moja au nyingine wanaendelea kuisaidia Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba, kupitia kwako, nitumie fursa hii kuwashukuru wote hawa kwa dhati kabisa. Nawaomba waendelee kushirikiana na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa michango yao mbalimbali ya mawazo na ushauri walioutoa ndani na nje ya Bunge hili kwa Wizara yangu, kwa nia ya kuboresha huduma ya maji na maendeleo ya mifugo hapa nchini. Aidha, kama nilivyotangulia kusema, shukrani zangu za pekee ziwaendee Wananchi wote, kwa michango yao ya hali na mali katika kutekeleza programu za maji na mifugo nchini. Naomba waendelee na moyo huu ili kuimarisha huduma zitolewazo na Wizara yangu. Wizara yangu itaendelea kushirikiana nao kwa lengo la kuboresha hali za maisha yao na kuongeza uwezo wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majukumu ya kuendeleza Sekta za Maji na Mifugo yanatekelezwa kwa ushirikiano na mshikamano wa hali ya juu na viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara yangu. Naomba pia nitumie nafasi hii kuwashukuru viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, pamoja na Mashirika na Taasisi zake katika ngazi mbalimbali kwa juhudi zao kubwa walizoonyesha katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa. Shukrani zangu nazielekeza kwa Mheshimiwa Anthony N. Diallo, Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa msaada na ushauri wake wa karibu sana. Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Ndugu Bakari A. Mahiza na Naibu Katibu Mkuu Dr. Charles Nyamrunda, kwa bidii, juhudi na moyo wao wa kujituma katika kusimamia utekelezaji wa majukumu tuliyopewa na Taifa na kufanikisha maandalizi ya Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawashukuru wafanyakazi wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kazi na mchango wao mkubwa kwenye hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu yaliyoelezwa katika hotuba hii kwa mwaka 2003/2004, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh.66,182,327,400/= kwa ajili ya matumizi ya Wizara yangu kwa kipindi cha mwaka 2003/2004. Kati ya fedha hizo matumizi ya kawaida ni Sh.15,428,131,400/= ambapo Sh.3,886,992,200/= ni mishahara ya watumishi na Sh.11,541,139,200/= ni fedha za matumizi mengine. Makadirio ya bajeti ya maendeleo ni Sh.50,754,196,000/= ambapo Sh.7,096,856,000/= ni fedha za ndani na Sh.43,657,340,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge ya 81 (1), naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Kilimo na Ardhi juu ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka 2002/2003, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niwatambue Wajumbe wa Kamati hiyo, nao ni Mheshimiwa Alhaji Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Anatory K. Choya, Mheshimiwa Musa A. Lupatu, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Abdillahi O. Namkulala, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Philip A. Magani, Mheshimiwa John E. Singo, Mheshimiwa Salama Khamis Islam, Mheshimiwa Charles H. Kagonji, Mheshimiwa Robert K. Mashala, Mheshimiwa Gwassa A. Sebabili, Mheshimiwa Paul N. Makolo, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Joel N. Bendera, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Edward N. Ndeka, Mheshimiwa Said J. Nkumba na Katibu Ndugu Elisa D. Mbise. Nawashukuru sana wote kwa ushirikiano wanaonipa katika Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wenzangu, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Naibu wake, pamoja na wataalam wake wote wa Wizara hiyo, kwa jinsi walivyoweza kueleza na kufafanua pamoja hoja mbalimbali zilizotolewa na Kamati wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ilitekeleza maagizo yote na kuzingatia ushauri wa Kamati ya Bunge ya Kisekta iliyochambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa kipindi cha 2002/2003. *(Makofi)*

Kabla ya kuanza kujadili Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2002/2003, pamoja na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati yangu ilipata fursa ya kutembelea baadhi ya Asasi zilizopo chini ya Wizara hii. Kamati iliweza kutembelea Makao Makuu ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam *(DAWASA),* pamoja na mtambo wa kuzalisha maji wa Ruvu chini. Aidha, Kamati iliweza kutembelea Mnada wa Mifugo uliopo Pugu, pamoja na Kiwanda cha Maziwa cha mtu binafsi kinachoitwa *Tommy Diary.*

Lengo la ziara hii ilikuwa ni kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge na Kamati hii, kujifunza na kujionea baadhi ya shughuli zinazotekelezwa na Wizara za kutekeleza Sera ya Maji na Mifugo nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea *DAWASA* ilipata maelezo juu ya historia ya *DAWASA*, majukumu iliyopewa kisheria, hali halisi ilivyo na mpango mzima wa ubinafsishaji au ukodishaji wa miundombinu ya *DAWASA*. Jukumu la msingi la *DAWASA* ni kutoa huduma ya maji safi na kuondoa maji taka katika Jiji la Dar es Salaam na Miji midogo ya Bagamoyo na Kibaha.

Kamati ilielezwa kwamba, *DAWASA* ina uwezo wa kuzalisha galoni milioni 62 za maji kwa siku ikilinganishwa na mahitaji ya galoni milioni 90 kwa siku. Hii ina maana kwamba, kiwango cha uzalishaji wa maji ni asilimia 69 ya mahitaji. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kwamba, kuna upotevu wa maji wa asilimia 55 yanayozalishwa, kiwango ambacho ni kikubwa sana. Kwa upande wa ukodishaji na uondoshaji maji taka, Kamati ilielezwa kwamba, ni asilimia 7 tu ya wakazi wa Dar es Salaam waliounganishwa kwenye mfumo wa maji taka. Kuhusu ukusanyaji wa mapato, *DAWASA* inakusanya wastani wa Shilingi bilioni 1.3 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba, kutokana na maelezo haya mafupi, ufanisi katika kutoa huduma ya maji safi na uondoshaji wa maji taka katika Jiji la Dar es Salaam na Miji midogo ya Bagamoyo na Kibaha, bado uko chini sana. Hii inatokana na ukweli kwamba, miundombinu ya *DAWASA* haitoshi na ni chakavu sana. Sehemu kubwa ya miundombinu hiyo ilijengwa mwaka 1940 na miaka ya 1980. Ili kuboresha huduma ya maji safi na uondoshaji wa maji taka, *DAWASA* imekodishwa kwa lengo la kupata teknolojia ya kisasa, fedha za kuwekeza katika mfumo wa maji taka na kuboresha ufanisi katika uendeshaji wa matengenezo. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia ya kumpa mwekezaji atakayeendesha shughuli za kutoa huduma ya maji safi na kuondosha maji taka pamoja na kukusanya mapato. Ni matarajio ya Wananchi kwamba, baada ya mwekezaji kupatikana huduma ya maji safi na uondoshaji wa maji taka itaboreshwa na itapanuliwa kwa Wananchi wengi zaidi katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea mnada wa mifugo wa Pugu, ambao ni mmoja kati ya minada 56 iliyojengwa kote nchini chini ya mradi wa kuboresha vituo vya kupeleka na kuuza mifugo (ng'ombe na mbuzi) na mazao yake. Chini ya mradi huu ulioanza rasmi mwaka 1997, jumla ya minada 56 ilijengwa, vituo 13 vya *quarantine* na kukarabati njia za mifugo. Mradi huu pia unajenga machinjio ya kisasa hapa Dodoma. Mnada wa ng'ombe na mbuzi Pugu ndio soko kubwa la mifugo hiyo hapa nchini kwani hata wanunuzi toka nje ya nchi hutegemea mnada huo. Moja ya matatizo yanayokabili shughuli za mnada wa Pugu ni uvamizi wa maeneo yake unaofanywa na wakulima pamoja na ujenzi wa makazi ya watu.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliweza kutembelea Kiwanda cha Maziwa cha *Tommy Diary,* kwa lengo la kujifunza jinsi Sekta binafsi inavyojihusisha katika kuendeleza Sekta ya Mifugo nchini. Kiwanda hiki kina uwezo wa kuzalisha lita 20,000 za maziwa kwa siku na kinatoa ajira kwa watu zaidi ya 100 wanaojishughulisha na kuuza maziwa kwenye viosk Jijini Dar es Salaam. Hii inaonyesha jinsi Watanzania wenyewe wanavyoweza kuendeleza Sekta za Uzalishaji ikiwa ni pamoja na Sekta ya Mifugo. Kiwanda cha *Tommy Diary* kinatoa soko kubwa la maziwa yanayozalishwa na wafugaji wa ng'ombe wa maziwa katika Mikoa ya Tanga na Iringa.

Mheshimiwa Spika, katika kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2002/2003 na Malengo ya Bajeti kwa mwaka 2003/2004, kwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Kamati ilipata maelezo ya kina juu ya Majukumu ya Wizara, Malengo ya Wizara na Utekelezaji wake kwa mwaka uliopita na mipango iliyowekwa kwa mwaka ujao wa fedha. Kamati inaipongeza Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa jinsi walivyotekeleza malengo waliyojiwekea na kutekeleza programu mbalimbali katika Sekta ya Maji na Mifugo kwa mwaka uliopita. Ni matumaini ya Kamati kwamba, malengo yaliyowekwa na Wizara katika Bajeti hii yatatekelezwa kwa ufanisi wa hali ya juu, kipimo kikiwa ni kuboresha maisha ya Wananchi walio wengi kupitia Sekta ya Maji na Mifugo.

Mheshimiwa Spika, ipo miradi mingi ya maji katika maeneo mbalimbali ya nchi ambayo imesimama au mitambo imekufa kutokana na kukosa matengenezo ya mara kwa mara. Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini kwa kutembelea na kutambua miradi yote ya maji iliyosimama au kufa na kuiwekea programu maalum ya kuifufua ili kuwaondolea Wananchi kero ya kusafiri mbali kutafuta maji au kutumia maji yasiyo salama. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, miradi inayotekelezwa na wafadhili inakabidhiwa kwa Mamlaka zitakazowajibika kusimamia utekelezaji wake mara wafadhili watakapoondoka. Kamati za Maji za Vijiji na maeneo mengine zihamasishwe na kuelimishwa kuhusu umuhimu wa kutunza miradi ya maji na vyanzo vya maji katika maeneo yao. Ili kuifanya miradi hii kuwa endelevu, Kamati inashauri kwamba, wataalam wa maji wajiwekee utaratibu wa kukagua miradi ya maji kwa maeneo mbalimbali hasa Vijijini ili uharibifu unapotokea udhibitiwe mapema kabla mradi wowote haujafa.

Mheshimiwa Spika, wakati akiwasilisha Bajeti ya Wizara kwenye Kamati, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, aliieleza Kamati kwamba, Umoja wa Mataifa unakataza uchimbaji na ujengaji wa mabwawa kwa nchi zinazoendelea na hivyo wafadhili hawatoi fedha kwa mipango ya kutengeneza mabwawa. Kutokana na umuhimu wa mabwawa na malambo katika maisha ya watu wetu, Kamati inashauri Serikali kuwa na msimamo katika suala hili na kuhakikisha kwamba, mabwawa na malambo yanatengenezwa kwa kutumia fedha za ndani, pamoja na nguvu za Wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvunaji wa maji ya mvua, Kamati inashauri Serikali kuwaelimisha Wananchi juu ya teknolojia rahisi ya kuvuna maji na kuyahifadhi kwa matumizi ya baadaye hasa kwa kuzingatia kwamba, itachukua muda mrefu kumpatia kila mwananchi maji ya bomba. Ni vizuri wataalam wakawafuata Wananchi Vijijini hasa Mikoa yenye ukame kuwafundisha jinsi ya kuvuna maji badala ya kutumia vipeperushi tu.

Mheshimiwa Spika, huduma ya maji ni muhimu na ni ghali, hata hivyo bado Wananchi walio wengi hawajatambua umuhimu wa kulipia huduma ya maji wanayotumia na hivyo kufanya wachache wanaolipia kutozwa gharama za juu. Kamati inaishauri Serikali kuweka kampeni maalum ya kuelimisha watu umuhimu wa kulipia maji. Aidha, Kamati inashauri Serikali kudhibiti utoboaji wa mabomba ya maji kiholela unaofanywa bila kibali kutoka kwa Mamlaka husika. Kuhusu mifumo ya maji taka Mijini, Kamati inashauri Serikali itengeneze mifumo hii ili kupunguza magonjwa ya kuambukiza yanayosababishwa na uchafuzi wa mazingira unaotokana na kutiririka maji ovyo yaliyo machafu.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vingi vya maji vimebaki ni vile vile kwa muda mrefu pamoja na kuwa idadi ya watu imeendelea kuongezeka na shughuli nyingi za kiuchumi zimekuwa zikipanuka. Kamati inaishauri Serikali kupanua wigo wa vyanzo vya maji badala ya kutumia vile vya zamani peke yake. Aidha, ili kuongeza kasi ya kutoa huduma ya maji nchini, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuangalia mfuko wa maji katika ngazi ya Taifa, ili uweze kugharamia miradi mikubwa ya maji katika maeneo mbalimbali. Pia, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha zaidi kwa ajili ya Sekta ya Maji ambayo ndiyo uhai wa kila kiumbe.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea *DAWASA* ilipewa taarifa kwamba, tayari mwekezaji amekwishapatikana, ambaye atatoa huduma ya maji katika Miji ya Dar es Salaam na kukusanya mapato yatakayotokana na huduma hiyo. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa hatua hiyo inayolenga kuboresha huduma ya maji Dar es Salaam na Miji midogo ya Kibaha na Bagamoyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu wafanyakazi wa *DAWASA*, Kamati ilielezwa kwamba, hatuna mfanyakazi atakayepunguzwa kutokana na zoezi hili la ubinafsishaji kwa utoaji wa huduma ya maji. Kamati inaishauri Serikali kuwaandikia barua wafanyakazi wote wa *DAWASA* kuwaeleza msimamo huo wa kutopunguzwa kazini ili kuondoa uwezekano wa kuzuka kwa mgogoro kati ya Mamlaka na wafanyakazi baada ya mwekezaji mpya kuanza kazi. Kuhusu uwekaji mita, Kamati inashauri kuondolewa kabisa kwa utaratibu wa sasa wa kumtaka mteja anayetaka kuweka maji kulipia fedha za mita. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, mita ya maji ni mali ya Mamlaka na siyo mali ya mteja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya tatu kwa wingi wa mifugo Barani Afrika, ikiwa na jumla ya ng'ombe milioni 17.7, mbuzi milioni 12.5 na kondoo milioni 3.5. Hata hivyo, idadi hiyo ya mifugo huchangia katika Pato la Taifa wastani mdogo wa Dola za Kimarekani milioni 7 kwa upande wa fedha za kigeni, fedha ambazo ni kidogo sana ukilinganisha na nchi ya Botswana ambayo ina ng'ombe milioni 2.5 na mazao yake ya mifugo huipatia nchi hiyo fedha za kigeni zipatazo Dola za Kimarekani milioni 600 kwa mwaka.

Hii inaonyesha kwamba kama Tanzania ingewekeza katika Sekta ya Mifugo kama ilivyo kwa nchi ya Botswana, mapato yetu ya fedha za kigeni yangekuwa mara sita ya mapato yanayopatikana Botswana kutokana na mazao ya mifugo, yaani Tanzania ingepata Dola za Kimarekani milioni 3,600 kwa mwaka. Kamati inaishauri Serikali kuchukua changamoto hiyo na kuweka haraka mkakati wa kuleta mapinduzi katika kuboresha Sekta ya Mifugo nchini.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina ardhi kubwa na inayofaa kwa kilimo na ufugaji kwa kuwa sehemu kubwa ya nchi inapata mvua za kutosha na kuna vyanzo vingi vya maji. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kutekeleza mpango wa kutenga maeneo ya ufugaji na kilimo kwa kuanzisha Kamati za kusimamia matumizi ya ardhi Vijijini kama ilivyoainishwa kwenye mkakati wa uendelezaji wa Sekta ya Mifugo. Ili kuharakisha mpango huu, Kamati inaishauri Wizara kuweka lengo na muda wa kukamilisha zoezi hili. Kamati inaamini kwamba itaondosha migogoro.

Mheshimiwa Spika, unapozungumzia kuboresha Sekta ya Mifugo, kimsingi unazungumzia kuboresha afya ya mifugo. Bila kuwa na utaratibu wa kudumu wa kuzuia maradhi ya mifugo ni vigumu sana kuinua uzalishaji unaotokana na Sekta hiyo. Kamati inaishauri Serikali kuongeza juhudi zaidi katika usimamiaji wa udhibiti wa magonjwa ya mifugo hasa katika chanjo za magonjwa ya milipuko, kuangalia uwezekano wa kutoa fidia pale mifugo inapochinjwa au kuangamizwa kutokana na magonjwa ya milipuko, kutenga maeneo yasiyokuwa na magonjwa kwa kuzungushia uzio wa kuzuia magonjwa na kuweka mfumo wa utambuzi wa mifugo nchini.

Ili kusimamia kwa ufanisi Sekta ya Mifugo nchini, Kamati inashauri kwamba, wataalam wa mifugo wawe wanasimamiwa moja kwa moja na Wizara badala ya utaratibu wa sasa ambao wataalam hao wanasimamiwa na Halmashauri za Wilaya au Miji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo ni sehemu mojawapo ambapo sera ya kuwezesha Wananchi inaweza kutekelezeka kwa ufanisi mkubwa kwa kuwa Wananchi wengi wana uzoefu wa masuala ya mifugo. Kwa kuzingatia ukweli huu, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu wa kuwawezesha wafugaji na wataalam wenye taaluma ya mifugo kuendesha shughuli za ufugaji kibiashara. Kwa kuanzia, Kamati inashauri kwamba, baadhi ya maeneo ya Ranchi za Taifa zinazobinafsishwa yatengwe kwa madhumuni ya kuwawezesha Wananchi hasa wenye utaalam wa mifugo kuendesha shughuli za mifugo kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafugaji nchini bado hawajaweza kunufaika ipasavyo na mifugo yao kutokana na kukosekana soko la uhakika la mifugo na mazao yake. Kwa kiasi kikubwa wafugaji wanategemea soko la ndani ambalo kwa kweli halitoi bei nzuri kutokana na ukweli kwamba, nguvu ya soko ni ndogo. Ili kuinua soko la mifugo hasa ng'ombe Kamati inashauri Serikali kuanzisha viwanda vya kusindika nyama ambazo baadaye vitabinafsishwa kwa kuwa siyo rahisi kwa sasa Sekta binafsi kuingia katika uwekezaji wa namna hii. Viwanda vya kusindika nyama vitaongeza thamani ya mazao ya mifugo na hivyo kumpatia mfugaji bei nzuri ya mifugo yake kwa kuzingatia kwamba biashara ya mifugo kwa sasa duniani ni biashara ya minofu. Kwa mfano, nchi ya Botswana inatumia teknolojia ya hali ya juu katika usindikaji wa nyama kiasi kwamba kila sehemu ya mnyama ni bidhaa safi, hakuna kinachopotea. Baadhi ya wataalam walioko huko ni wale waliotoka *Tanganyika Packers.*

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa maziwa nchini unakabiliwa na tatizo la soko hasa kutokana na kuwepo kwa ushindani mkubwa wa maziwa yanayoingizwa kutoka nchi za nje kiholela. Sehemu kubwa ya maziwa yanayoingizwa nchini yanatoka kwa nchi ambazo wazalishaji wake wanapewa ruzuku na Serikali. Ili kuongeza soko la maziwa yanayozalishwa hapa nchini na kuinua maisha ya wafugaji, Kamati inashauri kwamba: -

- Wenye viwanda vya maziwa wawezeshwe kwa kupewa mikopo ya riba nafuu ili waweze kununua mitambo inayoweza kuhifadhi maziwa yaliyosindikwa kwa muda mrefu. *(Makofi)*

- Serikali ihakikishe kwamba maziwa yanayoingizwa nchini yanadhibitiwa na yanalipiwa kodi zinazostahili badala ya kuacha yazagae tu.

- Wananchi wahamasishwe kunywa maziwa hasa wanafunzi shuleni kama mojawapo ya lishe bora mwilini. *(Makofi)*

- Wazalishaji wa maziwa humu nchini wapewe fursa na kipaumbele maalum cha kuuza maziwa katika Taasisi za Serikali hasa hospitalini, maofisini, mashuleni na kadhalika, badala ya Taasisi hizo kuwa na mazoea ya kununua maziwa yanayotoka nje ya nchi tu na hivyo kuwaacha Wananchi wetu bila soko la hakika la kuuza maziwa yanayotokana na mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, usafirishaji wa mifugo toka sehemu moja kwenda nyingine kwa kiasi kikubwa umechangia kuenea kwa magonjwa ya mifugo. Aidha, mifugo inaposwagwa kwa muda mrefu, huchoka sana na hata kupunguza ubora wake. Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu utakaowezesha utumiaji wa malori na treni wakati wa kusafirisha mifugo kwenda kwenye minada hasa iliyo mbali kama alivyosema Mheshimiwa Waziri hivi punde. Pia, Kamati inashauri kuanzisha minada mikubwa ya Kanda, badala ya kutegemea mnada wa Pugu peke yake. Uamuzi huo utasaidia kupunguza gharama za usafirishaji wa mifugo na pia utaongeza kipato cha mfugaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nchi yetu kuwa na mifugo mingi, bado ubora wa mifugo yetu uko chini sana kwa ufugaji wa kibiashara. Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu wa kuzalisha mbegu bora za mifugo na kuhamasisha Wananchi kubadilisha au kuchanganya mbegu ili kupata mifugo bora.

Ili kuweza kusimamia kikamilifu uzalishaji na ubora wa mifugo Vijijini, Kamati inashauri Wizara kuweka muundo utakaowezesha wataalam wa mifugo kuwatembelea wafugaji Vijijini ili kuwapa ushauri na kuhakikisha kwamba, wanazingatia misingi ya kitaalam katika ufugaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya maendeleo, bado kuna tatizo kubwa sana la kuweza kutekeleza miradi iliyoainishwa katika mpango wa maendeleo ya Wizara kutokana na kutegemea fedha za wafadhili. Katika Bajeti ya mwaka 2002/2003, Wizara hii ilitengewa fedha za maendeleo jumla ya Shilingi bilioni 37.87 na kati ya

hizo, Shilingi bilioni 34.1 ni fedha za nje ambayo ni sawa na asilimia 90 ya fedha zote za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Mei, 2003 kati ya shilingi bilioni 34.1 fedha za nje, ni Shilingi bilioni 1.2 tu sawa na asilimia 3.6 zilikuwa zimetolewa na kutumika kwenye miradi ya maendeleo.

Kwa maneno mengine ni kwamba, miradi ya maendeleo kwa Wizara hii ilitekelezwa kwa asilimia 3.2 tu ukijumlisha fedha za ndani na fedha za nje.

Kwa kuzingatia ukweli huu, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutenga fedha nyingi za ndani kwa ajili ya Sekta ya Maji na Mifugo badala ya kuwategemea wahisani kutoa fedha za kutekeleza karibu miradi yote ya maendeleo kwa Sekta hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati yangu, naunga mkono hoja ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MWADINI ABASS JECHA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO):** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vilivyomo ndani yake, kwa kutupa uhai na afya njema tukaweza kukutana hii leo ndani ya jengo hili kutekeleza wajibu wetu tukiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu. Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa mwaka wa fedha 2003/2004, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43 (5) (b) (c). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kutoa shukrani za pekee kwa wananchi wa Jimbo la Utaani, kwa hekima kubwa waliyonipa kwa kunichagua mimi kuwa Mbunge wao, katika uchaguzi mdogo uliofanyika Mei, 2003. Ninawaahidi kuwa nitaitumikia vyema nafasi hii waliyonipa kwa manufaa yao na kwa manufaa ya Watanzania wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mkosefu wa shukrani iwapo sitawashukuru Waheshimiwa Wabunge na wote wale ambao wamekuwa wakitupongeza sisi Wabunge wapya tuliojiunga na Bunge hili kupitia uchaguzi mdogo uliopita. Ninawaomba wapokee shukrani zetu za dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Naibu wake Mheshimiwa Anthony M. Diallo, Katibu Mkuu wa Wizara hii, pamoja na timu yake ya wataalam katika kuandaa na kuwasilisha Bajeti hii ambayo kwa namna moja au nyingine imejielekeza katika kupunguza kero kadhaa ambazo wananchi zinawasumbua. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, ajitahidi kadiri ya uwezo wake kuona kwamba yale yote aliyoahidi kuyatekeleza basi anayatekeleza ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie utangulizi wangu kwa kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi, pamoja na Wajumbe wake wote, kwa namna ambavyo wameandaa na kuwasilisha mapendekezo yao ambayo zaidi yamelenga katika kuboresha Bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kuchangia mambo muhimu yafuatayo katika Bajeti ya mwaka 2003/2004 kwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ni miongoni mwa Wizara muhimu ambazo shughuli zake zinamgusa kila Mtanzania, hivyo inabidi kutoa michango ya mawazo ili kuwezesha yale matatizo yanayoweza kurekebishwa, yarekebishwe na yale yanayoweza kuondolewa basi yaondolewe.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Wizara hii ina sekta kuu mbili ambazo ni Sekta Maji na Sekta ya Maendeleo ya Mifugo, Kambi ya Upinzani inatoa mchango wake kwa kila sekta kipekee.

Mheshimiwa Spika, sekta ya maji ni sekta ambayo shughuli zake zinamgusa kila Mtanzania awe wa kijijini au wa mjini. Hivyo ni sekta ambayo inabidi itazamwe kwa undani na umakini zaidi kwani athari itakayotokana na sekta hiyo kwa kutomudu shughuli zake inamuathiri kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, sekta ya maji ni nyenzo kubwa na muhimu sana katika suala zima la kupunguza umaskini hapa nchini. Kwani ni sekta ambayo inategemewa sana katika shughuli mbali mbali, iwe ni zile zinazotoa huduma kwa jamii au za Kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, Pia ninaipongeza Wizara kwa kufanikisha utekelezaji wa baadhi ya mambo muhimu yahusuyo Maji ambayo yameleta mafanikio mazuri, ikiwemo maandalizi ya Dira na mwelekeo wa Wizara juu ya Maji ambayo inasema: "Kuendeleza na kutunza raslimali ya Maji kwa ajili ya Maendeleo ya Jamii na Uchumi na kuzingatia hifadhi ya Mazingira". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa inajitahidi sana kuongeza Bajeti ya sekta ya Maji kila mwaka hasa kuanzia mwaka wa fedha 2001/2002, ambapo fedha za maji zilizotengwa zilikuwa Sh. bilioni 32.5, mwaka 2002/2003 shilingi bilioni 58.6 sawa na ongezeko la asilimia 80.3 na mwaka huu fedha inayoombwa ni shilingi bilioni 85.7 sawa na ongezeko la asilimia 46.3. Hii ni hatua nzuri ya kupongezwa. Aidha, Kambi ya Upinzani inaipongeza Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kuonyesha jitihada za kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama katika baadhi ya miji kama vile Manispaa ya Dodoma na kwingineko.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana Kambi ya Upinzani inahitaji kupata maelezo juu ya hatua iliyofikiwa katika kutatua mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tunaomba kupatiwa maelezo ni hatua zipi zimefikiwa na Serikali katika ule Mradi wa kuvuta Maji kutoka Ziwa Victoria na kupelekwa Mikoa ya Shinyanga, Tabora, Singida na Dodoma ili kuendeleza shughuli za Kilimo, kwani suala hili limezungumzwa tangu mwaka wa fedha wa 2000/2001 na utekelezaji wake hatujauona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mikoa nchini imezungukwa na mito, maziwa na mabwawa ya asili, huu ni utajiri mkubwa, lakini la kushangaza ni kuwa mpaka sasa Mikoa hiyo bado haijapatiwa maji safi na salama ya kutosha. Tunataka kujua Wizara ina mpango gani ulioandaliwa katika kuisaidia Mikoa hiyo kupata huduma ya Maji ambayo gharama yake itakuwa nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Kambi ya Upinzani inataka maelezo juu ya hatua za utekelezaji zilizofikiwa katika ujenzi wa bwawa la akiba katika Mto Ruvu litakalosaidia kutoa huduma ya Maji katika Jiji la Dar es Salaam, wakati wa kiangazi. Suala hili limewahi kuwasilishwa na Kambi ya Upinzani hapa Bungeni mwaka 1997. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya 2002/2003, Wizara Iliahidi kuunda Bodi za Mabonde za Mito, hatujui suala hilo limefikia wapi? Tunamwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anafanya majumuisho suala hili aligusie.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pia ingependa kupata ufafanuzi juu ya hatua ambazo Halmashauri za Wilaya, zimechukua katika ujengaji wa Mabwawa na Malambo ya Maji na uzuiaji wa uchafuzi wa vyanzo vya maji unaofanywa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, maji taka ni bidhaa ambayo inahitaji kufuatiliwa kwa makini sana na vyombo husika, kwani kutofuatiliwa kwa makini, madhara yake kwa jamii ni makubwa sana, hasa ukizingatia milipuko ya magonjwa ya binadamu kama vile kipindupindu, homa ya matumbo na kadhalika. Tunataka kujua ni hatua zipi Wizara imechukua kuweka mifumo mizuri wa Maji taka?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imepokea malalamiko ya ankara za Maji wanazotozwa wateja ni kubwa mno ukilinganisha na huduma ya Maji wanayopata. Aidha, kuna baadhi ya sehemu huduma ya Maji wanayopatiwa wateja hairidhishi. Kutokana na tatizo hilo imewafanya baadhi ya wateja kushindwa kulipia ankara zao za mwezi au kufanya baadhi yao kupata Maji kwa njia ya Wizi. Wateja wenye uwezo mkubwa wameamua kuchimba visima vyao kama hali ilivyojitokeza hivi kabuni katika Manispaa ya Dodoma. Mamlaka ya Maji safi na Maji Taka Dodoma *(DOWASA),* imepoteza wateja muhimu sana kama vile *VETA, CBE,* kwani wateja hao wameamua kuchimba visima vyao ili kuondokana gharama kubwa za huduma ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo ya Mamlaka za Maji kukimbiwa na wateja wao na hivyo kukosa mapato, Kambi ya Upinzani inataka kujua Wizara ina mpango gani wa kuangalia upya viwango vya ankara za maji

zinazotozwa kwa wateja wake. Kwani hatua za makusudi zisipochukuliwa, Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka Mijini zitashindwa kujiendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kutegemea mvua kuwa ndiyo chanzo kikuu cha maji kwa ajili ya matumzi ya kilimo limezua tatizo kubwa. Kwani katika miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia mvua katika sehemu nyingi hazinyeshi za kutosha hivyo, kusababisha upungufu mkubwa wa maji. Kutokana na hali hii tunaishauri Serikali kujishughulisha zaidi na uchimbaji wa mabwawa na visima virefu ili wananchi wapate maji ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya kilimo na shughuli nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, suala la kuvuna maji ya mvua ni teknolojia ambayo baadhi ya nchi zilizoendelea inaitegemea sana katika kupata maji ya kutumia kwa shughuli zao mbalimbali za kiuchumi. Ili Serikali ijikite vyema katika suala la uvunaji wa maji ya mvua, haina budi Serikali kuhakikisha kuwa teknolojia ya uvunaji wa Maji hayo inaimarishwa na kusambazwa kwa haraka kwenye maeneo mbalimbali hasa katika sehemu zile ambazo hupata mvua za muda mfupi kama vile Mikoa ya Dodoma, Singida na mingineyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaiomba Wizara kuongeza juhudi na nguvu zaidi katika ukarabati na upanuzi wa mitambo inayochuja maji safi na salama na kuyasambaza kwa watumiaji katika sehemu kubwa na kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuondoa tatizo la baadhi ya wananchi hasa vijijini ambao huharibu vyanzo vya Maji, Kambi ya Upinzani inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi hao juu ya faida ya kutunza mazingira na kutochafua vyanzo vya maji vilivyoko katika sehemu zao kwa manufaa yao na kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya kuendeleza Mifugo ni muhimu sana hapa nchini kwetu kwani asilimia 40 ya kaya za wakulima ni wafugaji. Vile vile Mifugo huchangia Mapato katika familia yatokanayo na bidhaa za Mifugo, chakula, usafiri na shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imeona kuwa yapo matatizo ambayo iwapo hatua madhubuti hazikuchukuliwa ipasavyo, maendeleo katika sekta hiyo yatakuwa si ya kuridhisha. Miongoni mwa mambo ambayo Kambi ya Upinzani inaona inafaa kutafutiwa ufumbuzi ni kutokana na kuwa sekta hii haina chombo maalum cha kutoa huduma ya mikopo kwa wafugaji. Kwani wafugaji iwapo watapatiwa mikopo yenye masharti nafuu, wataweza kugharamia shughuli za kuendeleza mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo pia inakabiliwa na tatizo la kutokuwepo na soko la uhakika la bidhaa zitokanazo na mifugo. Tunaishauri Serikali kuandaa miundombinu madhubuti ambayo itawahakikishia wafugaji kuuza bidhaa zao bila usumbufu na kwa bei nzuri. Tunachukua nafasi hii pia kuishukuru Serikali kwa kufuta kodi zote ambazo zimekuwa kero na kuwakandamiza Wakulima na Wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wafugaji wanatabia ya kuhamahama mara kwa mara kutokana na kutokuwepo sera nzuri ya kuwapatia ardhi ya kudumu au sehemu maalum kwa ajili ya malisho, hali ambayo wakati mwingine huleta migongano na wakulima wa mazao. Baadhi ya wakati wafugaji hunyanyaswa na wakulima. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Tawala za Mikao na Serikali za Mitaa, itenge maeneo maalum ya kudumu kwa ajili ya malisho ya mifugo *(Grazing Areas)*.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona ipo haja kwa Wizara hii kushirikiana na Wizara nyingine kuhamasisha wafugaji ili waunde Vyama vya Ushirika vya Mifugo ili kuwawezesha kutafuta masoko ya pamoja, kupata mikopo kwa urahisi na kutatuta matatizo yao kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, wafugaji walio wengi hawajapatiwa elimu ya kutosha kuendeleza Mifugo yao. Mara nyingi hutumia mbinu zao za asili walizorithi kutoka kwa wazazi wao. Wanakosa utalaam wa Kisasa wa Uzalishaji, hali hii husababisha maendeleo ya wafugaji wengi kuwa finyu. Kutokana na tatizo hilo, Wizara inashauriwa kufanya uchambuzi wa kina juu ya aina ya elimu ambayo ni muhimu kupatiwa wafugaji kwa kuzingatia aina ya mifugo waliyonayo, mazingira wanayoishi, hali ya soko ilivyo na mambo mengine kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wafugaji huona kumiliki mifugo mingi ni jambo zuri na ni utajiri mkubwa, bila ya kujali kuwa mifugo mingi inaweza kuleta athari kama vile uharibifu wa mazingira, magonjwa, upungufu wa sehemu za malisho, gharama za madawa na kadhalika. Wizara inashauriwa kubadilisha, haidhuru pole pole, mwelekeo wa wafugaji hao hasa wanaofuga mifugo ya kienyeji, kupunguza idadi na badala yake kununua mifugo michache yenye uzalishaji mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara nyingi Serikali imekuwa inaunda Bodi mbalimbali kusimamia uzalishaji hasa kwenye mazao ya kilimo, la kushangaza ni kwamba hadi hivi sasa Wizara haijaunda Bodi maalum ambayo itasimamia shughuli za wafugaji. Kuundwa kwa chombo hicho ni muhimu sana kwani kitakuwa kiungo kikubwa kati ya wafugaji na Serikali. Kukosekana kwa Bodi, shughuli za wafugaji zimekuwa zinaenda bila mwelekeo maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa kuwa na bodi inayohusu mifugo, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuangalia jinsi ya kuunda bodi ambayo itasimamia shughuli za mifugo, ili kuwaendeleza wafugaji na kukuza uzalishaji wa bidhaa za mifugo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafugaji wetu wanakabiliwa na shida ya kupata mahitaji yao ya dawa za mifugo. Kwani maduka mengi ya reja reja ya watu binafsi yamefunguliwa hasa sehemu za mijini. Maduka hayo huuza madawa kwa bei ya juu sana na baadhi ya wauza madawa huuza madawa ambayo muda wake wa kutumika umekwisha. Hali hiyo inaweza kuleta athari kubwa kwa wafugaji hatimaye kulikosesha Taifa pato litokanalo na bidhaa za mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na tatizo hilo la upatikanaji wa madawa ya mifugo kwa bei ya juu na katika hali isiyo salama, Kambi ya Upinzani inaishauri Wizara kusimamia vyema uagizaji na uingizaji wa madawa ya mifugo na ikiwezekana kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, kuangalia kodi zinazotozwa kwenye dawa za mifugo na ikibidi kodi zisizo za lazima zifutwe, ili kumpa unafuu mfugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa nchini mara kwa mara hupatikana taarifa za milipuko ya magonjwa ya mifugo kama sotoka, homa ya mapafu, ugonjwa wa miguu na midomo, *anthrax*, kichaa cha mbwa na kadhalika. Matukio hayo husababisha idadi kubwa ya mifugo kufa au kupoteza uwezo wa uzalishaji na kusababisha hasara kwa mfugaji. Serikali inaombwa kuchukua hatua madhubuti kuyakabili maradhi hayo ili kumpunguzia mfugaji gharama za uzalishaji na hatimaye kumwongezea kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba wafugaji wameenea katika Mikoa mingi ya Tanzania, lakini Serikali imejenga vituo vichache vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo. Mikoa mingi ambayo iko mbali na vituo hivyo inakosa huduma hizo za msingi kwa wafugaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwa vile tunaazimia kuinua Sekta ya Mifugo nchini, ni vyema Serikali ikaliangalia tatizo hilo ili vituo vingi vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo vikajengwa hasa katika Mikoa ile ambayo ina mifugo mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vyuo vya mifugo nchini viko vitano, lakini idadi ya wafugaji wanaopelekwa kwa mafunzo katika vyuo hivyo kwa mwaka ni wachache sana ukilinganisha na mahitaji. Aidha, vyuo hivyo huchukua idadi ndogo ya wanafunzi wanaohitaji kupatiwa utalaam wa ugani wa mifugo. Kwa mwelekeo huo idadi ya watalaam wa ugani vijijini haitaongezeka haraka.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wetu wanakabiliwa na tatizo sugu la ukosefu wa majosho na malambo kwa ajili ya kuoshea na kunywesha mifugo yao. Idadi ya majosho na malambo kwa ajili ya Mifugo ni machache. Aidha, majosho na malambo hayo yamejengwa sehemu za mbali kutoka waliko wafugaji wengi. Wizara inatakiwa kuliona hili na ifanye juhudi za makusudi za kujenga majosho na malambo ya kutosha karibu na maeneo ya wafugaji. Kwa yale majosho na malambo yaliyoharibika yafanyiwe ukarabati wa kutosha ili yaendelee kutoa huduma kwa wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa utaratibu wa kusambaza mifugo hasa ng’ombe wa kisasa katika Mikoa ya Kusini ikiwemo Lindi, Mtwara na Ruvuma. Kila mwaka iliamuliwa kupelekwa ng’ombe wapatao 90,000 katika Mikoa hiyo, lakini utekelezaji wa suala hilo hauendi vizuri. Aidha, idadi hiyo ya ng’ombe haikidhi haja

ukulinganisha na mahitaji halisi. Hivyo, Kambi ya Upinzani inaishauri Wizara na kwa kushirikiana na Sekta binafsi, iendeleze utaratibu huu wa kupeleka ng'ombe zaidi wa Kisasa katika Mikoa ya Kusini ili kutimiza lengo lililokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa maziwa ni mdogo sana ukilinganisha na idadi ya mifugo iliyopo nchini. Hata hivyo, kwa sehemu zile ambazo wanazalisha maziwa kwa wingi, maziwa hayo hayana soko la uhakika. Hali hii inatokana na kuwa Watanzania walio wengi hawana mwamko wa kutumia maziwa. Hali kadhalika masoko ya maziwa bado hayajaendelezwa. Kwa mfano, kila Mtanzania kwa wastani anatumia maziwa lita 50 tu kwa mwaka, ambayo ni sawa na wastani wa lita moja kwa wiki. Hiki ni kiwango cha chini sana. Ili kuondoa tatizo hilo tunaishauri Serikali kuhamasisha wafugaji kuzalisha maziwa mengi zaidi, lakini pia kupanua masoko ya ndani yenye uhakika.

Aidha, wananchi waelimishwe faida ya kutumia maziwa hasa yazalishwayo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hali ya uzalishaji wa chakula cha mifugo nchini haitoshelezi ukilinganisha na mahitaji ya vyakula hivyo. Katika Bajeti ya Wizara hii ya mwaka 2002/2003, takwimu za uzalishaji wa vyakula vya mifugo inaonyesha kwamba mwaka 2000/2001 tani 489,000 zilizalishwa, mwaka 2001/2002 tani 490,000 zilizalishwa na mwaka 2002/2003 tani 491,000.

Takwimu hizo zinaonyesha kuna ongezeko la tani 1,000 kila mwaka, ambalo ni sawa na asilimia 0.21, hilo ni ongezeko dogo sana halilingani na mahitaji ya ukuaji wa Sekta nzima ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kasi ndogo ya uzalishaji wa chakula cha mifugo, Kambi ya Upinzani inaiomba Serikali kuwahamasisha zaidi wazalishaji wa vyakula vya mifugo kuzalisha zaidi kwa kuwapunguzia kodi za mali ghafi wanazonunua kwa ajili ya uzalishaji. Hali kadhalika Wizara isimamie vyema uzalishaji wa vyakula vya mifugo ili viwe na ubora wa viwango kulingana na mahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, iliwahi kuzungumzwa hapa Bungeni katika Bajeti ya mwaka 2001/2002 kwamba, imeshindikana kubinafsishwa Ranchi za Taifa kutokana na tatizo la Hati Miliki. Kambi ya Upinzani inataka kujua ni hatua gani za ziada zimechukuliwa mpaka sasa kuona kuwa Ranchi hizo zinabinafsishwa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kumekuwa na wimbi kubwa la uingizaji wa vifaranga vya kuku kutoka nje ya nchi. Kwa bahati mbaya pameanza kujitokeza matatizo kadhaa. Miongoni mwa matatizo hayo ni kuua soko la vifaranga vinavyozalishwa ndani ya nchi. Lakini kubwa zaidi ni kuchipua na kuenea kwa maradhi mbalimbali ya kuku. Tunaishauri Wizara kufuatilia kwa karibu zaidi kuona kama kuna ulazima wa kuagiza vifaranga kutoka nje ya nchi, basi viwe na afya nzuri na viwe vimepatiwa chanjo muhimu za awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba wananchi wanafuga kwa kupata tija, upandishaji wa mifugo hasa ng'ombe na mbuzi uelekezwe katika kubadilisha damu ya kienyeji angalau kwa asilimia 50 mpaka 63. Aidha, vituo vya uzalishaji mbegu bora za mifugo viimarishwe na huduma ya upandishaji isambazwe zaidi.

Mheshimiwa Spika, sekta hii itaweza kufanikisha shughuli zake kama itakuwa na watendaji wa kutosha hasa wale ambao watakuwa karibu na wafugaji. Hivyo, ni vyema Wizara ikafanya jitihada maalum ya kuongeza wataalam zaidi wa ugani huko vijijini na Wilayani kwani huko ndiko waliko wafugaji ambao wanahitaji sana huduma za wataalam hao. Aidha, wataalamu hao wapatiwe usafiri utakaowawezesha kutoa huduma zao kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia mimi naamini kwamba lengo letu wote sisi Wabunge, ni kushirikiana kwa pamoja kwa nia ya kuleta maendeleo ya Taifa letu. Kwa msingi huo na kwa nia safi kabisa, napenda nieleze masikitiko yangu kwa jinsi ambavyo nimekosa ushirikiano na Mheshimiwa Edward Lowassa, katika muda wote tangu nilipopewa dhamana hii ya kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara hii, licha ya mimi kuchukua juhudi ya kujitambulisha kwake. Hali hii ni tofauti kabisa kwa Wasemaji Wakuu wenzangu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara nyingine, ambapo wanapata ushirikiano wa hali ya juu kutoka kwa Mawaziri husika. Mimi sioni kama itakuwa vyema iwapo nitaendelea kukosa ushirikiano wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa unaanza mjadala wa jumla. Nimepata maombi mengi ya Waheshimiwa Wabunge, wengine walishachangia mara mbili na zaidi. Napenda kuwataarifu kwamba, hawatapata nafasi, ambao hawajachangia na waliochangia mara moja tu wanatosha kabisa kumaliza muda uliotengwa. Kwa hiyo, naanza na ambao hawajachangia. Unaweza kuanza Mheshimiwa Major Jesse Makundi, unangoja kamera? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ili niwe mchangiaji wa kwanza katika Wizara hii nyeti ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Kabla sijatoa maoni yangu niliyonayo, naomba nichukue nafasi hii, kuwasalimu waajiri wangu wa Jimbo la Vunjo, nawasalimuni sana na nawatakieni kila la heri, kazi njema wananchi katika Kata za Kirua, Kilema, Marangu, Mamba Mwika, Himo, Makuyu na Kahe. Niwatakieni kila la heri na ufanisi tukizingatia kwamba, maji ni uhai na mifugo ni chakula bora. *(Makofi/Kicheko)*

Nimetembelea vijiji 68 kati ya vijiji 77 vya Jimbo la Vunjo tangu mwezi Machi mpaka nilipoingia hapa Bungeni kipindi hiki. Hakika wananchi wa Vunjo wanahitaji maji safi, maji ya kumwagilia mashamba, wanahitaji mifugo kwa ajili ya chakula bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza sana ndugu zangu wa Jimbo la Vunjo, kwa kujitahidi kulima kwa kiwango cha hali ya juu sana na Mwenyezi Mungu, ametubariki tumepata vyakula vingi sana mashambani kama vile mahindi na maharage. Vyakula kwa wastani ni neema ambayo tumepewa katika Jimbo la Vunjo, hakika nawatakia kila la kheri, watunze sana vyakula hivyo, waweke akiba ya kutosha na ile ya ziada wajitahidi kupata bei nzuri popote pale ili waweze kupeleka watoto wao shule, kupata fedha za tiba na mahitaji mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza Jimbo la Vunjo . Ninawatakia kila la kheri katika shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuchangia kinagaubaga hii Wizara nyeti ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasalimu wananchi wa Jimbo la Vunjo walionifikisha hapa, basi naomba nichangie Wizara hii lakini pia bila kusahau na kumtakia kila la kheri Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, ambaye yuko safarini Ulaya, ambaye ni Mwenyekiti wa *Tanzania Labour Party.* Tarehe 25 au 26 atawasili hapa nchini. Namtakia safari njema afike salama kwa sababu aliyekwenda kuchuma huko nje na kuleta huku nyumbani ndiye mtu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa hotuba yake nzuri sana yenye maelezo ya kina, yenye uchambuzi wa kila hali. Nina hakika Mheshimiwa Rais, amemchagua mtu ambaye nadhani taaluma yake hasa ukizingatia suala zima la Mifugo yeye ni Mmasai, sipendi kumtania, lakini naomba asijisikie vibaya wakati nikisema kwa kweli yeye ni Mmasai na sisi tunawategemea sana Wamasai kwa ajili ya kupata ng’ombe, nyama kwa ajili ya chakula bora. Mheshimiwa Waziri, kwa kweli anamudu hii Wizara kwa kiwango kikubwa sana. Hotuba yake inatudhihirishia, ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo letu sisi Wabunge hapa ni kuona kwamba, Mawaziri wetu wakifanya kazi zao vizuri na sisi tuwape yaliyo mazuri na pale ambapo wanakuwa na mapungufu Kambi ya Upinzani ni kama *side mirror* ya gari kuongoza ili wafanye vizuri zaidi hadi hapo watakapomaliza kazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na ufugaji. Masuala ya ufugaji yote yamezungumzwa na Kambi ya Upinzani katika hotuba yao, naomba Mheshimiwa Waziri, azingatie hayo. Lakini mimi linaloniumiza zaidi ni hii *VAT* ya Madawa ya Mifugo. *VAT* hii ni kubwa, nafikiri itakuwa ni vema akiiondoa hii *VAT* kwa sababu kama mifugo itatunzwa vizuri, itatoa nyama kwa wingi, maziwa kwa wingi, mayai kwa wingi, basi ina maana mazao haya yote yakiuzwa humo ndani kuna kodi kubwa sana. Kwa hiyo, itakuwa imejilipa yenyewe na *VAT* imekaa mahali pake. Naomba suala zima la *VAT* nalo liangaliwe ili tuweze kupata madawa ya kutibu mifugo yetu kwa bei nafuu ili kuongeza mifugo hii katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia vile vile sekta ya maji. Maji ni uhai na katika kutekeleza majukumu yangu katika Jimbo la Vunjo, nilichukua msahafu ambao niliupata kwa Mheshimiwa Rais, akifungua Bunge jipya

tarehe 20 Novemba, 2000 hapa Bungeni. Katika suala zima la maji, naomba kumnukuu kwa ruhusa yako, Amiri Jeshi Mkuu wangu, ambaye ni Rais wa Taifa hili alisema: "Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sera ya Maji nao upewe umuhimu unaostahili. Mamlaka za Maji katika ngazi mbalimbali zitapaswa kushirikisha nguvu za wananchi wenyewe katika usambazaji wa huduma hii. Kamati za Maji Vijijini na Mifuko ya Maji itaimarishwa na kuenezwa ili kujenga uwezo wa kuhimili gharama za utunzaji na utengenezaji wa miradi ya maji mara inapokamilika".

Mheshimiwa Spika, mara tu nilipopata agizo hili la Rais na Amiri Jeshi Mkuu, mimi kwa taaluma ni Mwanajeshi, nilikwenda kwenye Jimbo langu nikakuta kwamba hawana maji ya kutosha. Nikajiuliza kwa nini, nikagundua kwamba kuna wafanyakazi wachache sana wanaohudumia idara hii ya maji. Hili namwomba Mheshimiwa Waziri, aliwekee kipaumbele kwa kuwa katika Kata moja ambayo ni kubwa kutoka Kaskazini mpaka Kusini kuna mhudumu mmoja na huko anakokwenda kuhudumia hayo maji ni msituni zaidi ya kilometa 20. Hana uwezo wowote wa kufika huko, hana baiskeli, pikipiki hana chochote cha kumfikisha huko. Hivyo, anashindwa kutekeleza jukumu hili. Maji kwenye bomba yakikwama au yakikatika au bomba likipasuka, mpaka afike pale kulitengeneza inachukua muda mrefu na wananchi kuendelea kupata taabu.

Hivyo, naomba Mheshimiwa Waziri, aangalie uwezekano wa kuweka angalau wahudumu wawili wa maji katika kila Kata kuliko ilivyo hivi sasa. La Pili, ajaribu kuwapa nyenzo za kufanyia kazi, hii ni pamoja na usafiri angalau wa baiskeli, pikipiki, ni muhimu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuona maji hayapatikani kwa wananchi wangu, nilikwenda kule msituni kwenye vyanzo vya maji nikakuta kumbe vile vyanzo vya maji viliharibiwa wakati wa mvua za *El-Nino* mwaka 1997/98. Hakuna aliyefika kwenye vyanzo vya maji kuhakikisha kwamba vyanzo vile vinasafishwa na kuwekwa katika hali ya usafi inavyostahili.

Nilichukua vijana 5 nikafanya nao kazi kutoka mwezi Desemba, 2000 mpaka mwezi wa Septemba, 2001. Nilikuwa nawalipa kila siku shilingi 1,000/= kwa mwezi shilingi 30,000/= kutoka mfukoni mwangu. Kwa hiyo, watu watano shilingi 150,000/= zilikuwa zinanitoka nikisaidiana na yule wa Kata ambaye naye nilikuwa naangalia jinsi gani ya kumwezesha ili kazi ile iwe nzuri zaidi. Hatimaye maji yalifika kila mahali. Kwa upande wa Mwika yalifika maeneo ya Riata, Kileseu, Mawanjeni mpaka Lotima mpakani mwa Wilaya ya Mwanga, watu wakapata maji vizuri mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiingia upande wa Marangu, kujua kwa nini pale Himo Mjini hakuna maji ndipo nikaenda kwenye *intake* kule nikafungua yale maji na vijana wangu, nikaongozana nao mpaka Himo, sasa kuna maji mazuri pale himo. Ni juhudi hizo tunazofanya. Hii yote ni kumwezesha Waziri asipatwe na manung'uniko mengi kwa wananchi, kwa kuwa ni mimi Mbunge wao niweze kufanya kazi hii nikishirikiana na wananchi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipomaliza kazi hii nilijikuta niko Mahakama ya Mkuu wa Wilaya, kwenye Ofisi yake nikishitakiwa na Kampuni moja inayoitwa *Kili Water* na kwamba nimeingilia kazi zao na kwamba nimeharibu miundombinu na kwamba niache kazi yao mara moja. Kwa Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya nilisema nimekoma kama nilivyokoma kunyonya kwenye titi la mama yangu, kamwe sitaingilia tena. Niliacha hivyo hivyo. Lakini ilipofika mwezi wa Oktoba, 2001 maeneo yote hayana maji ya kutosha, maji ni ya mgao, ni shida mtindo mmoja hadi sasa. Mbaya zaidi hii Kampuni ya *Kili Water* imeingia ina umri wa miaka 10 Rombo na Mwika, lakini kwa miaka yote kumi hakuna matanki yaliyosafishwa hata kidogo. Yale matanki ni machafu kweli kweli na kwamba ukichota maji kule ukiyaangalia kwenye *glass* utaona viluilui na maji machafu hasa.

Mwezi Mei, tumekuwa na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya kwa maagizo ya Mkuu wa Mkoa ya kwamba aende na hawa watu wa *Kili Water* katika maeneo ya Mwika na kwingineko kuona nini cha kufanya ili kuboresha zaidi ile hali. Hakika tulifanya kazi hiyo vizuri, tulishirikiana nao. Wakawa wanaondoa vile vilula vyote asilimia 95. Kwa hiyo, watu walikuwa wanahangaika sana kwenda kutafuta maji waweze kusafirisha kahawa na yale maji wanayoyapata ni machache sana kiasi kwamba kahawa yenyewe haitakati na hivyo kahawa inakosa ubora. Wameanza sasa kutumia maji ya mto ambayo ukisafishia kahawa inanuka udongo kwa sababu kahawa ina uvutano sana na harufu mbalimbali, kwa hiyo ubora wa kahawa unashuka. Mbaya zaidi hawajarudishia vile vilula kama walivyopewa amri hiyo na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya. Hawajasafisha yale matanki mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema ya kutoa vile virula wamewekewa mita wale wenye maji nyumbani na matokeo yake Kitongoji kizima kinakwenda kuchukua maji kwa yule mwenye maji kule nyumbani. Bili ya maji inapanda, kwa mwezi shilingi 200,000/= au 300,000/= anashindwa kulipa hali inakuwa mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo na kwa vile hii Kampuni imekataa tu kwa makusudi kutekeleza wajibu wake, mimi naungana na Mheshimiwa John Magufuli, kwa kuwafukuza kazi makandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anasema mpaka Januari 2003 amefukuza makandarasi 115. Ni kwamba hawafai! Tukizingatia Kampuni ambazo zinaji-*register,* zinajua zinaweza kufanyakazi lakini haziwezi kufanya kazi za wananchi, hizo ni Kampuni uchwara. Hizo ni pamoja na *Kili Water.* Kwa hiyo, *Kili Water* haina manufaa kwetu. Lakini lengo zima la wafadhili ni zuri lakini yule aliyekabidhiwa ile kazi haijui na haithamini na haitekelezi kama yule mdhamini anavyopenda.

Kwa hiyo, inakuwa ni kero kwa wananchi na sio ubora wa yule mfadhili. Kero hii imechukua takriban miaka kumi. Viongozi wote wa Wilaya na Mkoa na Waziri mwenyewe alikuwa Mheshimiwa Pius Ng'wandu, wakati ule, amesuluhisha imeshindikana na hawataki kutengeneza *associations* za maji katika hivi Vijiji. Kamati za maji hakuna, katika Vijiji vile.

Kwa hiyo, ni kero tupu. Kwa hali hiyo, hii yamkiniki kwenye Wilaya nyingine na Majimbo mengine hali hii iko hivyo hivyo. Hili ni jambo la kutupiwa macho, la sivyo tutakuwa tumewaajiri watu kufanya kazi ile na hawawezi kufanya kazi hiyo vizuri. Kwa hiyo, kuanzia sasa, suala la *Kili Water* nimemalizana nalo na sitaki kuwaona.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya yote, naunga mkono hoja kwa asilimia mia. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa *DAWASA,* Mheshimiwa Mohamed na vijana wake pale Ubungo kwenye Idara ya Uchimbaji Visima kwa kazi nzuri ambayo wanafanya katika Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea kwanza naomba na mimi niungane na wenzangu kwa kuwapongeza Wabunge wapya waliochaguliwa hivi karibuni ambao ni Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Abu Kiwanga na Mheshimiwa Sumri Mohamed, wote Wabunge wa CCM. *(Makofi)*

Pia ningependa kutoa pongezi kwa Waheshimiwa wote walioshinda kupitia Chama cha *CUF.* Hongera sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia hoja hii kwa kuiunga mkono mia kwa mia. Lakini kama nilivyosema hapo awali, kwamba naomba nizungumzie maeneo mbalimbali. La kwanza ni eneo la elimu. Wote tunaisifia sana hii elimu mpya ya *MEMM and MMES,* lakini mimi nina wasiwasi kwamba tunaposema watoto wapate elimu ya msingi mpaka Darasa la Saba halafu waachiwe kufanya vitu vyao nadhani sio sahihi kwa sababu wote tunajua kwamba umri wao unabaki ni umri mdogo mno kwa kuweza kujitegemea na kuweza kukabiliana na ulimwengu wa leo.

Kwa hiyo, ningependekeza na kuiomba Serikali ianze kufikiria na labda wamekwishafikiria, kuhakikisha kwamba vijana wetu wanawezeshwa kufika hadi Darasa la 12, yaani *Form IV* kwani wakipata elimu hiyo, basi watakuwa na uelewa mkubwa zaidi wa kukabili maisha yao na kujiendeleza wao wenyewe na hata kujiajiri wao wenyewe. Vinginevyo wakimaliza Darasa la Saba wanakuwa bado ni wale watoto wenye umri wa miaka 14, ni wadogo sana hawawezi kumudu maisha yao. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ifikirie uwezekano wa kuongeza elimu ya lazima kutoka Darasa la Saba hadi *Form Four* ili vijana wetu waweze kuwa wamekomaa kidogo na kuweza kujiendeleza kimaisha.

Mheshimiwa Spika, sasa nigusie haraka haraka tena kwamba Serikali imetamka mara kwa mara hasa Waziri wa Afya, Naibu na wengi wamezungumza hapa kuhusu kuwasamehe akina mama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano na wazee wale ambao hawana uwezo wa kuchangia gharama za Hospitali.

Nashukuru kwamba Muhimbili inapata ripoti kwamba baadhi ya wazee wakienda pale akinamama wanapewa msaada huo, lakini bahati mbaya Muhimbili hiyo hiyo na Hospitali ya Mwananyamala akinamama wajawazito, watoto chini ya miaka mitano, wazee na wale ambao hawana uwezo wa kuchangia bado wananyanyaswa sana wanapokwenda kuomba matibabu ya bure kwa vile hawana uwezo wa kuchangia. Naomba Serikali ilitazame hili.

Lakini lingine pia ni kuhusu wagonjwa ambao wamekuwa ni wa maradhi mbalimbali. Pale Mwananyamala mpaka hivi sasa nimepata ripoti ya kwamba wagonjwa wawili au watatu wa magonjwa mbalimbali huwa wanalalia kitanda kimoja au godoro moja. Kwa kweli nasema hali hii haikubaliki. Tunaomba Wizara au Serikali ijaribu kulitazama hili na kutafuta ufumbuzi wa kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hilo niende haraka haraka kwenye eneo ambalo nilileta swali langu hapa juzi kuhusu wakazi wa mabondeni. Niliomba hapa kwamba tunaomba sisi wakazi wa Mabondeni Kigogo, Mzimuni, Magomeni na Kigogo kwamba tupate nafasi ya kuzungumza na Serikali. Sisi hatutaki kupambana na Serikali. Tunachosema, tukae tuelimishane. Tutoe mawazo yetu, Serikali isikie mawazo yetu, lakini tukae kama wanandugu, Watanzania, tuweze kuzungumza bila kuanza kutishiana au kutumia mabavu kusema tutawapeleka Mahakamani na hizi kesi hatuzitoi. Naomba kwa dhati kabisa kwamba tukae pamoja. Ni uungwana tu. Tukae pamoja tuzungumze namna ya kutatua haya matatizo. Lakini sio hilo, naambiwa pia kwamba kuna Shirika la Umoja wa Mataifa la *Habitat* ambalo wana uwezo wa kutusaidia sisi kuboresha maeneo fulani fulani katika maeneo ambayo kuna watu wengi zaidi. Sasa kwa nini tusiwatumie hao? Serikali ina uwezo wa kuomba Shirika hili litusaidie kwa kuwanusuru wananchi wake katika maeneo hayo ya mabondeni.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niendelee kuzungumzia suala la Waheshimiwa Madiwani. Katika vikao vyetu mbalimbali kwenye Manispaa, Madiwani wa Kitanzania wako tofauti sana na Madiwani wa kwa mfano Uingereza na sehemu nyingine. Diwani wa Uingereza ni mtu ambaye amejiajiri mwenyewe, ana uwezo.

Kwa hiyo, anapofanya kazi ya Udiwani kwenye Manispaa ni kama *Civic Duty* ambayo haina malipo kwake. Ni sifa tu ya kuwa Msaidizi. Lakini kwa Tanzania na hali yetu ya sasa hivi, Mheshimiwa Diwani ni mtu ambaye anafanya kazi yake kwa saa nyingi tu. Kwa hiyo, tunasema wanapoomba misaada kwa mfano kusamehewa kodi ya kununua magari, basi Serikali iwafikirie....

**SPIKA:** Kwa kuwa unachangia Wizara nyingine na sio hii iliyoko mbele yetu, hakuna Waziri atakayekujibu. Ni bora uchangie Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. *(Kicheko)*

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, nilifikiri hutanipata. Umeninasa vizuri sana. Ahsante. Nilikuwa nikifanya ujanja ujanja kidogo lakini samahani sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niendelee kuhusu mchango wa maji. Hapa umenibana kweli! Kwa sababu nilikuwa nimejiandaa.... lakini nitaendelea. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hili suala la maji. Kwanza ningependa kama nilivyosema hapo awali kwamba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, Katibu Mkuu na Wakurugenzi. Nadhani kwamba Dar es Salaam na hasa kwa Jimbo la Kinondoni ni Jimbo ambalo limepata Visima vingi sana vya kusaidia kupata maji safi na salama japokuwa baadhi ya Visima maji yake si salama. Lakini huko nyuma nilikuwa nimemwandikia Mheshimiwa Waziri barua na ninaomba anifikirie kwa hayo niliyomwomba.

Nilisema kwamba kuna maeneo ambayo hayana maji safi na salama kwa kipindi cha karibu miaka saba mpaka miaka 12. Kwa mfano Tandale, Tandale Kwatumbo, Mashuka, Mkunduge, Mhalitani, Mtoyole, Sokoni, Mwananyamala Kisiwani maji bado hayajafika kwenye Kituo cha mwisho pamoja na Mchangani. Kwa hiyo, naomba utusaidie kulifikisha huko. *(Makofi)*

Halafu kuna Ndugumbi Makumbusho, Ndugumbi Mpakani, Ndugumbi Kisiwani, Makurumura, Mzimuni, Mtambani, Kigogo, Magomeni, Kijitonyama Mpakani 'A' na Mpakani 'B', Alimaua 'A' na 'B', Mwenge Kijijini na Nzasa, Mwananyamala Kinondoni na Hananasif. Hayo ni maeneo ambayo mpaka sasa wananchi wanalia na

Serikali yao kwamba wanaomba wapatiwe maji safi na salama. Kwa sasa hivi wanachofanya ni kununua maji kutoka kwa baadhi ya wawekezaji fulani ambao sijui wanapataje haya maji lakini wanawauzia wananchi maji kutoka kwenye *reservoir* zao wenyewe, lakini mwananchi hawezi kupata maji safi na salama kutoka bomba la *DAWASA.*

Mheshimiwa Spika, naomba sana Waziri atakapokuwa anajumuisha, basi ningependa anipatie maelezo, majibu kwa vile wamekuja hawa wakala wa *City Water Services Limited,* naomba basi ombi langu lipitishwe kwao na waanze kutusaidia, vinginevyo kwa kweli naogopa kwamba 2004/2005 na Chama changu kinaweza kukosa nafasi pale.

Kwa hiyo, naomba sana watusaidie. Lakini hiyo sio sababu kubwa, maana kubwa ni kwamba wananchi kwa kweli wameteswa kwa kipindi kirefu sana, tunaomba wasaidiwe kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nitoe shukurani zangu tena kwa viongozi wote wa Serikalini na *DAWASA* katika Wizara hii, Wakurugenzi, ningependa tu niwataje kwa majina, Mheshimiwa Arcado Muttalemwa, kuna Bwana Mohamed, kule kwenye eneo la Visima kijana anaitwa Songea, wote hawa wamenipa msaada wa hali ya juu sana kwa kutusikiliza katika matatizo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Naibu wake, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu na timu yake yote kwa kuandaa hotuba hii nzuri na ambayo tumeielewa. Hivyo basi, naomba niseme kwamba naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Arumeru Magharibi, napenda kuipongeza Serikali kwa kuondoa kero mbalimbali. Kuondoa ada ya Shule za Msingi, kufuta kodi ya maendeleo na kufuta kodi ya mifugo. Naomba niipongeze sana Serikali kwa niaba ya wananchi wangu wa Arumeru. Aidha, wananchi wangu wa Arumeru wanaishukuru Serikali yao kwa kuwasaidia fedha za kuchimba malambo matano katika kipindi cha mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizidi kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri ambayo inafanya kujitahidi kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama katika sehemu mbalimbali hapa nchini. Lakini pia naomba niseme kwamba licha ya juhudi hizi nzuri za Serikali, bado tuna matatizo makubwa ya uhaba na ukosefu wa maji kwenye sehemu mbalimbali za nchi yetu ikiwemo Vijijini na Mijini.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu uhaba wa maji katika sehemu mbalimbali. Pamoja na kwamba Serikali inajitahidi kuboresha upatikanaji wa maji, kuna uhaba mkubwa sana wa maji katika sehemu mbalimbali. Yaelekea jukumu la kuwapatia wananchi maji safi na salama katika nchi yetu umekuwa mkubwa sana kuliko uwezo wa Serikali. Hivyo basi, nashauri kwamba kuna haja ya Serikali kutazama upya uzito wa jukumu hili kwa nia ya kuainisha mikakati mipya ya kufanikisha jitihada hizi.

Mheshimiwa Spika, moja ya mikakati ambayo nilikuwa nashauri ni kwamba Serikali itazame upya jinsi ya kuanzisha mfuko maalum wa maji katika ngazi ya Taifa kama ilivyofanya katika huduma nyingine za jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie matatizo ya maji katika Jimbo langu la uchaguzi. Katika Jimbo langu la Uchaguzi la Arumeru Magharibi, tuna uhaba mkubwa wa maji katika sehemu mbalimbali. Lakini ningetaka sasa hivi kusisitiza tatizo la uhaba wa maji katika Kata za Musa, Kisongo, Mateves na Sokon 2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kata hizi katika nyakati mbalimbali wameomba Serikali yao iwasaidie waweze kupata maji safi na salama. Lakini kila wakati niseme kwamba Serikali imetujibu kwamba tusubiri tupate Wahisani. Kwa sababu ya hali yenyewe, tumekubaliana na maelezo ya Serikali, lakini kwa sasa hivi tunaomba basi, wakati tukisubiri kupatikana kwa Wahisani ama wafadhili Serikali itusaidie kufufua malambo yafuatayo:-

Malambo ya Oleitushula, Olovoni, Kisongo na Mateves ili kupunguza ukali wa uhaba wa maji katika Tarafa hiyo ya Mukulat.

Mheshimiwa Spika, nimkumbushe Mheshimiwa Waziri ahadi ya Serikali katika jibu la swali langu Na.144 la tarehe Mosi Julai, 2003 inayohusu matatizo ya maji katika Vijiji vya Oljoro Vusi na Oleitushula. Naomba baadaye wakati atakapokuwa ana-*windup* hoja yake, akumbuke ahadi hiyo ambayo Serikali imetupa wananchi wa Arumeru.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu huduma za mifugo. Kwanza kabisa naomba nizungumzie ukosefu wa huduma za majosho. Majosho mengi katika sehemu nyingi za wafugaji, yamekufa kabisa. Huduma hii haipo kabisa na kutokuwa na majosho kwa kweli kuanaathiri kwa kiasi kikubwa tiba bora ya mifugo katika sehemu mbalimbali nchini kwetu. Ningeshauri Serikali iwasaidie wananchi wafugaji kufufua majosho mbalimbali ili tuweze kupata huduma hii ya kuosha mifugo yetu. Kama hiyo haitawezekana kutoka kwenye Serikali Kuu, basi Serikali iagize Halmashauri zetu zitoe huduma hii ya kufufua haya majosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu kuboresha mifugo. Mifugo mingi katika nchi yetu ni mifugo ya jadi, ni mifugo ya asili. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri ametueleza kwa kifupi kwamba Serikali inajitahidi kuboresha mifugo hapa nchini, ningeomba kasi ya uboreshaji huo iwepo ili kuhakikisha kwamba tuna mifugo bora hapa nchini ambayo inakidhi haja ya soko huria na pia itamwongezea mfugaji tija na atakuwa kwenye hali nzuri ya ushindani kwenye soko huria.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu Mfuko wa Pembejeo za kilimo na mifugo. Serikali ilianzisha Mfuko wa Pembejeo za Kilimo na Mifugo. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake naona hajagusia kabisa sehemu hii ya Mfuko wa Pembejeo katika Sekta yake ya Mifugo. Hapa kuna mambo mawili ambayo nataka kuyazungumzia. Moja ni kwamba, mfuko huu licha ya kwamba ni wa Pembejeo za Kilimo na Mifugo, lakini sasa hivi naona uko chini ya Wizara moja tu ya Kilimo. Mfuko huu kiutendaji kama unahusu Wizara mbili, basi ni vyema kila Wizara ipewe mfuko wake ili wadau wa mifuko yote miwili waweze kuhudumiwa vizuri katika kila Wizara ambayo inahusika.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, ningemwomba pia atueleze ni kwa nini mfuko huu usigawanywe katika Wizara zote mbili.

Naomba pia nimwulize Mheshimiwa Waziri na hasa hasa ningeweza kumwuliza pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba kwa nini Mfuko huu wa Pembejeo umepewa Benki ya *Exim* kusambaza fedha hizi wakati Benki ya *Exim* haina mtandao katika Wilaya mbalimbali na Mikoa mbalimbali hapa nchini. Je, Serikali haioni kwamba ni vizuri kwa hali ya sasa Mfuko huu wangepewa *National Micro Finance Bank* ambao wana mtandao mkubwa sana katika Wilaya mbalimbali na katika mahali pengine katika Vijiji mbalimbali ili waweze kutoa huduma hii ya kusambaza fedha hizi za pembejeo sehemu mbalimbali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie juu ya ubinafsishaji wa Ranchi za Taifa. Mwaka 2002 Mheshimiwa Waziri alitangaza azma ya Serikali kwamba wananchi watagawanyiwa Ranchi za Taifa ili waweze kuendeleza ufugaji wa kibiashara katika sehemu mbalimbali. Leo tena Mheshimiwa Waziri amerudia azma hiyo ya Serikali. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri kwamba mpango huu mzuri ambao una matumaini makubwa sana kwa wananchi wa Tanzania unaanza kutekelezwa lini na utaratibu utakuwa upi?

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache naomba nimalizie kwa kuunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. Kabla ya yote napenda kwa dhati nimpongeze Mheshimiwa Waziri Edward Lowassa, kwa jitihada anazozifanya akiwa na Naibu wake na Katibu Mkuu pamoja na watumishi ndani ya Wizara. Kwa kweli wanajitahidi kufanya kazi zao kwa nia nzuri na tuna imani kabisa tukiwapa kila aina ya msaada watafanya zaidi kuliko wanavyofanya hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nitakuwa na hoja mbili. Hoja ya kwanza ambayo nitapenda Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono, natarajia kuleta hoja binafsi ya kuiomba Serikali kwa dhati kabisa na kwa sababu nitakazozitoa kuanzisha Mfuko wa Maji Kitaifa. *(Makofi)*

La pili, hili niombe kwa Mheshimiwa Rais, nimekuwa nikirudia mara kwa mara ya kwamba kutokana na uzito wa suala zima la maji, ipo haja ya kuwa na Wizara peke yake ya Maji na nitatoa sababu zake.

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu ya kwamba kuwa na mfuko wa maji, huwezi kuuanzisha bila sababu. Mimi ninazo sababu kama kumi, nitazitaja chache.

Kwanza, fedha zinazotolewa kwa ajili ya maendeleo kwa suala zima la maji kwa Tanzania, ni kidogo sana. Wote mkiangalia, asilimia tatu, utafanya nini na asilimia tatu? Ukiangalia katika jedwali ambalo Mheshimiwa Waziri ametupatia, viporo peke yake vinavyohitaji fedha, ni zaidi ya 700. Lakini kwa sasa fedha walizopewa ni bilioni 1.3 kati ya Shilingi bilioni 45 zilizokuwa zimeombwa. Ni asilimia ngapi? 0.25, huwezi kufanya lolote na fedha hizo. Lakini pia tunaambiwa katika mikakati ya Taifa ya kuondoa umaskini ambayo imesema kabisa, huwezi kuondoa umaskini kama hutahakikisha kwamba wananchi wanapata maji safi katika maeneo yote. Huwezi! Hilo ni vizuri tukalielewa, umasikini hautakwisha bila maji. Maji ni msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni nani kati yetu ambaye aliwahi kufikiria kwamba bei ya maji itafikia sawa na bei ya soda au sawa na bia? Nani katika maisha yetu tulitegemea? Ndio huko tunakokwenda. Bei ya maji katika baadhi ya hoteli, chupa moja ya nusu lita ni *five hundred shillings* mpaka shilingi 1,000/=, maji hayo! Ni nani kati yetu ambaye aliwahi kutegemea wanaume tutakuwa tunateka maji? *(Makofi)*

Maji yameanza kuwa ni biashara na mwanaume ukiona anateka maji ni biashara hapeleki nyumbani. Ni nani kati yetu ambaye hajui ya kwamba ugomvi kati Israel na Jordan ni maji? Nani hajui ya kwamba Ethiopia na Misri walishika mpaka silaha kwa ajili ya maji? Nani hajui ugomvi kati ya wafugaji na wakulima wa mipunga wanavyogombana kila siku? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani ni vizuri tuliangalie suala zima. Serikali yetu kwa zaidi ya miaka 40 imekuwa ikijaribu kutumia maji ya *Lake Victoria* lakini inakuwa na kigugumizi kwa sababu ya hayo matatizo ambayo wenzetu wanayaona yanaweza kutokea, suala ni maji. Nataka niombe ya kwamba umuhimu wa maji wote tunaufahamu na wataalam wanatuambia. Ndiyo nimesema ni vizuri tukawa na Mfuko wa Maji.

Wataalam wanatuambia, asilimia 70 au 80 ya mwili wetu ni maji. Ukipungukiwa na asilimia moja unapata kiu. Ukipungukiwa na asilimia 10 una-*collapse* hata kufa, hiyo ndiyo tunaanzia hapo. Kwa sababu ni vizuri haya maji tukaja tukachukulia kama jambo la kawaida. Mimi ninavyoliangalia katika miaka ijayo tunaweza kuwa na matatizo makubwa sana. Je, ni nani hajui ya kwamba sasa mji wa Dar es Salaam pamoja na ongezeko la idadi ya watu wanaotumia maji safi inazidi kupungua mwaka hadi mwaka? *(Makofi)*

Vijijini ndiyo mbaya zaidi. Nilikuwa nazipitia takwimu hizi. Lindi Vijijini ni asilimia 11.3 *after forty years of independence,* asilimia 11. Sumbawanga angalau Rukwa, tuko asilimia 47. Lakini baadhi ya miradi iliyonayo karibuni mingi imekufa. Huko ndiyo tunakoelekea. Nini tufanye?

Mheshimiwa Spika, hali ya maji safi duniani si nzuri. Wataalam wanatabiri ya kwamba mwaka 2025 zaidi ya nchi 48 duniani zitakuwa na upungufu mkubwa wa maji na watu asilimia 35 wataathirika. Mwaka 2025 si mbali kutoka sasa. Je, kwa hali hii tutaendelea mpaka lini? Mimi naogopa sana. Matumizi ya maji kwa mwaka 1940 kufuatana na takwimu tulizokuwa nazo ilikuwa ni asilimia moja kwa mwaka. Sasa tunafikia asilimia nne mpaka nane kwa mwaka. Maana yake ukichukua hesabu hizo peke yake bado athari ni kubwa sana mbele yetu na si ajabu baada ya miaka 25 tutazungumza lugha nyingine hapa. Nini tufanye? Ni vizuri tukajiandaa upya na kuiangalia sasa Sera yetu, tukaiangalia kama itajibu baadhi ya haya ambayo tunatarajia yatajitokeza.

Mheshimiwa Spika, umwagiliaji wa mashambani, tunaambiwa asilimia 30 inapotea kabla haijafika kwenye mazao. Tunaambiwa pia maji mengi ya viwandani yanapotumika yanakwenda kwenye mito, yanazidi kuchafua. Tunaambiwa pia na sisi ambao tunatumia *flash toilets* kwa haja ndogo tu unatumia lita tano, una-*flash five litres* zitakwenda tu, *Technology* haijaingia. Maji ya bomba mijini asilimia mpaka 40, 30 yanapotea njiani. Tunapewa taarifa ya kwamba mji ulioendelea kama Geneva, Geneva peke yake asilimia 13 ya maji hupotea njiani. Sisi je? India ni asilimia 40. Sisi je, wataalam watusaidie, hali si nzuri. *(Makofi)*

Sasa nini tunajaribu, Mataifa yamekutana na yamejadiliana na Mheshimiwa Waziri, juzi ulikuwa kwenye mkutano Afrika Kusini kuhusu suala la maji. Mataifa yata-*sympathize* na sisi. Lakini hayawezi ku-*empathize* na sisi. Kiingereza maana ya ku-*sympathize* ni kule kusema pole, poleni. Lakini ku-*empathize* ni kule kujifanya tatizo hilo ni lako pia.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1977 walikuwa na mkutano Argentina, wakafanya kazi nzuri sana. Mwaka 1990 New Delhi wakafanya mkutano. Mwaka 1992 Iceland, mwaka 1997 kulikuwa *UN Conference* juu ya maji, mwaka 2002 huko Cape Town, wote wanazungumzia juu ya maji, maji, maji, maji. Lakini bado viporo vinazidi kuendelea. *For how long* tutaendelea na hali hii. Hatuna haja ya kuwasubiri hao. Ndio maana nikasema tunahitaji kitu kinaitwa *Blue Revolution. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Blue Revolution* ni sawa ni ile ya India walikuwa na *Green Revolution. Green Revolution* walileta mapinduzi katika kilimo, wakawa na mazao ambayo wanazalisha maradufu mpunga. Sisi tutake *Blue Revolution* ya maji na hiyo, nitaomba kabisa Waheshimiwa Wabunge tusaidiane, tunaweza kuamua kwa kusimamia vizuri maji kidogo tuliyonayo kwanza na pa kupunguza kasi ya ongezeko la watu. Nitaendelea kulisemea hilo, kadri watu wanavyozidi kuongezeka tutake tusitake mahitaji yetu yataongezeka ya maji.

Lakini pia tuamue kwa dhati kuwa miradi ya maji kwa kweli lazima ipewe kipaumbele. Kipewe umuhimu wake wa pekee. Nasema hakuna mtu yoyote ambaye anaweza kuishi kwa siku zaidi ya tatu, nne bila maji. Tunaweza kukosa vitu vingine lakini maji ukikosa ndiyo mwisho. Hilo nilidhani ni vizuri tukaanza kulifikiria kwa sababu litatuwezesha angalau tukawa na fedha ambazo zitamsaidia Mheshimiwa Waziri katika baadhi ya miradi hasa ile mikubwa mikubwa ili angalau aweze kufanya kazi yake kwa misingi ambayo tunakubaliana ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri waliangalie hilo upande wa Serikali waone kama tunaweza kuanzisha miradi au tukawa na Mfuko Maalum ambao unazungumzia suala zima la maji, kma tulivyoanzisha Mfuko wa Elimu au mfuko ule ambao unashughulikia Vyuo vya Ufundi wa maji nao tungeweza kuuanzisha kwa makusudi mazima.

Baada ya kusema hayo, la pili, Mheshimiwa Waziri nitaomba anapofanya *winding up,* anisaidie sana kunipa maelezo bayana kuhusiana na maji katika mji wetu wa Sumbawanga. Kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitatu mfululizo tumekuwa tukizungumzia suala la upungufu wa maji katika mji wa Sumbawanga na hotuba zote kuanzia za mwaka 1998 zimekuwa zikitoa ahadi kuhusiana na mipango mbalimbali ya mji wa Sumbawanga. Leo sioni mahali popote, nini tatizo? Nitapenda maelezo, kwa sababu linasaidia, tujue na wananchi wajue kuna kitu gani kinafanyika. Jitihada za Mheshimiwa Waziri ni zipi? Amekwama wapi? Ni vizuri wananchi wetu wakaelewa.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana wakati mwingine tatizo tunapoomba tupate misaada kutoka kwa Wahisani. Wote mmejionea Wahisani kwa suala la maji, wanaweza kuwa hawalichukulii *very serious,* lakini lazima tuwe na misingi yetu wenyewe ambao tunaweza kusema Mheshimiwa Waziri sasa una fedha mahali fulani ondoa. Fedha za Wahisani huwezi kutegemea sana.

Mheshimiwa Waziri, naomba nipate mawazo tu, mmefikia wapi namna ya kusaidia Halmashauri yetu ya Mji wa Sumbawanga angalau wakawa na miradi ya kuweza kujitahidi chini ya ya uongozi wa Ndugu Shirima ambaye anajitahidi sana. Ni Meneja wetu anafanya kazi nzuri sana. Sasa mtusaidie tufanye kazi vizuri ili malengo yetu yaweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijiji vinavyozunguka Halmashauri ya Mji, havina msaada wowote. Tangu tuanzishe Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka katika Halmashauri ya Mji wa Sumbawanga sasa vimebaki peke yake. Tulikuwa na mipango ya *project* maalum kwa ajili ya maeneo yote ya Pito, Wipanga na Matanga lakini mpaka sasa hakuna lolote linalofanyika. Mheshimiwa Waziri unatusaidia nini katika vijiji ambavyo viko nje ya Mamlaka tulizoziteua ama sivyo wanabaki hawana msaada wowote.

Pia Shule zetu za Msingi zimekuwa na matatizo hasa shule zile ambazo zina watoto wengi. Unakuta bili zao za maji sasa zinaanza kupanda na hatari iliyopo katika shule za Msingi walimu wataanza kufunga maji, kwa kuogopa kulipa gharama na ni hatari kwa watoto wetu wa shule. Hivi kwa nini kusiwe na utaratibu maagizo

yakatolewa ili shule zote za msingi kwa ajili ya umuhimu wa watoto kunywa maji wakapata angalau *flat rate* wakachangia kwa kiwango fulani, kuliko kuwawekea mita na watoto wenyewe wakashindwa hata kuweza kulipia gharama hizo. *(Makofi)*

Mwisho, ningemwomba Mheshimiwa Waziri, katika Bajeti inayofuata, muangalie sana hii taarifa ya *Human Development Index* ya mwaka 2002 na uone namna sasa ya kutumia taarifa hiyo katika kuandaa Bajeti ya mwaka huo unaofuata. Itatusaidia ili haki itendeke kwa pande zote zinazohitajika.

Ningeomba sana Mheshimiwa Waziri pia utakapokuwa una-*wind up* utusaidie sana kufafanua suala zima la haya mashamba kwa sababu tuna imani kabisa tumekuomba uje Sumbawanga tusaidiane wote pamoja. Tunachotaka tufanye kazi vizuri. Wote tukusaidie na wananchi wote wafurahi. Nina imani kabisa ukija tutajaribu kutatua baadhi ya matatizo ambayo yanaanza kujitokeza katika baadhi ya maeneo yetu.

Baada ya kusema hivyo, napenda kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na watumishi wote. Nina imani kabisa tutasaidiana kufanikisha kazi hii ya Wizara hii. Naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. *(Makofi)*

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nianze na kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nimshukuru Mheshimiwa Paul Kimiti, kwa kukusudia kuleta hoja binafsi juu ya kuiomba Serikali kuanzisha Mfuko wa Maji wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina takribani miaka mitatu kila ninaposimama katika Wizara hii kuishauri Serikali kuunda Mfuko wa Taifa wa Maji uwe kama *Road Toll* ili kila Wilaya si chini ya milioni 50, 60 kwa ajili ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilishamweleza Mheshimiwa Waziri katika Kamati yetu na juzi wakati ninachangia hotuba ya Waziri Mkuu, nimelirudia hilo. Kwa hiyo, madhali mimi ndiyo mwanzilishi Mheshimiwa Paul Kimiti utakuwa Katibu, mimi nitakuwa Mwenyekiti wa hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kawaida yangu ya kutumwa na wananchi wa Jimbo la Mtwara Vijijini, safari hii wamenieleza nimweleze moja kwa moja Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwamba wanaomba wananchi wa Mtwara Vijijini kupeleka wataalam kwenye Ziwa Chipwalapwata ili kuona kama kuna uwezekano wa maji yale kusukumwa na mashine ili kusambaza maji katika vijiji vyote vya Kata ya Nanyamba, Kiromba, Mtiniko, Njengwa, Nitekela na Namtumbuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanakuomba sana Mheshimiwa Waziri uwapeleke wataalam. Tukimaliza hapa tu uwapeleke wataalam ili kuondoa tatizo hilo. Nadhani Chipwalapwata kutakuwa na maji mengi na uwezekano wa kusukumwa kwa mashine kwa kutumia maji ya bomba.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, nimetumwa na wapigakura wa Mtwara Vijijini na nimepigiwa simu juzi kukumbushwa kwamba nimweleze Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwamba wana Jimbo la Mtwara Vijijini wameanza mpango wa kuchangana wakishirikiana na Halmashauri yao kwa nia ya kuchimba mabwawa na wameshaanza kuchimba mabwawa matatu, Nyundo, Mbambakofi na Mayembe. Walichogundua ni kwamba gharama ya uchimbaji wa bwawa moja ni kubwa sana haipungui shilingi milioni 25. Uwezo wao ni mdogo na wana mpango wa kuchimba mabwawa mengi zaidi kulingana na tatizo hili la maji. Wana mpango wa kuchimba bwawa la Malamba, Mtiniko, Njengwa, Kiromba, Madimba, Mayembe na Ziwani. Wanaiomba Serikali iwaunge mkono kwa kuwapa msaada kwa sababu uchimbaji wa mabwawa ni gharama mno, kasi yao ni bwawa moja kwa mwaka wanaona kwamba kasi hii ni ndogo sana. Wangependa wachimbe angalau mabwawa mawili matatu kwa mwaka, tatizo lao ni fedha. Wanaiomba Serikali Kuu kusaidia.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, nimetumwa nimwombe Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo na Serikali kwa ujumla, wawaongezee wahisani watakaobaini vyanzo vya maji Jimbo la Mtwara Vijijini, tatizo hili jimboni ni kubwa, ingawa tumepata *JICA* lakini si vibaya mkituletea wengine kama Benki ya Dunia, haswa. Kwa hiyo, tunakuomba fanya maarifa huko Wizarani Mheshimiwa Waziri uwabembeleze watu wa Benki ya Dunia waje Mtwara Vijijini.

Pia uzungumze na watu wa *RIPS* wajihusishe sana na kutupa msaada katika masuala ya maji. Wao kazi yao ni semina na makongamano tu. Tayari tumeelewa, mambo ya makongamano, semina kwa sababu ni mara kwa mara, tumewaelewa uwezeshaji na ndiyo maana tumehamasika na tumeelewa mpaka sisi wenyewe tunachanga. Tunaomba misaada ya vitendo kama shilingi milioni 20, namna hii ni vizuri ili tuongezee fedha zetu tulizonazo kwa kuchimba mabwawa mawili, matatu zaidi.

Mheshimiwa Spika, madhali niliyotumwa nimemaliza na wamenieleza nisitietie uremba uremba tena, peleka ujumbe na ukae chini. Naomba niunge mkono hoja. Nikae chini kutii amri yao. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja hii muhimu ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Kwanza kabisa bila wasi wasi wowote ningependa nitamke kwa heshima kwamba naunga mkono hoja hii bila kipingamizi chochote na namtakia kheri Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, utekelezaji mwema wa Sera za Chama Cha Mapinduzi katika kutekeleza masuala ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika uzoefu wangu mdogo kama Mbunge nimeelewa kwamba kati ya mambo ambayo wananchi hufurahi sana ni upatikanaji wa maji, kama mahali palikuwa ni pakame na pana hali ngumu ya kupatikana maji halafu yakaletwa maji pale au ikachimbwa *bore hole* yakapatikana maji, watu hufurahi sana sana, wakina mama hufurahi sana sana na vitoto vidogo unavikuta vinachukua vindoo vidogo vya *plastic* vinachota maji vinapeleka nyumbani, vinarudia tena na tena. Vinaoga tena na tena, kuonyesha furaha wanayokuwa nayo kunapokuwa na mradi wa maji, kwa sababu maji ni msingi wa maisha.

Mheshimiwa Spika, nimefurahi kwamba Mheshimiwa Waziri ametamka kwamba Wilaya ya Iringa Vijijini, ni moja ya zile Wilaya ambazo zitapata *funding* kutoka Benki ya Dunia katika miradi ya maji. Kutokana na hilo pamoja na kwamba kuna matatizo mengi yanayohusu maji katika jimbo langu, ningependa niweke mkazo juu ya mradi wa maji unaotoka Mlima Nyamlenge. Mlima Nyamlenge siyo Banyamlenge, Nyamlenge. Huko nyuma wakati wa awamu ya kwanza ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Mungu amweke mahali pema Peponi, *Amin,* kulibuniwa mradi mkubwa wa maji kutoa maji toka Mto Mtitu, Tarafa ya Kilolo ambayo sasa ni Wilaya ya Kilolo. Maji haya yalikuwa yatawanywe kwa Vijiji 36, ikiwa ni pamoja na Mji wa Iringa au Manispaa ya Iringa sasa.

Lakini mradi huu ulishindikana kwa sababu gharama yake ilikuja kuonekana ni kubwa mno. Kwa hiyo, uliachwa na mpaka sasa haufikiriwi kuja kutekelezwa tena. Mwaka 2001 nilieleza humu Bungeni kwamba kwa nini tusiwe na alternative ya mradi huo wa Mtitu. Kuna Mlima Nyamlenge ambao uko katika Tarafa ya Kilolo lakini jirani kabisa na Kata Magulilwa ambayo ni sehemu ya Jimbo langu. Kuna Mlima mkubwa kule na kuna maji mengi sana yanaporomoka toka mlima huo.

Kwa hiyo, maji hayo yanaweza yakatolewa na kusambazwa kwa kutumia nguvu, wakati huo aliyekuwa Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, alinielekeza kana kwamba niwaombe wataalam wa Maji wa Halmashauri ya Iringa waende wakapime kule, walete *data* Wizarani waone kama inawezekana na kweli walienda kupima wakaona kwamba kuna maji mengi sana. Ila hayatoshi hivyo vijiji 36 lakini yanatosha Vijiji 18.

Kwa hiyo, mwaka 2002 Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ilitoa fedha kidogo kwa ajili ya kuanza *survey* na ili-*survey* Kijiji cha Ihimbo ambacho iko upande wa Wilaya ya Kilolo halafu kwa upande wangu ili-*survey* kijiji cha Ndiwili, halafu Kijiji cha Magulilwa na Ng'enza na Kilambo. Lakini Vijiji ambavyo vinategemewa kunufaika ni vijiji 18 ambavyo viko katika Kata ya Magulilwa, Kata ya Mgama, Kata ya Mseke na Kata ya Ifunda.

Mheshimiwa Spika, inategemea kwamba tunaweza tukapata fedha kutoka Benki ya Dunia, naomba Mheshimiwa Waziri kwanza ahakikishe kwamba *survey* ya vijiji hivyo inafanyika mapema iwezekanavyo ili mradi huu, fedha hizi zikifika naomba sana Wizara yako Mheshimiwa Waziri utekeleze mradi huu. Utakuwa ni mradi utakaotatua matatizo makubwa kwa upande wa Iringa na hasa katika Jimbo langu la Kalenga.

Mheshimiwa Spika, chanzo cha maji kipo, maji mengi. Wananchi wako tayari kuchimba mifereji ya maji kushiriki katika kufanikisha mradi huu. Kama nilivyosema ni vyepesi kutawanya maji kutoka mlimani kwa sababu

yanatoka mlimani na yanakwenda kwa nguvu za *gravity.* Kwa hiyo, yanaweza yakafika vijiji vyote 18 bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Spika, nafikiri Mheshimiwa Waziri hapo amenielewa. Napenda nichangie juu ya mifugo. Wilaya ya Iringa Vijijini ni kati ya Wilaya ambazo hufuga ng'ombe na mbuzi. Lakini mifugo hiyo imekuwa inapungua mwaka hadi mwaka na tatizo kubwa ni maradhi na ni kwa sababu hakuna majosho. Mheshimiwa Waziri ameshasema huko nyuma kana kwamba majosho haya yaliyopo badala ya kuendeshwa na Serikali wananchi wayaendeshe.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana nayo, lakini ningeomba Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ishirikiane na Wizara ya Ushirika na Masoko kwamba wananchi waanzishe vyama vya msingi vya ufugaji ili vyama hivyo ndivyo vimiliki majosho. Kwa muda mrefu tulishapuuza vyama vya ushirika. Kwa hiyo, hata Maafisa Ushirika hawako. Lakini Maafisa Mifugo wako kila mahali na kila Kata ina Afisa Mifugo. Lakini ninavyoona ni kwamba wataalamu wetu wanaokuwa vijijini ni rahisi kutoa huduma kwa wananchi kama wananchi wenyewe wako *organized.* Kwa hiyo, wako *organized* kwenye Vyama vya Ushirika. Kwa hiyo, ni rahisi Afisa Mifugo kuweza kuwaelekeza wafugaji namna ya kufuga ng'ombe wao na vile vile namna ya kuendesha majosho yao. Ni rahisi kuweza kufufua majosho haya wakiwa katika *organization* ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini kama Afisa Mifugo anategemea kana kwamba lazima aende amfuate mfugaji mmoja mmoja ni wazi hawezi kufanikiwa kwa namna hiyo. Ni sawa vile vile na Maafisa Kilimo wangekuwa wanashughulikia suala la ushirika kwamba ili wakulima waweze kuwa *organized* kuweza kulima kilimo bora, wawe *organized* katika Vyama vya Ushirika ni rahisi kuwafikia na kuweza kuwaelekeza. Lakini inaonekana suala hili la Ushirika linakaa kando na hakuna namna ya kuweza kuwa-*organize* wakulima na wafugaji vijijini bila kutumia mbinu hiyo ya Vyama vya Ushirika.

Kwa hiyo, itawezekana sasa wakiwa na majosho yao wanaweza sasa kupata mifugo bora na mbegu bora na vile vile wanaeweza waka-*organize* kama wanapata maziwa mengi kuweza ku-*organize* masoko ya maziwa. Hapo hapo kwamba sasa wanaweza wakulima wakiongozwa vema wanaweza wakatumia samadi badala ya kutumia mbolea ya kemikali ambayo ni gharama kubwa na vile vile inaharibu ardhi.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atazame suala hili la kuwa-*organize* wafugaji wafanye kazi hiyo pamoja na Waziri wa Ushirika na Masoko ili nia yetu iweze kutimia na tuweze kuwa na mafanikio. Vinginevyo kama nilivyosema namna ya kuwaendea wafugaji mmoja, mmoja au mkulima mmoja, mmoja mafanikio ni madogo sana. Vyama vya Ushirika ndiyo makampuni ya wakulima na wafugaji. Kwa hiyo, nguvu yao ikiunganishwa inaweza ikafanya kazi kubwa sana. Lakini mara nyingi mambo haya kwa sababu huko nyumba tuliendesha vibaya Ushirika, kwa hiyo, watu wanaukwepa Ushirika ingawa ndiyo njia pekee tunayoweza kuitumia.

Wakati huo huo ni kwamba mafanikio makubwa ambayo tumeyapata kwa wananchi vijijini ni kwa sababu tumewa-*organize* kuwaweka kwenye vijiji na ndiyo maana tunaweza kuwa na shule za Msingi. Tunaweza kuwa na Zahanati kwa sababu wamewekwa kwenye vijiji. Katika suala la *production* vile vile lazima wawe *organized,* wawe na vyombo vyao ambavyo wanafanya maamuzi ya namna ya kulima kilimo bora na vile vile namna ya ufugaji bora, bila kufanya hivyo, tutakuwa *disorganized* na tutamaliza karne hii tuko hapa hapa na tunazidi kuongezeka. Sasa tunakuwa wananchi wengi halafu *disorganized. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini hoja yangu imeeleweka na nisingependa niendelee zaidi ya hapo kwa sababu muda ni mfupi. Ila naomba kurudia tena kwamba naunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia leo katika hoja hii ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa leo yenye kuleta matumaini katika Wizara hii ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Kwa hiyo, bila kusita Mheshimiwa Spika, naomba basi niunge hoja hii mkono asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba nzuri na pamoja na kuunga mkono ni wajibu pia kuchangia machache katika kuboresha hoja hii ili tuweze kujua na tuweze kupata angalau ufafanuzi wa yale na hayo ambayo tunayo katika sehemu zetu tunazotoka.

Mheshimiwa Spika, naomba basi kuchangia katika maeneo machache na hasa nikianza na maji katika mji wangu wa Singida Mjini.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Singida unakua kwa kasi sana na unakua karibu kila wakati na nasema unakua hivyo kwa sababu labda tuna bahati moja, viwanja katika Mji wa Singida bado ni bure. Kwa hiyo, napenda kuwakaribisha Waheshimiwa Wabunge kama mnataka viwanja, katika Miji ambayo bado inatoa viwanja bure basi ni Singida. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bado Mji unakua kwa kasi kila siku na kwa hiyo, *demand* ya maji kila wakati inaongezeka. Leo ukisema maji yametosheleza labda kwa asilimia 50 baada ya miezi miwili au mitatu unakuta maji hayo hayo ambayo ulisema juzi kwamba tunajitosheleza kwa asilimia 50, asilimia hiyo inateremka inawezakana pengine tuko kwenye asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Singida kwa sasa hivi ni kwamba unajitosheleza kwa asilimia chini ya 50. Ni Mji ambao mpaka sasa bado tunategemea maji ya kugawiwa, ukipata leo mgao basi ujue unakaa siku mbili au siku tatu ndiyo unapata maji mengine tena na inawezekana usiyapate mchana ukayapata usiku wakati umelala ndiyo maji yanaanza kutoka. Sasa katika hilo Singida bado tuna matatizo ya maji. Nashukuru kwamba ziko juhudi zinazofanywa na Mamlaka ya Maji Mjini ya kutuwezesha au ya kuongeza uwezo wa Mji wa Singida kupata maji. Lakini nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba juhudi hii iongezeke ili uwezekano uende sambamba na ongezeko la Mji wa Singida. Kwa hali hii tunavyokwenda, kila siku tutakuwa na upungufu wa maji kwa asilimia isiyozidi 50.

Mheshimiwa Spika, najua kuna juhudi za kuongeza maji kwa mfano kusambaza mabomba katika Mji wa Singida pembezoni na katikati kwa sababu Mji wa Singida katikati mabomba yake karibu mengi yameoza na maji yanapoongezeka wakati mwingine mabomba yanapasuka. Lakini ninachoweza kusema ni kwamba maji tunayoyatumia sisi ni ya visima na wakati hasa tusipopata mvua za kutosha, *water table* inakwenda chini na matatizo ya maji yanaendelea sasa kukua. Sasa kwa mwaka huu kwa mfano, tutakuwa na matatizo makubwa sana ya maji kwa sababu mvua hazikuwa zimetosha na kwa hiyo *water table* itakuwa imeshuka chini. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri aendelee kutupia macho, kwa kweli kuendelea kuboresha maji katika Mji wa Singida.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza wahisani kwa mfano kuna Mji mmoja Austria, Solsebery ambao wanatupatia misaada mizuri sana kwa ajili ya kuboresha maji. Sehemu kubwa katika Mji wa Singida tumesaidiwa sana na huu Mji ambao mfadhili wetu ni mama mmoja katika huo Mji anayetupatia fedha, ametuboreshea sana, ametupa pesa nyingi katika miaka mitatu au minne iliyopita na kwa kusimamiwa na *NGO* moja ya *CDTF* tumeweza kuboresha maji vizuri sana katika Mji wa Singida. Kwa hiyo, namshukuru sana huyo mama mahali alipo kule Austria pamoja na *CDTF* ambao wameweza kuzisimamia fedha tunazozipata kutoka Austria kwa ajili ya kuboresha maji Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sasa ili huyu mama naye aendelee au pamoja na hii Serikali ya Austria iendelee kuwa na moyo, napenda kuiomba Serikali basi nayo iendelee kuongeza nguvu zake ili Mji wa Singida kwa kweli hatimaye angalau ujitosheleze kwa asilimia 50 mpaka asilimia 70 ambayo ndio tunaambiwa Miji mingine inajitosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua pia kwamba Wizara inashughulika na inahangaika katika kutupatia au kujaribu kutafuta fedha kwa ajili ya Mji wa Singida kuutosheleza maji kwa asilimia kubwa zaidi. Mkopo ambao ameutamka leo asubuhi wa shilingi bilioni 11 utakaosaidia kuupatia Mji wa Singida maji kutoka kwenye Bwawa moja la Itamka kilometa kama 17 kutoka pale Mjini. Lakini sasa wakati nashukuru kwa hatua hiyo, ni kwamba maji hayo si chini ya miaka mitano labda pengine ndiyo yatafika. Sasa katika wakati huu kwa miaka hiyo, basi atuboreshee maji tukisubiri kupatiwa maji mengi kutoka Itamka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia matatizo ya maji Mjini, ni kwamba Halmashauri ya Mji wa Singida ina Vijiji 19. Vijiji 19 hivi havipo chini ya Mamlaka ya Maji ya Mji wa Singida, sasa Vijiji hivi havina

mwenyewe, havipo chini ya Mamlaka ya Maji na ukiiacha Halmashauri yenyewe ambayo ndio inaviangalia lakini sijaona taratibu zozote za Wizara za makusudi za kuweza kuvipatia Vijiji hivi maji.

Mheshimiwa Spika, sasa sielewi taratibu au miongozo ya Wizara katika hivi Vijiji ni ipi? Kwa sababu inaonekana tunajali Mjini kutokana na hizo mamlaka lakini Vijiji hivi ambavyo ndio Vijiji vya Mji, havina mtu wa kuweza kuviangalia kwa ajili ya kuvipa maji. Niwashukuru pia *NGO* moja ya *Water Aid* ambayo kwa makusudi wao waliweza kutafuta fedha na sasa hivi wanatusaidia sana katika kutuchimbia visima katika Vijiji vyetu 19. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana kwa sababu wamejitahidi sana, karibu kila Kijiji watachimba kisima ikiwa ni pamoja na ushirikishwaji wa wananchi wenyewe kwa kuchangia katika Mifuko ya Maji. Lakini ndugu zangu, hizi ni *NGOs* ambazo wao wanatafuta labda kwa kuangalia hali halisi katika Vijiji vyetu na matatizo tuliyonayo.

Ninachopenda kuelewa ni kwamba, Mheshimiwa Waziri anieleze kwa makusudi tukiziacha hizi *NGOs,* Serikali ina mipango gani katika hivi Vijiji vya Mji kwa makusudi ambayo inaviendeleza katika kuvipatia maji? Tumeona katika Miji Mamlaka ya Maji ina taratibu zake na nini lakini katika Vijiji vyetu vya Miji hakuna taratibu zozote ambazo naziona ziko wazi kwa ajili ya kuvipatia Vijiji hivyo maji.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri labda pengine mimi sijaona na sijajua hilo, anisaidie katika kunielewesha kujua namna Vijiji vyetu vinavyoweza kupata maji katika Miji yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, sasa naomba pia nichangie kidogo katika sehemu ya mifugo. Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri amesema uswagaji wa mifugo kutoka sehemu mbalimbali kupelekwa labda kwa mfano Mjini Dar es Salaam kwenye masoko ukome mara moja na kwa kweli katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, naye alikuwa amezungumza hayo kutaka magonjwa yasiendelee kuenezwa kwa mifugo inayoswagwa kutoka sehemu moja na kwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, sina ubishi na hilo lakini ninachotaka kujua kwa haraka ya namna hiyo, ni vipi tutamsaidia mwananchi huyu au ni vipi tutawasaidia wafanyabiashara hawa wa mifugo, kama njia mbadala ya kuweza kufikisha mifugo hii katika sehemu zinazotakiwa kwa sababu nikiangalia usafiri wetu, tukienda kwenye reli ng'ombe ni wengi sana kutoka sehemu za Magharibi, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Singida na pia tukipita na hapa Dodoma ng'ombe ni wengi sana. Lakini sasa ni kwa njia gani unayoweza kuwapatia watu mabehewa hayo ya kusafirisha ng'ombe hao ambao wanakwenda Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, sioni namna hiyo ya haraka kiasi kwamba ukisema leo wakome mara moja kesho wapate usafiri wa namna hiyo. Pia sioni uwezekano wa magari kuwachukua hao ng'ombe kwa wingi, mbuzi pamoja na kuku kuwapeleka katika masoko ya Dar es Salaam bila kuwasafirisha kwa njia ya barabara. Ninajua wazi kabisa kwamba uswagaji unaharibu mazingira na pia uswagaji unaeneza magonjwa lakini napenda kuiomba Serikali basi, kwa taratibu ambayo ilikuwa inafanya zamani, kulikuwa na vitu ambavyo vilikuwa vinasaidia kupunguza magonjwa haya.

Moja, ni kwamba zilikuwepo *holding grounds* katika sehemu mbalimbali. Katika *holding grounds* zile kulikuwa na majosho, wanafika ng'ombe pale wanapumzika kiasi kisha wanaogeshwa, kesho wanaondoka, lakini sasa *holding grounds* zote hizi zimekufa, kuna moja ilikuwepo pale kwetu Kindai lakini nayo imekufa na josho lililokuwepo pale nalo limekufa, hakuna kinachoendelea. Sasa vitu hivi vingefufuliwa.

Mheshimiwa Spika, halafu kulikuwepo na *stock roots,* hizi zilikuwa zimetengenezwa na zinajulikana kwamba ng'ombe wanapita wapi na wapi, moja kwa moja wanaelekezwa. Lakini kuna miaka miwili au mitatu tumeambiwa zinafufuliwa kupitia Singida pale kutokea Tabora, lakini sioni uwezekano wa haraka wa kufufua hizo *stock roots* ili ng'ombe hao waweze kufuata taratibu hizo na waweze kufika mahala wanapokwenda.

Namwomba Mheshimiwa Waziri basi ili kuweka hali nzuri kwa hawa wafugaji na wafanyabiashara, ili wasibabaike na tamko hili la kusema wakome mara moja wakati hakuna mbadala wa kuweza kuwasaidia kutekeleza hili, basi haya mawili ya *holding grounds* pamoja na *stock roots* hizi kwa kweli ziimarishwe na zitekelezwe inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo nalo linanikuna nilitaka nichangie kabla ya dakika zangu kwisha, ni machinjio katika Miji yetu. Tuna ng'ombe wengi, mbuzi na kadhalika lakini machinjio katika Miji yetu kila mahala kwa kweli! Sijui hili nani analisimamia, sijui ni Wizara hii au ni Wizara gani kwa sababu kila mahala unapokwenda machinjio yetu ni duni sana. Ni duni kiasi kwamba hata wageni wengine kwa mfano tuna wageni wa kutoka nchi mbalimbali, anashindwa hata kununua nyama ndiyo maana watu wengine walikuwa wanaagiza nyama, anamwagiza mtu wa Afrika ya Kusini nyama na pia sijui anaagiza wapi nyama kwa sababu anapoangalia yale machinjio yetu, hayana mazingira mazuri ya usafi yaani hayana mazingira mazuri jinsi yanavyotakiwa kuwa kama machinjio.

Sasa napenda niiombe Wizara hii ambayo nayo inatuangalia katika biashara hizi, itoe mwongozo na iyasimamie kabisa kwa ukamilifu machinjio yetu katika Miji mbalimbali, yawe ni machinjio ya kisasa na machinjio mazuri ya kuweza kutufanya kwa kweli tuwe na hamu hata ya kula hizo nyama ambazo wenzetu wanachinja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiboresha machinjio ni kwamba unaboresha pamoja na biashara ya ngozi. Sasa machinjio mabaya maana yake ni kwamba hata *products* zetu za ngozi zinazotoka pale unakuta ni za ovyo na kwa hiyo katika biashara hii unakuta ngozi za wananchi zinakosa bei.

Mheshimiwa Spika, mimi yangu yalikuwa ni hayo katika mchango wangu wa leo. Naomba basi, baada ya hayo nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nitamshukuru Mheshimiwa Waziri kama atanijibu kwa yale ambayo nahitaji majibu na nahitaji kueleweshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba kuunga mkono tena hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:**Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya mwisho asubuhi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia naomba nichukue nafasi ya kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri. Aidha, napenda nitumie nafasi hii vile vile kuwapongeza wataalam wake ambao wanafanya kazi nzuri sana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, sasa naomba na mimi nichangie katika maeneo machache.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ambalo ningependa kuchangia, ni huu Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Hapo kwa kweli sina lalamiko, hapo ni pongezi tu. Kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Kondoa Kusini, napenda niishukuru sana Serikali kwa jitihada kubwa ambayo imeifanya ya kutafuta wafadhili mbalimbali ili kuweza kuhisani Miradi ya Maji katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mradi huu wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, Benki ya Dunia imetoa mkopo wa riba nafuu ili uweze kutumika katika kuweza kutatua matatizo ya maji katika nchi yetu. Wilaya ya Kondoa ni moja ya Wilaya ambazo zimewekwa katika mradi huu.

Kwa hiyo, napenda niishukuru Serikali na Wizara kwa ujumla. Ninaamini kwamba kama mradi huu utatekelezwa kikamilifu tatizo la maji litapungua sana katika maeneo yale ambayo mradi huu umeanzishwa. Kwa hiyo, nashukuru sana na napenda kumwahidi Mheshimiwa Waziri kwamba tutakwenda kushirikiana na wananchi wetu wa maeneo haya ama Jimbo langu na Wilaya kwa ujumla ya Kondoa ili kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nichangie katika eneo lingine. Eneo la pili ambalo ningependa kuchangia ni suala la Mtaro wa Ntomoko. Mtaro wa Ntomoko ulijengwa miaka ya 1970 na ulikuwa na lengo la kutatua tatizo la maji katika Vijiji 19.

Napenda nitumie nafasi hii kuvitaja hivyo Vijiji. Hivi Vijiji ni pamoja na Goima, Jenjeruse, Milambo, Igunga, Hamai, Songolo, Madaha, Mtakuja, Chuluku, Lusangi, Jinjo, Jangalo, Itolwa, Mlongia, Mapango, Chandama, Nakirinya, Kerechang'ombe na Kinkima, Vijiji 19. Wananchi wanatoa shukrani sana kwa Serikali yao kwa kutekeleza mradi huu katika miaka ya 1970.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda niseme kwamba, pamoja na ukubwa wa huu mradi lakini mradi huu sasa umechakaa mno kiasi ambacho mradi huu hautoi tena huduma iliyokuwa ikitolewa hapo awali kwa maana ya kwamba mradi umechakaa, miaka zaidi ya 30 haujafanyiwa ukarabati. Kwa hiyo, tatizo la maji limerudi pale pale katika Vijiji hivi 19 nilivyovitaja.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 nilitoa maombi mawili nilisema hivi, kwa kuwa hivi karibuni Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Kondoa aliagizwa kwamba mradi huu aukabidhi kwa wanakijiji wa Vijiji hivyo 19 nilivyovitaja na kwa kuwa wananchi hawa hawana utaalam wala hawana fedha ya kuweza kusimamia mradi huu, nilitoa maombi mawili mwaka 2002 nilisema hivi, tunaiomba Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo itafute fedha kwanza ya kukarabati mtaro huu ili uweze kufanya kazi ndipo tuukabidhi kwa wanakijiji.

Ombi hili halijafanyiwa kazi wala sijapata jibu na wala hakuna kinachoendelea. Napenda kurudia kutoa ombi hilo kwamba, wananchi wetu hawana uwezo wa kuukarabati mtaro huu wala Halmashauri yetu haina uwezo. Napenda kuiomba Wizara itafute fedha mahala popote ili tuweze kufanya ukarabati kwa nia ya kuwasaidia wananchi wetu katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kwamba, mradi huu wa mtaro ni mradi mkubwa wanakijiji peke yao hawawezi kuumiliki na kuusimamia, hawawezi. Sasa niliomba vile vile kwamba Wizara itoe utaalam, narudia kwamba Wizara itoe utaalam wa kusaidia kuunda chombo cha kusimamia mradi huu na hilo ombi nalirudia kwa sababu mwaka jana katika mchango wangu wa maandishi nilitoa ombi lakini halijafanyiwa kazi.

Sasa naomba tena kwamba Wizara basi ichukue jukumu hilo la kutusaidia utaalam wa kuunda chombo cha kusimamia mradi huu kwa sababu wanakijiji hawana utaalam huo wa kuunda chombo wala hawana uwezo wa kusimamia. Kwa hiyo, maombi yangu haya mawili naomba niyafikishe kwa Mheshimiwa Waziri ili aweze kutusaidia. Nia ni njema kabisa kwamba tuwasaidie hao wananchi ama Vijiji 19 ambavyo nimevitaja ambapo sasa hivi wanapata matatizo ya maji kutokana na uchakavu wa mtaro huo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na Mradi wa Ntomoko katika miaka ya 1980, Serikali ilibuni vile vile mradi mwingine wa Bwawa la Mwisanga na lengo lilikuwa ni kuongeza maji ama ujazo wa maji katika mtaro wa Ntomoko ili kuweza kuongeza ujazo wa maji na vile vile kuboresha huduma ya maji kwa Vijiji 19 nilivyovitaja.

Mheshimiwa Spika, Bwawa hili limekamilika miaka 20 iliyopita lakini maji yake bado hayajaanza kutumika, miaka 20 iliyopita bwawa lilikwishajengwa lakini maji yake mpaka leo hayatumiki, sababu ni nini? Sababu ni kwamba maji hayo ni machafu yanahitaji kuchunjwa ndipo yaunganishwe kwenye bomba ama mtaro wa Ntomoko ndiyo maji yaanze kutumika. Lakini kwa miaka 15 sasa, Wizara ilikuwa ikiahidi kila mwaka katika Bajeti zake kujenga chunjio la kuchuja maji ili maji haya yaweze kutumika. Tangu mwaka 1990 mpaka leo hakuna kitu kilichofanyika, kwa hiyo maji yako pale pale.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa naona Mheshimiwa Waziri anaashiria kwamba tatizo lilikuwa ni pesa. Lakini ninashangaa kuna miradi mingine inaanzishwa na inakamilishwa wakati Mwisanga bado haijakalishwa na ina miaka 20. Sasa tatizo najua ni pesa lakini lazima tuangalie kwamba pale tumetumia pesa nyingi ili kuweza kuchimba ama kujenga bwawa hilo. Sasa kuuachia mradi wakati bado tuna tatizo la maji, mimi nafikiri si busara, busara ni kutafuta fedha za kuweza kuukamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Spika, labda ningependa kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kidogo kwamba Waheshimiwa Mawaziri wenzake walisema nini kuhusu mradi huu katika Bajeti mbalimbali. Naona kwa kuwakumbusha na wataalam vile vile, naona wataalam nao wameusahau mradi huu.

Mheshimiwa Spika, nikianzia mwaka 1991/1992 katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri mwaka ule katika Bajeti, alisema hivi kuhusu mradi huu: “Aidha, katika Mradi wa Ntomoko - Mwisanga shughuli zitakazofanywa ni pamoja na usanifu wa chunjio,” lakini hakuna kitu kilichofanyika.

Mwaka 1992/1993 Mheshimiwa Waziri alisema: “Aidha, Wizara itaanza usambazaji wa maji wa Bwawa la Bariadi na kukamilisha usanifu na kuanza ujenzi wa chunjio la maji katika Mradi wa Mwisanga,” hakuna kitu kilichofanyika. Mwaka 1993/1994 katika hotuba ya Bajeti Mheshimiwa Waziri alisema kama ifuatavyo: “Usanifu

wa chujio la maji katika Mradi wa Mwisanga umekamilika na ujenzi utaanza katika mwaka 1993/1994," hakuna kitu kilichofanyika.

Katika Bajeti ya mwaka 1995/1996 Mheshimiwa Waziri vile vile alisema: "Mheshimiwa Spika, mpango wa mwaka huu katika Sekta ya Maji utatilia mkazo katika maeneo dashi dashi kuendelea na ujenzi wa Mabwawa ya Kilimi, Bariadi - Mgumu na Mwisanga," hakuna kitu kilichofanyika. Mwaka 1996/1997 katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri alisema hivi: "Aidha, ujenzi wa *sedimentation tank* na ujenzi wa chujio la maji vitaendelezwa kwa Bwawa la Mwisanga," hakuna kitu kilichofanyika. Katika Bajeti ya mwaka 1999/2000 katika hotuba Mheshimiwa Waziri alisema hivi: "Aidha, Wizara yangu inakusudia kuendelea na ujenzi wa mabwawa ambayo yalikwishaanza kujengwa ya Kilimi, Mwanahinya, Bariadi, Meatu na kukamilisha ujenzi wa chunjio la Mwisanga," hakuna kitu kilichofanyika.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi huwa najaribu kujiuliza kwamba, hivi unapoahidiwa namna hii kwa miaka 15 na unakwenda kuwaambia wananchi, hivi wananchi wanakuelewa kweli? Mimi naonekana sasa ni mwongo kule. Napenda tusifikishane hapo, mimi simlaumu Mheshimiwa Waziri, lakini napenda kuiomba sana Serikali kwa kweli ijitahidi kuangalia suala hili, naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu cha kushangaza zaidi ni mwaka jana na mwaka huu kwamba katika Bajeti ya mwaka 2002/2003 na mwaka huu wa 2003/2004, wataalam nafikiri wamemshauri Mheshimiwa Waziri kwamba asitaje suala la Mwisanga tena. Kwa hiyo, hakuna kitu kilichoandikwa humu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa huwa najaribu kujiuliza hivi ni nini kinachoendelea? Mimi napenda kuomba, mimi nawaomba sana, kwa sababu hapa ni kupoteza fedha za Serikali, kuwekeza katika miradi mikubwa kama hii halafu tunaachia njiani.

Mimi nakuomba Mheshimiwa Waziri ufanye jambo la uungwana tu, uje uliangalie hilo bwawa, nimewaangalia hapa wataalam wote nafikiri nyuso ni ngeni kwa hiyo hawajui hata Bwawa la Mwisanga liko wapi.

Kwa hiyo, naomba kama wewe unashindwa kuja kuangalia uwatume wataalam wako ili waje waangalie ili wajue hali halisi ya mambo katika Bwawa la Mwisanga. Hilo ndilo ninaloliomba sana. Mimi mwaka huu sitakuwa na ugomvi sana lakini mwakani naomba utenge pesa ya kufanya hiyo kazi, naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia suala la maji sasa naomba nizungumzie kidogo kuhusu huduma za tiba za mifugo.

Kwanza, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 11 ametoa msimamo kuhusu maradhi ambayo yametapakaa katika nchi yetu.

Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa waraka ule Na. 1 wa mwaka 2002 na kutoa maelekezo ya jinsi ya kuweza kushughulikia mifugo yetu katika nchi hii. Ni kweli kabisa kwamba mifugo inaathirika mno na maradhi hasa ya milipuko.

Kwa hiyo, mimi naomba waraka wa Mheshimiwa Rais iwe ni changamoto kwa ajili ya Wizara na sisi sote tuweze kuzingatia na tuweze kuinusuru mifugo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ombi langu hapa ni kwamba Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara yake, wajitahidi kuangalia masuala ya dawa na hasa ya chanjo. Tuweze kupata dawa za kutosha kwa ajili ya kuchanja mifugo yetu kwa maradhi yote ambayo ni ya milipuko.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba sana suala la ufufuaji wa majosho nalo tuliwekee maanani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba nirudie kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na naomba nitamke kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo ndiyo tunafikia mwisho wa kipindi cha asubuhi.

Napenda niwafahamishe watakaochangia mchana kwa sababu mjadala wa jumla unakwisha saa 12.00 jioni kwa hiyo, kuna nafasi ya wachangiaji wanne na waliopangwa ni wafuatao, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz na Mheshimiwa Njelu Kasaka. Kwa wengine tunaomba radhi kwa sababu ndiyo hivyo tunatawaliwa na muda.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi Saa 11.00 Jioni.

*(Saa 06.56 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 Jioni)*

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kwa hotuba yao ndefu, nzuri na inayoeleweka, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mawazo yangu nitayaelekeza katika huduma za maji vijijini. Wizara hii ni kubwa na naungana na wenzangu wenye mawazo kwamba maji ingestahili kuwa na Wizara yake peke yake. Unapochanganya maji vijijini, huduma za majisafi na majitaka mijini na maendeleo ya mifugo ni lazima sehemu fulani itaathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoona huduma za maji vijijini zinaathirika kabisa. Ukweli huo unajionyesha kwa orodha ndefu ya miradi ya maji vijijini ambayo imeshindwa kukamilika au imekufa kabisa. Wizara au Serikali imetuonyesha kima cha chini cha maji ambacho kila mtu anatakiwa apate ni lita 25 kwa siku na hiyo ni kwa watu wote nchini. Kwa hiyo, huduma ya maji inapaswa ienezwe kwa wananchi wote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai, maji ni hitaji la msingi na haki ya kila mtu. Kwa hiyo, iko haja kufuata sera zinazofanana kwa Wizara za huduma za jamii kama vile elimu, afya na maji. Kwa mfano, utaratibu wa *Basket Fund* unaotumiwa na Wizara ya Afya kuelekeza fedha Wilayani pia ungetumika kwa ajili ya Wizara ya Maji. Vile vile iko haja ya kuwa na Mfuko wa Maji Kitaifa kama vile tulivyo na Mfuko wa Afya ya Jamii katika afya. Maji ni huduma ya msingi kabisa*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sera ya Maji imetamkwa kabisa kwamba maeneo yale ambayo yana ukame ndiyo yapewe kipaumbele lakini wakati mwingine najiuliza kama kweli nguvu za kutosha zinaelekezwa kwenye maeneo yenye ukame. Nikichukulia mfano wa Jimbo langu la Gairo lenye uhaba wa maji. Kiasi cha mvua tunachopata kwa mwaka ni milimita 600 tu kwa ajili ya Mji mdogo wa Gairo na Vijiji vya Kisitwi, Rubeho, Kwipipa, Msingisi, Luhajwi, Kibedya na Chakwale tuna chanzo cha maji ya mtiririko kutoka kijiji cha Masenge katika Milima ya Ukaguru. Chanzo hicho ni cha muda mrefu na maji sasa hayatoshelezi kabisa kwa jinsi mji mdogo wa Gairo ulivyokuwa umepanuka sana na kuwa na wakazi wengi, hivi sasa Gairo ina wakazi 35,638.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazielewa na kuzipongeza juhudi za Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo zinazochukuliwa kupanua na kukarabati chanzo hiki kwa kutumia msaada wa Shirika la *ASD* la Ufaransa. Lakini nasikitika kusema kuwa kumekuwa na ucheleweshaji wa muda mrefu kuanza kazi hiyo. Naiomba Wizara isaidie kuweka msukumo ili kazi hiyo ianze. Kwangu mimi maji Gairo ni suala nyeti kisiasa na hasa kwa kufikiria tunakokwenda mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema Tarafa ya Gairo ni eneo lenye uhaba wa maji. Vijiji vilivyobaki vinahitaji visima virefu na visima vifupi. Visima vilivyopo vingi ni visima vifupi lakini baadhi ya visima hivyo maji yake ni ya chumvi. Kwa hiyo, kuna haja ya kuvipatia vijiji hivyo visima virefu. Lakini tatizo mtambo wa kuchimba visima virefu umekuwa ni nadra sana kupatikana. Uliwahi kuletwa katika Tarafa ya Gairo miaka mitano iliyopita lakini cha kushangaza mtambo huo ulihamishwa kabla ya kuchimba hata kisima kimoja.

Naomba Wizara ifanye juhudi kutupatia mtambo wa kuchimba visima virefu ili vijiji vile ambavyo havina maji vipate maji na kama nilivyosema visima vifupi tumepata maji ya chumvi tu vijiji viko katika shida kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika Tarafa ya Gairo tuna wafugaji na mifugo yao inahitaji maji. Naelewa lengo la Wizara ni mifugo nayo ipatiwe maji ya kutosha na njia inayotumiwa ni uchimbaji wa malambo na mabwawa. Hapa vile vile napenda kuishukuru Wizara katika mwaka wa fedha 2002/2003, walitupatia shilingi milioni tatu kwa ajili ya uchimbaji wa bwawa moja ingawa kwa bahati mbaya bwawa hilo silioni katika orodha iliyopo katika Kiambatisho Na.7 cha kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijui na fedha hizo nazo zimenyofolewa au vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyoelewa uchimbaji wa mabwawa na malambo unashindikana kutokana na kukosekana kwa zana hasa matingatinga (*bulldozer*) na katapila. Wilaya ya Kilosa katika Idara ya Maji haina zana hizo. Ninachoshauri labda Serikali ingeweka utaratibu wa kuazimana zana hizi kati ya sekta moja na sekta nyingine. Kwa mfano matingatinga yanayotumiwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara au kilimo yatumiwe kwa ajili ya kuchimba mabwawa na malambo kwa kuelewa kwamba Serikali ni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuendeleza ile hoja ya kuwa na Mfuko wa Maji. Gharama ya kulipia ujenzi wa miradi ya maji ni kubwa mno. Wananchi vijijini hawana uwezo mkubwa wa kuweza kulipia gharama za ujenzi, uendeshaji, ukarabati, upanuaji wa miradi. Kwa hiyo, napendekeza vile vile katika Wilaya nazo kuwe na mfuko ambao wananchi watachangia na wachangie kwa ule utaratibu wa changa nikuchangie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nimeona kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya miradi ya maji kinatofautiana sana kati ya Wilaya moja na Wilaya nyingine. Wilaya nyingine katika miradi ya maji zimetenga fedha nyingi na Wilaya nyingine zimetenga fedha kidogo sana. Iko haja kwa Wizara kutoa miongozo ya namna ya kuandaa miradi ya maji Wilayani ili tuweze kufikia lengo lile ambalo linakusudiwa la usawa wa upatikanaji wa maji kwa watu wote nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kuzungumzia juu ya hifadhi ya vyanzo vya maji. Kwa mfano Milima ya Ukaguru ndiyo yenye vyanzo vya maji kwa ajili ya Mto Wami. Lakini bahati mbaya wananchi wameanza kukata miti hovyo katika vyanzo hivyo vya maji. Iko haja ya kuelimisha wananchi waelewe na wapewe majukumu ya kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji na ikiwezekana wamilikishwe vyanzo hivi ili wawajibike katika kuvilinda na kuvihifadhi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, uvunaji wa maji ya mvua ndio kimbilio pekee la maji ya kuaminika katika kipindi cha kiangazi katika sehemu zenye ukame. Mapendekezo yangu ni kwamba Halmashauri zingeshauriwa kutunga sheria ndogo kuwataka wale wote wanaojenga nyumba za kisasa basi waingize teknolojia ya uvunaji wa maji kwenye ujenzi wa nyumba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ipo haja ya kuunganisha huduma za maji, usafi wa mazingira na elimu ya afya ili kuwa na jamii yenye afya bora. Ukosefu wa maji safi na salama na kutofuata kanuni za afya na usafi wa mazingira ni vyanzo vikubwa vya vifo na magonjwa ya watu nchini. Ili kuboresha afya ya jamii, mkazo uwekwe kwenye mipango ya pamoja inayojumuisha utoaji wa huduma za maji, usafi wa mazingira na elimu ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, narudia tena kusema naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kusema kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila siku tunaimba kwamba maji ni uhai na ukitaka kutoa giza lazima ulete mwanga, mwanga na giza havikai pamoja vile vile umaskini haukai pamoja na maji. Kwa hiyo, tukitaka kuondokana na umaskini suala kubwa ni kuhakikisha kwamba tuna maji ya kufanyia kazi ya kutosha kwa mfano ya kunywa

binadamu, mifugo, viwanda na shughuli nyingine mbalimbali maana yake hata gari haliwezi kwenda kama hakuna maji. Unaweza ukaringa kwamba mafuta yanakusaidia lakini vile vile bila maji gari haliendi na binadamu bila maji, unachemsha haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisamehewe sana kama nitasema maneno ambayo wengine wataona ni mabaya, katika huduma za jamii tungejaribu ku-*restructure* kwa sasa hivi tunaanza na elimu, afya, maji. Nafikiri tungefanya *the other way round,* kama alivyosema Ndugu yangu Mheshimiwa Paul Kimiti, tungeanza na maji, afya halafu elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili niliwahi kulisema kwa Walimu wakaniona kama Shetani lakini nilikuwa nawaambia ule ukweli. Ni kitu gani unachotumia kila siku tangu mama yako amekudondosha ulimwenguni humu kwanza lazima uoshwe na maji halafu na wewe lazima utatumia maji mpaka kufa. Kama una bahati nzuri siku ya kufa maji yanakuaga, sio bwana? Halafu tunaweza tukajiuliza maswali je, unaweza kuishi bila maji*, the answer is no.* Je, unaweza kuishi bila afya, *the answer is somehow no.* Kwa Tanzania ukitazama ile *percentage* ya wagonjwa ukilinganisha na wazima *it is a very minimal,* siyo? Elimu *is very important* lakini mtu ataihitaji *seven years later on* sio Bwana wakati kila siku unatumia maji.

Mheshimiwa Naibu Spika*, lets us be very serious,* ndio maana nimesema kwamba palipo na umaskini ukileta maji umaskini unaondoka *automatically* ni kama vile palipo na giza ukileta mwanga giza linaondoka*,* kwa hiyo lazima tu-*restructure planning* zetu. Kwa kweli naishukuru Serikali kwa upande wa elimu imejitahidi sana.

Napenda kutumia nafasi hii kuishukuru Serikali, wakati nimeingia hapa Bungeni *the biggest agenda* ilikuwa ni maji na kama kwa kweli Wizara hii isingesimama kidete kwa kweli *I wouldn’t be here today.* Kwa sababu agenda ya brother wangu Bwana Bob Makani ilikuwa ni maji lakini kwa kweli Wizara na Rais kwa kweli walisimama kidete na bahati nzuri *today I am speaking as a Member of Parliament for Shinyanga.* Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuna matatizo makubwa ya maji lakini kwa kiasi kikubwa sana yamepunguzwa. Kwa bahati nzuri kwenye hotuba imeonyeshwa kwamba baada ya mradi wa *Lake Victoria* kukamilika kwa kweli sisi tutakuwa tumebahatika sana. Kwa kweli tunaishukuru sana Wizara hii pamoja na Serikali ya Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Aongezewe.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Ooh yes if it is possible. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua suala la muda ni lingine sababu ya Katiba yetu. Wapo Watanzania ambao hatukujua kwamba Rais Benjamin Mkapa, angeweza kuwa mtu mzuri namna hii, ninaamini kwamba yule Baba yake na Daudi alikuwa anaitwa nani?

**MBUNGE FULANI:** Esau.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Aliambiwa kwamba nipe watoto wako wote nione mtu wa kumpaka mafuta. Wakaletwa watoto wake wote. Daudi akashindwa kuletwa pale. Baba yake akaulizwa hivi wewe una watoto hawa tu? Akasema yupo na Daudi lakini yule ni mchungaji tu hata hana maana lakini *this was Mkapa, isn’t it.* Ninaamini kwamba Tanzania ni nchi ya watu wengi na watoto wa Esau wapo wengi, sio?

**MBUNGE FULANI:** Ndio.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Yawezekana Mungu atatubariki Watanzania tutapata mtoto mwingine mzuri kama Daudi.

**MBUNGE FULANI:** Kama Mkapa.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Kama Mkapa*. (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Shinyanga Mjini, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wizara hii kwa sababu wametusaidia mabomba ya shilingi milioni 30 tunayaweka na vile vile tumesaidiwa mita.

Katika kijiji chetu cha Ibadakuli walikuwa na kisima chao cha siku nyingi sana ambacho kilikuwa kimeharibika, Wizara hii imetupa shilingi milioni 20 na bahati nzuri nimeongea na *Managing Director* amesema fedha hizo zimeshafika na wanakikarabati. Kwa hiyo, naishukuru sana Wizara hii kwa kutuweka sawa katika tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru sana wafadhili ambao wametusaidia katika kutatua matatizo yetu hasa Serikali ya Uingereza ilitusaidia mradi kupitia *Department for International Development (DFID)* kupitia *OXFAM* walitusaidia *sterling pound* kama laki tano na elfu thelathini na tano hivi ambazo zimetusaidia kuweka mtandao wa maji kilomita kama 26 halafu tumeweka matanki ambayo yanatusaidia ku-*improve ile pressure.*

Kwa kweli wametusaidia sana na ninamwomba Mheshimiwa Waziri atufikishie shukrani zetu kwa Serikali ya Uingereza kupitia mashirika yake. Matatizo ya maji bado hayajaisha tuendelee kufanya nao kazi ili kusudi tuweze kutatua kabisa tatizo hili sababu hata kama yakiwepo maji kule kwenye bwawa kuna sehemu nyingi sana katika mji wa Shinyanga mabomba hayafiki. Kwa bahati nzuri juzi wakati wanasema kwamba mradi umeisha wameahidi kwamba watatusaidia vile vile mita 3,000 ili tuweze kuboresha mapato ya maji katika mji wetu wa Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati naomba kura nilikuwa nawaambia kwamba kidole changu hiki na vidole vyenu hivyo vitasaidia kuvunja chawa na chawa huyo ni kero zinazotukabili hasa katika suala la maji. Pia niliwambia kwamba kidole changu kitasaidia kuta-*solicit* wafadhili na kuisukuma Serikali lakini kidole chenu mlipe bili za maji. Naomba wananchi wa Shinyanga kama inawezekana kidole chao kilipe bili za maji halafu mimi nitasaidia kusukumana na Serikali na wafadhili mbalimbali ili kusudi waweze kututatulia matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kutusaidia pesa, mimi natoka Shinyanga Mjini lakini vile vile nina vijiji ambavyo havina tofauti na vijiji labda vya Shinyanga vijiji kwa mfano Mwawaza, Chibe, Kolandoto, Kizumbi ili kusudi tuweke mabwawa ya kuwasaidia wananchi hawa kwa sababu wana mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunateka maji kutoka Bonde wa Mwawaza baada ya kuchimba visima kwenye Bonde la Mwawaza vile vile vidimbi ambavyo wananchi walikuwa wanavitumia katika kunyweshea mifugo vilikauka. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri ameonesha dalili kwamba atatusaidia katika kutatua tatizo hili.

Sisi watu wa Shinyanga tuko kwenye Bonde la Bubu yaani *the internal basin* ambayo iko Shinyanga, Singida na Arusha. Naomba kama inawezekana Serikali iweke *authority* ya kulinda Bonde hili kwa sababu limeathirika sana na lingeboreshwa tungeweza kuwa na uchumi mkubwa sana. Katika Bonde hili kuna *Lake* Natron, wenzetu wa Kenya kule Magadi walijenga *infrastructure,* nafikiri Wizara hii ijaribu kufanya kazi kwa kushirikiana na Wizara nyingine ili tuwe na reli kutoka Arusha mpaka *Lake Natron* halafu kuboresha bandari ya Tanga sababu haya magadi ni *basic* kwa ajili ya *chemical industry.* Wenzetu wa Kenya wanauza magadi ya *sterling pound* milioni 180 kwa mwaka, ni uchumi mkubwa sana kwa hiyo naweza kusema na lenyewe hili lifanyike kwa kutumia Wizara hii na *of course* na sisi Shinyanga tuko katika Bonde la Bubu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nataka kuishauri Wizara hii wafanye *mapping* ya *underground water resources* kama walivyofanya wenzetu. *Kule South America* kuna ile *Gwaran Aquifer* waliifanyia *mapping, North America* kuna *Ogalala Aquifer,* Australia kuna *Artisen Aquifer* na sisi hapa ni vema tukafanya *mapping* ya *underground water* resources lakini lazima iende na utaalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kusema hapa kwamba shape ya dunia ni pamoja na maji ambayo yako kwenye ardhi uki-*pump* maji mengi sana ile ardhi huwa in*a-collapse.*

Kwa mfano kule California, Pakistan hata Afrika Kusini ardhi ime-*collapse.* Wakati fulani nilimuuliza Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwamba kule Shinyanga kwa kuwa wana-*pump a lot of water* wanatakiwa

watengeneze mabwawa ya kusaidia ku-replenish underground water. Kwa mfano, hata Mzakwe hapa mnapo-*pump about 40,000 cubic meter for 100 years* uta-*create vacuum later on* Mzakwe inaweza ika-*collapse.* Kwa hiyo, kinachotakiwa ni kufanya *research* na kuona haya maji ya Mzakwe yanaingilia wapi halafu kule wasimamishe maji ili kusaidia *ku-replenish sehemu nyingi za ulimwengu wanafanya hivi na sisi sio vibaya tukafanya hivi.(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mifugo, napenda kushauri kwamba ni vema tuboreshe machinjio. Bahati nzuri sasa hivi nchi yetu itajengewa barabara nzuri, tukiboresha machinjio, ninaamini kabisa tutapata nafasi ya kuuza nyama katika nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie katika hoja hii iliyo mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. Kwanza, naomba niseme kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Naomba vile vile kutoa pongezi na shukrani kwa Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, watendaji wakuu wa Wizara, lakini vile vile naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Nasema hivi kwa sababu nimegundua Mheshimiwa Waziri wa Fedha kila inapofika Wizara korofi huwa anakuwepo kusikiliza maneno ya Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Daniel Yona, anachekelea pale, lakini yeye alikuwa hakai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema Mheshimiwa Basil Mramba kila Wizara korofi huwa anakuwepo. Hii inamsaidia kusikiliza maneno ya Waheshimiwa Wabunge kwamba nini matatizo yao na pengine yeye na Waziri mhusika wanasaidiana kuweka mambo sawa. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishukuru Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa msaada mkubwa walioufanya wa Mji wa Lindi. Mwaka huu Mji wa Lindi ulikuwa na upungufu wa maji kwa asilimia 86, tulikuwa tunapata maji asilimia 14 tu ya mahitaji yetu. Wizara ikatupatia shilingi milioni 339 kwa ajili ya mradi wa dharura ya kuchimba visima kumi ili kuongeza vyanzo kwa sababu vyanzo vya awali vilikuwa vinakauka.

Naomba nichukue nafasi hii kumwarifu Mheshimiwa Waziri kwamba msaada ule au mradi ule umetoa mafanikio mazuri kwani tumeweza kupata vyanzo vyenye kutoa maji takriban lita milioni nne sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maji yale yapo ng’ambo ya bahari na tunahitaji bomba kubwa la kuweza kupitisha maji yale kutoka kule ng’ambo kuleta Mjini. Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Waziri aangalie namna ya kutupatia fedha ya kutosha ili tuweze kuweka bomba kubwa la kuweza kuchukua maji yote yale kuleta Mjini huku kwa ajili ya kutumika pale Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maelezo nimemwandikia Mheshimiwa Waziri katika mchango wangu wa maandishi, siwezi kuyarudia tena yale, lakini nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano mwingine, kule ng’ambo vipo Vijiji lakini vyenyewe havina maji. Sasa si vema tuchukue maji yote yaje Mjini tuwaache wenyewe kule hawana maji. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano wa Vijiji vya kule ng’ambo vya Kitumbikwela na Mungwe na Jitegemee nao tuwapatie maji kutokana na vyanzo vile ambavyo sasa hivi yapo maji mengi kabisa ya kutosha kwa Mji mzima wa Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba vile vile nimwombe Mheshimiwa Waziri anisaidie kunipa maelezo kwamba uko mradi wa *JICA* na vipo baadhi ya Vijiji katika Jimbo langu ambavyo vilikuwa viingizwe katika mradi huu kimojawapo ni Kineng’ene. Kineng’ene ni Kijiji ambacho kina watu wengi lakini lipo tatizo kubwa la maji. Wananchi wanakesha visimani kusubiri maji na kule ni porini, kuna simba. Wakaambiwa wachangie shilingi milioni moja, wakachanga shilingi milioni moja, lakini mpaka leo *JICA* hawajafika bado, sisemi hawatafika lakini wao ni wafadhili wana mipango yao wenyewe. Lakini wananchi wale hawawezi kuendelea kubaki vile bila maji mpaka hapo wafadhili watakapoamua kuja.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali kama ilivyofanya kwa Lindi Mjini ifanye vile vile kwa Kineng’ene kutupatia fedha tuchimbe angalau visima viwili vitatu vya dharura wakati tukisubiri hao *JICA,* ili watakapokuja waweze kutusaidia katika mradi mkubwa. Lakini kwa hivi sasa hali ni mbaya sana na kwa sababu wewe ni

mwepesi wa kusafiri safiri nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri akipata nafasi twende akaangalie wale watu wanavyotaabika. Twende Kineng'ene nimpeleke akaone wananchi wanapoishi na hapo wanapochukua maji. Nadhani hii labda itasaidia kupata nguvu ya kutafuta fedha ili awasaidie ili na wao waondokane na adha hii ya kukaa visimani mpaka usiku wa manane wakisubiri maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba vile vile nizungumzie suala la mifugo. Katika Mikoa ya Kusini mifugo si mingi sana na baadhi yao ni waoga hata ng'ombe wanawaogopa. Lakini nilidhani yapo maeneo ambayo yalikuwepo mashamba kwa ajili ya mifugo kama pale Ngongo au Tulieni. Shamba lile sielewi maana lipo pale lakini mifugo hakuna, sasa sijui Mheshimiwa Waziri ana maelezo gani au Serikali ina mpango gani? Sasa nilikuwa nadhani ni vizuri Serikali ikaipa nguvu zaidi au msukumo zaidi Mikoa ile ambayo haina mifugo mingi ili na wao waweze kujiendeleza katika suala la mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, ningeomba niwaunge mkono Mheshimiwa Abdillahi Namkulala na Mheshimiwa Paul Kimiti, waliozungumzia suala la Mfuko wa Maji. Ni kweli kwamba Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ni kubwa sana lakini miradi ya maji ni ghali sana. Mradi mdogo ni wa bilioni, sasa kuchanganya hivi vitu viwili pamoja naona kama vile mnampa Waziri tabu namna ya kujipanga vizuri katika mambo yake. Lakini vile vile kama tumeweza kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Elimu, Afya na Barabara, kwa nini isiwezekane basi tukawa na Mfuko vile vile wa Taifa kwa ajili ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa sababu upo hapa labda mliangalie hili kwa undani wake lakini kwa kweli miradi ya maji ni ghali, kutegemea wafadhili peke yake haitoshi. Kwa kutegemea Waziri mwenye dhamana, miradi kama hii ya Lindi sijui, kwa kweli tunaomba sana tuwe na uhakika wa miradi yetu ya maji. Kila mahali lipo tatizo la maji, kila Mkoa hata kule ambako maji ni mengi, sasa hivi kuna tatizo la maji kuwa si masafi wala si salama. Kwa hiyo, kila mahali lipo tatizo kuhusu maji. Tunaomba sana Serikali iliangalie kwa kina hili ili tuweze kupatiwa au kuanzishiwa Mfuko wa Taifa wa Maji uweze kupunguza kero za maji hasa katika maeneo ya Vijiji vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani nimefikisha maelezo yangu mengi kwa njia ya maandishi kwa Mheshimiwa Waziri na yeye aliniomba nisiyarudie kuyasema hapa wala hatonijibu na mimi nimekubaliana naye asinijibu. Naomba nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. NJELU E.M. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hoja ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Kwanza, nampongeza Waziri, pamoja na Wizara yake kwa kazi nzuri wanayoifanya na juhudi wanazozifanya na napenda kusema kwamba naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono nina mambo machache tu ambayo nataka niyaseme. Moja ni kwamba hivi karibuni mimi niliuliza swali hapa Bungeni kuonyesha kwamba kuna hali ya ukosefu wa maji katika Tanzania yaani kiwango cha maji katika Tanzania katika maeneo mengi kinazidi kupungua. Nikataka kujua kama Serikali inakuwa na mkakati gani katika kuhakikisha kwamba tunajiandaa na kujiepusha na janga la namna hiyo pindi linapoweza kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, inavyoonekana hali bado ni mbaya katika maeneo mengi nchini hata yale ambayo katika siku za nyuma yalikuwa na maji mengi. Sasa maji hayaonekani na mito midogo midogo hata mito mikubwa imeanza kukauka maji na kwa hiyo kuhatarisha hali ya maisha ya wananchi hivi sasa ninapozungumza hapa katika Wilaya kama Chunya kuna baadhi ya maeneo watu wanajipanga mstari kufuata maji.

Kwa hiyo, hali hii siyo nzuri sana, lakini sasa ukiangalia kwenye upande wa Serikali na Bajeti inayotengwa kila mwaka unaiona Bajeti inakuwa ni ndogo ingawa tatizo ambalo lipo mbele yetu linaonekana kuwa ni kubwa. Tungetazamia kwamba Serikali ingeliona suala la matatizo ya maji kama ni moja ya *crisis* kubwa ambayo inanyemelea nchi yetu na kwa hiyo kuweza kutenga fedha za kutosha katika eneo hilo ili kusudi kuondokana na tatizo linayolinyemelea nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya sekta hata ukikosa unaweza bado ukaendelea kuishi, ukawa mzima lakini maji ukiyakosa unakufa na wananchi wetu kutokana na kukosa maji yaliyo safi na salama wanakunywa maji ambayo ni machafu. Matokeo yake wanapata magonjwa na wakipata magonjwa wakienda hospitali dawa hakuna au wanaambiwa wakanunue, fedha hawana na wengi wanakufa na magonjwa ambayo

yangeweza kuzuilika lakini kutokana na kwamba wamekunywa maji machafu, wamepata magonjwa, wamekwenda hospitali wamekosa dawa ama wameshindwa kununua dawa, kwa hiyo mwananchi anakufa.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri suala la kulishughulikia tatizo la maji lazima lifanyiwe mikakati mizito na ya haraka kama vile, mimi huwa wakati mwingine nashangaa kuna mambo fulani Serikali ikiamua kufanya inayafanya kwa nguvu zote. Lakini linapokuja suala ambalo linawahusu watu wengi kama hili, unakuta yanafanyika kwa nguvu ambayo siyo kubwa kama vile ambavyo yanafanyika mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Serikali ilipokuwa inataka kununua *Radar* hapa ilileta ile kwanza na ilipotokea hapa ilizungumziwa kwa nguvu zote kwamba lazima fedha zipatikane *Radar* inunuliwe, lakini unakuta miradi ya maji inachukuliwa kwa wepesi wepesi hivi. Kwa mfano, katika hotuba ya Waziri amesema miradi ambayo haijakamilika inahitaji bilioni 43. Kwa kweli kabisa suala kama hili Serikali ingeweza kabisa kujifunga mkanda na kusema katika kipindi cha miaka miwili ihakikishe kwamba fedha zinapatikana na miradi hiyo Vijijini inakamilika. Lakini tunashangaa kuona kwamba wanakwenda polepole, itachukua miaka mitano.

Leo Waziri anasema baada ya miaka 25 nchi hii itakuwa sehemu kubwa ya wananchi wanapata maji safi na salama lakini tukumbuke kwamba huko nyuma kulikuwa na azimio kama hilo kwamba kabla ya mwaka 2000 kila mwananchi atapata maji katika umbali usiozidi mita 400. Lakini hilo jambo halikufikiwa na leo tunazungumza juu ya miaka 25 ijayo. Hapa katikati hali ni mbaya sana kiasi kwamba wananchi wetu wanaweza kufa kutokana na kukosa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshangaa kuona mwaka huu mpaka Mtama unanyauka katika Mkoa wa Morogoro ambako kawaida kuna mvua nyingi. Mvua sasa hivi imepungua sana hapa nchini kwetu. Matokeo yake ni nini? Ukichukua labda Wilaya ya Chunya kutokana na mvua kidogo iliyonyesha, Mji wa Chunya sasa una matatizo makubwa ya maji. Mheshimiwa Waziri alipokuja nashukuru mwaka jana Naibu Waziri aliyekuwa Wizara hiyo Dr. Festus Limbu kabla hajahama alitembelea Wilaya ya Chunya. Baadaye Waziri mwenyewe akatembelea Wilaya ya Chunya, nawashukuru sana kwa hilo na Waziri alipokuja Chunya tulimpeleka mpaka kwenye chanzo chetu cha maji.

Kwa taarifa yake Mheshimiwa Waziri sasa kile chanzo cha maji *water table* imeshuka, sasa zile *pump* haziwezi kunyonya maji yale kutoa nje kupeleka kwenye matanki ya maji kwa hiyo tuna matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunapata maji kila siku baadaye tukaanza kupeana kwa zamu, sasa hata zamu imeanza kuharibika kwa sababu maji yanayonyonywa kutoka kwenye kisima ni machache sana. Kwa hiyo, sasa hivi ninavyoongea tuna mashaka huu ni mwezi Julai, maji yameshashuka kwenye kina chake, utakapofika mpaka mwezi Oktoba, huenda Mji wa Chunya ukawa hauna maji kabisa.

Kwa hiyo, tunachoomba sasa hivi ni kuchimba kisima kipya kirefu ili tuweze kuyafikia maji kule ambako yameteremka chini. Bila kuwa na kisima kipya cha maji sisi Wilaya ya Chunya na hasa Makao Makuu ya Chunya yatakuwa na matatizo ya maji mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, katika Bajeti ya mwaka 2002/2003 Waziri nilimtajia juu ya bwawa la maji katika eneo la Kijiji cha Matwiga na katika Bajeti iliyofuata Waziri alitenga shilingi milioni tatu kwamba watafanya uchunguzi ili waone ni jinsi gani mradi huu wanaweza kuufufua. Baadaye wataalam walikwenda mpaka Matwiga wakaangalia lile bwawa la zamani la maji katika Mto Mkowiji na waliniahidi kwamba watalishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapema mwaka huu nilionana na Katibu Mkuu wa Wizara nikamwambia, akasema alikuwa hana *data* akaniomba aende Wizarani akalishughulikie kule. Lakini nashangaa leo sioni kwenye Bajeti, labda nimeangalia haraka haraka sijaiona, lakini kama ipo nitafurahi sana na nitashukuru wakati anapojibu kama atanieleza kwamba ni nini wanachokifanya sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya maji pale kwa sasa hivi ni ngumu sana. Kadhalika mwezi huu nilikuwa pale Kijijini Mtanila maji ni shida. Watu wanajipanga kwenda kuchota maji kwenye kisima, itakapofika mwezi wa Kumi sijui hali itakuwaje.

Kwa hiyo, programu kama hiyo Mheshimiwa Waziri angeiharakisha kwa sababu huo mradi ni ule ambao uliachwa wakati wa Benki ya Dunia ambao ulikuwa unakusudia kusambaza maji hayo kutoka pale kwenye Mto Mkowiji kupitia Kijiji cha Igomaa kwenda Mtanila na ulikuwa unakwenda mpaka Kijiji cha Mamba wakati ule, lakini kwa sasa hivi mradi ule unaishia Mtanila. Kama wataweza kuufanikisha basi wananchi hawa tutaweza kuwaepushia matatizo wanayoweza kukumbana nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, mwaka jana Serikali katika Wilaya ya Chunya walijitahidi kuwatenganisha wakulima na wafugaji kwa kuwahamisha kutoka bonde la Mto Songwe katika Bonde la Ziwa Rukwa na kuwapeleka milimani ili kuepusha migogoro iliyokuwa inaendelea. Kwa bahati mbaya tuliwaambia Serikali kwamba tunachoomba tupate mabwawa, siyo malambo madogo madogo, tupate mabwawa katika maeneo ya Nselewe, Mapogoro huko pamoja na sehemu inayoitwa Mpembe na Mbuguni ili kusudi wafugaji waliopelekwa huko wasipate tena tamaa ya kurudi kule walikoondolewa. Kwa bahati mbaya fedha ile bado haijapatikana, tunashukuru mwaka jana zilitolewa fedha chache kwa ajili ya kujenga malambo madogo madogo yanaitwa *charcol* ambayo yaliwezeshwa kujengwa pale Mbugani, tukajenga bwawa lingine Mbugani na Nselewe lakini wakati wa mvua liliharibika na pia naomba fedha zingeongezwa ili liweze kujengwa lingine katika Kijiji cha Mpembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vi-*charcols* hivi vidogo vidogo haviwezi kumudu makundi makubwa ya ng’ombe yaliyohamishwa kutoka kwenye bonde la Ziwa Rukwa. Tunachohitaji tupate mabwawa. Tulitengeneza mabwawa matatu moja kule Mpembe, lingine Mbangala na lingine pale Mjini Chunya ili kupunguza tatizo la maji. Naomba Waziri atakapokuwa anazungumza labda atatueleza ni hatua gani ambazo Serikali itazichukua katika kukabiliana na hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kwa taarifa wale wafugaji waliokuwa wameondolewa wameanza kurudi tena kwenye bonde la Ziwa Rukwa na migogoro imeanza na tarehe 10 Julai, 2003 mwananchi mmoja aliuawa katika Kijiji cha Mbala katika bonde la Ziwa Rukwa ambaye inadhaniwa ilitokana na mgogoro kati ya wafugaji na wakulima. Sasa hali hii itaendelea mpaka lini? Mbaya zaidi kwa siku zijazo na Serikali hawawezi kurudi tena kuanza kuwaondoa kwa nguvu kama tulivyofanya kipindi kilichopita, hao walikwishatoka na sasa wamerudi.

Tunaomba sana hili suala la kujenga mabwawa haya matatu tuliyopendekeza Serikali ijitahidi tupate fedha tujenge haya mabwawa ili kusudi kuepusha migogoro ambayo inapelekea mpaka kunakuwa na mauaji au watu kujeruhiana baina yao wenyewe. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapojibu ajaribu kutusaidia hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo lingine, katika taarifa yake Mheshimiwa Waziri amesema wamepima au wametafiti maeneo saba ya kuchimba visima katika Wilaya ya Chunya. Mimi sielewi ni maeneo yapi. Kama Mheshimiwa Waziri anayakumbuka ningependa ayataje kwa sababu mimi Wilaya ya Chunya naifahamu, ningependa kujua ni wapi kwa sababu mwaka jana katika hotuba yake alisema kwamba wametafiti maeneo sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maeneo yale sita hakuna mahali ambapo pamefanyika mradi wowote. Mwaka huu ametaja saba lakini yale ya mwaka jana hatuoni mahali walipochimba na tangu walipoondoka *DANIDA* mpaka sasa hakuna miradi mipya ya maji inayoendelea ndani ya Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tungependa sana hebu ajaribu kutueleza ni maeneo yapi ambayo mmefanyia utafiti na ni nini kinachoendelea ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata maji. Lakini katika miradi ile ambayo imeorodheshwa kwamba haifanyi kazi baadhi ya maeneo hayo ni kuyapatia zile mashine za kusukuma maji. Tukiweza kupata mashine za kusukuma maji inawezekana katika Vijiji kama Mapogoro, Ngandu, mpaka Mbangala kule na Matwiga unaweza ukapata maji kwa urahisi kwa kuweka mashine ya kusukuma maji tu kwa sababu baadhi ya visima vipo.

Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anatujibu ajaribu kutusaidia Wilaya ya Chunya kutokana na tatizo kubwa la upungufu wa maji kutokana na mvua ambazo zimepungua sana katika Wilaya hiyo tofauti na miaka ya zamani ambapo mvua zilikuwa nyingi na mito mingi ilikuwa inatiririka maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilipenda zaidi nizungumzie suala hili la maji kwa sababu hali iliyopo ndani ya Wilaya ni mbaya. Baada ya kusema hayo narudia tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa juhudi

anazozifanya na yeye amekuwa ni Waziri ambaye kwa miaka kumi ametembelea mara mbili Wilaya ya Chunya, nampongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara ya Maji. Kabla ya yote kwanza niseme naunga mkono hoja ya Wizara ya Maji mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina haja ya kuchangia katika Wizara hii ili kuweza kumsaidia Mheshimiwa Waziri katika baadhi ya mambo ambayo yamekuwa ni matatizo na kero katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Tuna mabonde katika nchi yetu ambayo baadhi ya mabonde haya yamepewa Bodi mbalimbali ili kuratibu shughuli na kudhibiti maji katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba wananchi wa Tanzania sasa hivi wamehamasika katika kilimo katika baadhi au katika maeneo mengi sana kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji maji na hutumia maji ya mito katika mabonde haya. Lakini vile vile tufahamu kwamba nchi yetu jinsi ilivyokuwa kubwa na vyanzo vya maji ambavyo vinaanzia juu kwa maana ya *up stream* hadi kufika *down stream,* mwisho kushuka baharini. Kwa bahati mbaya mimi katika Jimbo la Pangani nakuwa ni victim, matumizi ya maji katika maeneo mbalimbali tukianzia Rombo na kushuka chini nikimaanisha kwamba katika Majimbo mbalimbali ambayo wananchi huwa wanayatumia maji haya kwa masuala ya matumizi ya maji na kilimo. Lakini hatimaye yakifika mwisho kwa maana ya Pangani maji yale yanakuwa yamepungua sana na huwa tumeathirika kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tufahamu kwamba maji haya yana kazi tofauti nikiacha kwa matumizi ya binadamu, mifugo pamoja na kilimo, lakini vile vile kuna miradi ambayo Serikali imeweka katika mito hii ya kuzalisha umeme na Serikali imegharamia fedha nyingi sana kwa ajili ya kutengeneza mitambo hii.

Katika bonde la Mto Pangani tuna nyumba ya Mungu ambayo inazalisha *megawatts* nane lakini hivi sasa *capacity* ya uzalishaji ni *megawatts* nne. Ukifika Hale inazalisha karibu *megawatts* 60, lakini vile vile sasa hivi inazalisha wastani wa asilimia 50. Sasa hata urudishaji wa mikopo iliyokopwa *World Bank* na maeneo mengine kama umeme huu hautatumika *hundred percent* kwa kweli mchango wa umeme katika Taifa hili kwa maana ya kulipia gharama za umeme hautaweza kukidhi kwa haraka kulipa gharama za madeni haya.

Mhehsimiwa Naibu Spika, haya yote ni kwa sababu ya upungufu wa maji unaotokea katika mabonde haya. Sasa mimi nahisi kwamba kuna haja na umuhimu kabisa kwamba matumizi ya maji ambayo yanatumika wahakikishwe kwamba wale wanaotumia maji watumie kwa kiasi wanachokihitaji na umuhimu kwamba yale maji sasa hivi yarudi mtoni ili wote tuweze kushiriki na kutumia maji hayo kwa usawa kwa vile nchi hii ni moja na sera ya maji ni hiyo hiyo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nataka niseme kwamba tuna upungufu wa watendaji katika mabonde haya na hasa ma -*Hydrologist.* Ma-*Hydrologist* ni wachache na hawa ndiyo wanaweza kutusaidia katika kuratibu hizi shughuli na vile vile kusaidia kiutalaam na kuhamasisha wananchi wakishirikiana na viongozi mbalimbali katika Vijiji ili kudhibiti haya maji.

Sasa mimi nasema kwamba kuna watu ambao wanatakiwa walipie hati miliki zao na kwa wale ambao wenye hati miliki na wale wasiokuwa na hati miliki sasa shughuli hizi kwa kweli ni kubwa na ni nyingi na kwa upungufu wa wataalam inakuwa ni vigumu. Mimi nashauri kwamba sasa hivi Serikali kwa kupitia Wizara yako Mheshimiwa Waziri atumie *Tender Board* ya Wizara kwa kuidhinisha kazi hiyo ili kuharakisha wananchi walipie *water rights.* Hii ni muhimu kwa sababu kila mmoja lazima ajue umuhimu wa kutumia haya maji ili yaweze kutumika vizuri na hatimaye wote tuweze kushiriki kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka nizungumzie ni kwamba kuna vituo mbalimbali nchini ambavyo kuna vipimo vya kupimia maji na hizi kazi zinafanywa na *Gauge Readers.* Hawa *Gauge Readers* kwa muda mrefu kwanza wanalipwa pesa kidogo sana, wanalipwa shilingi 17,500/=, kitu kama hicho lakini umuhimu wa *Gauge Readers* katika maeneo haya ni muhimu sana kwa sababu hii ni sawasawa na Sensa, takwimu zinazopatikana zinaweza zikasaidia katika mambo mengi sana ukishirikiana na hali ya hewa pamoja na kilimo. Lakini sasa utakuta kwamba hata hawa *Gauge Readers* sasa hivi hawalipwi sawasawa, tukiuliza Wizara wanasema wanatoa pesa hizi za

*Gauge Readers. Director of Water Resources* anasema zinakwenda Mikoani, lakini kule Mikoani wanasema hazifiki.

Mimi nafahamu kwamba *Gauge Readers* mara ya mwisho wamelipwa mwaka 2000 mwezi Januari. Kwa hiyo, kuna haja ya kutazama upya suala hili na sijui lawama tumpatie nani kwa sababu *Director of Water Resources* anasema pesa zinakwenda na *Principal Water Officer* anahisi kwamba zinafika, lakini ukifika kule unakuta hizo pesa hazijafika. Mimi ningeshauri kwamba hizi shilingi 17,000 zimeshapitwa na wakati, waongezewe ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu mchango wa Serikali katika *River Basin Management,* ni mdogo sana. Ningeomba Serikali iongeze fedha katika *River Basin Management* ili kuweza kukidhi haja ya shughuli zenyewe zinazotakiwa zifanywe katika maeneo haya.

Vile vile kumejitokeza sasa hivi wawekezaji wa nje kutaka kulima katika mabonde haya, labda yapo mabonde, lakini kwa *experience* tuliyokuwa nayo katika bonde la Mto Pangani mimi nafikiri wananchi waliokuwepo katika maeneo hayo wanakidhi haja ya kutumia mabonde haya bila kutafuta wawekezaji kutoka nje. Hii ni kwa sababu hawa wanahitaji maeneo makubwa sana, kwa hiyo wapelekwe katika maeneo ambayo ni makubwa zaidi ya kuweza ku-*invest* huko kuliko kuwafuata wale wananchi na wenyeji ambao tayari wamekwishahamasika katika kilimo hicho, halafu mkawapeleka wawekezaji kutoka nje, kwa kweli itaathiri hasa ukizingatia kwamba sasa upungufu wa maji umekuwa mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho mimi kidogo nizungumzie matatizo ya maji hasa katika Jimbo langu la Pangani. Kama nilivyosema kwamba sasa hivi Mto Pangani ukifika Pangani unakwenda kwa boti zaidi ya saa moja na nusu lakini unapambana na maji ya bahari. Maji ya mto yote yamekwishapotea yamerudi juu, kwa hiyo mashamba yote zaidi ya hekari 30,000 yameharibiwa na maji ya chumvi na kilimo kwa kule kimekufa. Kwa kweli sisi kule Pangani ndiyo *victim* katika masuala haya, kwa hiyo kuna haja ya kudhibiti haya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nimwombe tu Mheshimiwa Waziri, nilimwandikia barua kuhusu tanki la maji lililoanguka katika Kijiji cha Mwera. Kijiji cha Mwera kina watu wengi sana na lile tanki limejengwa toka mwaka 1973. Halmashauri ya Wilaya pamoja na wananchi wanajitahidi kukusanya fedha ili waweze kujenga tanki jipya ili waweze kukidhi haja ya matatizo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa vile imeonyesha wazi jinsi Serikali ilivyoandaa mikakati ya kuimarisha sekta za mifugo na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mikakati mizuri ya Serikali, naomba nizungumzie tatizo sugu la ukosefu wa maji katika mji wa Ushirombo ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe. Pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali kupeleka maji vijijini na Makao Makuu ya Wilaya bado Wilaya ya Bukombe haijaguswa na jitihada hizi. Mji wa Ushirombo pamoja na kupiga hatua kubwa za kuboresha mazingira pamoja na kujenga nyumba za kisasa, kuna tatizo kubwa kabisa la maji linaloufanya mji huu usiwe na usafi wa kutosha kwani mani ni usafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, naiomba Serikali iliangalie tatizo hili na kulipatia ufumbuzi kwani kwenye Bajeti haionyeshi kama Wilaya ya Bukombe imepewa fedha kwa ajili ya mradi wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie hali ya upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo kwenye Wilaya ya Bukombe. Wilaya ya Bukombe ina ng'ombe zaidi ya 320,000 lakini huduma zake ni duni kwa sababu hakuna majosho, mabwawa wala malambo.

Namshukuru Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Anthony Diallo, kwa kutembelea Wilaya ya Bukombe mwaka huu na kuona matatizo yanayoikabili mifugo yetu. Alitoa ahadi ya Serikali kuchangia shilingi 1,000,000/= kwa vijiji vya Bukandwe na Maguta ili vichimbe malambo kwa ajili ya kunyweshea mifugo fedha ambayo haitoshi na mbaya zaidi Serikali mpaka sasa haijatuma fedha hiyo. Hivyo, naiomba Serikali itoe kipaumbele ili Wilaya yangu iwe kwenye mpango wa kuchimba malambo kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri aeleze mradi wa kusambaza maji mji wa Ushirombo utaanza lini na utagharimu kiasi gani cha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara na wataalam wake kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara kwa kukamilisha zoezi la kutathmini miradi ya vijiji iliyoshindwa kuendelea kutoa huduma ya maji kwa walengwa. Katika orodha ya miradi ya maji isiyofanya kazi, miradi mitatu ya Jimbo la Muleba Kaskazini imetajwa, nayo ni Kamachumu, Omurunazi na Bulyakashaju. Miradi hii iliathiriwa na kukosa fedha za matengenezo na uendeshaji. Hivi sasa miradi ya Kamachumu na Omurunazi imeacha kabisa kutoa huduma.

Aidha, mradi wa Bulyakashaju unatoa huduma isiyoridhisha. Hali hii imekuwa ni kero kubwa sana maana maeneo yote haya yaliyokuwa yakipata huduma hiyo sasa yanakabiliwa na taabu kubwa sana ya ukosefu wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara wakati itakapokuwa inatoa kipaumbele kukarabati ama kujenga upya miradi hii (Kamachumu na Omurunazi) ambapo hata mabomba yamechimbuliwa na wezi na *system* nzima ya maji kuharibiwa kabisa, itoe kipaumbele katika mojawapo ya mradi wa Jimbo langu ili kuwapatia wananchi huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine mapya pia yameongezeka kwa kuwa na idadi kubwa ya watu lakini hakuna maji ya kutosha. Mfano Kata ya Ngenge Kijiji cha Rutoro, Kata ya Izigo vijiji vya Izigo na Katoke na shule ya Sekondari Izigo, Kata ya Muhutwe vijiji vya Kangantebe, Nyakashenye na Bisole vina tatizo la upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vijiji vyote hivyo vina maji yanayopatikana mabondeni, zikipatikana pampu na matenki kujengwa, tatizo hili linaweza kudhibitiwa ipasavyo. Nashauri Wizara itusaidie katika hili nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko tatizo lingine ambalo ni kero kubwa nalo ni umwagaji wa majitaka katika Ziwa Victoria unaofanyika kwa miaka mingi katika Jiji la Mwanza. Upo mtaro mkubwa karibu na shule ya Msingi Nyakahoja, unaokusanya majitaka mengi na kuyamwaga Ziwani.

Nashauri utaratibu huu utafafutiwe mbadala, majitaka yasiendelee kumwaga Ziwani. Huu ni uchafuzi mkubwa wa mazingira kwa kuchafua maji ya Ziwa na kusababisha ajali kwani huu mtaro uko wazi na maji yake yana kasi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Muleba walio wengi ni wafugaji wa ng’ombe wa kienyeji na mbuzi. Licha ya kupata mazao kidogo kutokana na aina ya mifugo waliyonayo na kuogopa gharama kubwa za kutunza ng’ombe bora na mbuzi, wana tatizo kubwa la uogeshaji wa mifugo waliyonayo. Nashauri Wizara ione uwezekano wa kuhakikisha mifugo yote nchini inapata huduma ya kinga ikiwa ni pamoja na uogeshaji na tiba pale inapotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ubinafsishaji wa Ranchi uzingatie maeneo. Ranchi za Mkoa wa Kagera ziangaliwe kwa makini kwani hivi sasa wakimbizi wanatusumbua kwa vitendo vya ujambazi na kwa kuwa Ranchi zetu ziko mpakani ni vizuri Serikali iendelee kuziendesha lakini iboreshe mazingira, vifaa, utaalam na mifugo yote iwe na alama ili kukwepa udanganyifu uliowahi kutokea Kitengule kwa ng’ombe wakubwa kubadilishwa na ndama

wa kienyeji. Idadi ilionekana ni ile ile lakini ubora uliharibiwa na haikuwa rahisi kugundua tatizo hili la ukosefu wa uaminifu.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya katika mwaka 2002/2003 na mpango mzuri walioandaa kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hotuba ya Waziri w Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutoa maoni yangu kuhusu hotuba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo ya mwaka 2002/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Serengeti, tatizo kubwa linalokabili watu wake na mifugo ni maji. Wakati Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, alipotembelea Wilaya ya Serengeti tarehe 2 Oktoba, 2000 aliahidi kuwa Mji wa Mugumu utapatiwa maji kabla ya mwaka 2005. Mheshimiwa Rais aliahidi kuwa Bwawa la Manchira litachimbwa na kukamilika kabla ya uchaguzi wa 2005. Kwa kufuatia ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais, Bwawa hilo la Manchira limekuwa linawekwa kwenye Bajeti (2001/2002 na 2002/2003) lakini hadi sasa hamna kazi yoyote iliyoanza. Bwawa la Manchira tena limewekwa katika Bajeti ya mwaka 2003/2004. Wananchi wa Jimbo la Serengeti tunaomba sana tena sana kuwa kazi ya uchimbaji wa Bwawa la Manchira ianze mwaka huu hata kama pesa zilizotolewa hazitoshi kwani tukifanya kazi hii kwa awamu ndio tutalikamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka 2002/2003, Jimbo la Serengeti lilitengewa kuchimbiwa visima vinne lakini hadi leo hakuna hata kisima kimoja ambacho kimechimbwa. Katika Bajeti ya mwaka 2003/2004 tena Wizara imesema kwamba Wilaya ya Serengeti itachimbiwa visima. Wananchi wa Serengeti tunaomba sana tena sana Wizara itimize ahadi yake ya kutuchimbia visima.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia tena kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na naunga mkono hotuba kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nakupongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu na watendaji wako wote kwa kazi nzuri mnayoifanya katika sekta hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchangia kuhusu ankara kubwa za maji kwa mji wa Dodoma. Ninasikitishwa na ankara kubwa za maji ninazopokea toka Dodoma. Daima bili hizo hazina tofauti ukiwepo au ukiondoka. Jirani yangu anaishi daima katika nyumba yake na daima yupo na watu wengi kwake lakini bili yake ni ndogo kuliko yangu.

Naamini fika matumizi yake ya maji ni makubwa kuliko yangu. Kisingizio cha bili yangu ni *meter*. Je, ni wakati gani *meter* hizi zinafanyiwa *check-up* na *service?* Je, tuna uhakika gani kuwa meter hizi ni sawa? Nyumba yangu tuko watu wawili na usiku huwa mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaposafiri anabaki mlinzi kwa saa za usiku tu, je iweje bili iwe kubwa kama ninapokuwepo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu viongozi kuwezeshwa kuwa mfano bora katika ufugaji. Naomba Mheshimiwa Waziri atuwezeshe sisi tulio na *interest* katika ufugaji ili tuwe wafugaji bora na tunaowawakilisha waweze kuiga toka kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchimbaji visima, bei kidogo iko juu, wananchi vijijini wanashindwa je, katika maeneo yenye ukame na yenye wakazi ambao uwezo wao ni duni, Wizara yako inaweza kusaidia upatikanaji wa visima ili wananchi waweze kupata maji mfano Kiluvya - Makuvunge na kadhalika?

**MHE. ALI SAIDI SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni moja kati ya mambo muhimu ya maisha ya kila siku. Ni jambo la kusikitisha sana kuona huduma hii muhimu inakosekana kwa muda mrefu sana na hivyo kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi wa kawaida. Moja katika maeneo hayo ni Manzese hasa maeneo ya Tandale Sokoni na maeneo ya jirani.

Naishauri Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kuliangalia suala hili kwa hali ya dharura ili wananchi waishio maeneo hayo ya Tandale waondokane na tatizo hilo la kudumu la muda mrefu la kutumia maji ya mashimoni ambayo ni hatari kwa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kupitia Wizara hii kuongeza juhudi zaidi katika kudhibiti maradhi mbalimbali ya mifugo kama Mifugo kupatiwa chanjo za mara kwa mara na wafugaji kufidiwa inapotokea hasara ya kupotea, kuibiwa au kufa kwa mkupuo mifugo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara iwahamasishe wafugaji ili waunde Vyama vya Ushirika vya Mifugo ili waweze kutafuta masoko, kupata mikopo kwa urahisi na kufikisha matatizo yao Serikalini ili yashughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iandae utaratibu wa kutoa elimu kwa wafugaji kwa kuzingatia aina ya mifugo, mazingira wanayoishi na hali halisi ya masoko yalivyo.

**MHE. SALIM OMAR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ina juhudi ya kuhakikisha kuwa maji yanapatikana Tanzania nzima tena maji safi na salama, hivyo basi sasa Wizara hii itizame upya suala la uuzaji wa mbegu bora za ng'ombe. Watanzania wanapenda sana kufuga ila mbegu bora za mifugo hiyo hawaipati kutokana na mbegu bora kuuzwa kwa bei ya juu zaidi kuliko uwezo wa wafugaji wetu wa vijijini. Nashauri bei ya mbegu hizo ipunguzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa *Luck* ni dume kubwa na bora, kwa nchi nyingine mbegu zake zinauzwa kwa dola 12.00 sawa na shilingi 13,000, je, kwa hapa Tanzania mbegu yake dume huyo inapatikana kwa shilingi ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kujua je mbegu hizi Pemba zinaweza kufikishwa au anayependa kupata mbegu za ng'ombe hao bora Wizara itahakikisha kufika kwa mbegu hizo zikiwa salama?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Tanzania tunayo Sheria ya Kudhibiti Kulawiti Watoto na kwa sababu wako watu ambao wanawalawiti wanyama ambao ni mboga na hutupatia maziwa kwa hiyo ili tuweze kudhibiti hali hii mbaya na ya aibu Wizara ilete Muswada hapa Bungeni ili Sheria ya Kulawiti Mifugo ikomeshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu soko la maziwa. Pamoja na uhaba wa maziwa pia pana uhaba wa soko la maziwa. Inashangaza kuwa hapa Dodoma nje kidogo ya Manispaa ya Dodoma maziwa yanapatikana karibu bure kabisa kutokana na kutokuwa na soko la kuuzia maziwa yao. Lakini maziwa ambayo yamepitia katika kiwanda au maziwa ya paketi ni ghali sana. Hii inatokana na kukosekana kwa soko zuri na mahali bora pa kutunzia maziwa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia madawa ya mifugo ni ghali mno nayo pia yapunguzwe bei ili wafugaji waweze kumudu kununua madawa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nawatakieni kila la kheri, *Amin*.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, yaonekana Wizara haipati taarifa sahihi kuhusu miradi ya maji inayoendelea katika Wilaya mbalimbali mfano ni Wilaya yangu ya Mbulu.

Nafahamu miaka ya 2002/2003 na 2003/2004 kuna miradi kadhaa ya maji inayoendeshwa na wadau mbalimbali kama vile mradi wa maji Mbulu Mjini pekee unatugharimu zaidi ya shilingi milioni 400. Sasa wadau hawa ambao wengine huomba fedha toka nje huuliza kwa nini Serikali Kuu isiunge mkono jitihada hizi?

Ombi letu kwa mwaka jana ilikuwa ni msaada wa kubadilisha mtandao wa maji safi na taka mjini Mbulu. Gharama ni kubwa kwa vile *master plan* ya mji huu ni ya enzi za Mjerumani na Mito kadhaa hupitia katikati mwa mji. Kwa hiyo, nilitarajia Mbulu ingefikiriwa katika kuhusishwa katika mradi wa maji na usafi wa mazingira katika mwaka wa fedha 2003/2004.

Kwa vile katika *stock route* kati ya Maswa - Meatu - Iramba - Mbulu - Makuyuni uswagaji wa mifugo utaendelea pamoja na kuwepo kwa Waraka Na.1 wa mwaka 2002 kwa vile katika maeneo hayo hakuna reli wala barabara ya lami, basi njia hii yenye kupitisha mifugo mengi ichunguzwe upya ili kubainisha njia yenyewe na maeneo ya minada ya kupumzisha mifugo. Hili ni suala muhimu na la haraka kwa vile kwa sasa kuna ugomvi wa mara kwa mara kati ya waswagaji mifugo na wanavijiji mbalimbali (wakulima na wafugaji ) katika maeneo nililiyoyataja.

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri Mheshimiwa Edward Lowassa na kupitia kwake Viongozi na wataalam wote walio chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Bukoba Vijijini lina matatizo ya aina mbili. Kwanza Tarafa ya Rubale hususan Kata za Kibirizi na Kyarumtaile zina shida kubwa ya maji. Utafiti wa awali umeonyesha kuwa chini ya ardhi kuna miamba na hivyo njia ya visima haiwezekani. Suluhisho la tatizo hilo kwa kuzingatia hatua ya maendeleo ya wakati huu ni kuwachimbia mabwawa, uwezo wa Halmashauri kulingana na ukubwa wa Kata hizi ni mdogo, hivyo naomba Wizara yako kufikiria Kata hizi. Kimaendeleo Kata hizi zimebaki nyuma sana sababu kubwa ikiwa ni tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la pili ambalo kwa bahati mbaya linahusu vile vile Kata ya Kibirizi, ni kuwa jirani na Ranchi ambayo iko kati ya Jimbo langu na Karagwe, hivyo pamejitokeza kuwa na matatizo ya mipaka. Bahati nzuri tatizo hili linajulikana Kimkoa lakini hata hivyo ni vizuri kwa Wizara kujua tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Halmashauri tunajitahidi kushughulikia uchimbaji wa visima kwenye Kata nyingine zenye matatizo ya maji pale inapowezekana lakini kwa sasa sehemu inayoteseka sana sana na tatizo la maji ni hizo Kata mbili nilizotaja hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwasilisha matatizo haya, napenda kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri kwa jinsi anavyoongoza Wizara yake na naunga mapendekezo aliyotoa kwa asilimia mia moja, ahsante.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeomba kuchangia lakini huenda nisipate nafasi ya kuongea. Kwa hiyo, ninaleta muhtasari na maoni yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wote kwa kufanya kazi nzuri, mfano wamemaliza tatizo la maji Dodoma na kupunguza kero katika miji mingine na vijijini, wametuletea hotuba safi, yenye kina na yenye matumaini makubwa kwa Watanzania na wana uhusiano mzuri sana na wadau wote. Ninawashukuru sana hasa wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri na akina Dr. Mohamed na Songea, pale Ubungo.

Pia nawapongeza kwa kutekeleza vizuri sana sera za CCM na Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 200, nawapongeza kwa maadhimisho ya wiki ya maji, makongamano ya wataalam wa maji na mikutano ya kila mwaka ya Mamlaka za Maji. Matokeo ya yote hayo ni huduma bora kwa Wananchi na nawapongeza kwa kubuni utaratibu wa kuwapatia maji wasiojiweza kwa bei nafuu. Lakini nashauri mratibu hatua za mamlaka mbalimbali katika kuwatambua wasiojiweza ili wasiwaache baadhi ya walengwa. Pia, wachunguze tatizo la utoaji wa ankara kwa watu ambao hawapati maji, pawe na dira au la.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeza kwa uamuzi wa kukamilisha miradi ya zamani iliyoachwa. Katika suala hili ninawashukuru kwa kukumbuka mradi wa Mzenga lakini ninakumbusha kuwa licha ya mradi huu

kutekelezwa katika miaka ya 1970 na 1980 Mheshimiwa Waziri na mimi tumeuongelea sana mradi wa Mzenga. Ninamwomba aendeleze imani ya watu wa Kisarawe kwake na Wizara kwa kukamilisha mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbusha ahadi zake mbili alizotoa hapa Bungeni. Mwaka 2002 aliahidi kutatua tatizo la maji la Mji mdogo wa Kisarawe. Kwenye Ibara ya 56 amesema hili litatekelezwa. Mheshimiwa Waziri amedanganywa na wataalam wake, namwomba tufuatane Kisarawe baada ya mkutano huu akaone Wananchi wanavyoteseka na pili, Mheshimiwa Waziri aliahidi kutafuta fedha za kujengea mabwawa ya Titu na Gumba (Kisarawe) na Kitanga (Kibaha) wakati akijibu moja ya maswali yangu Bungeni, bado ahadi hii haijatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa fedha za kusaidia nguvu za wananchi kujenga malambo matatu ya Kazimzumbwi, Kihale na Marui. Lakini ninaomba Mheshimiwa Waziri atutengee malambo zaidi kati ya 180 anayotarajia kusaidia katika Bajeti hii. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa jitihada ya kuchimba visima Vijijini lakini ninashauri kuwa kwenye maeneo kama ya Kisarawe na Kibaha ambako wataalam wamethibitisha kuwa visima vifupi havitoi maji, mkazo uwekwe kwenye malambo.

Kuhusu maji taka, naiomba Serikali isimamie utozaji wa uunganishaji wa mabomba kwenye mifereji ya Manispaa. Pale Dar es Salaam gharama ziko kati ya shilingi milioni 20 na shilingi milioni 10 kutegemea na umbali wa nyumba tokea iliko mifereji. Wananchi wengi hawawezi kumudu gharama kama hizo.

Namalizia mchango wangu kwa kuipongeza Wizara kwa kuleta Bajeti ya kimaendeleo kwani kati ya Bajeti ya shilingi 66,182,327,400/= asilimia 77 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na asilimia 23 tu ndiyo matumizi ya kawaida, hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa hotuba yake nzuri na kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuiomba Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kuzingatia mambo yafuatayo: -

Kuangalia uwezekano wa kuwa na mradi wa Kitaifa wa kutumia maji ya Ziwa Victoria kwa kilimo cha umwagiliaji kwa Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Tabora, Singida na Dodoma. Jimbo la Singida Kaskazini litanufaika moja kwa moja na mpango huo.

Kutenga fedha kwa ajili ya malambo 15 katika Jimbo la Singida Kaskazini kwa ajili ya mifugo na matumizi ya Wananchi. Kata za Ngimu, Mguri, Merya, Ilonyea, Mtimko na Ighanoda zinahitaji sana mabwawa.

Pia uchimbaji wa visima virefu 15 katika Jimbo la Singida Kaskazini na uwezekano wa kutumia maji ya mabwawa na maziwa madogo kwa kilimo cha umwagiliaji na kuboresha huduma ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nawashukuru sana Mheshimiwa Waziri na wote katika Wizara kwa kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema kwamba naunga mkono hoja.

**MHE. SUMRI A. S. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa shukrani nyingi kwa kupata fursa hii ya kuchangia hoja ya Wizara hii nyeti katika uhai wetu viumbe wote. Binafsi nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na wote katika Wizara hiyo kwa maandalizi ya makadirio na upembuzi wa kina katika Sekta ya Mifugo na Maji. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wananchi wa Mpanda Magharibi tuna matatizo makubwa ya maji safi na salama katika vijiji vifuatavyo vyenye hali ngumu. Vijiji hivyo ni Kakese, Mbugani, Mkwajuni, Igalula, Sijonga, Igagala, Kamsanga, Ntumba, Nkungwi, Kasekese, Kapagamsenga, Milundumo, Kaiswa, Kamalamansa, Kasanga Tongwe, Kaselamyage, Kalumbi, Ipakomatana, Mwese, Nkuswe na maeneo mengine mengi katika Tarafa za Karema, Mwese na Kabungu. Maeneo haya yote yana mifugo mingi ambayo inahitaji sana maji.

Tunaomba Wizara itupie jicho katika jimbo hili ambalo lina visima 158 vikiwemo visima virefu 19 na vifupi 56. Kati ya visima hivyo 75 ni visima 67 tu vinavyofanya kazi na visima 8 ni vibovu. Vinavyohitaji ukarabati ni 47 na mahitaji ya visima vipya virefu ni 83.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika makazi ya wakimbizi wa Mishamo kuna visima virefu 179 na vifupi 82 kati ya visima hivyo 261 visima 52 vinahitaji ukarabati. Tunaomba Wizara iweze kutupa msaada wa upendeleo ili Ilani ya uchaguzi ya 2000 - 2005 iweze kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu kuna eneo la mbung'o huko Kasekese. Hivyo, tunaiomba Wizara itupe wataalam ili tuweze kufaidika na mpango huu wa *Tsetse Survey* toka katika mpango wa *PATTEC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la *Integrated Water Resources Management* kwenye Jimbo langu kuna maeneo ya Mto Kaseke na Mto Ifume kuna bonde kubwa la Mito inayohamahama na kuwafanya wakulima wasiwe na mashamba ya uhakika. Hivyo, naiomba Wizara nasi tuwekwe katika utafiti wa kuwekewa mabwawa ili maji yaweze kuwa na manufaa kwa kilimo na mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamtakia afya na furaha Mheshimiwa Edward Lowassa na napenda tena kuunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa hotuba nzuri yenye mipango mizuri. Hivyo, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 41 amesema amekamilisha kutathmini miradi inayohitajika kukamilishwa, jumla ya miradi 794 imepatikana. Ningeomba kujulishwa kama miradi ya maji iliyojengwa na *DANIDA* bila kukamilika katika Kata ya Chiwanda, Mtipwili na Ngumbo imo katika orodha hiyo. Vile vile, ninaomba kufahamu ni lini miradi hiyo Serikali itafanya utaratibu wa kuimalizia ili iweze kuwanufaisha wananchi wa kata hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata yangu ya Mhaha haina maji safi na salama. Naomba sana Mheshimiwa Waziri aiingize Kata hii katika mipango yake ya kupatiwa maji hivi karibuni ili waweze kuondokana na tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu mwaka 1999 alitusaidia shilingi 2,000,000/= kwa ajili ya kuwaunga mkono wananchi wa Kata ya Kingirikiti kufanikisha gharama ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya mradi wa maji katika Kata hii na sasa umekamilika. Wananchi wa Kata ya Kingirikiti wamefungua Mifuko ya Maji na wote wameanza kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake atamke ni kwa namna gani yuko tayari kuwasaidia wananchi wa Kata ya Kingirikiti wanaotapatapa kutatua kero kubwa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Kijiji changu cha Litumbakuhamba Kata ya Lituhi upembuzi yakinifu umekamilika na tunaendelea kuhamasisha wananchi waanze kuchangia Mifuko ya Maji. Lakini kwa nguvu zao pekee kwa kweli itachukua muda mrefu sana kufanikisha mradi huu wa maji katika Kijiji cha Litumbakuhamba. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aweke utaratibu wa kusaidia mradi huu wa maji katika Kijiji cha Litumbakuhamba Kata ya Lituhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga tena mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa sifa nyingi kwa Wizara nzima, Mawaziri na watendaji wote Mikoa hadi Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa sababu kazi inaonekana katika Wilaya hadi Kata kwani Wizara inashirikisha wananchi ambao ndio walengwa. Wizara inashirikisha wananchi kwa kutoa mawazo yao wakati wa Wiki ya Maji ambapo viongozi hutoa maelezo kwenye mikutano ya hadhara, nami nikiwa ni mshiriki kama mwananchi katika Kata yangu hutoa mawazo yangu. Hivyo basi, natoa pongezi kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mchango wangu kuhusu sehemu mbalimbali ambazo wananchi wanahangaika sana kutafuta maji. Wizara ingeanzisha utaratibu wa kushirikisha wananchi kama inavyofanya kwa *TASAF* kwa kutoa michango yao ili wapate maji hata kidogo yaani visima vifupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo sehemu tunapata maji lakini huko vijijini wanapata shida sana. Naomba Wizara iangalie hasa huko Vijijini ambapo wananchi wanahangaika sana na ukosefu wa maji. Suala la *TASAF*, nina imani litasaidia sana kama tutawapa elimu wananchi wetu watatuelewa. Nina imani Wizara ina njia nyingi na iko katika utaratibu huo wa maandalizi lakini kutoa wazo au mawazo si kama Wizara haioni ila ni maoni ya mtu.

Katika nchi yetu kuna mifugo mingi tu na kuna watu ambao wana ng'ombe 400 na huishi nao na kuwalipia kodi hata kwa miaka mitano, je, kwa nini tusiwe na viwanda katika Mikoa husika yenye ng'ombe wengi kama ilivyo kwa samaki? Kwani samaki hao hutuingizia fedha nyingi sana katika nchi yetu? Ng'ombe, mbuzi na kondoo wako wengi sana, je, hatuoni kama nchi yetu inakosa fedha nyingi na wananchi ambao wana mifugo hiyo kuwa maskini wakati wanaishi na utajiri katika mazizi ya ng'ombe?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madawa ya mifugo, wako wananchi ambao wana mifugo lakini hawaoni umuhimu wa kuwa na dawa au Daktari wa Mifugo. Ni lazima na si hiari kuwafanyia utaratibu wafugaji ili mifugo yao iwe inakaguliwa na Madaktari wa Mifugo ili kusiwe na maambukizo ya magonjwa kwa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo mchango wangu ni huo.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Edward Lowassa Mbunge, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa hotubanzuri sana, yenye maelezo ya wazi na takwimu muhimu. Ameisoma kwa ufanisi mkubwa.

Aidha, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Anthony Diallo, Mbunge, Naibu Waziri, Ndugu B. Mahiza, Katibu Mkuu. Pamoja na Wasaidizi wao kwa kazi nzuri wanayofanya ya kumsaidia Waziri kwa uadilifu katika utekelezaji wa majukumu mazito ya Wizara hiyo. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa juhudi zinazofanywa na Wizara hii kupitia kwa Wahandisi wa Maji wa Mkoa wa Tanga na Wilaya ya Lushoto za kuandaa michoro ya miradi ya maji katika Jimbo la Bumbuli. Maji ni Uhai.

Naomba Wizara iendelee kututafutia wafadhili/wahisani wa kusaidia utekelezaji wa miradi iliyona michoro tayari. Kwa upande wetu, tutaendelea kuhimiza uanzishaji wa mifuko ya maji.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya mwaka 2002/2003. Kwa niaba ya wakazi wa Mji wa Kasulu katika Jimbo la Kasulu Mashariki, natoa shukrani za dhati kwa Wizara kwa kupanua tanki la maji na mtandao wa maji mjini Kasulu. Ahsante sana.

Hata hivyo, nitashukuru zaidi iwapo Wizara katika mwaka 2003/2004 itazingatia yafuatayo:-

Kwanza, maeneo mengi ya Jimbo la Kasulu Mashariki kukosa maji. Mkoa wa Kigoma hasa vijiji vya nyanda za juu *(highlands)* ulinufaika miaka ya 1980 na 1990 kutokana na mradi mkubwa wa maji uliosimamiwa na *NORAD* kupata maji ya gravity ambayo hayahitaji mashine za dizeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu haukugusa maeneo ya *low lands* ambayo mengi yako katika Jimbo Kasulu Mashariki na hivyo maeneo haya hayana maji safi na salama na hasa vijiji katika Kata za Nyamidaho na Kitagata. Serikali inaombwa ielekeze nguvu zake huko ili wananchi waishio huko na wafaidi maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhamasisha ufugaji katika maeneo ya *low lands* jimboni Kasulu Mashariki. Jimbo hili lina tatizo la kuwa na ndorobo wengi na hivyo ufugaji ni mdogo sana kiasi kwamba wananchi wanalazimika kwenda umbali mrefu kupata kitoweo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatakiwa ichukue hatua za makusudi kupambana na ndorobo hao na kuhamasisha ufugaji wa mifugo mbalimbali ili kusaidia kupambana na lindi la umaskini uliokithiri katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ahsante.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa juhudi zake za kueneza maji vijijini. Lakini kiwango bado ni kidogo na hakionyeshi uwiano sahihi kimkoa. Je, ni vigezo gani vinatumika kuhakikisha kwamba maji yanafika vijijini? Kwa mfano Mkoa wa Lindi wamefikiwa 11% tu hata nusu haijafika, Serikali haioni hali hiyo itadumaza maendeleoya wananchi ambao wataacha shughuli za uzalishaji kwenda kutafuta maji. Naishauri Serikali iliangalie hili kwa makini ili kuhakikisha maendeleo yanalingana nchi nzma.

Mkoa wa Lindi bado hauna ng'ombe wa kutosha wa kufuga hivyo hata upatikanaji maziwa ni mdogo. Hivi sasa wananchi wa Lindi wakitaka kufuga, hawana mahali pa kununua ng'ombe. Nashauri shamba la mifugo la Ngongo libinafsishwe ili tupate mahitaji yetu ya nyama, maziwa na hata mahali pa kununua ng'ombe wa kufuga.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo maafisa mifugo wachache katika Wilaya ambao hawana hata vyombo vya usafiri vya kuwawezesha kuwafikia wafugaji wachache waliopo Lindi. Nashauri Mikoa kama Lindi ambapo wananchi wanahitaji kuendelezwa na kufundishwa ufugaji bora, basi maafisa mifugo wapewe usafiri wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Edward Lowassa, *well presented Budget Speech.* Lakini ibara uliyosema ya *World Bank* kusaidia miji kadhaa *including* Sumbawanga, mbona haiko *clear.* Nisaidie nielewe taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia na niko pamoja nawe lakini naomba *brief* tu ya Sumbawanga Mjini. Ahsante sana.

**STANLEY H. KOLIMBA:**Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutambua na kubaini matatizo makubwa inayokabili mradi huu. Kwa taarifa zaidi mradi huu ulikusudiwa kutoa maji kwa ajili ya shule ya sekondari Manda ambayo hadi sasa ina wanafunzi takriban 400 na mipango ya kuongeza *intake* imekamilika lakini kikwazo ni maji. Kwani vyanzo vya maji ikiwemo Ziwa Nyasa vipo zaidi ya kilometa nane.

Aidha, juhudi za Wizara yako kuchimba visima katika eneo hili vilisitishwa na nashauri ufumbuzi wa eneo hili ni kutekeleza mradi wa Lifua-Manda kama ulivyopangwa hapo awali au kusaidia shule hiyo na mtambo wa kusukuma maji toka Ziwa Nyasa wakaazi wa eneo hili wapo tayari kugharimia uendeshaji wa mtambo huo. Vinginevyo Wizara inatakiwa kuendeleza utafiti wa maji katika eneo la shule licha ya kusitishwa kwa kukatishwa tamaa na matokeo hafifu usafiri wa awali unaonyesha maji yapo chini zaidi ya mita mia na siyo hata chini ya mita sabini.

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya Kamati ya Kilimo, Ardhi, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo imeshauriwa kufanya tathmini kwa kutembelea na kutambua miradi yote ya maji iliyosimama au kufa na kuweka programme maalum ya kuifufua.

Kwa kuzingatia ushauri huo naomba, Wizara itakapokuwa na programu maalum ya kufanya tathmini itembelee kijiji cha Kitete, Kata ya Dumila, Wilaya ya Kilosa. Katika kijiji hiki pana kisima ambacho tayari kimechimbwa kwa zaidi ya miaka 20 sasa na taarifa zilizopo zinaonesha kisima hiki kina uwezo wa kutoa maji safi na salama kwa vijiji vya Kitete, Mfufu na Madudu vyenye watu zaidi ya 10,000.

Aidha, nashauri Wizara itembelee kijiji cha Mbwade, Kata ya Chanjuru. Katika Kijiji hiki karibu na nyumba ya ndugu Bozeni na John Andolile pana kisima kirefu kilichochimbwa zaidi ya miaka 20. Kisima hiki kina

uwezo wa kutoa maji safi na salama kwa vijiji vya Mbwade, Kimamba B na Kimamba A, vyenye watu wanaokadiriwa kuwa 20,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitafurahia kama Mheshimiwa Waziri atanithibitishia vijiji hivyo vitakuwa katika programme Wizara ya kutathmini miradi yote ya maji iliyosimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shamba la mifugo la Mkata kwa upande a Kilosa wakati shamba hili lilipokuwa linaendeshwa, palikuwa na Tanki kubwa la maji kwa upande wa Kilosa mara tu baada ya kupita kijiji cha *Mkata Station.* Kwa kuwa shamba limekufa, haliendeshwi kama ilivyokuwa zamani hivyo hili tanki kubwa la maji nalo halitumiki. Hali ilivyo sasa zipo dalili kubwa ya tanki hili la maji kuibiwa kama jitihada madhubuti zisipochukuliwa tanki hili litapotea. Naomba kumshauri Mheshimiwa Waziri, akubali kulitoa tanki hili kwa watu wa Kata ya Kimamba A.

Kwa hali ilivyo sasa Kata za Kimamba A na Kimamba B watu wake wanaongezeka sana, hasa pale Mamlaka ya Mkonge Tanzania kabla ya kubinafsishwa ilipotoa eneo kubwa la ardhi kwa ajilii ya upanuzi wa Kimamba A na Kimamba B. Tanki la sasa ambalo lipo Kimamba B haliwezi kabisa kutosheleza kutoa maji safi na salama kwa watu wa Kimamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kutoa ombi kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, akubali kulitoa tanki hilo kwa watu wa Kimamba A badala ya kuliacha bure bila kutumika kwa pale lilipo na kupelekea vishawishi vikubwa vya kuibiwa kwa hili tanki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kuwawezesha wataalam wake kuwa wabunifu wa vyanzo vya maji. Katika Wilaya ya Kilosa, Mhandisi wa Maji wa Wilaya kwa kushirikiana na Mhandisi wa Maji Mkoa pamoja na wanavijiji vya Rudewa. Rudewa Gongoni, Kijiji cha Peapea na Kijiji cha Rudewa Mbuyuni wanaweza kubuni njia ya kuyapata maji kwa njia ya gravity kutegemeana na *pressure* ya maji, Mhandisi wa Wilaya amekubali maji hayo kufika Rudewa Tembeni, Madoto na Kimamba. Utekelezaji huu ukifanikiwa gharama ya umeme kwa matumizi ya maji yatapungua kwa asilimia kubwa kwa vijiji hivyo. Haya yakifanikiwa utakuwa mfano bora wa kuigwa. Narudia tena kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kuwa na mpango katika Wizara yake kuwawezesha wataalam wake kuwa wabunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kamati ya Kilimo, Ardhi, Maji na Maendeleo ya Mifugo imeshauri Serikali iharakishe kutekeleza mpango wa kutenga maeneo ya ufugaji na kilimo na Kamati imeshauri pia Wizara kuweka lengo na muda wa kukamilisha zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa *Mkata Ranch* ni moja ya maeneo haya namwomba Mheshimiwa Waziri, atamke utaratibu mzima utakaotumika katika kugawanya shamba hili la Mkata na atamke utekelezaji wake utaanza lini na utamalizika lini ili kutoa nafasi kwa watakaohitaji maeneo hayo kuanza kupanga maandalizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni nchi ya tatu kwa wingi wa mifugo Barani Afrika. Tuna ng'ombe milioni 17.7, mbuzi milioni 12.5 na kondoo milioni 3.5. Lakini bado idadi hiyo ya mifugo inachangia Pato la Taifa dola za Kimarekani milioni 7 *(US $ 7 million)* kwa upande wa fedha za kigeni kiasi hicho ni kidogo sana ikilinganishwa na nchi ya Botswana ambayo ina ng'ombe milioni 2.5 pamoja na mazao yake ya mifugo huipatia nchi hiyo fedha za kigeni zipatazo dola za Marekani milioni 600 (*US $ 600 million).* Hii inaonesha mapato yetu ya fedha za kigeni yangekuwa mara sita. Tungeweza kupata dola za Kimarekani milioni 3,600 *(US $ 3,600 million)* kwa kulingnisha idadi ya wingi wa mifugo yetu na idadi ya mifugo ya nchi ya Botswana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa kuwa na utaratibu wa kuwawezesha wafugaji na wataalam wenye taalam ya mifugo kuendesha shughuli za ufugaji kibiashara ni jaribio jema, nashauri kwa kuwa Waziri wa Fedha katika Bajeti yake amesema Serikali itaanzisha Benki ya Wavuvi, wafugaji na wakulima, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo awe mstari wa mbele katika ufuatiliaji wa kuanzishwa kwa Benki hiyo. Hiyo ndiyo njia pekee itakayoweawezesha wafugaji, wakulima na wavuvi kuweza kuendesha shughuli zao kibiashara.

Aidha, nashauri Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo katika hoja hii ya kuanzishwa kwa Benki, aanze kufikiria sasa kuwa mtindo wa taratibu za kupata mkopo wa fedha benki kama ulivyo sasa hautowezesha wataalamu

wa kazi za mifugo, wafugaji na wakulima. Namshauri akubali mfumo wa dhamana *(Collateral)* kama mabenki yanavyotaka sasa hautowezesha ufugaji kuendeshwa kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili hii naomba kumshauri Mheshimiwa Waziri aweke utaratibu wa kujua idadi ya wataalam wa mifugo walio tayari kufuga kibiashara. Awe na idadi ya orodha ya wataalam hao kwa nchi nzima na awe na idadi ya wakulima/wafugaji nchi nzima. Baada ya kujua idadi hiyo ajenge hoja Serikalini ya kutaka dhamana ya mikopo kwa wataalam wa mifugo iwe elimu yao na dhamana ya wafugaji na wafugaji/wakulima iwe ni uzoefu wao katika sekta hii ya mifugo.

Bila kuwa na mikakati ya kuwahusisha wafugaji na wakulima wadogo wadogo, haitakuwa rahisi kuendesha sekta ya mifugo kibiashara, kadhalika bila ya Serikali kuangalia upya vigezo vya utowaji wa mikopo hiyo benki inayokusudiwa kuanzishwa kwa ajili ya wavuvi, wafugaji na wakulima haitokidhi haja ya kuwa na benki hiyo kwa sababu wavuvi, wafugaji na wakulima itakuwa vigumu kwao kuwa dhamana *(Collateral)* itakayohitajika benki, kwa ajili hii benki hii itawanufaisha matajiri wenye fedha na raslimali kubwa kubwa ambao katika nchi yetu watu wenye sifa hizo wapo wachache na hawana uzoefu wa ufugaji au ufugaji wa kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshauri Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kuwa hoja ya Elimu ya Wataalam wa Mifugo, na Wataalam wa Taasisi nyingine kuchukuliwa kuwa ndiyo dhamana ya kuomba mikopo katika benki ya wavuvi, wafugaji na wakulima ndiyo msingi mkubwa wa kuwawezesha wataalam hao kuendesha ufugaji wa kibiashara.

Kwa kuwa Serikali imewekeza mtaji mkubwa katika kuwaelimisha wataalam hao, sioni vipi Serikali isiweze kukubali uwekezaji huo unafaa kumuwezesha mtaalam kupata dhamana ya kukopa. Aidha, kwa kuwa uzoefu wa wafugaji na wakulima unafahamika sioni sababu vipi uzoefu wao usiwawezeshe kuwa dhamana ya kupata mikopo katika benki inayokusudia kuanzishwa ya wavuvi, wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa lipo tatizo linalosababishwa na wafugaji kupendelea kuwa na mifugo mingi kuliko maeneo yao ya malisho na kwa kuwa mara nyingi hutokea migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji naomba kumshauri Mheshimiwa Waziri jambo hili alifuatilie kwa karibu zaidi yeye mwenyewe binafsi. Kwa maoni yangu naona haitoshi kwa Mheshimiwa Waziri kufikiria mgogoro huu utatatuliwa na Halmashauri za Wilaya peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika ni jambo lililo wazi ili wafugaji wapunguze mifugo yao yapo mambo ya msingi ambayo lazima kwanza yashughulikiwe. Baadhi ya mambo hayo ni kupatikana kwa soko la mifugo. Haitoshi peke yake kuwataka wafugaji wapunguze mifugo yao bila ya kuwapatia soko la uhakika la kuuza mifugo yao. Jambo hili kwa maoni yangu halitoshi peke yake kuadhiwa uongozi wa Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika kwa ajili hii nashauri Wizara iweke mikakati ya dhahiri istakayo wahakikishia wafugaji watakapo punguza mifugo yao watakuwa na uhakika wa soko la mifugo yao. Pili kwa kuwa baada ya kupunguza mifugo yao wafugaji watahitaji kutoa matunzo makubwa na mazuri kwa mifugo yao, ili kuwawezesha kuwa na mifugo bora, nashauri, Mheshimiwa Waziri asimamie yeye mwenyewe binafsi tamko la Waziri wa Fedha la kufungua na kuanzisha benki ya wavuvi, wafugaji na wakulima.

Katika kufanikisha na kuwawezesha wafugaji, nashauri masharti ya kuwakopesha wafugaji iwe ni uzoefu na mifugo walionayo ya kukopa. Aidha, kwa kuwa uzoefu wa wafugaji na wakulima unafahamika sioni sababu vipi uzoefu wao usiwawezeshe kuwa dhamana ya kupata mikopo katika benki inayokusudiwa kuanzishwa lya wavuvi, wsafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa hotuba nzuri aliyowasilisha Bungeni. Halikadhalika nampongeza Naibu Waziri na Maafisa wote walioandaa hotuba hiyo yenye mwelekeo wa kutatua na kuboresha mahitaji ya maji kwa watu na mifugo yao. Kwa malengo mazuri yaliyopo kwenye hotuba hii, naunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ya Maji na Maendeleo ya Mifugo imejitahidi sana kufunga mita kwa wateja wake kwa misingi ya kutoa haki kwa watumiaji. Lakini nimeshangaa kuona Bodi ya Maji Shinyanga inafanya makadirio ya ulipaji wa matumizi ya maji kwa wateja wake badala ya kusoma mita. Ni jambo la kushangaza wanafanya makadirio hata kwa matumizi ya ng'ombe na bustani hata kama haya inakisima kwa matumizi ya mifugo na bustani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi wa mabadiliko haya, ametoa yeye au Bodi za Maji zinafanya hivyo kwa maslahi yao? Kwa sababu Mheshimiwa Waziri Edward Lowassa anapenda sana kutenda haki kwa watumishi wake kwa misingi hiyo namwomba asimamie haki kwa wananchi wa Shinyanga wasidhulumiwe na hivyo utaratibu wa mita utumike.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Waziri kuwa wanawake wa Mkoa wa Shinyanga wanatoa huduma nzuri ya maji kwa kutumia visima walivyochimba wenyewe katika vikundi vyao. Katika hili, namwomba Mheshimiwa Waziri, wanawake hao wapewe mafunzo ya jinsi ya kutumia dawa za kusafisha maji ili kuwa na maji safi na salama ili kuepusha magonjwa ya mlipuko kama kuhara, kuhara damu na kipindu pindu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu dawa za kutibu na kuzuia magonjwa ya mifugo, namwomba Mheshimiwa Waziri, maduka ya dawa hizo zikaguliwa ili wasiuze dawa zilizopita muda wake. Kwa sababu baadhi ya dawa za kutibu ni mifugo zinawadhuru wanapotibiwa na kusababisha upofu hasa ng'ombe. Hii ni hasara kubwa hasa kwa ng'ombe dume kwani wanashindwa kutekeleza wajibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, inawezekana sitapata nafasi ya kuchangia kwa mdomo. Hivyo naomba sana nichangie ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yao kwa kazi nzuri wanayofanya katika sekta ya Maji na Mifugo na mwelekeo mzuri walioonyesha kwa muda mfupi.

Pamoja na shukrani na pongezi hizo, narejea tena ombi letu kuwa mwaka 2002 niliwasilisha ombi letu kwa Mheshimiwa Waziri kuja kuzindua miradi mikubwa ya maji Wilayani Karatu, ambayo imegharimu zaidi ya shilingi bilioni 2 kwa msaada wa *MISEREOR, CARITAS AUSTRALIA, ISF-SPAIN,* Ubalozi wa Uholanzi na karibu yote hutekelezwa na *Diocese of Mbulu* kwa kushirikiana na Bodi za Maji. Kwa bahati mbaya ilishindikana, pamoja na barua ya *DC* na kupitishwa na *RC.*

Tunaomba, ili kuwapa moyo wafadhili wetu ambao wamefanya kazi kubwa sana kutufadhili miradi hiyo ambayo nayo tulipata mchango wa Serikali kwa mfano, miradi hiyo izinduliwe mwaka huu kati ya Oktoba na Novemba. Ningependa kupata ahadi ya Waziri ili tufanye maandalizi yanayoikabili.

Mwaka 1977 niliomba Hati Miliki ya maji Wilaya ya Karatu itazamwe upya, kwa lengo la kusaidia wanavijiji walio wengi kupata maji kwa matumizi ya nyumbani. Serikali iliahidi kufanya kazi hiyo. Je, sasa tumefikia hatua gani, kutazama upya hati miliki hizo, ambazo zote zinamilikiwa na mashamba makubwa ya mikataba (isipokuwa chache tu) na kurekebisha pia sheria husika.

Serikali iko tayari kukarabati Bwawa la Bashay ambalo ni muhimu sana kwa matumizi ya mifugo kwa Kata za Bashay/Qurus na vijiji vyote vya jirani. Bwawa hilo lilibomoka mwaka 1994 na Serikali ilijulishwa. Tunaomba Wizara itupe msaada katika hili. Wataalam wa *Oxfam* walitaka kufadhili na walikisia 38 milioni mwaka 1999, lakini baadaye walibadili sera yao.

Wizara isaidie kuimarisha Bodi 7 za Maji tulizounda kwa Sheria ya *Trustees Cap. 375* mathalan Kaviwasu ambayo inasimamia mradi wa maji wa vijiji 6 ikiwemo mji wa Karatu. Je, Wizara iko tayari kutusaidia kwa *Capacity Building* ili Bodi hizo zifanye kazi zake kwa ufanisi zaidi kufuatana na sera na sheria za maji?

Natanguliza shukrani za dhati. Naunga mkono hoja, lakini napenda kupata msaada katika maeneo hayo.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia japo kwa maandishi Wizara hii nyeti ambayo inashughulikia maji na Maji ni Uhai na pia Mifugo na Mifugo ni Chakula bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa hotuba yake nzuri mno ambayo kwa kiwango kikubwa sana imeshatekelezeka na mafanikio yake tumeshayaona. Ahadi zinatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri anapojumuisha hotuba yake aliambie Bunge lako Tukufu idadi ya majosho yaliyoko kwenye kila Wilaya ya wafugaji na yako umbali gani toka josho hadi josho na kila mwezi inagharimu shilingi ngapi za dawa ya kuchanganya kwenye maji kuua kupe, chawa, viroboto na magonjwa ya ngozi ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maji amejitahidi kwa kiwango kikubwa sana na pale ambapo Serikali inashindwa kukamilisha huduma ya maji kwa wananchi wake anapata Wafadhili/Wahisani kutafuta vianzo vya maji na kusambaza maji kwa walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya wafadhili hawa kukamilisha mradi wa maji anatafutwa mzawa awe na *NGO* iliyoandikishwa na kutambuliwa rasmi kuhodhi mradi na kuuendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko *NGO* nyingi zilizomudu kuhudumia wananchi kwa maji safi na salama bila manung'uniko yoyote kama vile *Karatu Water Users Association, Losaa - KIA Water Users Association, Uchira Water Users Association* na kadhalika, kwa bahati mbaya sana, kuna Kampuni za kuendeleza mradi wa maji zimeshindwa kusimamaia ipasavyo kuanzia walipokabidhiwa mradi wa maji na Wazungu/Wafadhili hadi leo kwa zaidi ya miaka 10 kama vile *Kili Water Co. Ltd.* ya Wilayani Rombo yenye tawi lake Kanda ya Mwika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Kili Water* haina uwezo kama *JR* ya Arusha. Matokeo yake hubinafsisha vianzo vya maji, miundombinu waliyoikuta, kung'oa vilula vilivyowekwa kila umbali wa mita 400 na kuacha vya mtu kutembea kilomita 2 hadi 3 kutafuta maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kusafisha kahawa na kuwapa (mifugo) ng'ombe ambapo mmoja kwa siku hunywa debe 4 hadi 6.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi toka *Kili Water Co. Ltd.,* ilipoingia Mwika 1993 hadi 2003 kiasi cha miaka 10 haijasafisha matanki hivyo na hasa zile mvua za *El Nino* 1997/98 zimejaza udongo, mizoga ya vyura, mijusi, wadudu, nyoka na hadi leo hawajali kusafisha matanki hayo wala kuweka dawa kama vile *Waterguard/Chlorine.* Wananchi sasa wanakunywa maji taka yenye viluwiluwi na hivi sasa hospitali, Zahanati na Vituo vya Afya vimejaa wagonjwa wa matumbo, homa za matumbo kwa wanafunzi, watoto na watu wazima. *Med-kit* husika haitoshi hata kidogo kwa muda uliokusudiwa.

Bajeti za Wizara zote zimeathirika kwa ujinga na uzembe wa Kampuni hii uchwara. Wanafunzi kila mara ni hospitali, hivyo elimu kushuka watu wazima kila mara ni hospitali hivyo nguvu kazi, uzalishaji chakula na pato la Taifa kushuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya hayo, Kampuni hii ya *Kili Water* imepunguza maji waliyoyakuta ya *Mtiro Pipe line* na *Matala Pipe line* toka 60% hadi 33% na hata Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo alipotembelea mradi huu wa *Kili Water Co. Ltd.* Wilayani Rombo Machi/Aprili, 2003 alishuhudia na kuliarifu Bunge lako Tukufu katika kikao kilichopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake ni wananchi kupata maji kwa mgao na hayatoshi, kahawa kutosafishwa kwa maji ya kutosha kama debe moja la kahawa kwa debe 5 hadi 6 za maji hivyo kahawa kubakia na uvundo unaoharibu bei ya kahawa, viwanda vya kupukuchulia kahawa kutopata maji ya kutosha hivyo hata ile kahawa ya daraja la "AAA" halipatikani na matokeo yake bei ni ya chini kwani daraja ni la chini. Mifugo hasa ng'ombe za maziwa wameathirika sana hivi sasa hawatoi maziwa ya kutosha hivyo lishe ya jamii na kipato kimeshuka mno na ukichangia bei ya kahawa kushuka ulimwenguni, basi, wananchi kwa ujumla wamekumbwa na umaskinji, ada za shule kushindikana hasa wa sekondari na malipo ya matibabu kushindikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na unyanyasaji huu wananchi wa Kata za Mwika, Mamba, Makuyuni na Himo toka mwaka 2000 hadi Aprili, 2003 wametozwa jumla ya shilingi 9,898,313/= na 10% yao ni shilingi 989,831/30 lakini hawakupewa wala hakuna *Bank Account* iliyofunguliwa kwa hii ijulikanayo kama *Kili Water Co. Ltd., Mwika Zone* wangelipwa fedha hizi matangi yangesafishwa na maji kuwekwa dawa watergard kwa afya yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi waliowahi kushika madaraka wamewahi kuongoza na kushauri *Kili Water Co. Ltd.,* ikashindikana wala hawajali. Nao ni Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, akiwa Waziri wa Maji na Nishati, Mheshimiwa Profesa Ngwiliza, aliyekuwa *RC* Kilimanjaro, Mheshimiwa Phillemon Sarungi, aliyekuwa *RC* Kilimanjaro, Mheshimiwa Mbesere, aliyekuwa *DC* Moshi na Mheshimiwa Clemence Orauya, aliyekuwa *DC* Moshi, Ndugu James Mbatia aliyekuwa Mbunge wa Vunjo, tarehe 24 Julai, 2003 Mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema na mimi Mbunge wa sasa wa Jimbo la Vunjo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 5 Mei, 2003 kwenye mkutano mkuu wa washika dau wa *Kili Water Co. Ltd.,* uliofanyika *Uhuru Hostel* Moshi, Mwenyekiti wa Kikao hicho Mheshimiwa Hilda Ngoye, Mbunge na *RC* Kilimanjaro alimuamuru *DC* wa Moshi na mimi Mbunge wa Vunjo pamoja na Wajumbe wa *Kili Water Co. Ltd.,* kutembelea vijiji vya Mwika na kazi hiyo ilifanyika mwezi huo wa Mei, 2003 na hadi sasa *Kili Water Co. Ltd.* hawajarudishia vilula walivyong'oa Kanda ya Mwika wala kusafisha matanki/visima walivyosiriba milango yake kwa sementi, kuondoa vifuniko vya *Cast Iron* na kuweka vya mbao zinazooza na kufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Kili Water* imepuuza hata amri ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro aliyewekwa na Mtukufu Rais. Wazee kadhaa kwa kuchukizwa, wamemwandikia Mtukufu Rais barua ambayo mimi hakika sikuifahamu, kumwomba Rais afukuze kampuni hii kutoka Mwika. Matokeo yake wazee hawa wanahojiwa kila siku na Uongozi wa Mkoa kwa kitendo hicho cha kumwandikia Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninaamini Mheshimiwa Waziri ni mwelewa na kampuni hii imeshaipa Kanda ya Mwika *grace period* hadi Oktoba, 2003 nami nasema hakika waondoke Mwika kwani wameshafedhehesha Serikali ya Mtukufu Rais vyakutosha na kwamba warudishie kile kiwango cha maji cha 60% Kanda ya Mwika ili Mwika ijitegemee kwa kuzingatia agizo la Rais akifungua Bunge jipya 20 Novemba 2000 kuhusu maji.

Mheshimiwa Naibu Spia, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Waziri kwa hotuba yake yenye mwelekeo wa maendeleo. Naomba kutoa ushauri kwa mambo yafuatayo:-

Kwanza, Mkoa wa Kigoma Kata ya Ikigalu, ingawa Kata hii inayo maji ya Ziwa Tanganyika na Mto Malagarasi karibu, lakini vijiji vyake vina tatizo kubwa la maji. Naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuipatia maji kata hii ili kuwasaidia kina mama wanaopoteza muda kutafuta maji.

Kuhusu huduma ya mifugo, nashauri wafugaji wapewe mafunzo ya kuhudumia mifugo yao kama vile kuchoma sindano na kutambua matatizo ya magonjwa. Umezuka mtindo wa waganga wa mifugo kufanya biashara. Hawatoi dozi kamili na wanadai malipo makubwa bila risiti toka kwa wafugaji. Serikali inakosa mapato na mfugaji hapati huduma inayofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, afadhali mfugaji akajinunulie dawa na kuhakikisha mifugo yake inapata dozi kamili kuliko ilivyo kwa sasa. Hebu fanyeni utafiti na kuona jinsi tatizo hili lilivyokubwa. Watumishi wanapewa mishahara lakini kazi yao ni biashara siyo huduma. Hivi Serikali inaingiza fedha kiasi gani kutokana na huduma za mifugo?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

**MHE. DR. CHEGENI R. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kuandaa Bajeti nzuri napevu kwa ajili ya Wizara yake. Hotuba ya mwaka huu ni mkakati endelevu kufuatia bajeti ya mwaka jana.

Hata hivyo pamoja na mkakati huo napenda tu nimshukuru sana kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Busega kwa Wizara yake kutenga fedha kwa ajili ya kufufua mradi wa maji wa Nassa kwa mwaka 2003/2004. Aidha, sambamba na utekelezaji huo naomba sana Wizara itenge fedha kwa ajili ya kukarabati malambo ya Nyaluhande, Shigala na Dilanda (Mkula). Malambo haya yalijengwa zama za kale lakini yamwashaziba.

Hivyo naomba sana kupitia Bajeti hii yapatiwe fedha ili yakarabatiwe na kuwawezesha wananchi kupata huduma ya maji safi kwa ajili yao na mifugo.

Mwisho, naomba msaada wa fedha kwa ajili ya kukamilisha mradi wa maji ya Kalemera - Mkula.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hotuba ya Wizara ya Maji na Maendeleoya Mifugo na kuwapongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mbunge Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na timu ya Wataalam wake wa maji na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara hii kwa jinsi inavyotekeleza wajibu wake kwa umahiri na kutekelea matatizo yanayoletwa kwake. Nina machache ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usimamizi wa raslimali za maji na uendelezaji kilimo cha umwagiliaji (mabonde ya maji ya Pangani na Rufiji). Sikuelewa kwa nini mabonde ya mito mikubwa ya kusini imeachwa katika mpango huu. Mabonde ninayozungumzia ni Mto Ruvuma, Mto Matandu Kilwa, Mto Lukuledi Wilaya ya Masasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kuzungumzia mara nyingi humu Bungeni kuhusu mabonde haya na hasa kuhusiana na Wizara ya Kilimo na Chakula. Wakati fedha zinapopatikana, mara kwa mara mabonde lhaya ya kusini yanaachwa ama kwa kusahauliwa ama kwa makusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namsihi Waziri safari hii asiyaache mabonde haya katika mpango yake ya umwagiliaji. Mabonde haya yana uwezo wa kuzalisha mazao ya kutosha kulisha nchi nzima. Kuendeleza mabonde haya kutatoa ajira kwa wananchi wengi vijijini na hivyo kuinua kiwango kiwango cha uwezo wao kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia mikakati ya Wizara kufufua miradi ya maji vijijini. Nakubaliana na sera hiyo ila katika jimbo langu kuna maeneo ambayo kwa miaka zaidi ya 10 wananchi wanatafuta maji kwa kiasi cha kilomita 10. Matatizo haya tumeyaleta Wizarani pamoja na kitengo cha *Japanese Counterpart Fund* lakini hatujafanikiwa sehemu husika zimetajwa katika kitabu cha Nyongeza ya Taarifa ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. Sehemu hizo ni Mlingula, Chikoweti, Chiwale, Namajani, Nanyuindwa, Mpanyajni na Mihima ama eneo karibu lote la Masasi Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili linahitaji mpango maalum ambao namwomba Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo aliweke katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mpango wake huu. Nitashukuru pia akinipa maelezo ya awali juu ya atakavyotekeleza mpango huu, ili nikawaeleze wananchi wa eneo hili kwani wamekwishakata tamaa. Suala hili ni kero kubwa kweli.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kusaini makubaliano ya mradi wa Nyahiti kuja Misungwi. Ombi langu ni kuwa tafadhali sana katika majumuishio liongelee kwani jana Makamu wa Rais aliliongelea na kukerwa na mradi huo. Natafurahi sana katika majumuisho kuisikia.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, salaam. Utakapokuwa una-*wind - up* ukiitaja hoja yangu utanisaidia maana wenyewe watajua kuwa nawapigania.

Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Katika hoja hii nauelekeza mchango wangu katika kurejea ombi langu la kuwaondolea shida ya muda mrefu ya maji wananchi wa Kilolambwani na Chikonji.

Nimemwona Mheshimiwa Edward Lowassa na kisha kumwandikia barua juu ya suala hili. Kufuzu au kufeli kwa CCM katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 Jimboni Mchinga kutatokana na suala la maji Kilolambwani na Chikonji. Ahadi ya tatizo hili kutatuliwa na Wajapan ni ya muda mrefu na wananchi wamechoka

nayo. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anatoa maelezo awafahamishe wananchi wa Kilolambwani na Chikonji juu ya azma ya Serikali katika kuwaondoshea kero hii.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu hotuba ya Bajeti ya Wizara yake kwa ufasaha na utaalam wa hali ya juu. Ingawa hotuba yake ameisoma kwa ufupi maelezo yaliyomo ndani ya kitabu ni ya kina na yanatosheleza.

Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Naibu Waziri na Wataalam wote chini ya Katibu Mkuu kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri kuandaa hotuba hii.

Naipongeza Wizara chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri kwa kuonyesha mwelekeo mzuri wa kufufua miradi ya maji. Kwa jumla pamoja na uwezo mdogo wa kifedha lakini tunaona kuwa malengo yaliyopo yanakidhi haja ya Wizara hiyo kuwapo *(justify existance).* Namshukuru Waziri kwa kuitambua miradi ya maji isiyofanya kazi kwa mfano, *Ngara Heights Water Scheme.* Kwa vile pia Ngara imeingizwa katika mradi wa *RWSSP* unaotekelezwa kwa mkopo wa Benki ya Dunia ni matumaini yangu kuwa sasa mradi huo wa *Ngara Heights* unafufuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia ufugaji wa ng'ombe wa maziwa ambao sasa umeenea sehemu nyingi vijijini na mijini, hasa kutokana na utaratibu wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe. Mradi huu ni mzuri kwa vile una manufaa mengi kwa mfano maziwa kama chakula bora na kuuzwa ili kuleta fedha lakini samadi husaidia sana kurutubisha mashamba. Ufugaji ni ajira nzuri. Tatizo linalowakumba wafugaji ni kwamba wataalam wa mifugo ni wachache sana hivyo wakulima hawapati huduma za ugani za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utumiaji wa maziwa bado halijapata kueleweka vizuri huko vijijini na mijini kwa kulinganisha bei ya chupa ya soda ml 250 ni kubwa zaidi kuliko bei ya lita moja ya maziwa au katika baadhi ya maeneo bei huweza kulingana unakuta watu wanakunywa zaidi soda lakini kwa kuangalia ubora maziwa ni bora zaidi kwa maana hiyo hiyo watu hupendelea kunywa pombe ambayo haina ubora au ni sumu mwilini (gongo) badala ya maziwa ambayo hujenga mwili.

Nashauri kampeni ya kutosha ifanyike ili watu wapende kutumia maziwa. Watoto wapatiwe maziwa, wanawake wajawazito wanywe maziwa, watu wote wanywe maziwa. Naomba nimalize kwa kuwatakia Mheshimiwa Waziri na Naibu wake utekelezaji mzuri wa Bajeti yao. Naunga mkono hoja.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji wote, Wakuu wa Idara na wafanyakazi wote nchini wa mamlaka zilizoko ndani ya Wizara hii.

Mnamo mwaka 1994 *JICA* ilifanya tathmini ya ujenzi wa Bwawa la hifadhi ya maji Mto Ruvu eneo la Mkulazi. Je, mpango huo umeishia wapi?

Maeneo ya mijini likiwemo jiji la Dar es Salaam, maeneo ya Kipawa, Gongo la Mboto ambako familia ipo, Mbunge wetu alilalamika sana sana maji kutoka mara moja au mara mbhili kwa mwezi lakini *bill* huletwa za mwezi mzima. Hii inatokana na nini?

Malambo yaliyochimbwa Morogoro Vijijini. Katika jedwali inaonyesha kuwa Malambo ya Ekenywa, Mlilinawa, Mkulazi tayari.

Ni kweli Mlilingwa lilijengwa na *World Vision,* lakini lilibomoka na *El-Nino* ya kwamba Wizara yako ilinipatia 9,000,000 kwa ukarabati wa malambo matatu lakini hadi sasa bado hadi jana nilienda huko, hakuna lolote linalofanyika. Nina wasi wasi kama fedha hiyo 9,000,000 kama ipo kweli!

Kuhusu kodi za mifugo, naomba wakati unajibu hoja ulieleze Bunge hili kodi zipi halali na zipi ambazo zimefutwa ili wafugaji wasibabaike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu migogoro ya wafugaji na wakulima, tunafanya nini? Mambo mengi sana tuliamua kule Arusha mwezi Aprili, 2001. Kwanza ninafikiri ma-*DC* bado kuunda zile Kamati hadi leo. Hivi sasa

Tarafa ya Mikese na Ngerengere yapo matatizo mazito ambayo yataleta matukio mabaya. Hii leo nimepokea taarifa ya Mgongola ng'ombe walikula mipunga ya wakulima.

Ninaomba Serikali isaidie wafugaji kwa kuwapa maeneo ya kudumu na kutoa huduma muhimu huko, kufuta kodi ambazo zinakera wafugaji, kuwapa madawa kwa bei nafuu na shamba la Dakawa wafugaji waligawiwa lakini eneo hilo halifiki mtoni, kupitisha mifugo yao ni shida wanaomba sana wapewe eneo hadi mtoni.

Natoa pongezi za dhati kwa Wizara hii kuamua kuhamia Dodoma. Hata tukibadili hali hii na kusema kuwa Makao Makuu yawe Dar es Salaam naomba mbaki huku huku au mdai *disturbance allowance.*

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa umakini wake katika kazi zake za kila siku za uwaziri. Pia namshkuru Naibu Waziri wake kwa kuwa msaidizi wake mzuri sana, aidha nampongeza Katibu Mkuu, Makamishna, Wakurugenzi na Wasaidizi wake mbalimbali walioshiriki sana kuandaa hoja hii vizuri na kwa makini sana.

Pamoja na hayo naomba kujua Wilaya ya Kondoa tupo katika programu ya mradi wa maji na mazingira, chini ya Benki ya Dunia. Vijiji 10 na mji mdogo wa Kondoa vipo katika miradi ya kwanza kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba unaohusu vijiji hivyo 10 tayari umesainiwa Wilayani ili shughuli zianze. Lakini kuhusu mradi wa maji na mazingira katika mji mdogo wa Kondoa bado Mkataba haujasainiwa hadi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kupata maelezo ya kuridhisha ni kwa nini kazi hii ichelewe na kwamba sasa shughuli za kusaini mkataba zitafanywa lini? Wananchi wanataka kufahamu hilo na kazi zitaanza lini? Hata hivyo, naunga mkono hoja.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Katika hotuba ya Bajeti ya mwaka 2002/2003, Mheshimiwa Waziri alilieleza Bunge uamuzi wa Serikali wa kubakiza Ranchi ya Kongwa mikononi mwa Serikali kwa madhumuni ya eneo hilo kuwa ni *Disease Free* kwa *Export* ya nyama na pia Ranchi kuwa *hub* ya kueneza ufugaji bora kwa wananchi wanaozunguka Ranchi.

Baada ya uamuzi huu muhimu tunaamini mwaka uliopita ulikuwa ni wa maandalizi. Mwaka huu 2003/2004 napendekeza yafuatayo yafanyuike.

Ranchi iimarishwe kimiundombinu kwa mfano waongezewe magari, watumishi, *fencing, distribution* ya maji, masoko ya uhakika ya nje yatafutwe kwa ng'ombe wa ranchi na wa wananchi jirani katika Wilaya ya Kongwa, Ranchi iwe na programu maalum ya ujirani mwema na uwezeshaji wa wananchi kwa *Extension Services* na mbegu bora za ng'ombe wa nyama na maziwa wenye soko zuri ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili ranchi isivamiwe na magonjwa, ni vema iwepo *system* ya majosho na ugharamiaji wa huduma unaochangiwa na wafugaji lakini ranchi ikisaidia kwa kila hali kuwelea wafugaji na wananchi binafsi wawezeshwe kuanzisha ranchi ndogo ndogo zenye mifugo bora kama ilivyo huko Botswana. Ili hayo yafanyuike hakuna budi, Wizara kuisaidia management ya ranchi ya Kongwa ili imudu majukumu yake mipya.

*Kongwa grass* inajulikana kwa kuwa na *very high crude protein content* kwa chakula cha mifugo. Lakini upatikanaji na usambazaji wa manyasi haya ambayo ndiyo *base* ya ufugaji huko Australia bado ni mdogo. Nashauri kuhusu umuhimu na wafugaji kufundishwa na ku-*practice range management* kwa kuanzia na wananchi kumilikishwa *Privately* maeneo yao. *Common ownership* ya maeneo inaleta *open access* ambayo kwa wafugaji matokeo ni *land degradation.*

Naishukuru sana Wizara kwa mipango mizuri upande wa sekta ya maji kwa Wilaya ya Kongwa. Bado tatizo ni kubwa lakini tunashukuru kwa mabwawa, maji vijijini na maji miji midogo. Wananchi wanaishukuru sana Serikali yao. Naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Edward Lowassa, Mbunge Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mbunge, Naibu Waziri na wataalam wakuu wa Wizara na asasi zake kwa Bajeti nzuri sana. Hongera sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kulitambua tatizo kubwa la maji safi na salama Wilayani Mwanga na hivyo kuiingiza Wilaya yangu katika mradi wa maji na usafi wa mazingira na vijijini unaotekelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia. Nashukuru sana.

Tatu, naona bado iko nia ya ukarabati wa bwawa la Nyumba ya Mungu. Naomba utafiti huo juu ya ukarabati huo uanzie katika Ziwa Jipe. Ziwa Jipe linavamiwa na magugu na magugu haya yamevamia bwawa la Nyumba ya Mungu. Hivyo utafiti uliopangwa hautakuwa na mafanikio kama chanzo cha *polution* hakitaangaliwa. Nawashukuru sana. Ahsante.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wake kwa kuchapa kazi vizuri, ikiwa ni pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara, chini ya uongozi wa Wizara hii, imefanya mambo mazuri na mipango iliyopo ni mizuri ambayo itatatua tatizo kubwa la maji nchini.

Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kutuweka katika mradi wa Benki ya Dunia ambao unahusisha Wilaya 12, Singida Vijijini ikiwa miongoni mwao. Aidha, mradi wa Serikali ya Japan ambao imehusika katika hotuba yake. Naomba kupatiwa baada ya Bunge hili vipi, jimbo langu litafaidika na mradi huu wa Japan. Kwa ujumla natoa pongezi nyingi.

Napenda kukumbusha ahadi alizotoa Mheshimiwa Waziri Edward Lowassa, wakati alipotembelea jimbo langu la Singida Kusini, ambazo bado hazijatekelezwa. Ahadi hizo ni Kisima cha Mlandalo, Kata ya Mwaru Tarafa ya Sepuka, bado na mashine ya maji kijiji cha Msiuwi, Sepuka na Madrikam bado.

Nashukuru fedha za mabwawa ya Mgungila, Ntuntsua na Iglangoni zimepokelewa. Ngungila bwawa tayari.

Naomba mabwawa zaidi kwani nina vijiji zaidi ya 90 na hali ya maji ni mbaya mifugo inaathirika sana kwa ukosefu wa maji. Aidha suala la dawa ya mifugo nalo ni tatizo kubwa. Naomba Wizara ilipe kipaumbele suala hili.

Katika takwimu zilizotolewa katika mwisho wa hotuba yake, zinaadhihirisha kuwa Singida vijijini kuna matatizo ya utafiti wa visima virefu hakuna, visima vilivyochimbwa tokea mwaka 2002 Singida Vijijini hakuna. Naomba takwimu hizo zitumiwe kuthibitisha hoja yangu.

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa hii ya kuchangia katika hoja ya Waziri wa Maji na Maendeleo na Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Edward Lowassa, Naibu wake Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na timu nzima ya wataalam wa Wizara walioshiriki kuandaa hoja hii inayojumulisha Bajeti ya Serikali ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Waziri imeandaliwa kwa makini juu ya misingi miwii muhimu kama Sera mpya ya maji iliyozinduliwa na Mhehsimiwa Rais mwaka jana, 16 Machi, 2002 huu ni msingi muhimu kwa sababu ni sera yenye kujenga mazingira shirikishi ya wadau mbalimbali wa sekta ya maji.

Waraka wa Rais Na. 1 wa mwaka 2002 unaolenga kuendeleza sekta ya mifugo kwa kudhibiti kuenea kwa kwa magonjwa ya mifugo kuhimiza moyo na mpango thabiti ya kujitegemea kupitia Halmashauri kwa kutenga asilimia 15 ya mapato tokana na mifugo kutumika kuendeleza sekta yenyewe. Kwa sababu ya kina na upeo wa hoja hii, na kwa sababu ya misingi hiyo miwili iliyojengwa juu yake, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze katika maeneo matatu kama ifuatavyo:-

Maji katika ukurasa 33 aya 43 Mheshimiwa Waziri amebainisha kununuliwa mitambo mitatu kwa ajili ya mji wa Kigoma. Hii ni habari njema na naipongeza Wizara na Serikali kwa ujumla kwa hatua hiyo kwa sababu hatua hiyo itatoa matunda yafuatayo itatatua kero ya mgao wa maji mjini Kigoma/Ujiji.

Itaijengea heshima Serikali ya kutekeleza ilani ya uchaguzi ya mwaka 2000 kwa vitendo, kwa kupunguza kero ya maji kama si kuondoa kabisa. Mitambo mitatu kati ya sita inayofanya kazi isingeweza kukidhi mahitaji ya maji ya miji hiyo miwili.

Upinzani utapungukiwa na hoja katika sekta hiyo. Hata hivyo ni vema Serikali izingatie kwamba hali ni mbaya vijijini, hususani katika Jimbo langu la Kigoma Kusini, Vijiji vifuatavyo vinakabiliwa na matatizo makubwa ya maji Kashagulu, Sibwesa Kata ya Kaliya, Sunuka Kata ya Sanuka, Kasuku na Simbo/Machazo Kata ya Siimbo.

Natoa mwito kwa Wizara itoe kipaumbele kwa vijiji hivyo katika kukamilisha miradi na ilivyobaki kati ya miradi 13 baada ya kutekeleza mitano katika kipindi cha Julai 2002 hadi Juni, 2003. Jedwali Na. 1 ukurara 92 na Jedwali Na. 2 ukurasa 95 zahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa na utambuzi na msisitizo wa Waziri kuhusu uendelezaji wa nyanda za malisho kama moja ya mikkati ya kuendelza mifugo. Nampongeza kwa hilo.

Pamoja na pongezi hizo nina ushauri kuwa Wizara inafahamu kwamba uendelezaji wa nyanda za malisho ni poamoja na kuondoa ndorobo, na kwa kuwa inafahamika kuwa 70% ya eneo linalofaa kwa malisho la ha. 1504,800 Mkoani Kigoma linakaliwa na mbung'o na kuacha hekta 305,000 sawa na 20% tu zinazotumika. Sasa, Wizara haini ni vema; badala ya kutumia fungu dogo la Bajeti ya Maendeleo kuendeshea mafunzo shirikishi ya uzuiaji mbung'o kwa maafisa 20 wa mikoa, ikiwa ni pamoja na Kigoma, Fungu hilo lingetumika kuulia hao mbung'o kwa kununulia vitambaa vyeusi vyenye dawa ya kuua mbung'o?

Maeneo yenye kero kubwa ya mbung'o katika Mkoa na Kigoma yanajulikana toka enzi na enzi. Natoa mwito wa kuanza programu ya kuua mbung'o katika tarafa ya Nguruka vijiji vya Ilunde, Mpeta, Malagarasi, Mambwe, Ilalangulu, Chagu.

Wananchi wako tayari mno kushirikishwa kusambaza na kuvilinda vitambaa vya dawa ya kuua Mbung'o katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni suala zima la miundombinu hususan ujenzi wa majosho. Majosho yaliyopo Mkoani Kigoma kwa mujibu wa kiambatisho Na. 10 ukurasa wa 117 wa hotuba ya Waziri ni 67, kati ya hayo yanayofanya kazi yakiwa 29, sawa na asilimia 43 tu na kuacha 38 sawa na asilimia 62 yasiyofanya kazi. Ni vema Wizara ikafahamu kwamba kufanya kazi kwa majosho hayo 29 ni matokeo ya ukarabati uliofanywa na vikundi vidogo vidogo vya wafugaji, hususani, Wilayani Kasulu. Pamoja na kuwapongeza wananchi hao kwa kutekeleza vema sera ya ushirikishwaji, na Waraka wa Rais Na. 1 wa 2002.

Wizara inapaswa kutambua mwamko huo kwa kuvipongeza vikundi hivyo kupitia Halmashauri zao, kuunga mkono jitihada za wananchi hao kwa kutoa fungu la kukarabati majosho yaliyobaki 38 katika mwaka wa fedha 2003/2004. Hatua hiyo itawahamasisha kujenga mengine mapya. Naunga mkono hoja hiyo nzuri na ya kina.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. Pamoja na Mheshimiwa Naibu wake na watendaji wake kwa kazi nzuri ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa mwaka 2002/2003 na kuandaa mpango mpya na mzuri kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kitaifa, naomba kupongeza uamuzi wa Serikali kuandaa matumizi ya maji kutoka Ziwa Victoria ili kupunguza matatizo ya maji kwa mikoa inayozunguka Ziwa hilo. Historia inaonyesha nchi yetu kutoona nafasi njema na ya dhahabu ya kutumia maji ya Ziwa Victoria wakati nchi nyingine zikinufaika na maji ya Mto Nile ambao chanzo chake ni ziwa Victoria. Bomba la maji kutoka Ziwa Victoria kuleta maji Dodoma, ni fikra sahihi na endelevu na ziendelee kufanyiwa kazi kuwezesha Dodoma kuendelea kujitosheleza kwa maji kwa miaka 50 hadi 100 ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mji wa Muheza una matatizo makubwa ya maji mwaka 1982 Shirika la misaada ya ufundi la Ujerumani, kwa niaba ya Serikali, *(GTZ)* ilifanya utafiti wa kuondoa tatizo hilo na kupendekeza msaada mkubwa *Muheza Main Trunk,* kutoka Mto Pangani. Mradi huu ulikuwa utoe maji kwa vijiji 27 lakini gharama zake za shilingi zaidi ya bilioni saba, ulikuwa ghali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi mbadala uliofanyiwa utafiti ni mradi wa *Ubembe Kwemhosi Gravity Water Scheme* ambao Mheshimiwa Waziri aliahidi mbele ya viongozi wa Mkoa wa Tanga, Wilaya ya Muheza, Halmashauri na mbele ya Wabunge wawili wa Wilaya ya Muheza kusaidia kuutekeleza alipofanya ziara mwanzoni mwa mwaka 2002. Mwaka 2002/2003 mradi hu haukuingizwa katika mpango wa Wizara, na hata sasa 2003/2004 sikuona mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji kwa mji wa Muheza inaonekana kuwa ghali kwa sababu Muheza inabeba gharama za kupeleka maji mjini Tanga kwa kutotumia maji ya Mto Ziggi ambao unaanzia ndani ya Milima ya Amani, Wilaya ya Muheza. Iwapo chanzo hiki kingetumiwa maji yangepatikana Muheza kwa mtiririko wa moja kwa moja *(gravity)* na gharama nafuu. Pamoja na gharama hizo, Wilaya ya Muheza ndio inalinda chanzo cha maji ya mto huo wa Ziggi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo sioni kwa nini Muheza itekelezwe kwa sababu ya miradi mbadala kuwa ghali. Nilitoa mapendekezo ya kutekeleza kwa mradi wa *Ubembe Kwemhosi Gravity Water Scheme* kwa awamu tatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya kwanza shilingi 236,500,000/=, awamu ya pili shilingi 93,780,000/= na awamu tatu shilingi 87,780,000/= na jumla shilingi 417,505,000/=

Mradi huu utatoa maji katika vijiji saba na kata sita, zikiwemo kata tatu za Muheza mijini kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| Vijiji saba | Kata tatu | Kata Jirani Muheza Mjini |
| Ubembe | Masuguru | Lusanga |
| Kwemhosi | Majengo | Kilulu |
| Kisiwani | Mbaramo | Mkuzi |
| Kibanda Ukumba | | |
| Misangeni | | |
| Bambani | | |
| Bwembwera | | |

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi utaongeza maji katika mji wa Muheza kiasi cha *cubic* mita 1,060 sawa na 75% zaidi ya kiwango cha sasa. Hivyo kufikia zaidi kidogo ya asilimia 100 ya mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa maji uliofanywa na Serikali na Mkoa pia unaonyesha kwamba hakuna uwezekano wa kuchimba visima virefu ndani ya umbali wa kilo mita 10 kuzunguka mji wa Muheza hivyo ni dhahiri njia pekee iliyopo ni aidha kupata maji toka mradi wa Mto Pangani au kuanza na mradi huu wa Ubembe Kwemhosi, hivyo naomba sana Wizara sasa itekeleze ujenzi wa mradi huu ikiwa pia ni kwa heshima kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Kata ya Mkuzi na jirani ya mji wa Muheza, naomba Serikali isaidie ujenzi wa kisima kimoja kirefu kwa ajili ya kituo cha afya cha Mkuzi, kisima ambacho pia kitakuwa jirani na Shule ya Msingi Mkuzi na Shule ya Sekondari Mkuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya mwisho kijiji cha Mkuzi pamoja na vijiji vingine vya Enzi, Kilulu na Mafere vilipata maji mwaka 1979 kutoka bomba lilolotaka Mjini Muheza kwa chanzo cha maji kutoka Magoroto. Vijiji hivyo ambavyo vyote vina matenki makubwa ya hifadhi ya maji pamoja na mfumo wa usambazaji maji wa bomba kwa muda wote sasa hauna maji kutokana na kukua haraka kwa mji wa Muheza, na hivyo kuacha matenki hayo ambayo bado ni mazima kuwa *White Elephant.*

Mwisho naomba ufafanuzi kutoka ukurasa 46 iwapo mji Igombe ulikuwa na maana ya mji wa Kigombe Wilaya ya Muheza ambapo Wizara ilikuwa hadi wiki mbili zilizopita haijachimba kisima kimoja kirefu licha ya Mheshimiwa Waziri na pia wakala wa maji Ubungo kukiri kupata fedha toka Wizarani ili kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kisima kinachotarajiwa kuchimbwa Kigombe kimeunganishwa na mradi wa *TASAF* ili kusambaza maji katika mji wa Kigombe na jirani zake hivyo kuchelewa kuutekeleza pia kuwachangia kuchelewesha mradi wa maji wa pango wa *TASAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Muheza kuwa katika hali mbaya ya maji, naunga mkono hoja.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii ili nichangie hoja ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa mawasilisho mazuri ya hotuba yake. Pia nampongeza Naibu Waziri wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Anthony Diallo, kwa kazi nzuri ya kumsaidia Waziri katika kutekeleza majukumu muhimu sana ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Aidha, natumia nafasi hii kuwapongeza Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kazi nzuri ya kutekleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa kwanza unahusu matatizo yaliyopo kwenye shamba la mifugo la Nangaramo katika jimbo langu la Nanyumbu, Wilaya ya Masasi. Shamba la Mifugo la Nangaramo linakabiliwa na tatizo la umeme. Hali hiyo inapotokea uongozi kushindwa kutmia vifaa kama *computer* ambavyo wamepelekewa hivyo hubakia kuwa mapambo tu sasa kwa kuhusu umeme vile vile kunakaribisha wanyama wakali kama simba, chui, fisi na nyoka kushambulia mifugo wakati wa usiku. Ukosefu wa umeme vile vile huwaweka wafanyakazi katika hatari ya kushambuliwa na wanyama wakali wakati wa usiku. Naomba Serikali ilipatie shamba la mifugo la Nangaramo umeme ili waondakane na adha zote hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba la mifugo la Nangaramo vile vile linakabiliwa na ukosefu wa vifaa vya kusafiria kama magari, pikipiki, na matrekta. Kwa kukosa usafiri wafanyakazi hushindwa kuwasiliana na makao makuu ya wilaya kwa wakti. Vile vile hushindwa kuwapeleka watoto wao shuleni kupitia kwenye misitu yenye wanyama wakali kwa kukosa usafiri shamba la mifugo la Nangaramo huonekana kama limetengwa na dunia ya leo. Naomba Serikali ilipatie shamba la mifugo la Nangaramo vifaa vya usafiri ili kuwapunguzia adha wanazopata wafanyakazi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo mengine ya shamba la mifugo la Nangaramo ni ubovu wa barabara, ukosefu wa maji wakati wa kiangazi, upungufu wa malisho wakati wa kiangazi, upungufu wa nyumba za wafanyakazi na ukosefu wa mawasiliano ya simu. Naomba Serikali itatue matatizo yoe hayo ili shamba hilo la Mifugo liweze kutekeleza majukumu yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie tatizo la ukosefu wa maji katika jimbo langu la Nanyumbu. Bado tatizo ni kubwa sana kwani maeneo mengi hayana maji hasa wakati wa kiangazi. Hali hii imetokana na historia ya huko nyuma ambapo Jimbo la Nanyumbu lilikuwa kama limesahaulika kwa miradi mingi ikiwemo ya maji. Hali hiyo inahitaji upendeleo maalumu ili jimbo liondokane na hali hiyo.

Maeneo ambayo wananchi wanapata shida sana ya maji ni Kata za Mikangaula, Nangomba, Likokona, Lumesule, Napacho, Chipuputa, Nanyumbu, Sengenya, Mkonona, Maratani, Nandete na Masuguru. Ndiyo kwanza miradi ya maji imeanza kwenye baadhi ya vijiji lakini bado inaonekana kuwa ni sawa kuweka kijiko cha sukari kwenye bahari ambapo haiwezi kubadili hali ya maji ya chumvi. Naomba Seriali kuongeza kasi zaidi katika kulipatia jimbo la Nanyumbu maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho natamka kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na nashukuru tena kwa kupata nafasi hii ya kuchangia. Ahsante sana.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Kwa kuwa nimeshamwandikia Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo juu ya uhaba wa maji safi na maji ya malambo ambayo hutumiwa na wanyama. Katika Vijiji vifuatavyo kuna uhaba mkubwa sana wa maji navyo ni Kijiji cha Itindi, Kijiji cha Namkukwe, Kijiji cha Malangali, Kijiji cha Iseche, Kijiji cha Mbala, Kijiji cha Patamela, Kijiji cha Kininga/Kapalala, Kijiji cha Gua na Kijiji cha Udinde.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba walau visima viwili viwili katika kila Kijiji kwani hali ya maji katika maeneo haya ni mbaya sana. Wananchi wanakunywa maji ya kwenye madimbwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu kumekuwa na matatizo makubwa ya ukosefu wa fedha kwenye Halmashauri yetu ya Wilaya. Licha ya kuwa na maji ya Ziwa Rukwa mito mbalimbali suala la maji limekuwa ni tatizo kubwa kwa vile vijito na mito hiyo hukauka. Jambo lingine ni kwamba maji ya Mto Songwe si salama kwa vile uchafu wote wa *Sewerage* za Mbeya huingia katika mto huo na hivyo kuhatarisha afya za wananchi wa maeneo wanayoyatumia maji hayo ya mto.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kunipa visima vitano katika maeneo ya Galula Mbuyuni na Mbangala. Nashukuru sana kwa kuweza kutusaidia. Lakini lipo tatizo kubwa la migongano iliyopo kati ya wafugaji na wakulima, tatizo kubwa ni upungufu wa malambo eneo ambalo ng'ombe wanatakiwa wawepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kama tutapewa walau malambo matatu zaidi maeneo ya Kapalala, Magamba na Namkukwe**.** Hali siyo nzuri katika suala hilo hivyo naomba kwa makusudi kabisa Wizara iweze kusaidia suala la malambo zaidi zidi ya yale yaliyochimbwa kwa sababu ng'ombe ni wengi sana eneo hilo la Jimbo la Songwe hivyo kuleta mitafaruku ya mara kwa mara kwa wananchi. Tusaidieni tupate malambo ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusu wafugaji kukaa katika maeneo yaliyopangwa, ni vyema basi Wizara iangalie uwezekano wa kuwepo na huduma za kimsingi juu ya jambo hilo. Wafugaji wanawajibika kufuata maji maeneo ambako wapo wakulima hivyo kuleta migongano isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie juu ya matatizo hayo ya kimsingi. Tuliambiwa tutafute miradi miwili katika Wilaya ili *SADC* watoe fedha za ujenzi wa mabomba ili maji yapatikane pale Kapalala na Vijiji vingine vya Kininga na Udinde. Sasa Wilaya haijui ule mradi upo au laa! Mheshimiwa Waziri tungependa kupata maelezo juu ya Miradi ya *SADC* kama bado ipo?

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbegu Bora ya Ng'ombe wa Maziwa Kijijini Namabengo. Pale Kijijini upo Mradi wa "Kopa ng'ombe Lipa ng'ombe". Naomba nipewe/niuziwe shahawa (mbegu) za ng'ombe kwa ajili ya Kijiji cha Namabengo toka *NAIC* Arusha. Mbegu hizo zinahusu yule dume anayesaidia kuzalisha lita 45 za maziwa kwa siku, ni dume la *South Africa.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kwa matumizi ya wanakijiji katika Wilaya ya Namtumbo. Kijijini hapo tumekarabati josho (2003) ambalo lipo katika eneo la Parokia ya Namabengo. Binafsi nilisaidia kuwaletea dawa kwa gharama ya Shs. 49,000/=. Wananchi wanalikarabati josho hilo.

Aidha, naomba nipatiwe mtaalam wa kuandaa malisho (shamba) kwa ajili ya matumizi ya mifugo yangu bondeni kwenye Kaya yangu pale Namabengo. Gharama husika natarajia kuzilipia hasa kuhusu mbegu za majani ya kulishia ng'ombe wangu wakati wa 2003/2004

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru kutengewa fedha za kuboresha upatikanaji wa maji katika Mji mpya wa Wilaya ya Namtumbo.

Maji yanapatikana kwa wingi sana mlimani Matogoro. Naomba lijengwe Tanki la *Reservoir* kilimani Libango toka huko yatatiririka hadi *site* mpya ya Mji wa Namtumbo. Tayari lipo bomba kubwa toka Matogoro lakini yanatakiwa yaje kwa mtiririko wa *gradient* kufika mlimani Libango toka *reservoir* hiyo yatatiririka hadi *new site* bila ya mashine kuhusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachohitajika ni *re-routing* bomba zilizoko. Hatuhitaji mashine ya kusukuma maji haya bali yatatiririka bila gharama. Ni mpangilio mpya wa mabomba unaohitajika. Gharama ni *reservoir* mpya tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukrani. Naunga mkono hoja.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Wizara hii inajitahidi sana katika kuhakikisha kuwa maji yanapatikana kwa asilimia kubwa ingawa yapo maeneo ya Vijijini ambayo hawajapata maji ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumiaji wa maji wengi ni wananchi ambao hawana uwezo. Ninapenda kuiomba Serikali iangalie upya ulipiaji wa maji kwa wananchi ambao hawana uwezo wa kulipia maji hayo. Ninaiomba Serikali isiwatoze *bill* ya maji wananchi ambao uwezo wao ni mdogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Kilimo na Chakula ili maji yapatikane ya kutosha ili wakulima waweze kuyatumia badala ya kungojea maji ya mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ng'ombe wa Maziwa *DAPRO.* Wizara ijitahidi kusimamia mifugo ya aina mbalimbali hasa mifugo ya ng'ombe wa maziwa. Wananchi walio wengi hawajafahamu umuhimu wa ng'ombe wa kisasa. Hivyo, ninaiomba Serikali na Wizara hii kwenda Vijijini kwa ajili ya kuwafahamisha wananchi umuhimu wa ng'ombe wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ijitahidi kuweka mabwawa ya kuogeshea ng'ombe ili waepukane na maradhi ya mifugo. Vile vile, yapatikane madawa ya aina mbalimbali kwa ajili ya kutibu mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kurudia tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na wafanyakazi wote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu pamoja na viongozi na watumishi wengine wa Wizara hii na asasi zake, kwa hotuba nzuri na yenye wingi wa takwimu na kwa kazi nzuri sana ambazo Wizara imekuwa na inaendelea kuzifanya katika kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na maendeleo ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mkinga ninaloliwakilisha lipo katika maeneo yaliyoendelea kwa jumla ya Kaskazini mwa nchi yetu. Ingawaje Jimbo hili lipo huko na kwa jumla linachukuliwa kama moja ya maeneo yaliyopiga hatua kubwa kimaendeleo, ukweli ni kwamba lina nafasi nzuri sana ya maendeleo lakini bado ni moja ya maeneo ya pembezoni yaliyo nyuma kimaendeleo. Jimbo la Mkinga lina raslimali nyingi sana ambazo kama zikiendelezwa ipasavyo zitawezesha Jimbo hili kupiga hatua kubwa katika kupambana na umaskini na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa. Kuwepo karibu mito tisa katika Jimbo hili na ardhi ya kutosha pamoja na hali nzuri ya hewa, kunatoa nafasi nzuri kwa kuendeleza Sekta ya Maji kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawaje nilikwishatoa mapendekezo kwa Wizara kuhusu haja na umuhimu wa kuiendeleza sekta hii Jimboni Mkinga, Wizara ilinishauri nipeleke mapendekezo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza. Kwa bahati mbaya, uwezo wa Halmashauri ni mdogo na utaendelea kuwa mdogo kutokana na kupungukiwa na vianzo vya mapato. Hata wananchi hawana uwezo mzuri wa kuchangia katika mipango shirikishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukweli huo nashauri pawepo na Mfuko wa Maji na Mfuko wa Kuendeleza Mifugo kwa ngazi ya Taifa. Halmashauri za Wilaya na wananchi peke yao hawawezi kupiga hatua za maendeleo stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali halisi Jimboni Mkinga, hali ya upatikanaji wa maji. Takriban asilimia 70 ya Vijiji Jimboni Mkinga vina upungufu mkubwa wa maji safi na salama kwa ajili ya wananchi na mifugo hasa wakati wa kiangazi. Visima vifupi vilivyochimbwa katika Vijiji kadhaa havitoshelezi haja. Baadhi ya mabwawa

yaliyopo kama vile Duga Maforoni, Gombero, Kilulu na Manyinyi yanastahili kukarabatiwa ili kuondoa silting *na* matatizo mengine. Malambo na majosho yaliyopo Gombero, Duga na kwingineko nayo yanahitaji ukarabati. Kihalisi itachukua muda mrefu kupata watu binafsi ambao wangeweza kuendesha huduma hizi. Bado Serikali Kuu na Halmashauri zitaendelea kuwa na mchango mkubwa kwa maendeleo ya Sekta hii Jimboni Mkinga. Hivyo nashauri Wizara ilihusishe Jimbo la Mkinga katika mpango kamambe wa Taifa unaogharamiwa na Benki ya Dunia *(World Bank).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Uendelezaji wa Mifugo. Zaidi ya kuwepo wafugaji wengi wa ng'ombe wa kiasili, Jimbo la Mkinga lina wafugaji wengi wa kisasa ambao wanaunganishwa na kuendelezwa na *Tanga Dairy Farmers Cooperative Union (TDCU),* Vyama vyake Tanzu na Serikali. Wafugaji wa Jimbo la Mkinga wana nafasi nzuri sana ya kuendeleza ufugaji wa kisasa. Ninaloomba ni jitihada za makusudi za Serikali kulitambua Jimbo la Mkinga na Wilaya ya Muheza kwa jumla kama miongoni mwa sehemu zenye nafasi nzuri za kuendeleza mifugo na mazao ya mifugo. Kutokana na hali hiyo kuwaongezea huduma za ugani na kutoa misaada yote kwa wafugaji, vyama vyao vya ushirika na wahisani wao katika kuendeleza ufugaji hasa wa ng'ombe wa maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Naibu Waziri wake na wataalam wote Wizarani kwa kazi nzuri inayofanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika*, Manolo Group.* Leo maji ni tatizo kubwa sana katika maeneo mengi ya nchi yetu. Unaweza kushangaa kusikia kwamba yako maeneo katika milima ya Usambara kwa sasa ni sawa na jangwa. Kata ya Shume katika Jimbo la Mlalo ina hali mbaya sana ya upungufu wa maji, ndiyo maana tukabuni Mradi wa Maji wa *Manolo Group.*

Mradi huu ni mkubwa na ghali sana ndiyo maana bado hatujapata mhisani mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nilikualika na bado nakualika ufike katika eneo hilo ujionee mwenyewe hali hiyo. Kwa kuwa inaonekana mradi huo utachukua muda mrefu, naomba msaada wa visima katika Vijiji vya Nywelo, Mkunki, Manolo, Madalo na Mavumo. Bado tunakuomba Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Edward Lowassa, kuendelea kusaidia kutafuta wahisani kwa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashamba ya Ng'ombe ya Serikali. Kwa yale mashamba ambayo yataendelea kubakia katika mikono ya Serikali kwa ajili ya mbegu, yatunzwe na kuangaliwa kitaalam. Baadhi ya mashamba ya Serikali ya ng'ombe hayana mbegu bora, ng'ombe wa kisasa ataweza vipi kutoa lita nne za maziwa? Tatizo hili nina ushahidi nalo na nilikwisha kuiambia Wizara. Nashauri jambo hili liangaliwe kwa makini zaidi ili kumsaidia mkulima/mfugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuku chotara. Ufugaji wa kuku chotara ni muhimu sana na tena ni rahisi kwa wakulima wa kawaida. Utaalam wa ufugaji wa kuku chotara haujafahamika katika maeneo mengi. Mradi kama huu unaweza kuwa msingi mkubwa wa kupunguza umaskini miongoni mwa wananchi wengi. Nashauri mpango huu upanuliwe ufike katika maeneo mengi zaidi ya wananchi wetu. Mradi wa Mbuzi wa Maziwa. Kama ulivyo mradi wa kuku chotara, mradi huu wa mbuzi wa maziwa ni rahisi kuuendesha kwa kuwa mbuzi ni mnyama mdogo na ufugaji wake sio ghali sana. Nashauri pia mradi huu upanuliwe ili uyafikie maeneo ya nchi yetu mengi zaidi. Kwa mradi huu mapambano ya kuondoa au kupunguza umaskini yanaweza kuonekana dhahiri. Mradi ufikishwe nchi nzima na Jimboni kwangu haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvunaji maji ya mvua. Kwa wakati huu uvunaji wa maji ya mvua ni teknolojia muhimu sana. Sioni nia na kasi ya wazi ya kuendeleza mpango huu. Haja ya maji hivi leo ni kubwa kuliko wakati mwingine hasa kwa sababu popote duniani maji yanapungua sana. Nashauri mpango huu utiliwe mkazo wa pekee ili Watanzania wengi zaidi wajue namna ya kuvuna maji ya mvua, yasipotee bure baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba uthibitisho wa suala la Benki ya Dunia kuhusu mpango kamambe wa kusambaza maji katika Wilaya ya Kigoma Vijiji ili kwenda kuwaelimisha na kujitayarisha kunywa maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sehemu zifuatazo: Nyarubanda, Mukigo, Kalinzi, Matiazo, Mkabogo, Mahembe, Kwitanga, Chankele, Msimba, Kamala Chankabwimba, Kizenga na Nkungwe hivyo ni Vijiji vyangu vilivyo katika Jimbo langu la uchaguzi ambavyo havina maji kwa muda mrefu hivyo ufafanuzi wa wazi tunaomba uwe bayana juu ya suala hili ili liweze kukamilika. Ni muda mrefu sana havijapata maji ijapokuwa vyanzo vya maji vipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NGOs* huonyesha kuchangia kwa kiasi kidogo sana na pengine mradi huwa mkubwa kuliko uwezo wa *NGOs*. Hivyo, Benki ya Dunia inaweza kulimaliza tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni kulipa deni, basi deni hilo tunalipokea kwa gharama yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kazi njema na mafanikio mema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutumia nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kazi nzuri sana anayoifanya katika Wizara hii. Wananchi wetu na sisi wawakilishi wao tunaridhika na utendaji wake. Tunapenda kusema kuwa tutamuunga mkono kwa hali na mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu wa Wizara na wataalamu mbalimbali kwa kazi yao nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutamka kuwa ninaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuichangia Wizara hii, napenda kuzungumzia suala la usambazaji wa maji Vijijini. Tunajua fedha zinazotolewa ni ndogo hazikidhi matatizo ya maji katika Vijiji. Hivyo tunaomba Wizara iweke mikakati ya uchimbaji wa visima vya maji virefu na vifupi japo kimoja kimoja kwa kila Kijiji ili kusaidia upatikanaji wa maji ya uhakika kwenye Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo makubwa ya maji katika maeneo ya Jimbo la Mpanda Magharibi hususan Kata ya Ikola. Naomba Serikali iweke kila aina ya mkakati kwa ajili ya kusaidia uchimbaji wa visima vya maji kwa kila Kijiji. Tunaomba *Budget* inayokuja izingatie hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Natoa pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wake, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika Wizara hii ili kuhudumia ipasavyo (licha ya uwezo mdogo) umma wa Watanzania katika Sekta ya Maji na Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kumshauri Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa juhudi zake alizoweka katika Mji wa Wilaya yangu pale Same, Kilimanjaro wakati mitandao yake yote ya maji iliposimama. Tulishirikiana usiku na mchana na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Edward Lowassa hadi tuliponusuru hali mbaya ya maji Mjini Same. Hali bado haijaridhisha lakini ile kero ya kufuata maji kwa magari au punda kwa umbali wa kilometa 15 imekwisha. Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Edward Lowassa anastahili pongezi na amethibitisha kwetu Wabunge na umma wa Tanzania kuwa ni Waziri makini, hodari, mwenye uwezo mkubwa na ambaye anaijua nchi yetu vema ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Same.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri mambo matatu katika maendeleo ya maji na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza kwenye maji ni uhaba na uduni wa huduma ya maji katika Mji wetu wa Wilaya ya Same. Wilaya ya Same ni moja ya Wilaya zenye maendeleo duni ya huduma za jamii na uchumi. Hii ni kwa sababu hatuna miundombinu yoyote ya kuwafaa Wananchi wetu wa Wilaya ya Same katika maji, barabara, simu na umeme. Wananchi wetu wengi 80% wanaishi milimani ambapo huduma zote hizi hazipo. Mji wa Wilaya nao japo una huduma ya barabara, simu na umeme lakini nao hauna maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutuweka katika mpango wa mradi wa maji na usafi wa mazingira Vijijini *(RWSSP)* wa mkopo wa *World Bank.* Ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kutoa kipaumbele kwa maji ya Mji huo wa Same kwa sababu kero hii ya maji imekuwa ni kero sugu tangu wakati wa mkoloni yapata miaka 45 hivi! Tunaomba Mheshimiwa Waziri katika uongozi wake sasa aukomboe Mji wetu wa Same na adha hii ya maji sambamba na kero hii ya maji katika Mji wa Same, ni Miradi ya Maji Vijijini katika milima na mabonde ya Wilaya ya Same.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitika kuona kuwa katika kitabu chake kwenye sehemu Na. 2 ya Miradi ya Maji Vijijini isiyofanya kazi, Mkoa wetu wa Kilimanjaro hauna taarifa yoyote ile wakati kule katika Wilaya yangu ya Same ipo miradi kadhaa ya maji ambayo haifanyi kazi kama Mradi wa Maji wa Bangatala, Vumari, Didokwamomo, Mbono, Njoro, Ishinde na Mhezi Mtunguja. Ninaiomba Wizara isaidiane na mimi Mbunge katika Wilaya ya Same ili kufuatilia ni nini kimetokea mpaka Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo haina takwimu za Miradi ya Maji Vijijini ambayo haifanyi kazi. Namwomba Mheshimiwa Waziri aniruhusu baada ya hapa niwakilishe kwake takwimu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine katika maji ni mabwawa ya maji kwa ajili ya mifugo. Kule katika Wilaya ya Same lipo bwawa la kihistoria la Chato. Bwawa hili lilitoboka miaka michache baada ya nchi yetu kupata uhuru. Bwawa hili liko katika Hifadhi ya Wanyama ya Mkomazi na linahudumia hapo mifugo mingi ya wafugaji wetu wa Same. Kwa sababu bwawa hili pia linahudumia na kuboresha mazingira mazuri ya Hifadhi ya Mkomazi, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii amekubali kuchangia gharama za kulifungua bwawa hili kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Mheshimiwa Waziri huyo ameonyesha nia ya kuchangia gharama hizo katika mwaka wa fedha 2004/2005.

Nakuomba Mheshimiwa Waziri atuunge mkono ili tuweze kufufua bwawa hili katika mwaka wa fedha 2004/2005. Nakuomba Mheshimiwa Waziri upokee ombi letu hili na kilio cha wafugaji wa Same. Tuwaahidi wafugaji wetu kuchangia gharama za mabwawa mengine madogo madogo ya kuhudumia mifugo ndani ya maeneo ya malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili ni katika huduma za majosho ya kuogesha mifugo. Mifugo yetu mingi imekufa kutokana na maradhi ya kupe yanayosababishwa na mifugo kutoogeshwa. Hata mazao yetu ya mifugo ya ng'ombe, mbuzi, kondoo na punda yanakuwa duni kutokana na sababu ya magonjwa ya kupe. Katika Wilaya ya Same yapo majosho 11 lakini ni josho moja tu linalofanya kazi. Hii ni kutokana na uwezo mdogo wa Halmashauri yetu. Naomba pale udhaifu na uwezo mdogo unapotokea, Wizara iwe tayari kuitembelea Halmashauri hiyo na kuitaka ifanye marekebisho. Kwa Wizara kuziachia Halmashauri zetu kufanya kile inachoweza au isichoweza ni kuwapatia uhuru wa kuwa Miunguwatu. Tunaomba Wizara ishirikiane na sisi Wabunge ianzishe mpango wa kuzikabili Halmashauri zinazozembea katika huduma ya majosho kama kule kwangu Same.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa tatu na wa mwisho ni kuhusu masoko ya mazao ya mifugo ya ng'ombe, mbuzi, kondoo na kadhalika. Naiomba Wizara isisitize na kuhitimisha Kisheria mpango wa kudhibiti uswagaji wa mifugo kutoka eneo la soko kwenda kwa walaji. Ili hili liweze kufaulu, naiomba Wizara itupatie msaada kule katika Wilaya yangu ya Same wa kutuwezesha kuelekeza mauzo ya mazao yetu ya mifugo niliyoitaja nje ya nchi. Hivi sasa soko ni dogo na hivyo wafugaji wanapunjwa. Soko la mifugo ya Same limeelekezwa eneo moja la Moshi na hivyo kuleta ukiritimba wa biashara *(Trade Monopoly).*

Nashauri tupatiwe masoko ya nje na hivyo mifugo iweze kusafirishwa kwa *train* hadi Dar es Salaam. Naiomba Wizara itupatie masoko ya nje ikiwa ni pamoja na kutusaidia kutangaza soko la mazao yetu ya mifuko ya Same nje na ndani ya nchi kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia mchango wangu kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri na kumpongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja yake kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote waliounga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia kwani kazi unayoifanya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Edward Lowassa pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo ni nzuri na njema machoni pa Watanzania, hivyo kama Waheshimiwa Wabunge na viongozi vijana nawapongeza sana kwa kutokuwa vikwamishi kwa wale wenye shida nanyi, hata kwenye corridor mpo tayari kuwasikiliza watu. Naomba muendelee na moyo huo na muwe mfano kwa Wizara nyingine. Pia nawatakia kazi njema na utekelezaji wa majukumu yenu ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, pokeeni pongezi za dhati na mmekuwa mfano kwa Mawaziri wengine. Pongezi hizi ni uamuzi wenu wa kutambua kuwa Mheshimiwa Mbunge ni kiongozi wa watu, ndiyo maana mmethubutu kumweka kila Mbunge kuwa Mjumbe wa Bodi ya Maji. Hili si suala dogo, linawezekana tu kwa watu wenye kuona mbali na wenye kulipenda Taifa lao. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri pamoja na hoja yake tunayoijadili, nitoe pongezi na shukrani za dhati kwake binafsi, Mheshimiwa Naibu Waziri wake pamoja na Katibu Mkuu toka kwa wananchi wa Jimbo langu la Mbeya Mjini kwa kututafutia mfadhili mahiri wa *Water Supply Programme Regional Centres Phase I,* ambapo mkataba utasainiwa rasmi tarehe 30 Julai, 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kazi nzito mliyoifanya katika kuwashawishi wafadhili mpaka kukubali kutoa *EURO 4,700,000.00* za awali na kukubali pia kuongeza *EURO 4,862,918.81* na pia EURO 250,000 kwa ajili *ya* Technical Support. Naamini fedha hizi zitasaidia sana kuondoa au kupunguza matatizo ya maji safi maeneo ya Itagano, Itezi, Isyesye, sehemu za juu za Iganzo, Igodima, Ilindi hadi *Block X* upande wa Mashariki. Pia fedha hizi zitatusaidia kuwapatia maji safi wananchi wa Iziwa na Nsoho. Maeneo yote haya yapo ndani ya Manispaa ya Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi zangu naomba kuchangia maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuanzisha Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Mradi huu ukitekelezwa vizuri utaondoa tatizo la maji Vijijini. Kwa kuwa mradi bado haujaanza katika Wilaya nyingi ikiwemo Wilaya ya Kondoa, naomba mradi huu uanze kutekelezwa mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukarabati wa mtaro wa Ntomoko, mradi huu unanufaisha Vijiji 19 lakini kutokana na kuchakaa, mradi huu hautoi huduma iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiomba Wizara itusaidie mambo mawili, kwanza, Wizara itafute fedha za kufanya ukarabati mkubwa katika mradi huu na pili, Wizara isaidie utaalam wa kuunda chombo cha kumiliki na kusimamia mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Mwisanga lilikamilika zaidi ya miaka 20 iliyopita lakini maji yake bado hayajatumika kwa sababu yanahitaji kuchujwa. Kwa miaka zaidi ya 15 Wizara ilikuwa ikiahidi kujenga chujio lakini mpaka sasa halijajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka 2002/2003 na mwaka 2003/2004 hakuna fedha iliyotengwa kwa kazi ya ujenzi wa chujio.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifahamu kwa nini mradi huu umefutwa wakati tatizo la maji linazidi kuongezeka katika eneo husika.

Kuhusu huduma za tiba za mifugo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa Waraka Na. 1 wa mwaka 2002. Naomba Waraka huu uwe changamoto katika kuinusuru mifugo yetu ambayo inateketea kutokana na magonjwa mbalimbali hususan Homa ya Mapafu. Wizara ifanye jitihada za kununua na kusambaza katika Wilaya zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe mchango wangu kwa niaba ya wananchi wa Misungwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri za maandalizi ya hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati hii ya Ardhi na Maendeleo ya Mifugo hivyo mengi nimeyaona yalivyoshughulikiwa bali naomba yafuatayo yatiliwe maanani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji katika Wilaya ya Misungwi ni kubwa sana na limechukua muda mrefu bila ufumbuzi kitu ambacho wananchi wa Misungwi kinawafanya washindwe kufanya kazi nyingine za maendeleo kutokana na umbali wa kufuata maji zaidi ya kilometa 8 hadi 10 badala ya kufanya kazi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Misungwi inao mradi ulioanzishwa miaka ya nyuma. Nyumba eneo la mradi zilishajengwa na mabomba umbali wa kilometa mbili yametandazwa. Wananchi tayari walishirikishwa kuchimba mtaro na walifanya hivyo, tanki limejengwa kwa ajili ya kazi hiyo lakini hadi leo hii bado tatizo hilo lipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2000 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa aliwaahidi wananchi wa Misungwi kuwa suala/tatizo la maji atalimaliza mapema. Pia Mheshimiwa Naibu Waziri alipata nafasi ya kutembelea mradi huo. Tarehe 20 Julai, 2003 yaani jana Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dr. Ali Mohammed Shein, alitembelea mradi huo alisikitishwa na kutelekezwa kwa mradi huo ambao ungewapunguzia matatizo wananchi wa Misungwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kuwa, ni vyema Serikali ikakamilisha mradi huo kwani katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa kwa kuhusisha Miji ya Musoma, Misungwi na Bukoba itakamilisha mradi huo kwa gharama ya *EURO 166,000.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu mimi na wananchi wa Misungwi ni pale Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake alipomaliza kwa kusema, Serikali ya Ufaransa imeonyesha nia ya kugharamia ujenzi wa Miradi ya Maji katika Miji hii yaani Musoma, Misungwi na Bukoba usanifu utakapokamilika, ni lini? Huo ndio wasiwasi wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo juu ya usanifu huo utaanza lini na utategemewa kukamilika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama - Shinyanga na kuvihudumia Vijiji sehemu bomba litakapopita, ni mzuri ila ni vyema wataalam wakaongeza Vijiji hasa sehemu ya Misungwi ambako ndiko mwanzo kwani kuna Vijiji vinne hadi vitano tu. Naomba viongezwe Vijiji vya Isesa, Mbarama, Nyamayinza, Buhingo, Gulumungu na Seeke ili wananchi wa maeneo hayo wapatiwe maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, wafugaji wanashukuru kwa juhudi za malambo yaliyochimbwa. Ombi ni ukarabati wa majosho. Tatizo kubwa la magonjwa ni kwamba yanaletwa na kupe hii ni sababu ya kutoogesha mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ishughulikie majosho mfano Misungwi ni majosho matano tu yanayofanya kazi na majosho 34 hayafanyi kazi, hii ni ishara tosha kuwa tatizo ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa Bajeti hii yenye mwelekeo wa kuboresha huduma ya maji kwa wananchi na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi sasa nianze kuchangia nikianza na suala la uvunaji wa maji. Ni ukweli usiofichika kuwa tatizo la maji ni kubwa ingawa Serikali inajitahidi sana. Hivyo basi, naiomba Serikali itoe elimu kwa wananchi kuvuna maji kwa kutumia nyumba zao za bati na kuwa na tanki za kuhifadhia au karo wakati wa masika ili yawafae wakati wa kiangazi kuliko kuacha maji yamwagike ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa juhudi ya kuwaondolea kero wafugaji kwa kuwachimbia malambo ya kunyweshea mifugo Vijijini katika Mkoa wa Singida hasa Iramba Mashariki, Singida Kaskazini na kadhalika. Naomba juhudi hizo ziendelee katika maeneo mengine kwa mfano Iramba Magharibi, Tarafa ya Shelui, Kisiriri na Ndago.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya bado mifugo inatembea mwendo mrefu kufuata maji kwa kuwa wananchi sasa hivi wanayo Mifuko ya Maji basi ni kiasi cha Serikali kuwaunga mkono tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie suala la vyanzo vya maji kukauka. Katika Mkoa wa Singida vyanzo vingi vya maji vimekauka kwa sababu ya aina ya miti ya Mikaratusi kupandwa kwa wingi ambayo hunyonya maji lita 40 kwa siku. Naiomba Serikali akazie agizo la kukata hiyo miti inayonyonya maji na kuhimiza upandaji wa miti inayohifadhi vyanzo vya maji. Kuna miti mingi sana Mkoani Singida iliyopandwa na inayofyonza maji kweli kweli bila agizo kali, tatizo hili halitaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kuona kuwa kuna haja wafugaji kupunguza mifugo ili waweze kuwa na ufugaji wa kisasa. Hii itawasaidia kupata malisho ya kutosha na kuwatibu wanapoingiliwa na maradhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuweka maeneo au mashamba ya wafugaji wa kisasa kwa kila Wilaya ili wafugaji wengi waweze kutembelea na kujifunza kutoka kwao. Wafugaji wengi wanakosa mahali pa kujifunza. Vile vile, wafugaji wapelekewe mbegu au madume bora ili wapate ndama wa kisasa wenye kutoa maziwa na nyama nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kutoa huduma ya maji katika maeneo mengi Mkoani Singida kwa Bajeti hii ya mwaka 2003/2004. Maeneo yaliyopewa kipaumbele ni Singida Mjini kutokea Bwawa la Itamka, Mji mdogo wa Shelui, maji toka Mto Wembere na kadhalika. Naiomba Serikali iongeze bidii ya utekelezaji ili miradi hii iweze kukamilika upesi na kutoa huduma kwa wananchi hususan wanawake ambao ndio wanapata taabu ya kutafuta maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa Serikali kujenga Vituo vya Maji Singida Mjini. Hivyo basi, naiomba Serikali iwape vioski hivi vikundi vya wanawake na vijana wanaojitahidi kuzalisha mali ili kuongeza vipato vyao kuliko Taasisi yenyewe kusimamia vioski hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, naishukuru Serikali kwa kutoa huduma bure ya maji kwa wananchi wasiojiweza. Naiomba Serikali itoe tangazo la wazi kwani wananchi tamko hili hawalijui bado wanaendelea kupata taabu ya kununua maji wakati Serikali imeshatoa msamaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali inajitahidi kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi. Bali bado maji hayo yana vijidudu vinavyoleta homa ya *Typhoid*. Naomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuhakikisha maji yanawekwa dawa ya kuua vijidudu hivyo vya *Typhoid*, kwa kuwa ugonjwa huu ni kero kubwa sana kwa afya za binadamu hasa katika Mikoa ya Singida na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iwasaidie wananchi wa Mtaa wa Kindai, Mjini Singida, kwani hawana maji kwa kushindwa kuvutiwa maji kwa sababu ya njia ya reli. Naomba Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ishirikiane na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ili wapate muafaka wa kuchimba mtaro wa maji kuvuka reli. Wananchi hawa wanapata shida. Vile vile wana kilimo cha bustani za mboga, sasa wamekwama kwa vyanzo vya maji kukauka na kukosa maji ya bomba kutoka visima vinavyosambaza maji Mjini Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia Serikali kwa kuliona tatizo la ng'ombe kuswagwa kwa miguu kwa mwendo mrefu. Naiomba sasa Serikali kwa kuwa ipo reli ya Dodoma – Singida ya abiria na mizigo iongeze mabehewa ya mifugo ili mifugo itumie usafiri huo kuliko inavyoswagwa barabarani na kuharibu barabara. Kwa maeneo ambayo hayana njia ya reli, basi watumie malori kusafirishia mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mikoa ya Singida na Dodoma sasa wanajenga uwanja wa Kanda wa Nanenane na Wizara hii ni mdau wa Nanenane, basi naiomba ione umuhimu wa kutuunga mkono katika ujenzi huu na itamke rasmi imechangia shilingi ngapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu naomba nitamke rasmi kuwa naunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. Tunawatakia utekelezaji wenye juhudi kubwa.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mikumi maji ni kero kubwa sana. Tunayo Kampuni ya maji, naambatanisha na kitabu hicho cha maelezo ya matatizo ya maji. Tunahitaji kubadili mabomba kutoka yanakotoka kwenye chanzo cha kuchukulia maji, yale mabomba ni madogo *size* yake ni inchi nne. Mabomba haya hupeleka maji kidogo katika tanki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba fedha za kubadilishia mabomba ya inchi 6 au nane, thamani yake ni Shilingi milioni 45. Tunaomba wataalamu wa Wizarani waweze kusaidiana na wa Wilayani ili tuweze kufanya utafiti mzuri. Kwani Mhandisi tuliye naye bado hawezi kufanya ufumbuzi wa maji Mikumi. Matokeo yake anataka kuanza kutoboa *tank* sehemu tatu badala ya kubadilisha bomba. Tunaomba wahimizwe wataalamu wakaangalie maji Mikumi. Bomba linalotoa kutoka kwenye *tank* ni inchi sita. Hilo ndio tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika,wakati tunahangaikia mpango wa kupata fedha ya mabomba ya inchi sita, naomba visima virefu vitano ili tuokoe uhai wa Mji Mdogo wa Mikumi na wakazi wa Mikumi. Kuna matatizo makubwa ya kipindupindu kwani wanakunywa maji ya mto Ruembe.

Pia kuna Kampuni ya Maji Ruaha, naomba watakapotumwa wataalamu hao toka Mkoani wakaangalie na Kampuni ya Ruaha nayo imesajiliwa na kuna uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwenye tatizo la Vijiji vya Wafugaji katika Jimbo langu. Kuna Vijiji viwili, Kijiji cha Kiduhi na Kijiji cha Mfilisi. Naomba majosho ya Kiduhi na Mfilisi yakarabatiwe. Majosho hayo yalichimbwa mwaka 1988 na sasa yamechakaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo hayo ya Kiduhi kuna bwawa linachimbwa sasa ni miaka miwili hawajamaliza. Kinachoonyesha, ni yule mhandisi hana uwezo wa kazi yake. Naomba afuatiliwe ili akitendee haki Chama cha Mapinduzi (CCM)

Mheshimiwa Naibu Spika, ranchi ya Mkata imeguswa na Jimbo la Mikumi. Tunaomba tufikiriwe maeneo ya kufugia, kuondoa kero. Ahsante.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi ya kumpongeza Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, pamoja na Naibu Waziri na wataalam wake kwa kuandaa hotuba nzuri iliyojaa matumaini kwa Watanzania.

Pia nachukua nafasi kuishukuru Wizara kwa kuiweka Wilaya ya Kiteto katika Mradi wa Benki ya Dunia kwa masuala ya Maji. Wananchi wa Kiteto watashirikiana kikamilifu kufanikisha mradi huo. Tatizo la maji ni kubwa sana katika Wilaya ya Kiteto. Tatizo lingine la kuangalia ni gharama au mchango wa wananchi kwani asilimia ya miradi ya maji ni kubwa kwani ina gharama ukilinganisha na miradi mingine.

Suala la majosho ni tatizo kwa nchi nzima. Idadi ya majosho yanayofanya kazi ni 476. Majosho yasiyofanya kazi ni 1,574. Hii ni hatari sana kwani bila kuogesha mifugo maradhi mengi yanashambulia mifugo. Tatizo kubwa linatokana na gharama kubwa ya dawa za kuogeshea. Naomba Serikali iangalie tatizo hili kwa upana wake kwa kutoa ruzuku kwa wafugaji kama inavyotoa kwa wakulima.

Wizara kwa jitihada zangu hususan katika Kikao cha wadau walizungumzia kwa nguvu zote kuhusu maeneo ya wafugaji. Tatizo hili bado ni kubwa sana na wakulima wanaendelea kuvamia maeneo ya wafugaji kwa kulima. Mfugaji bado hajatendewa haki na Serikali inawasikiliza sana wakulima. Mara nyingi mfugaji huonewa kutokana na hali yake ya kutokwenda Shule. Wizara iunde Kamati ya kufuatilia maeneo ya wafugaji na wawekwe watu ambao ni jasiri, wenye kufuata haki na kutoa taarifa Serikalini.

Kuhimiza ufugaji bora ni jambo muhimu sana lakini la muhimu zaidi ni soko. Kujenga viwanda vya kusindika nyama. Bila viwanda hivyo ufugaji utakuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu unahusu uboreshaji wa huduma kwa Wizara hii pamoja na kutilia maanani malalamiko mbalimbali ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilipochaguliwa kwenye Jimbo langu la Moshi Vijijini, wananchi walinituma mambo mbalimbali ya kuja kuwawakilisha humu Bungeni, yaliyokuwa yakiwakera kwa muda mrefu. Katika moja ya mambo waliyonituma ni kuwasilisha kilio chao cha muda mrefu kuhusu maji safi ya bomba kwani wengi wao wanasikia mabomba ya maji kwenye redio na magazeti tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri atakumbuka kuwa niliwahi kuhoji hapa Bungeni kuhusu matatizo ya maji ya bomba katika Jimbo langu mwaka 2001 na pamoja na mambo mengine nilimtajia Vijiji ambavyo vina matatizo makubwa ya kupatiwa maji safi ya bomba na niliwaeleza kuwa maji yapo lakini yanatiririka kutoka mlimani na kuzoa uchafu mwingi kama vile vinyesi vya mbwa, wadudu waliokufa na kuoza kupitia kwenye mifereji ya asili iliyowekwa na babu zetu. Nilimweleza Waziri pia kuhusu hali ya maji hayo kwamba, hayahitaji umeme wa kuyasukuma wala mashine ya kuyachimba ila ni kuyaweka tu kwenye bomba na kutiwa dawa, basi. Maana yenyewe yana uwezo wa kujisukuma. Pia nilimweleza Waziri kuhusu ahadi ya Serikali ya mwaka 1980, iliyowataka wananchi hao kuchangia Sh.40,000/= za wakati huo, mwaka 1980, ambazo Kijiji cha Singa kilichanga. Shilingi 40,000/= ukilinganisha na dola wakati huo ni Sh.9/= kwa Dola moja, aidha Sh.100/= Dola 12, Sh.1,000/= Dola 120, Sh.40,000/= sawa na Dola 5,000/= ambazo ni zaidi ya Shilingi milioni tano kwa sasa. Kama wangekuwa wameweka fedha hizo Benki, kwa fidia ya asilimia 31 leo hii zingezaa na kufikia zaidi ya shilingi milioni 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zilizochangwa wakati huo zilipokelewa na Wizara hii na hadi leo Wizara imekaa nazo bila kuonyesha hatima ya ahadi yao ya kuwawekea maji ya bomba wananchi hao, pamoja na kelele za mara nyingi. Wengi waliochanga fedha hizo akiwemo baba yangu mzazi wameshafariki bila kushuhudia ahadi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya kuwawekea mabomba ya maji. Mwaka 2002 nikiwa kwenye Kamati ya Uzalishaji, Waziri aliamua kutuma wataalamu wake ili kuona hali halisi na wataalamu hao walishuhudia Shule Kongwe ya kufundishia Walimu, *Singa Chini Teachers Training College* ikiwashangilia wataalam hao na ni pamoja na kuwakaribisha chakula nikiwemo mimi. Kwa kuona kuwa tunawakumbuka, lakini nilivyokuja kutazama Bajeti sikuona mgao na nikapewa ahadi nyingine ya kupatia huduma hiyo mwaka huu wa fedha na sijaona mahali palipoandikwa kuhusiana na mradi huo. Kijiji cha Singa kina maendeleo kama vile *Kibosho Girls Secondary*

*School, TTC*, Chuo cha Maendeleo, Kanisa Kuu la Kibosho, *Nsoo Secondary School*, Wananchi na *Primary Schools* kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali halisi ya Utawala Bora, nisingetegemea Waziri au Wizara kudanganya wananchi hao kama watoto wadogo. Nisingependa Serikali yangu kufanya hivyo. Naiomba Serikali kutimiza ahadi zake katika Vijiji hivyo vya Moshi Vijijini ambavyo ni kuanzia huko Kibosho. Umbwe Onana, Kirima, Dakau, Singa, Uru Kyaseni Mbokomu, *Old Moshi Kimochi, Old Moshi, Old Tela,* Mande, Uru Ongama, Uru Mdawi, Uru Kishumundu, Mwasi Kaskazini, Mwasi Kusini, Mandaka Mnono, Chekereni, Mabogini, Ntakuja, Uru Shimbwe, Mweka Sungu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nategemea kuondoa Shilingi ya mshahara wa Waziri ili wananchi wangu waamini kuwa ni kweli nilipeleka kilio chao cha siku nyingi kinachohusu maji ya bomba kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Maji, pamoja na Naibu Waziri na wataalam wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mifugo kuwekewa utaratibu wa kupita kwenye *stock route* nadhani kwa sasa umeshapitwa na wakati kwa sababu Waraka ulioandaliwa na Mheshimiwa Rais kwamba, wananchi wasiswage mifugo kwa kupita barabarani, inaelekea utekelezaji wake ni mgumu kwa sababu agizo ni pana mno. Agizo hilo pamoja na kusema wamepewa jukumu hilo Watendaji kudhibiti hilo, imekuwa vigumu sana kulidhibiti kwa sababu ya rushwa.

Napendekeza suala hili lishughulikiwe na iwe ni maalum, wateuliwe maaskari maalum kwa ajili ya kudhibiti hilo tu kwa maana ya kuhakikisha kuwa kuanzia sasa mifugo isiswagwe badala yake isafirishwe aidha kwa magari, treni na njia nyingine yoyote lakini wakiwa ndani ya chombo cha usafiri. Hii itasaidia kudhibiti kutawanyika kwa maradhi ya mifugo. Sisi katika Wilaya yetu ya Mpanda, tumeathirika sana kwa maradhi ya mifugo ya kuambukiza ambayo yamesababisha kufa kwa mifugo mingi sana. Naomba hilo lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, alifika Wilayani Mpanda. Naomba Mheshimiwa Waziri, aendelee kutusaidia kutafuta wafadhili watakaotusaidia kuweka mtandao mpya wa mabomba kwa sababu Mji wa Mpanda umepanuka sana, hivyo wanaopata maji ya bomba wamebakia ni watu wachache sana katika eneo la Mji wa Mpanda. Suala hili kama wataachiwa Halmashauri ya Wilaya hawataweza kwa sababu uwezo wao ni mdogo. Katika fedha zinazotolewa na Wizara, kwa maana ya fedha za maendeleo kwa Halmashauri zinazotolewa na Wizara, inatakiwa fungu hilo liongezwe mara dufu katika Mji wa Mpanda ili tuweze kufanikisha upatikanaji wa maji Mji mzima wa Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa itachukua muda mrefu kukamilisha mtandao wa mabomba Mjini Mpanda, naomba nimkumbushe Waziri kuwa aliniahidi kunisaidia kuchimba visima virefu Mjini ili kuweza kupunguza tatizo la upatikanaji wa maji katika Mji wa Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hotuba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuweka Mradi wa Maji Nachingwea Mjini. La muhimu ni Wizara kufuatilia upatikanaji wa fedha (Hazina). Naomba nipate ratiba ya kazi kuhusu *Mbwinji Study* na uchimbaji wa visima kumi ulioahidiwa mwaka huu 2003/2004. Je, visima hivyo vitachimbwa eneo gani? Je, kutakuwa na mabomba yatayonunuliwa katika programu hiyo? Je, zile fedha shilingi milioni 32 zilizotengwa za kuchimba kisima kirefu Nachingwea Mjini zilitolewa? Je, kisima hicho kimechimbwa?

Je, progarmu ya Wajapan ya kuchimba visima Lindi na Mtwara imefikia wapi *(JICA)?*. Je, kwenye programu hiyo ya *JICA* Nachingwea itapata visima vingapi na vitachimbwa wapi (*sites*, kwa majina ya Vijiji)?

Mwisho, nategemea programu za *Mbwinji Project* (Nachingwea - Masasi). Nampongeza Waziri kwa utendaji kazi wake mzuri, *action oriented* na wasaidizi wake wote (Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wengine).

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa hotuba yake nzuri sana lakini pia kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara yake.

Maendeleo ya wazi yanaonekana katika Wizara hii chini ya Mheshimiwa Edward Lowassa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo matatizo mawili hivi katika Jimbo langu la Babati Magharibi. Kwanza niliwahi kuuliza mpango wa Serikali kuhusu bwawa la Setcheda lililopo Kata ya Ufana mpakani na Wilaya ya Hanang. Bwawa hili limeendelea kujaa *(silted up)* na nilikuwa naomba lisafishwe kuondoa matope ili kurudia kina chake cha awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kuomba kwa namna ya pekee, Serikali itoe kipaumbele kwa bwawa hili ambalo ni tegemeo kubwa wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ombi langu hili la bwawa la Setcheda limefika Serikalini tangu mwaka 2001, kwa njia ya swali nililouliza na mwaka huu 2003/2004 halipo kwenye Bajeti. Naomba Waziri alifikirie kwa namna ifaayo ili matope yatakapokauka kiangazi hiki yaweze kuondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la pili ni la stock route. Sasa hivi mifugo inayopita kwenye barabara ya Mbulu - Bashanet - Babati inafanya uharibifu mkubwa kwa barabara. Naomba hatua za haraka zichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali, hotuba ni nzuri na hivyo sina zaidi ya kuboresha isipokuwa hayo mawili kwa umuhimu wake. Kwa hiyo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu, Ndugu Bakari A. Mahiza, Naibu Katibu Mkuu Dr. Charles Nyamrunda, wafanyakazi wote wa Wizara na wadau wengine kwa jitihada wanazofanya kuboresha huduma za maji nchini na kuleta mageuzi katika maendeleo ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu katika hotuba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, utahusu maeneo mawili, matatu tu. Mradi wa maji wa Ziwa Victoria kwa wakazi wa Mji wa Kahama, Mradi wa Dharura wa Maji kwa Mji wa Kahama na mkakati wa uchimbaji mabwawa ya kunyweshea ng’ombe na huduma za Mabwana Mifugo Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kwanza kupata ufafanuzi wa Waziri kuhusu upeo na ukubwa wa mradi wa maji ya Ziwa Victoria kwa Mji wa Kahama. Kama nilivyosema katika swali langu la nyongeza katika Swali Na.271, Mji wa Kahama unakua kwa kasi ya asilimia 10.44 kwa mwaka na inakadiriwa kwamba, ifikapo mwaka 2024, miaka 20 kuanzia sasa, Mji wa Kahama utakuwa na wakazi wapatao 622,000. Hivyo, lazima kubuni mradi utakaolenga kukidhi mahitaji ya maji na idaidi hiyo ya zaidi ya laki sita ya wakazi wa Mji wa Kahama. Aidha, lazima kubuni mradi utakaolenga kukidhi mahitaji ya eneo la Halmashuari ya Mji wa Kahama ambao kulingana na taarifa zilizopo, Halmashauri ya Mji Mdogo wa Kahama umeanza kutumika rasmi kuanzia Julai, Mosi 2003.

Ningependa kulisisitizia suala la mradi huu kwa kuzingatia upana na upeo huo. Aidha, ningependa kusahihisha kwamba, ukuaji wa Mji wa Kahama hautegemei kuwepo kwa wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu tu na sio kweli itapungua kama machimbo haya yatakwisha. Uchumi wa Kahama unashamiri kutokana na misingi mingine mikubwa. Kilimo endelevu cha mazao ya chakula na biashara, mahindi, mpunga, alizeti, karanga, pamba, tumbaku, biashara inayoendeshwa kwenye barabara kuu ya lami ya Isaka - Rusumo, Kitovu cha biashara baina ya Tanzania na nchi za Maziwa Makuu kwa kupitia Bandari kavu ya Isaka, mazao ya misitu, asali, nta, mbao na kadhalika. Hali ya hewa kwa maeneo mengi yaliyo wazi yataendelea kuifanya Kahama kuwa kivutio kwa wahamiaji wengi. Mhandisi Mshauri *GIBB (Eastern Africa) Limited* hawakukosea kulenga idadi ya wakazi 622,000 kuwa ndio takwimu ya kufanyia kazi katika kuupatia Mji wa Kahama maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai. Namwomba Mheshimiwa Waziri, anifafanulie hatma ya mradi wa Dharura wa kuupatia maji Mji wa Kahama wakati tunasubiri Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria. Hivi sasa ninavyozungumza, Mji wa Kahama hauna maji. Kwa taarifa tu, kwa Mheshimiwa Lowassa, ni watu 59 kati ya wakazi wanaokaribia 80,000 wa Mji wa Kahama ndio wanaopata maji ya bomba. Wengine wanapata maji ya mashimo na kusambazwa kwa kutumia matoroli na mikokoteni. Si maji yenye uhakika kwa utumiaji wa watu. Hayana uhakika wa upatikanaji, wakazi wa Mji wa Kahama wametiwa moyo sana na uamuzi wa Wizara kupitia Idara ya Raslimali za Maji kufanya utafiti yakinifu mara mbili kutafiti vyanzo vya maji kwa ajili ya mradi huu wa dharura. Kulingana na taarifa nilizozipata kufuatana na tafiti hizo, tayari wataalam wamegundua maji katika maeneo ya Kagongwa, Nyamhela Bukondamoyo na Nyandekwa, ambako takriban visima virefu 13 vitachimbwa kwa ajili ya kupokea maji Mji wa Kahama. Ni matumaini yangu ya dhati kwamba, mradi huu wa dharura utatekelezwa mwaka huu wa fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, tabu ya kupata na kusambaza maji kwa Mji wa Kahama imejenga kada ya vijana ambao wamepata uzoefu mkubwa katika kusambaza maji kwa kutumia matoroli na mikokoteni. Kada hii ni muhimu katika jamii. Imejenga uzoefu katika shughuli za utafutaji na usambazaji maji. Imebuni mkakati wa kujiajiri na kujipatia kipato halali pasipo kujiingiza katika shughuli za uzururaji na uhalifu.

Ninaomba sana, Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria usiwatenge na kuwapuuza. Ninaomba Serikali ifikirie kuwaongezea ujuzi vijana hawa na mradi wa maji ya Ziwa Victoria ufikirie kuwajengeja Vituo vya kuwawezesha kuendelea kusambaza maji hayo kwa wakazi wa Kahama kwa mfano kupitia vioski na mabomba ya pamoja hasa katika maeneo ambako hakutakuwa na mabomba nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchimbaji wa mabwawa ya maji ya kunyweshea mifugo, naomba Serikali irejee utaratibu wa kutoa asilimia 50 ya fedha na Halmashauri zitakiwe kuchangia asilimia 30 na wananchi asilimia 20. Baada ya Serikali kufuta vyanzo vya mapato ya Halmashauri za Wilaya, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, afafanue nia za kufidia pengo lililojitokeza, ukiangalia jedwali Na.7 la Hotuba ya Waziri utaona kwamba, fedha zilizotengwa na Wizara kwa ajili ya uchimbaji wa mabwawa katika Vijiji vya Chambu, Nyamilangano, Nyandekwa, Jimbo la Kahama, Mpaka sasa hazijatumika kutokana na uchangiaji mdogo.

Mwisho, ninaomba Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo iboreshe huduma za ughani kwa wafugaji wa Vijijini. Kinachofanyika sasa ni kwamba, Mabwana Mifugo wengi wamehamia Mijini ambako kuna *Effective Demand* ya ufugaji ng'ombe wa maziwa na ufugaji wa kuku kibiashara. Vijijini ambako ndiko kuliko na wafugaji na mifugo mingi zaidi, hakuna huduma hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na safu nzima ya uongozi za Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Ninaunga mkono hoja ya Waziri mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Arusha pamoja na kuitwa Geneva ya Afrika, bado inakabiliwa na upungufu wa maji wakati wa kiangazi. Kuna umuhimu basi wa kuongeza vyanzo vingine vya maji yatakayohudumia Manispaa hii inayokua kwa kasi. Shirika la Maji Arusha *(AUWASA),* lina mpango wa kuanzisha chanzo kipya cha huduma. *KfW* Ujerumani tayari imekwishatoa vifaa vyenye thamani isiyopungua Shilingi milioni mia sita. Vifaa hivyo vipo Arusha. Kinachokosekana ni fedha za kukamilisha ujenzi wa chanzo hiki. *AUSWA* imekwishatenga Sh.200,000,000/=. Zinahitajika karibu Sh.800,000,000/=. Wizara inaombwa izitafute hizi fedha ili kukamilisha mradi huu. Vinginevyo vifaa vilivyotolewa na *KfW* Ujerumani, hazitaweza kutumika vizuri. Pia tatizo la maji wakati wa kiangazi pale Arusha litazidi kuwa sugu. Hii itawatia nguvu wale wanaotutakia mabaya kwa kusema kuwa Manispaa ya Arusha haifai kuwa Makao Makuu ya *EAC* kwa kukosa huduma muhimu ya maji wakati wa kiangazi. Tunaomba Wizara ituondolee aibu hiyo.

Nawasilisha kwa kuipongeza *AUWSA* kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia shughuli za *AUWSA* Arusha.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Naomba nieleze kwamba, Jimbo langu lina Tarafa mbili zenye Kata 17. Tarafa ya Misenyi yote ina matatizo ya ukame. Naomba Wizara itambue kwamba, Tarafa ya Misenyi ni kati ya Tarafa kame hapa Tanzania. Kwa sababu

hiyo, naomba Wizara iwe inakumbuka Tarafa ya Misenyi katika mipango ya Wizara ya kupatia maji maeneo kame. Eneo la Misenyi lina watu zaidi ya tisini elfu. Wananchi walio wengi hulazimika kutembea zaidi ya kilometa tano hadi kumi kutafuta maji. Naomba Wizara isaidie chochote itakachoweza kupata. Wizara ikiweza kutupa visima virefu tutashukuru. Wizara ikiweza kutupa mabwawa vile vile tutashukuru. Wananchi wako tayari kutoa michango yao katika kutekeleza miradi ya maji.

Aidha, katika Jimbo la Nkenge, kuna miradi mingi iliyoanzishwa miaka ya sabini na hivi sasa haifanyi kazi. Miradi hiyo ni kama vile Gera/Katoma, Kilimilile, Kisambya, Ruzinga , Kanyigo 'A', *Nkenge Gravity,* Mtukula, Bugandika, Kanyigo 'B'. Aidha, wataalam walinieleza kwamba, tunahitaji shilingi bilioni 1.3 kufufua miradi hiyo. Naomba Wizara itusaidie kuongezea nguvu Halmashauri ya Bukoba kufufua miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla fedha tunazotenga kwa ajili ya miradi ya maji Tanzania ni kidogo mno. Kwa mwendo huu, Wizara haitaweza kukidhi kiu ya Watanzania ya kupata maji safi na salama. Ili tuweze kupata fedha za kutosha napendekeza yafuatayo:-

(i) Tuanzishe mfumo wa maji wa Taifa ambao utafanya kazi kama Mfuko wa Marabara;

(ii) Tuanzishe *Windfall Tax* na fedha itakayokusanywa tuipeleke kwenye Mfuko wa Maji. *Tax on Super Normal Profit Made on Water Services Rendered;*

(iii) Tuondoe kodi za aina zote kwenye shughuli zote za utafiti, uzalishaji na usambazaji wa maji;

(iv) Tuondoe kodi zote kwenye mitambo yote inayotumika kuchimba na kusambaza maji; na

(v) Kwa kuzingatia uzito wa majukumu na umuhimu wa Maji na mifugo, ni vizuri Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo igawanywe na tuwe na Wizara mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba maazimio yote ya Mkutano wa Wadau wa Mifugo uliofanyika Arusha chini ya Mheshimiwa Rais, yatekelezwe. Tusipoyatekeleza tutakuwa hatuitendei haki Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. DR. IBRAHIM S. R. MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali naomba Waziri arejee barua yangu niliyomwandikia tarehe 9 Julai, 2003 juu ya tatizo kubwa la ukosefu wa maji katika Wilaya ya Kibaha.

Kwanza, namshukuru sana kwa usikivu wake na jitihada zake zilizolenga kutatua tatizo hilo mara baada ya kumwona juu ya tatizo hili. Namshukuru pia Mkurugenzi Mkuu wa *DAWASA (PGA),* Bwana Mutalema, kwa kunitafuta na kuzungumza nami kutokana na maelekezo ya Waziri. Hata hivyo, tatizo la ukosefu wa maji Kibaha bado liko pale pale na naomba nirejee maelezo yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilayani Kibaha kuna tatizo kubwa la ukosefu wa maji kiasi cha kuhatarisha usalama na ustawi wa jamii. Inaelekea tatizo ni la kimfumo na kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba mtazamo huzaa mfumo na mfumo nao unaweza kuzaa mtazamo *(perception)*, kihistoria na kimfumo, maji ya Mto Ruvu yalilengwa kuhudumia wakazi wa Dar es Salaam. Wakati huo Dar es Salaam ilikuwa sehemu ya Mkoa wa Pwani. Baada ya kuundwa kwa Mkoa wa Dar es Salaam, Mkoa mkongwe wa Pwani haukuwa na mfumo wake wa maji na hivyo kupelekea Mkoa/Kibaha kuendelea kuonekana kama ni sehemu ya Dar es Salaam.

Wilaya ya Kibaha ina mifumo miwili ya maji. Kuna Kata sita ambazo baadhi ya maeneo yake huhudumiwa na Mamlaka ya Maji Safi/Maji Taka, Dar es Salaam (Mlandizi, Visiga, Kibaha, Soga, Tumbi na Maili moja) na Kata tatu (Magindu, Kwala na Ruvu), ambazo hutegemea maji yatokanayo na Mto Ruvu, Mabwawa na Visima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji maji katika maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka ya Maji imekuwa mbaya sana katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita kiasi kwamba wananchi/viongozi wanaamini kuwa *DAWASA* haikuwa ikiwajali kabisa. Vikao vya *RCC* Mei, 2003 vyote vilizungumzia kwa undani suala hili

linalotishia ustawi wa jamii wa wananchi wa Kibaha. Hivi sasa hali inatisha. Wananchi kwanza wanategemea maji ya visima ambavyo vimekauka kutokana na ukame, pili, wanakwenda masafa marefu kutafuta maji na kuzorotesha kazi nyingine za maendeleo na hata Taasisi muhimu kama vile Shirika la Elimu Kibaha lenye hospitali muhimu ya Tumbi inakabiliwa na tatizo kubwa la maji.

Uongozi wa Mkoa wa Pwani/Kibaha umejitahidi sana kushirikiana na *DAWASA* katika kuondoa kadhia hii bila ya mafanikio. Mimi mwenyewe nimewahi hata kuingilia kati mara kadhaa ili *TANESCO* warudishe umeme kwenye Vituo vya kusukumia maji ambavyo vinadaiwa na Shirika hilo la Ugavi wa Umeme.

Pamoja na maelezo mazuri ya mara kwa mara ya *DAWASA* ya matatizo ya mitambo ya Ruvu Juu na mgao wa maji, taarifa hizo hazitoshelezi kujibu hoja za ukosefu mkubwa wa maji kwa kipindi kirefu kwa Wilaya ya Kibaha kwenye chanzo cha maji, wakati Dar es Salaam inapata maji, hata ikiwa kwa mgao.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana basi tatizo la mfumo wa maji umezaa utendaji usioridhisha, kwa mfano katika mradi wa Maji Kongowe - Soga, Kata ya Soga ina shamba la Mkonge/Mifugo Alavi, Shule ya Sekondari, Shule ya Msingi, Shamba la Mbegu Vikuge, Zahanati na watu wengi. Kufikisha maji Alavi pekee, kungeweza kulipia mradi mzima. Aidha, Kata hii ambayo ingeweza kunusurika na ukosefu mkubwa wa maji sasa inaongoza kwa tatizo hilo na kutishia kufungwa kwa Shule ya Sekondari ya Soga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri aingilie kati ili wakazi wa Wilaya ya Kibaha wapate maji. Huu ni wakati muafaka ili Mamlaka mpya ya Maji inayoanza kazi hivi punde, isije ikaambukizwa mtazamo huu wa sasa unaotokana na mfumo uliopitwa na wakati na usiowatatendea haki wananchi wa Mkoa wa Pwani/Kibaha. Hivyo basi, nashauri:-

(a) Pawe na mfumo mwingine mahususi (kama vile Bomba na matanki maalum kutoka Ruvu Juu) utakaohudumia Mji na Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha. Ukosefu wa mfumo mahususi wa maji kwa ajili ya Mji na Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha umepelekea utendaji unaotafsiriwa kuwa maji ya Ruvu ni kwa ajili ya Mkoa wa Dar es Salaam. Kuna wakati hata wafunguaji maji katika Vituo vya maji vya Kibaha walikuwa wanatoka Dar es Salaam, licha ya kwamba *DAWASA* imekuwepo Kibaha;

(b) Pachimbwe visima virefu kwenye maeneo yenye maji ili kuongeza upatikanaji wa maji kwa wakazi wa Mji na Halmashuari ya Wilaya ya Kibaha;

(c) Mradi wa Maji - Kongowe - Soga ukarabatiwe na uunganishwe na wateja wenye uwezo wa kifedha wa Shamba la Mkonge la Alavi wanaohitaji sana maji safi kwa ajili ya uzalishaji wa maziwa, bidhaa zitokanazo na maziwa na matumizi ya binadamu ili mradi huu uwe endelevu na ujilipe;

(d) Mamlaka ya Maji ishirikiane na *TANESCO* ili Kituo cha kuvutia maji cha Kongowe kirejeshewe umeme. *TANESCO* imekuwa ikinilalamikia kuwa *DAWASA* haikuwa inatoa ushirikiano wa kutosha na hivyo kupelekea kukatiwa umeme katika Kituo chake cha kusukumia maji cha Kongowe;

(e) Mamlaka ya Maji ipitie upya orodha ya wateja wa maji na ikusanye ankara za maji mara huduma hiyo inapopatikana katika maeneo husika. *DAWASA* imewahi kutoa orodha ya wateja hewa na kudai kuwa wakazi wa Soga hawataki kulipa ankara za maji; na

(f) Taasisi muhimu kwa Taifa hili kama vile Shirika la Elimu Kibaha, lipatiwe maji ya uhakika ili kunusuru wagonjwa na wengineo wanaotegemea sana maji ya Mto Ruvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukurani zangu kwa ushirikiano wako na naunga mkono hoja.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu, Ndugu R. Kijazi, Watendaji wake Wakuu wote bila kuwasahau Mr. Sayi, Mr. Mziray na kadhalika kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa huduma za maji hapa nchini na pia kutoa huduma nzuri upande wa mifugo. Kazi zote wanazofanya zinaonwa na Watanzania wote hapa nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa fedha zilizotolewa kwa ajili ya kununua mashine za maji kwa ajili ya Vijiji vya Tumuli, Kinyangoni na Matongo. Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ilipokea Sh.14,000,000/= kwa ajili ya kazi hiyo nazo zimetosheleza kununua mashine mbili kwa ajili ya Tumuli na Kinyangivi na zimebaki Shilingi milioni 3.9 kwa ajili ya *windmill* ya Matongo ambayo inagharimu Shilingi milioni 10.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina wasiwasi, naamini kabisa kwamba, mwaka huu wa fedha Wizara itaniongezea fedha hizo ili wananchi wa Matongo ambako ndiko nilikozaliwa, waweze kupata *windmill* hatimaye wapate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Iramba wamenituma nimpongeze sana Waziri na kumshukuru kwa kutuletea *World Bank* waweze kutupatia maji mengi kwa kushirikiana na wananchi. Namhakikishia Waziri kwamba, tutashirikiana na Benki ya Dunia kuhakikisha wananchi wanatoa michango yao ya hali na mali ili mradi huu uweze kufanikiwa kwa kiwango cha juu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda nimpongeze Waziri na Watendaji wanaomsaidia katika kuendeleza Sekta ya Mifugo. Sasa hivi wananchi wengi wameshaona umuhimu wa kupunguza mifugo yao ili waanze kufuga kisasa badala ya kuwa na mifugo mingi ambayo haina faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshauri Waziri kuwa awasiliane na Waziri wa TAMISEMI, waweze kuwahamisha wataalam wa mifugo ambao wamekaa eneo moja kwa miaka mingi na kusahau wajibu wao na kuanza shughuli za biashara. Wilaya ya Iramba tunaye Daktari wa Mifugo ambaye amekaa hapo zaidi ya miaka 15 na alishasahau kazi yake, sasa hivi amekuwa mfanyabiashara.

Pia nashauri sana Maafisa mifugo waongezwe kwenye Kata zetu ili kuwahudumiwa wafugaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia na ninamwomba Waziri na wasaidizi wake, waendelee na kasi hii ya kuwasaidia wananchi upande wa maji hasa Mikoani na kuendeleza mifugo.

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali naomba Waziri arejee maombi yangu kwake kwa mradi wa maji Likamba, ambao wananchi na Halmashauri ya Arumeru, wamekwishachangia jumla ya Sh.6,700,000/= kama inavyoonekana katika barua ya maombi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutashukuru kwa msaada wowote.

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali naomba ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa utafiti wa kuchimba visima katika Miji pamoja na Kahama (aya ya 25, ukurasa wa 19 - Hotuba ya Waziri).

Nadhani Mheshimiwa Waziri, atakumbuka kilio cha muda mrefu cha wakazi wa Mji wa Kahama kuhusu haja ya Mradi wa Dharura. Sikuridhika sana na jibu la Waziri katika swali langu Na.271. *Thrust* yake ni Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria, ambapo hoja za Kahama ni kuwa tunaomba *an immediate supplementary project.* Naomba ufafanuzi.

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri Edward Lowassa kwa jitihada kubwa aliyoifanya kuweza kutupatia maji safi na salama hasa hapa Dodoma.

Naomba nielewe hatua zilizochukuliwa na Serikali kupata maji kutoka Mto Ruvu ili kuweza kusaidia kutoa huduma ya maji ya kutosha kwa Jiji la Dar es Salaam. Mfano maeneo ya Segerea maji hayapatikani kabisa kwa sababu yote yanatumiwa na Kiwanda cha Nyuzi cha Gongo la Mboto. Hivyo mabomba ya Segerea hayatoi maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu Soko la Zanzibar kwa ajili ya nyama ya ng'ombe na mbuzi. Taarifa ya sasa ya bei ya nyama ya ng'ombe Zanzibar imeshafikia Sh.1,800/= mpaka 2000/= kwa kilo. Bei hii ni ya juu, kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri, aandae utaratibu ili Ushirika wa Wafugaji waweze

kuleta nyama ya ng'ombe Zanzibar. Soko lipo kubwa na walaji wa nyama wengi pamoja na Mahoteli ya Kitalii yaliyozagaa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ile ranchi ya Makurunge kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaendeleaje? Tatizo la Hatimiliki kwa ranchi hiyo lilimalizika?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wafugaji wanaomba Wizara iandae taratibu za mikopo kwa ajili ya kununua mbegu bora za mifugo.

**MHE. VENACE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na timu yake kwa jinsi alivyoweza kuiwasilisha hotuba yake vizuri na kueleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natoa pongezi kwa Wizara hii kwa kukubali kufuta baadhi ya kodi ikiwemo hii ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutaka ufahamu wa mpango ambao umetayarishwa kwa Wilaya hizi mpya ikiwepo hii ya Kilolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa Mheshimiwa Waziri wakati anajibu hoja za hotuba yake, aweze kueleza ana mpango gani wa kusaidia tatizo la maji katika Mji Mdogo wa Ilula kwani Mheshimiwa Waziri alitoa ahadi hapa Bungeni kusaidia kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ahadi hii, wananchi wa Ilula wamekuwa na imani kubwa na Waziri pamoja na Serikali yetu. Ikumbukwe kuwa kwa kutatua kero hii, Serikali itakuwa imetekeleza Ilani ya Chama Tawala (CCM). Pia wananchi wameshafanya kazi kubwa sana katika jambo hili pamoja na kuchimba mifareji na kununua baadhi ya vifaa.

Mwisho, ningeomba Mheshimiwa Waziri, apange ziara katika Wilaya hii ya Kilolo hasa katika Mji Mdogo wa Ilula. Gharama ya mradi huu hazizidi Shilingi milioni 15.

Pia ningeomba Mheshimiwa Waziri, awape pongezi za maandishi baadhi ya Wahisani ambao wamejitolea kutusaidia kutatua tatizo hili. Hao ni kama wafuatao: Kanisa la Kilutheri Tanzania - Uchimbaji wa visima, Kanisa la Anglikana - usambazaji wa maji na Jumuiya ya Kiislamu - uchimbaji wa visima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itawapa moyo Wahisani hao.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji Wakuu wote wa Wizara hii, kwa kuweza kuiendesha Wizara kwa makini na uelewa wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo hayo yanatokana na busara za Rais wetu, kuwachagua Mawaziri husika kutoka katika maeneo ya wafugaji ambao kwa kiwango wanajua matatizo na mafanikio ya mifugo yanaenda sambamba na upatikanaji wa maji.

Napenda kuishukuru Wizara hii kwa kuweza kutuonyesha wana Geita katika miradi midogo midogo ya Nyakagombe, Nyang'hwale na uchimbaji wa Malambo matatu ambayo ni chanzo tu katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2000. Kwa mantiki hiyo na uendelezaji wa miji, naomba Wizara hii iuangalia Mji wa Geita kama miradi mingine mikubwa ambayo inatakiwa kupata maji kutoka Ziwa Victoria. Itakuwa ni kichekesho Mji wa Shinyanga/Kahama kupata maji kutoka Ziwa Victoria ambapo iko umbali wa km 250 wakati kutoka ziwani hadi Mjini Geita ni kilometa 24 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara kwa umakini wake ambapo nina uhakika Mji wa Geita utapewa maji ya uhakika hasa tukizingatia kuwa Wilaya inachangia kiasi kikubwa katika Pato la Taifa. Wananchi watafurahi kama wangepata maji na sisi wawakilishi wao tungeacha hata kitendo cha kudai mrahaba kwa kuwa tungeona kuwa Serikali inatujali kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuishukuru Wizara hii kwa kuiweka Wilaya ya Geita katika mradi wa maji na usafi wa mazingira vijijini *(RWSSP)* unaotekelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia napenda kusema kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA S. KIDUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, dhumuni langu ni kumpongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Wataalam wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu wake kwa umahiri wao mkubwa sana.

Naomba niishukuru Wizara kwa kuliona tatizo kubwa la maji kwa mifugo yetu katika Kata ya Saunyi Kilindi kama ulivyoonyesha utekelezaji wake katika ukurasa 112 wa hotuba yako. Umesema fedha kwa uchimbaji wa Lambo la Saunyi zimetolewa tangu Aprili, 2003. Naomba kujua ni kiasi gani ili nisaidie kufuatilia. Lakini hali halisi ni kuwa Bwawa la Saunyi halijaanza kuchimbwa hadi leo ingawa lile la Kilimilang'ombe limeanza kuchimbwa tangu mwezi Mei. Je, hili la Saunyi litaanza kujengwa lini?

Mji Mdogo wa Songe ambao ndiyo Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Kilindi umepangiwa kufufuliwa mradi wa maji ya kusukumwa kwa *pump.* Tunaishukuru sana Wizara. Hata hivyo, kuna maji mengi juu ya Mlima wa Bokwa karibu sana na Mji Mdogo wa Songe. Naomba Wizara ikakione chanzo hiki cha mlimani ili maji ya kusukumwa na *pump* yajumuishwe na mradi huu mkubwa wa *Gravity* wa Mlima Bokwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kurudia kutoa shukrani na pongezi nyingi kwa kazi nzuri ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu sekta ya maji na mifugo.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Pamoja na kuunga mkono napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa, napenda kuishukuru sana Serikali kwa kupeleka wafadhili wa Benki ya Dunia Wilayani Mpwapwa. Hivi sasa Benki ya Dunia imekwishatoa zaidi ya shilingi 960,000,000/= kwa ajili ya miradi ya maji Wilayani Mpwapwa. Vijiji vitakavyonufaika na miradi hiyo ni Mazae, Chiseyu, Berege, Sazima, Igoji II, Chipogoro, Mtera, Ukuyu, Chamtumile na Chaludewa. Utekelezaji wa miradi hiyo tayari umekwishaanza na maji yamepatikana bado kufunga mabomba ili wananchi wapate huduma ya maji. Vijiji ambavyo bado vina matatizo makubwa ya maji ni Makutupa, Mzase, Kimagai na Mji wa Mpwapwa una tatizo kubwa la maji, naomba msaada kwani Mji wa Mpwapwa unazidi kupanuka na idadi ya watu inazidi kuongezeka. Hivi sasa Mji wa Mpwapwa na vitongoji vyake wapo wakazi zaidi ya 50,000 lakini vyanzo vya maji bado ni vile vile vya zamani. Ipo haja ya kuongeza vyanzo vingine vya maji ili kuongeza huduma ya maji katika Mji wa Mpwapwa na Vitongoji vyake.

Pili, Sekta ya Mifugo ni muhimu sana katika uchumi wetu. Sekta ya mifugo imegawanyika katika idara 3 ambazo ni utafiti wa mifugo, afya ya mifugo, uzalishaji wa mifugo.

Katika idara ya utafiti wa mifugo kuna vituo vya utafiti kama vile Mpwapwa, Kongwa, *Tanga TTRI* na *LRC, West Kilimanjaro* na *ADRI - Temeke,* vinahitaji ukarabati na kupatiwa vitendea kazi vya kutosha ili viweze kuboresha utafiti wa mifugo. Katika vituo hivyo kuna maabara, majengo, mifugo pia kuna wafanyakazi, majengo yanahitaji ukarabati, vituo hivyo vina mifugo inayohitaji madawa ya tiba na kinga hivyo ipo hoja ya kutengewa fedha za kutosha. Pia vituo vina mashamba ambayo yanatakiwa kutunzwa *(Bush Clearing)* kama Kituo cha Utafiti cha Mpwapwa kiongezewe idadi ya mifugo, mifugo iliyopo ni michache sana. Ng'ombe waongezwe kwa ajili ya utafiti.

Kwa kuwa katika idara ya afya ya mifugo wataalam wengi wapo Wilayani na Makao Makuu Dar es Salaam, imebaki kutoa sera tu na idara hii hutengewa fedha nyingi hivyo nashauri fedha nyingi zipelekwe Wilayani

kwa ajili ya kununua madawa ya tiba na kinga ya mifugo. Serikali ipeleke wataalamu wengi zaidi Wilayani ambako ndiko kwenye mifugo badala ya kubaki Makao Makuu ya Wizara/Mkoa.

Kwa kuwa nchi yetu ina mifugo mingi sana ambayo ingesaidia sana kuchangia Pato la Taifa, lakini mifugo hiyo inachangia asilimia 18 tu kwa kuwa mifugo yetu haina afya nzuri kutokana na ufugaji duni. Kwa mfano, Tanzania ina mifugo ng'ombe 17,000,000, mbuzi 12,000,000, kondoo 3.5 milioni. Mifugo yote hiyo *demand* ya madawa ya tiba na kinga ni kubwa ili kuweza kuboresha ufugaji wetu. Katika nchi yetu kuna wataalam wengi wa taasisi, kwa nini wataalam wetu wasifanye utafiti wa madawa haya na kutengenezwa hapa hapa nchini? *Temeke - ADRI* madawa yanayoingizwa mengi yana *side effect* mbaya kwa mifugo yetu, kuna mengine huwa yana *expire* na kutupwa hivyo kuiletea hasara Serikali yetu.

Utafiti wa madawa ya tiba ya kinga ya mifugo utachukua muda mrefu lakini baadaye utasaidia madawa yatatengenezwa hapa hapa nchini na gharama zitapungua. Serikali isitegemee *donnors* tu ndiyo wafanye utafiti kwa mfano *TARP II.*

Serikali ina mpango gani wa kusaidia ukarabati wa majosho Mkoa wa Dodoma ambapo yapo majosho 140, yanayofanya kazi 19, yasiyofanya kazi 121. Vituo vya tiba ya mifugo *(VC)* vipo 52 vinavyofanya kazi 9 vibovu ni 43. Halmashauri ya Wilaya hazina uwezo wa kukarabati majosho na vituo hivyo. Madawa ya kuogesha mifugo ni ghali sana yapunguzwe bei.

Baada ya mchango wangu huo, napenda tena kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri anayofanya yeye, Naibu wake na Wataalam wake, ninaunga mkono hoja hii. Mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, mwaka2002 niliijulisha Wizara juu ya visima ambavyo vilijengwa katika Tarafa ya Manyora, Kata ya Munanila Vijiji vya Munanile, Mukatanga, Kibwigwa na Kata ya Muhinda Kijiji cha Mwayaya. Kata hizi pia zilitandazwa mabomba miaka ya nyuma lakini yote haya yameuzwa na wananchi wanapata tabu kubwa ya kupata maji. Ninaiomba Wizara itusaidie kulishughulikia tatizo hilo.

Pili, katika kitabu cha nyongeza ya hotuba, Wilaya ya Kasulu ina miradi mingi ambayo haijatekelezwa. Mradi wa Nyanga/Kalege/Kasumo ni wa siku nyingi na tunachohitaji ni karibu shilingi milioni 250 ili kutandaza mabomba yanayofaa kutoa maji kwa vijiji hivyo.

Tatu, miradi ambayo haifanyi kazi nchini inahitaji kiasi cha shilingi 43 bilioni. Miradi yote hii, *in my opinion,* inatekelezeka. Tafadhali naomba utoe mpango wa kuitekeleza miradi hii katika mwaka huu .

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Edward Lowassa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Antony Diallo, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri ya kuhakikisha kuwa wananchi wanaondokana na umaskini kwa kuboresha huduma ya mifugo na kuhakikisha wananchi wote wanapata maji safi vijijini na mijini. Naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kwa upande wa sekta ya mifugo. Pamoja na jitihada na kazi nzuri zinazofanywa na Serikali kuhakikisha kuwa sekta ya mifugo inaboreshwa ili kuwaletea wafugaji maendeleo na kuchangia kwenye Pato la Taifa, lakini bado maendeleo ya sekta hii yamekuwa yanategemea zaidi juhudi zinazofanywa na wafugaji na Wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mbarali imekuwa ni kivutio kikubwa kwa wafugaji wa kutoka mikoa mingine. Hadi sasa idadi ya ng'ombe ukiondoa mifugo mingine ni zaidi ya 600,000 na wanazidi kuongezeka, kitu ambacho kimefanya malisho kupungua sana na wafugaji hutembea masafa marefu kutafuta malisho. Hali halisi iliyopo ni kwamba, kumekuwa na migongono mikubwa kati ya wakulima na wafugaji. Uharibifu wa mazingira unaotokana na kuhama hama kwa mifugo. Idadi ya watoto wa wafugaji ambao hawajaenda shule ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi kwa Mheshimiwa Waziri ni kuwa Serikali iwasaidie wananchi wa Mbarali katika zoezi la kutenga maeneo ya ufugaji, kwani zoezi hili linaonekana ni gumu sana, linahitaji gharama kubwa na utaalamu wa kujua maeneo bora ya mifugo, kuiachia Halmashauri pekee imeonekana kuwa uwezo wao ni mdogo kwani Mbarali inajumuisha wafugaji wengi sehemu mbalimbali za wafugaji. Ninapendekeza kuwa ichukuliwe kama eneo la kufanya zoezi la majaribio ili likileta mafanikio iwe mfano kwa Wilaya zingine zenye ukame mkubwa kama Mbarali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na utengaji wa maeneo, Serikali isaidie katika kuongeza idadi ya uchimbaji malambo kwa ajili ya kuvuna maji wakati kuna mvua. Kwani mpaka sasa tuna malambo 2 tu katika Wilaya yote yenye ng'ombe 600,000.

Wataaalamu wa mifugo wanahitajika ili kutoa ushauri wa karibu kwa wafugaji ili kujua ni aina gani ya ng'ombe wanastahili kufugwa. Ninaomba pia utoaji taarifa za kuhusu ufugaji ng'ombe bora na wa biashara na jinsi ya kupata mbegu bora uboreshwe ili uweze kuwafikia wafugaji kwa urahisi, wataalamu wengi wanapotembelea Wilaya zetu huishia kufanya mikutano kwa Watendaji wa Halmashauri tu bila kuwahusisha wafugaji wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa vile vile kuchangia kwa upande wa maji. Pamoja na jitihada nzuri za Mheshimiwa Waziri za kuhakikisha maji safi yanapatikana, bado kuna maeneo mengi ya vijijini maji yamekuwa ni kero kubwa sana. Katika Jimbo langu la Uchaguzi la Mbarali maji ya matumizi ya binadamu na mifugo ni tatizo kubwa sana. Eneo kubwa la wananchi wanatumia maji ya visima virefu vyenye gharama kubwa. Naomba Mheshimiwa Waziri, atusaidie kufanya utafiti wa kuona ni vipi inaweza kutumia vyanzo vya maji kutoka Wilaya jirani ili maji ya bomba yatumike. Kuna mapendekezo ambayo tuliyaleta Wizarani kama ushauri kwa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wakala wa uchimbaji visima virefu wamekuwa wakitumia utalaamu wa uzoefu wa kujua sehemu ya kupata maji. Mbarali mpaka sasa tumechimbiwa visima 4 na pesa zimelipwa lakini maji hayatoki, ningeomba kutoa mapendekezo kuwa waboreshewe utaalamu wa kujua ni wapi maji yanaweza kupatikana badala ya kubahatisha, kitu ambacho kimeleta hasara kwa wachimbaji na wananchi wanaochangia.

**MHE. IDDI M. SIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salamu za kheri na kuunga mkono hoja, ningependa kukupongeza wewe Mheshimiwa Waziri, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri na wataalamu wenu wote, kwa matokeo ya juhudi zenu hasa katika sekta ya maji. Nafahamu kwamba matatizo bado ni mengi na makubwa mno yanayotokana na historia. Malalamiko pia ni mengi lakini katika kipindi kifupi cha uongozi wenu mmeonyesha mambo yanayotoa matumaini. Mnastahili kupewa moyo tufike kwa kazi kubwa zaidi. Watu wa Ilala wanawasalimu.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza Wizara hii ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo, kwa hotuba nzuri, yenye ufafanuzi. Nawapongeza watendaji chini ya Uongozi wa Katibu Mkuu wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kaka yangu Bakari A. Mahiza.

Pili, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia masuala machache. Suala la maji kama tunavyojua maji ni uhai. Naipongeza Serikali kwa kujitahidi kuhakikisha angalau kuna miradi ya maendeleo ya maji kama majedwali yanavyoonekana Jedwali la 3 (a) na jedwali la 3 (b).

Lakini swali, ukiangalia mwaka 2002/2003, Mkoa wa Tanga Wilaya zake 6 ulipewa fedha mwaka 2002/2003 Mkoa wa Tanga Wilaya zilizopatiwa fedha zimepungua achilia mbali ukweli kwamba Wilaya mpya ya Kilindi imezaliwa. Ni kusema kwamba Wilaya za Tanga imejitosheleza kwa maji kiasi kwamba hiyo miradi haijaendelea?

Pili, Wilaya ya Handeni imetengewa fedha 7.5 milioni, ingawa kuna shida kubwa ya maji, je, Wilaya ya Kilindi mmeiunganisha katika mgao huu wa Handeni na huku fedha ikawa ndogo kulingana na 2002/2003? Kwa nini Kilindi haimo? Kama imeunganishwa kwa nini, ukizingatia Wilaya ya Kilindi ni Wilaya mpya katika Wilaya yenye matatizo ya maji ni mojawapo na hata katika orodha ya miradi ya maji vijijini isiyofanya kazi Kilindi

ina miradi 8 haifanyi kazi na wananchi hawawezi kuchangia/kufufua? Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze atatusaidije Handeni/Kilindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo niishie hapa. Nakushukuru nategemea majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kwa faida ya wananchi wa Handeni na Kilindi. Nawatakia kila la kheri.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Antony Diallo na timu nzima ya Wizara, kwa kazi nzuri kwenye hii Sekta ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na hotuba nzuri ya Bajeti yenye matumaini na dira yenye mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo: Umuhimu wa maji kwa maisha ya binadamu, viumbe hai na maendeleo ya jamii kwa jumla, unafahamika. Bila maji, hamna uhai! Hii ndiyo sababu maji ni sehemu muhimu ya mpango wa kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupongeza Serikali kuyapa maji kipaumbele kwenye programu ya kuondoa umaskini hiki kipaumbele hakijionyeshi kwenye Bajeti na hasa Bajeti ya fedha za ndani. Je, ni lini Serikali itatambua umuhimu wa kuongeza Bajeti ya maji ili kupunguza utegemezi wa fedha za nje? Napendekeza Serikali iwe na *deliberate budgetary allocation policy* kwa ajili ya maendeleo ya Sekta ya Maji. Kwa mfano, uwiano kati ya fedha za ndani na fedha na nje uwe kama ifuatavyo: *Current ratio* 40:60 (2004/2005), 50:50 (2005/2006), 55:45 (2006/2007), 60:40 (2007/2008) *and so on until we reach at least 80:20* (2014/2015) *at which we should have met all the key development targets for water.*

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya *utilities* (maji, umeme) kwenye uzalishaji wa viwanda ni mkubwa wenye viwanda wanalalamika. Viwanda vyetu siyo *competitive* kwa sababu mojawapo kwamba, gharama za uzalishaji ni kubwa kulinganisha na washindani kwenye soko la ndani na nje. Mara nyingi tumekuwa tukilalamikia gharama za umeme na kusahau gharama za maji. Maji yanaleta gharama kwa aina mbili. Matumizi na ukosefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Wizara ina *role* gani kuhakikisha gharama za uzalishaji zitokanazo na maji zinadhibitiwa kuhakikisha haziathiri uzalishaji na *competitiveness* ya viwanda vyetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Kijiji cha Samaria ulibuniwa 1992. Wizara ilitengenezwa *project document* ikapotea Wizarani. Mkoani Arusha tuliomba Wizara itutengenezee *project docoment* nyingine ili Wizara iwe na kigezo cha kusaidia mradi huo. Hiyo ilikuwa 2001. Awali, mradi wa *Adventist Relief Agency (ADRA)* ulidhaniwa ungelifadhili huo mradi wa Kijiji cha Samaria. Mpaka sasa wananchi wa Samaria, Kata ya Maroroni, Arumeru Mashariki, wanasubiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Wizara itoe tamko kwa wananchi wa Kijiji wa Samaria Kata ya Maroroni, Arumeru, kuhusu *status* ya ombi lao la kupatiwa maji. Je, wasubiri mpaka lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba Wizara ione umuhimu wa kushawishi wafugaji wakubwa wapunguze mifugo maana mifugo inaharibu vyanzo vya maji kwa kiwango kikubwa sana na pia kuharibu mazingira na hii ni hatari kwa siku zijazo.

Pili, pamoja na juhudi za Serikali kuanza kuujali Mji wa Namanyare, ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Nkasi, kuupatia maji hata hivyo, naiomba Serikali ichimbe lambo katika Mto Nairobi pale pale Namanyere ili litunze maji kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Wizara kwa kutupatia Shilingi 1,000,000/= kwa msimu uliopita ili kisima kimoja kichimbwe pale Namanyere. Kwa kuwa hakijachimbwa na tanki kubwa la kupandisha maji linajengwa bali hatuna *pump* yenye uwezo wa kupandisha maji juu ya tamko hilo. Basi naiomba Wizara ikubali ombi la Halmashauri ya Nkasi, fedha hiyo inunue *pump* badala ya kisima kimoja.

*Pump* hiyo itasaidia sana kusambaza maji eneo kubwa la Namanyere ikiwa ni pamoja na lile ambalo kisima kingechimbwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Lowassa, kwa hotuba yake nzuri na yenye uchambuzi wa kina ambayo imetolewa leo asubuhi.

Jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuhakikisha kwamba vijiji mbalimbali vinapata huduma muhimu za maji zinaridhisha na kwa kweli zinastahili pongezi. Ipo haja kwa maoni yangu ya kutoa elimu zaidi kwa wananchi kuhusu suala zima la wananchi kuchangia huduma ya maji ili watu wengi zaidi waweze kupata huduma hii muhimu na pia miradi ya maji iweze kuwa endelevu. Elimu hii ni muhimu pia kwa viongozi kwa sababu kama wao wenyewe hawalielewi vizuri suala la uchangiaji wa huduma ya maji miradi mingi itakufa.

Kipekee napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Serikali ya Ujerumani kupitia Benki ya Wananchi ya Ujerumani *(KfW)* na kushirikiana na Serikali ya Tanzania, kwa kazi nzuri ambayo imefanywa katika Wilaya ya Hai. Kwa jitihada hizi miradi ya Losaa Kia, Uroki Bomang'ombe, Magadini Makiwaru na Lawate Fute imeweza kukamilika. Nawashukuru wananchi wote wa Wilaya ya Hai na kipekee wale wa Jimbo la Siha, kwa kutambua umuhimu wa mradi huo na hivyo kujitolea katika kuchimba mitaro, kusomba mabomba na kuyalaza katika mitaro na kadhalika. Naahidi kwamba, tutaendelea kushirikiana na *KfW,* pamoja na *Project Manager* wake Mr. Michael Braasch, pamoja na Serikali kwa ujumla, ili watu wengi zaidi waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba kuwasilisha tena kilio cha wananchi wa Jimbo langu la Siha la kupatiwa majosho hasa katika maeneo ya wafugaji kama vile Donyomoruak, Ngumbaru, Olkolili, Olmelili, Makiwaru, Ngaritati, Naibilie, Karansi, Kandasini, Magadini, Lekrimuni, Ndinyika na kadhalika. Jambo hili nimelizungumza mara kwa mara kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa hiyo, kwa kweli ninachofanya hapa ni kukumbushia tu.

Mheshimwia Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa hotuba yake nzuri, ambayo imejaa ufafanuzi wa kina, yeye na watalaam wake wanajituma sana.

Kuhusu mifugo inafahamika kuwa Tanzania ni nchi ya pili katika Bara la Afrika kwa kuwa na ng'ombe wengi. Tatizo ni kuwa bado Taifa halifaidi katika Pato la Taifa kutokana na mifugo hiyo kwa vile wafugaji hawana haja ya kuuza mifugo yao. Kwa upande wa Serikali hakuna juhudi iliyofanyika kwa miaka mingi ili kuboresha ng'ombe wa asili kwa kupandisha kwa mbegu bora ili kupata chotara wanaoweza kutoa nyama zaidi. Nchi kama Botwana na Swaziland wamefanikiwa sana katika mpango huu.

Kuhusu ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, ninaipongeza Wizara kwa kuleta nchini madume ya kisasa kutoka Afrika ya Kusini. Ninashauri kuwepo na utambuzi wa wafugaji wa maeneo ambayo mbegu ya madume hao itapelekwa.

Kuhusu Jimbo langu kuna shida kubwa sana ya maji katika Kijiji cha Laela na Kijiji cha Ikozi, ambavyo tayari nilikwisha mwandikia Mheshimiwa Waziri. Napenda kushukuru kuwa, tayari wataalamu wa Wizarani na Mkoani wamefika katika vijiji hivyo. Ili kuonyesha nia yetu ya kutaka tupate maji na kwa vile lazima vijiji vyenyewe kuwa na mifuko ya maji. Tarehe 9 Julai, 2003 na tarehe 10 Julai, 2003 niliongoza harambee ya kuchangia maji katika vijiji hivyo. Katika Kijiji cha Ikozi viongozi walichangia shilingi milioni 16 na Kijiji cha Laela walichangia shilingi milioni 14. Ninakusudia kumwandikia Waziri, taarifa kamili. Kutokana na juhudi iliyoonyeshwa na wananchi wa vijiji hivyo naomba Serikali ituunge mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, niliomba kuchangia kwa kuzungumza lakini inaonekana jicho lako halijatambua jina langu. Imenibidi nichangie kwa maandishi hoja moja tu ambayo naona ni muhimu sana kwa maisha ya wananchi wa Wilaya ya Kyela.

Kwanza, ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Edward Lowassa, kwa hotuba yake nzuri sana. Pongezi hizi vile vile ziende kwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara hii.

Pili, ningependa kumshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa ziara yake aliyoifanya katika Wilaya yangu mwishoni mwa mwaka 2002. Mheshimwia Waziri, alijionea yeye mwenyewe jinsi gani wananchi wa Kyela wanavyopata matatizo ya maji katika mradi wao wa Maji wa *Kanga Ground.*

Mradi huu ulijengwa kwa madhumuni ya kupeleka maji katika Mji wa Kyela miaka 40 iliyopita. Wakati huo Mji wa Kyela ulikuwa na wakazi 1,500. Leo Mji wa Kyela una wakazi zaidi ya 30,000. Maji ni haba sana, wakazi wa Mji wa Kyela wanakunywa maji machafu sana kutoka kwenye visima wanavyochimba kienyeji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali ni kukarabati au kupanua Mradi wa Kanga ili mradi huu siyo tu upeleke maji Mjini Kyela, bali pia usambaze maji katika vijiji 25 vilivyoko kandokando ya bomba kutoka kwenye chanzo cha maji hadi Mjini Kyela. Kata zitakazofaidi mradi huu ni Kata za Ipinda, Ipande, Ikama, Mwaya, Kyela na Kajunjumele. Ninaishukuru Serikali kwa maana ya Mheshimiwa Waziri, kuwa *very positive* kwa suala hili. Nimechangia ili kuikumbusha Serikali na kuweka kumbukumbu kwa marejeo hapo baadaye.

Mwisho katika hotuba ya Waziri, ukurasa 118 kiambatanisho Na. 10, ni kweli kuwa jumla ya majosho Wilayani Kyela ni 12. Yote haya hayafanyi kazi. Siyo kweli kwamba majosho 3 yanafanya kazi. Ninaomba takwimu hizi zisahihishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. LAWRENCE M. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakuomba upokee pongezi kutoka kwangu kwa jinsi hotuba yako ilivyoandaliwa kisayansi. Viambatisho kuna katalogi ya madume, imekuwa elimu mpya kwa upande wangu. Hongera sana. Nimefurahi kuona kwamba kwa kushirikiana na Serikali ya Kijerumani kupitia *KfW* imekamilisha uchunguzi na usanifu wa miradi ya maji safi na maji taka kwa Mji wa Songea. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara itaanza kazi ya ukarabati na upanuzi wa mfumo wa maji saji Mjini Songea kwa gharama ya *Euro* milioni 6.38. Kwa msingi huo naunga mkono hotuba yake kwa asilimia mia moja.

Kero kubwa na nzito inayowakabili wanaoishi kando kando ya mito ambayo imetajwa ndiyo chanzo cha maji na wameambiwa wasikae ndani ya mita 100 kutoka kwenye mito hiyo. Wananchi hao wamekuwa wakitegemea maeneo hayo. Wameishi kwa kutegemea maeneo hayo kwa muda wa miaka mingi. Kama chanzo cha maji kitaendelea kuwepo maeneo yaliyopendekezwa, wananchi wameomba kufidiwa na Serikali yao kabla ya Agosti, 2003 ili wajiandae kutafuta maeneo mengine. Hatua za awali za kujua gharama ya zoezi hili zimefanywa. Wananchi kwa unyonge wanangojea malipo haraka iwezekanavyo. Kazi kwako Mheshimiwa Waziri, kwa kulitatua tatizo hilo kama litaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayofanya ingawa ni katika hali ngumu ya ufinyu wa Bajeti Wizara inayopewa. Pia, nawapongeza kwa kuandaa hotuba nzuri na inayoeleweka. Kwa upande wa ufinyu wa Bajeti, makubaliano na ushauri wa Kamati kuwa uanzishwe Mfuko wa Maji Kitaifa ambao utaongeza nguvu za Wananchi katika miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nchi yetu ina matatizo makubwa ya maji kiasi kwamba, bado Wananchi wengi wanaendelea kupata maji umbali wa zaidi ya kilometa kumi na wakati mwingine wananchi wanadhurika kwa kushambuliwa na wanyama wakali kama simba na kadhalika katika harakazi hizo za kutafuta maji, kwa mfano, katika Kijiji cha Mtiniko Wilaya ya Mtwara Vijijini nilipata taarifa hiyo kutoka kwa akina mama ambao

walilalamika kuhusu uhaba wa maji katika kata nzima ya Mtiniko. Nilielezwa haya katika ziara niliyoifanya katika Mkoa wa Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji liko pia katika Wilaya ya Masasi kwa vile chanzo kikuu cha maji ambacho kilkuwa Bwawa la Mchema limekauka. Vyanzo vingine vilivyopo ni Mto Magumuchila na Ndanda, lakini inahitajika pump (mashine) kubwa ya kusukuma maji ili yaweze kusambazwa kwa urahisi katika maeneo ya Mjini Masasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuwa teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua ienezwe nchini kwa vile mvua huwa inanyesha katika maeneo mengi ya nchi yetu wakati wa msimu wa mvua hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuandika haya, naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMED ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani kubwa kwa Waziri wa Maji, kwa kutupatia Mji wa Lindi fedha Sh.339,000,000/= kwa mradi wa dharura. Naomba sana Waziri apokee shukrani za Wananchi wa Lindi. Kwa taarifa yake ni kwamba, visima vipya vilivyochimbwa eneo la Kitunda vimetoa maji mengi hivyo, tunaomba fedha za kutosha ili maji hayo yafikishwe Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Lindi ni Mji wenye matatizo makubwa ya maji kuliko Mji wowote ambao ni Makao Makuu ya Mkoa. Lakini kwa nini Mji wa Lindi haupati fedha za Wafadhili kama ilivyo Mikoa mingine? Hivi hawa Wahisani kama *BADEA, ADB, World Band, UNDP, GTZ, KfW* hawaitaki Lindi? Hata Mradi wa *USRP* umeelekezwa katika Miji ile ile ambayo Wananchi wake hawana tatizo kubwa la maji isipokuwa ni kuangalia hali itakavyokuwa kwa mahitaji ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni haki hii wakati Lindi leo hii hatuna maji, fedha za mkopo zinaelekezwa kuangalia mahitaji ya baadaye! Naomba maelezo ya Mheshimiwa Waziri, kuhusu hoja zote mbili za fedha za wahisani kutoletwa Lindi na umuhimu wa Mpango wa *USRP* kwa miji ile ambayo haina maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isiache Wananchi wa Kineng'ene ambao wanasubiri Mradi wa *JICA*, fedha wamechanga hatujui *JICA* watafika lini na Wananchi wanaendelea kuteseka sana. Naomba Wizara itupatie fedha ili tuchimbe angalau visima 3 vya dharura kwa Wananchi hao wanaotaabika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, anipe majibu na mwisho namwalika atembelee Lindi mwaka huu.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ambayo imegusa nyanja zote za Wizara yake na imeweka tathmini za kutosha. Nampa hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kufanya ziara Wilayani Babati na kuona matatizo ya maji Mjini Babati na Magugu mwishoni mwa mwaka 2002. Tulikubali ushauri wake na kuutekeleza.

Pia, nampongeza kwa kusikiliza ushauri wangu kuhusu matatizo ya maji hasa katika kukarabati njia ya maji ya mradi wa Magugu (kutoka Karakuta - Visima vitatu). Nawashukuru kwa kuweka mradi huu kwenye Bajeti ya 2003/2004, kifungu 54 na 56 katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 43 - 45. Kwa ujumla matatizo ya mradi huu unachukua 60% - 70% ya kero ya Jimbo la Babati Mashariki. Hivyo, ukarabati wa mradi huu kwa kiwango kikubwa, utaweza kurudisha imani ya Wananchi kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuwa awamu ya sasa ilenge kufikisha maji Kijiji cha Mwada, Kitongoji cha Ngoley kutoka Magugu na kuimarisha chanzo cha maji. Naomba wataalam watakapoanza wapate na ushauri wetu. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Waziri kuwa Wananchi watakuwa tayari kwa hali na mali endapo ukarabati utazingatia Shirikishi *(Participatory).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maji - Minjingu, Mheshimiwa Waziri, atakumbuka kuwa niliwahi kueleza tatizo la Kijiji cha Minjingu kuwa hawana chanzo cha maji ya uhakika na sasa tatizo litakuwa kubwa baada ya *Minjingu Phosphate Company* kufilisiwa kwa sababu Kijiji kilikuwa kinategemea *borehole* ya Kampuni hiyo.

Kwa mara nyingine nashauri kuwa utafiti ufanywe na kama upo tayari kwa ushauri wa wakati ule, basi ni muhimu Wizara itueleze ili tuanze mikakati ya kuhamasisha Wananchi kuchangia fedha kwa hali na mali.

Pia, katika ziara yangu ya Kijiji cha Minjingu, Wananchi waliniomba hadharani kuwa wangependa sana kutembelewa na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa. Kwa mchango huu, naomba kuwasilisha ombi la Wananchi wa Kijiji cha Minjingu kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maji Mjini Babati, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa ushauri wake wakati alipotembelea Babati kuhusu upanuzi wa shughuli za maji Mjini Babati. Kwa kuwa sasa Babati ni Makao Makuu ya Mkoa, Wizara inahitaji kuweka mikakati mipya ya upatikanaji wa maji Mjini Babati hasa visima virefu. Pamoja na hayo, tunasubiri kauli ya Mheshimiwa Waziri, kuhusu uanzishwaji rasmi wa Bodi ya Maji Mjini Babati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara kwa kusaidia uchimbaji wa malambo katika maeneo ya wafugaji ya Gedmar, Mamire na Minjingu. Naomba Wizara sasa iangalie maeneo zaidi ya Tarafa ya Mbugwe katika Vijiji vya Vilima vitatu, Mwada na Sarame.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, namshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa juhudi zao katika kuendeleza sekta hii muhimu ya maji na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu nichangie hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wao wote, kwa kuandaa hotuba hii kwa wakati muafaka. Napongeza jitihada zinaazofanyika za kuwapatia Wananchi maji safi na salama, lakini lazima nionyeshe masikitiko yangu kuwa Wizara hii inaangalia zaidi maeneo yenye mifugo mingi kuliko maeneo yasiyo na mifugo hususan Mkoa wa Ruvuma hasa Wilaya ya Mbinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wanaonyesha kusahau Wilaya ya Mbinga hasa katika Sekta ya Maji kwa sababu hawatembelei sehemu hizo. Wangepata nafasi ya kutembelea wangekuwa na picha sahihi kuhusu hali ya Wilayani Mbinga na tatizo la maji. Karibu Wilaya yote ya Mbinga inaweza kupata maji kwa kutumia *gravity*. Kwa hiyo, tunachohitaji ni Mheshimiwa Waziri, kutembelea aone tunachofanya ili atusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama watu wa Kusini mwa Tanzania hatuna jadi ya uchungaji mifugo, sisi tunaweza kuwa wafugaji wazuri, kwa hiyo, tuleteeni madume bora ambayo yameonyeshwa kwenye katalogi, yasiendelee kubaki kwenye picha!

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Maofisa wa Mifugo kuwa Madaktari wa Wanyama, nashauri utaratibu huo uangaliwe upya ili suala la kusomesha *Animal Breeders* liwe linatiliwa mkazo kwa sababu kama tunazalisha mifugo wenye afya basi gharama za kutibu zitapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa imani kwamba, Wizara hii na hasa Mheshimiwa Waziri au Naibu wake, watatembelea Wilaya ya Mbinga.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Barabara unachangiwa na watumiaji wa barabara, nani achangie wa maji? Naona ni bora kuwa na miradi maalum hata kwa kukopa, *targeted.*

Mfano huo wa *World Bank* uliotangaza katika *paragraph* ya 58, ule wa Elimu ya Juu ni *pathetic.* Hauna wachangiaji ni Serikali tu!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi napenda niungane na wachangiaji waliochangia katika bajeti ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kuwashukuru kwa kiwango kikubwa kwa yote ambayo wameyazungumza na nina hakika yatatusaidia sana kama Wizara kurekebisha makosa yetu na kuweza kujiweka katika hali ya kuridhisha katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyoona wachangiaji walikuwa wengi. Kwa hiyo tutajaribu tutakavyoweza kwa sababu ya kubanwa na muda kutoa majibu kwa kila mchangiaji kwa hoja ambazo amezitoa. Lakini ikiwa hatutaweza kuwamaliza wachangiaji wote tutajaribu kutoa majibu kwa maandishi kwa hoja mbalimbali tulizozipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi napenda niunge mkono hoja hii iliyo mbele yetu, na kusema kwamba bajeti nzuri na Wizara imejitahidi sana kujibu matatizo mengi tuliyonayo. Lakini kama mnavyofahamu na kama walivyosema wasemaji wengi tatizo letu kubwa ni fedha na siyo katika sekta moja tu fedha zinaathiri miradi na mipango mingi ya Wizara. Lakini ni vizuri pia kukumbushana kwamba hapa tulipofika tumefika pazuri kutokana na kuboreka kwa hali ya uchumi. La sivyo utaona kwamba maeneo mengi tunayoshughulikia na Waheshimiwa Wabunge wanayoyazungumza wengi wetu tuliyakuta yapo matatizo hayo. Ukiangalia kwamba kulikuwa na miradi ya miaka ya 70 kule. Lakini tunajitahidi sana hata kuoanisha hii miradi na kuifahamu kama tulivyoitoa kwenye orodha ni kazi ambayo haikuwa rahisi kulingana na hali ilivyo.

Kwa hiyo, tunawaomba sana Waheshimiwa Wabunge lile jedwali la nyongeza mliangalie vizuri kama tumesahau mradi wowote kwenye hiyo orodha na ni mradi ambao mnajua ulianzishwa kama mradi wa Taifa mtukumbushe. Kwa sababu inawezekana uongozi wa Wilaya au uongozi ambao tuliufuata kwa ajili ya kutupatia taarifa hakutupatia taarifa sahihi. Kwa hiyo tunawaomba sana msaada wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kwa kumshukuru kwa dhati mchangiaji wa kwanza Mheshimiwa Eliachim Simpasa ambaye ametusaidia sana kujaribu kuonyosha mahali ambapo tulikuwa tumepata matatizo ya tufanyeje na Kamati yake nzima imetusaidia sana kutatua matatizo mengi ya kuweka sawa bajeti ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nitaomba niende haraka haraka. Mheshimiwa Eliachim Simpasa ameomba kupanua wigo wa vyanzo vya maji kama wasemaji wengi walivyochangia hasa kwa hawa waliochangia katika kipindi hiki cha jioni. Ni kweli hali ya maji nchini inazidi kupungua na hiyo inatokana na matatizo mengi. Kwanza tumefyeka misitu katika maeneo mengi. Pili tumebadilisha maeneo mengi kuwa ya kilimo. Mnafahamu sehemu zote ambazo kwa mfano tunalima mpunga sasa hivi zilikuwa ni njia za maji ambazo sasa hivi zimekuwa *blocked.* Kwa hiyo *stream* ya maji kwenda kwenye maeneo yanayokohitaji inakuwa na upungufu wa hali juu sana. Kwa hiyo nina hakika kwamba kampeni ambayo imeanzishwa sasa hivi na Wizara ya Maliasili na Utalii itaweza kujaribu kuboresha hali ya misitu na ni jukumu la kila Mtanzania. Kwa sababu siyo kwa Tanzania tu.

Kwa hiyo, hali ya kupungua kwa maji duniani kama ilivyotolewa kwenye hotuba ya Mheshimwia Waziri. Tatizo la kupungua kwa maji duniani ni kwa karibu nchi zote na sisi Tanzania mnaweza kuona kwamba tuko katika hali nzuri zaidi kuliko nchi nyingine yoyote katika Afrika. Kwa hiyo, tusichukue hiyo hali kwamba ndiyo *guarantee* ya sisi kuendelea kuharibu vyanzo vya maji na kuchafua vyanzo vyetu vya maji. Kwa hiyo, ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani, Halmashauri zetu na wananchi wa ujumla tulielewa hilo kama ni tatizo. Njia mojawapo ambayo Wizara tumeanza kuichukua ni kujaribu kupunguza upotevu wa maji. Kwa sababu mahali ambapo upotevu wa maji unazidi kwa kiasi cha asilimia 50 una uhakika kwamba ukipunguza kwa asilimia 25 ina maana umeongeza *supply* kwenye maeneo yale kwa kiwango hicho hicho badala ya kutafuta vyanzo vingine vya maji. Kwa hiyo, maeneo mengi sana ambayo yamezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge tutajaribu kusaidiana kwa pamoja na Serikali na wananchi kwa ujumla kujaribu kuyatatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limezungumziwa ni kukosekana kwa Bodi zinazohusu kuendeleza ubora na kulinda maslahi ya mifugo. Lakini lazima tuelewe kwamba Bodi hapo awali zilikuwepo. Kulikuwa na Bodi za Maziwa, kulikuwepo na Bodi ya nyama na kadhalika. Lakini Bodi hizo kwa sababu ya utendaji na kuwepo matatizo ya kiuchumi zilipungua nguvu zake au utendaji kazi wake na ikafikia hatua zikaonekana kama ziliishakufa. Sasa hivi Wizara inafanya bidii kurudisha Bodi hizo zifanye kazi inayohitajika. Moja ni Bodi ya Maziwa na pia kama mnavyoelewa juzi juzi tumepitisha Sheria hapa ambayo inaunganisha Bodi ya Madawa na Madawa ambayo yanahusu binadamu na madawa yanayohusu mifugo na pia vyakula vitakavyotokana na mifugo na kadhalika. Kwa hiyo ni njia mojawapo ambayo Serikali inajaribu kuchukua ili kurudisha ubora na matumizi sahihi ya mifugo na mazao yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nitajaribu kuligusia ni lile ambalo Msemaji wa Kambi ya Upinzani amelizungumzia. Kwanza napenda nimshukuru kwa kuisifia Bajeti ya Wizara na nimesikiliza mara nyingi sana *comment* za upande *opposition* mara kwa mara zina *criticize* tu. Lakini kwa bahati nzuri huyu

Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha ametufurahisha sana kwa kuunga mkono mahali ambapo Serikali inafanya vizuri na kutupa ushauri tunakubali kwamba tunaweza tukasaidiana pamoja ili kutatua tatizo. Kwa mfano, elimu kwa wafugaji sasa hivi tumewaweka wote kwenye programu zetu za kuwafundisha kuhusu maeneo mbalimbali, maeneo ya uzalishaji nyasi, maeneo ya ufugaji bora na kama mlivyoona sasa hivi Serikali imeanzisha Mfuko wa kuendeleza mifugo ambapo kitu kikubwa kitakacholengwa kwenye eneo hilo ni uboreshaji wa mazao yanayotokana na mifugo kama ngozi na kadhalika. Kwa hiyo, mafunzo kwa ajili ya wafugaji tutayaendeleza kulingana na hali ya bajeti inavyoturuhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Major Jesse Makundi nitaomba maswali yake au hoja yake Mheshimiwa Waziri atajaribu kuijibu.

Mheshimiwa Peter Kabisa, maji katika eneo lake hayafiki. Naomba Mheshimiwa Peter Kabisa uwe na subira kwa sababu ni juzijuzi tu City Water Services tumewakabidhi. Kwa hiyo, nina hakika huyu operator atajaribu kutatua matatizo mengi ambayo yalikuwa yanalisumbua Jiji la Dar es Salaam. Na hii inatokana na kwamba *World Bank* wanatoa Fund sasa hivi kwa ajili ya kuendeleza na kurekebisha miundombinu ya maji katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Peter Kabisa awe na subira.

Mheshimiwa Elisa Mollel tunapenda tupokee shukrani na pongezi ambazo umezitoa. Uhaba wa maji kama ulivyoomba Mfuko wa Maji ni wazo nzuri na tayari Wizara tumeishaanza kujadiliana ili kuona utaratibu gani utakaowezesha tuwe na Mfuko wa Maji. Lakini lazima tuelewe kwamba hatuwezi tukafika mahali tukawa na mfuko kwa kila kitu. Kwa hiyo tutaangalia mawazo ya Waheshimiwa Wabunge ili tuone uwezekano upi unaofaa na *source* ipi tutakayoitumia na kadhalika. Nina hakika kwamba Waheshimiwa Wabunge hasa Wabunge wa Sekta inayotusimamia watakuwa muda mwingi tu wa kuweza kutushauri ili tupate ufumbuzi na tuweze kufikia mahali pazuri.

Mheshimiwa Paul Kimiti Mfuko wa Maji utaleta hoja binafsi. Nadhani kama nilivyoeleza tutashukuru kama utatupa mawazo kwanza kabla ya kutu-*surprise* na hoja binafsi ili tuone na tuangalie hoja binafsi yako hiyo tutaiboreshaje. Kwa sababu hii ni wakati wa ushirikiano katika utawala. Kwa hiyo, nina uhakika kwamba utafanya hivyo na tutajaribu kusaidiana. Wazo lake la kusema Wizara ya Maji iwe pekee, nina hakika Mheshimiwa Rais alipokuwa anaiunganisha na Mifugo alikuwa na sababu za msingi, na nina hakika pia kwamba upande mwingine lazima tukumbuke kwamba katika Bunge lililopita tulikuwa tunaomba kupunguza idadi ya Wizara. Kitu ambacho inawezekana ndiyo sababu iliyomfanya Mheshimiwa Rais kuanzisha Wizara hii kwa kuona umuhimu wake kwa jamii na kwa Watanzania.

Halafu nakubali kwamba tunapoteza maji mengi sana uncounted for water kama nilivyoeleza tunajaribu kutafuta mbinu za aina mbalimbali ili kupunguza upotevu wa maji usio na maelezo au usio na umuhimu, na hivyo tunafikiria njia mbalimbali. Njia mojawapo huenda tukaanza kuwa tunapiga faini kwa mtu anayepoteza maji. Hiyo itasaidia watu waone kwamba kupoteza maji siyo kitu cha kutojali kwa sababu unapopoteza maji ina maana una misuse capital ambayo imetumika. Kwa hiyo, hilo tunakushukuru sana umetukumbusha na tunajaribu kuendelea kulijadili ndani ya Wizara. Kuhusu maji Sumbawanga Mjini namuachia Mheshimiwa Waziri atalijibu.

Mheshimiwa Abdillahi Namkulala kuhusu Mfuko wa Maji nakubaliana naye. Ziwa la Chibwalabwata tutapeleka watalaam, nina hakika tutawaelekeza wataalam wetu waende wakaangalie. Fedha za malambo kama tulivyoeleza tumepeleka fedha nyingi sana katika maeneo ya mifugo ambapo malambo mara kwa mara ni mazuri sana kwa mifugo yetu badala ya maji ya bomba. Kwa hiyo, kama ombi la kutoka kwenye Wilaya ya Mtwara Vijijini tutalipata nina hakika tutaangalia uwezekano wa kusaidia.

Mheshimiwa George Mlawa, tunashukuru kwa hongera zako. Mradi wa Nyamlenge tutajaribu kupeleka watalaam wetu ili waangalie badala ya ule Mradi wa zamani wa Mtitu ambao ulikuwa una *serve* vijiji 36. Kuhusu Vyama vya Msingi vya Ufugaji. Sasa hivi Vyama vya Msingi vya Ufugaji vimeanza kuhamasishwa. Juzi juzi nilikuwa katika Wilaya ya Rombo. Mpakani mwa Tanzania na Kenya kuna wafugaji ambao wamejiunga pamoja na walikabidhiwa na Wilaya ya Rombo kuendesha josho na lile josho ni nzuri kweli. Kwa hiyo, tunawaomba wananchi katika maeneo mengine kuunda Vyama Hiari vya Wafugaji kwa sababu Vyama vya Hiari vya Wafugaji havihitaji msukumo wa aina nyingine yoyote kama wenye jambo lao wanalifahamu. Nina hakika kwamba tuna Maofisa wengi katika Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kadhalika ambao wanahamasisha nina hakika tunakokwenda tutakuwa katika hali nzuri.

Mheshimiwa Hamisi Nguli tunakushukuru kwa pongezi. Matatizo ya Singida yanaeleweka. Lakini tumekueleza *BADEA* wanaleta fedha, nina hakika baada ya kutatua matatizo ya katikati ya Mji, tutaangalia uwezekano wa kusaidia peril urban kwa sababu kuna mradi bado wa *World Bank* ambao utaendelea kuwepo kwa kipindi kirefu kijacho. Mipango ya vijiji vilivyo kando kando kama nilivyoeleza tutajaribu kuviingiza kwenye programu nyingine. Kwa hiyo, *Alternative ways transport ya Animals.* Mimi nadhani Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mkuu wa Mkoa wa Singida amefanya kitu kizuri sana hivi majuzi kwa kuwaandikia Wakuu wa Mikoa jirani ambao walikuwa hawatekelezi agizo au Waraka namba moja wa Mheshimiwa Rais. Kwa sababu si kweli kwamba magari hayatoshi na si kweli kwamba treni hazitoshi. Lakini ni kweli pia kama alivyosema Mheshimiwa Njelu Kasaka upungufu wa maji nchini umeanza kuanza kuonekana. Sasa njia mojawapo inayosababisha upungufu wa maji ni uharibifu wa mazingira.

Sasa mimi nilitegemea kwamba Mheshimiwa Hamisi Nguli atatuunga mkono na kuhamasisha kwamba hao wafanyabiashara watatumia taratibu ambazo zimeelekezwa kwenye Waraka namba moja. Hivyo hivyo hii ya kuzuia usafirishaji wa mifugo inasaidia pia kuzuia watu ku-move ovyo. Kwa sababu sasa hivi afikirie kama mtu ana ng'ombe 2,000 alitaka kuhamia Morogoro ina maana ataajiri au atakodi magari karibu 50 kupeleka ng'ombe wake 2,000. Sasa kama yeye hatataka ku-*benefit* kutokana na mifugo yake basi acha *transporter* na wengine walioajiriwa kwenye *transport* sekta wapate hicho kipato. Kwa hiyo, hii ina *discourage* kwa njia moja au nyingine kuswaga mifugo, wanarandaranda nchi nzima hii itasaidia sana kupunguza hilo na wakati huo huo inatusaidia kulinda mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Paschal Degera pongezi kwa *RWCC* nakubali tunakushukuru sana. Mradi wa Ntomoko, bwawa la Mwisanga. Kwa bahati mbaya sana Mheshimiwa Paschal Degera tulipowapelekea Mradi wa *Rural Water and Sanitation Programme,* tulitarajia kwamba Wilaya ya Kondoa wataweka huo mradi katika maeneo mengi ambayo hayakukamilishwa ili yafaidike na fedha hizo za *World Bank.*

Lakini kwa bahati mbaya walichagua vijiji 10 na wakachagua Mji mdogo wa Kondoa kunufaika na mradi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Paschal Degera tusaidiane ili kuangalia uwezekano wa kupata mradi mwingine. Lakini hata hivyo rehabilitation ya mradi wa Ntomoko itaunganishwa na kuweka chujio la bwawa hili la Mwisanga, kwa sababu maji ya bwawa la Mwisanga ukiyatumia hivi hivi kwa kweli siyo mazuri kwa afya ya binadamu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Paschal Degera akubali maelezo, na ni kwa nini tuliacha kuonyesha baada ya miaka ya huko nyuma kuonyeshwa. Lakini lazima Mheshimiwa Paschal Degera akumbuke kwamba miradi mingi ya huko nyuma kabla mwaka 2000 ilikuwa inawekwa kwenye programu za Serikali lakini inakosa fedha. Kwa hiyo, huu mradi ulikuwa ni victim kati ya miradi ambayo ilikuwa inaachwa kwa sababu ya kukosa fedha, inakuwepo kwenye Bajeti lakini kunakuwa hakuna fedha za kutoka Hazina. Kwa hiyo, hiyo nina hakika inaweza kuwa ndiyo sababu iliyosababisha huko nyuma mradi huu usionekane.

Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo namshukuru sana kwa maelezo yake, mengi ambayo yameelezwa ya Wizara kwa nini isianzishe *Basket Funding.* Lakini *Basket Funding* ni njia mojawapo. Lakini mwisho wa siku inategemea fedha kiasi gani kinapatikana kwa ajili ya matumizi mnayoyahitaji. Kuna method nyingi sana. Lakini nina hakika kwamba mawazo yake ni mazuri na tutaangalia uwezekano mwingine kama t huu utaratibu tulionao utakuwa na matatizo. Lakini *so far* ninavyofahamu matatizo hayapo tunajitahidi kadri tunavyoweza kufuata programu ambazo zinaletwa na Wilaya na kushirikisha wananchi mahali ambapo inahitajika.

Mheshimiwa Leonard Derefa namshukuru ni *philosophy* nzuri na nina hakika tumemuelewa alichokuwa anamaanisha. Progamu za *Shinyanga Peril Urban* tumeanza kujitahidi kama alivyoeleza Ipatakuli tumejaribu kusaidia kufufua tatizo lililokuwepo pale la kisima. *Internal Basin Management* ni hakika kweli hii bodi inaanzishwa katika kipindi hiki cha fedha, kwa hiyo nina hakika matatizo mengi yaliyojitokeza yataweza kutatuliwa. *Taping the under ground water* kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake tumeishaanza na tumefanya maping katika baadhi ya maeneo, na tunaposema kwamba kupima vyanzo vya maji nadhani ni lugha mojawapo tu ya kusema tunafanya *maping.* Kwa sababu *original maps* zilichorwa miaka mingi sana. Sasa *geophysical changes definitely* zinabadilika kila mwaka. Kwa hiyo, hizo ulizokuwa unazieleza hapa zina-*shift* na njia za maji kubadilika na kuendelea kubadilika. Hiyo study uliyosema ya kujua vyanzo maji. Kwa mfano, Makutupora tulishafanya kwa kusaidiwa na *International Atomic Energy Agency* tulishafanya tunajua maji ya Dodoma unayokunywa leo ni ya mvua ya mwaka gani. Kwa hiyo, tunaelewa *on average* maji yanayonywewa Dodoma leo yalitokana na mvua ya miaka 40 iliyopita. Kwa hiyo, tunafahamu kwa sababu ya msaada wa vipimo ambavyo tulipewa *International Atomic Energy Agency.*

Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz tunashukuru Lindi tutaangalia matatizo ya vijiji vinavyozunguka *water source* iliyopo sasa hivi na tayari tulilijua hilo kwa sababu ni sera ya Serikali sasa hivi sehemu ambako tunachukua maji lazima wananchi wa sehemu ile wafaidike.

Mheshimiwa Njelu Kasaka, nakubaliana naye ukosefu wa maji umeanza kuonekana na tunachukua hatua. Lakini moja linalochangia ambalo tena naona ni *contradiction* kwa sababu sababu kubwa inayosababisha misuse ya maji ni kwa sababu wananchi wengi bado hawajaona maji yana thamani. Kwa hiyo, maji bado ni *cheap* sana ukilinganisha na nchi nyingine. Juzi nilikuwa na Waziri wa Maji wa Ethiopia, sisi hapa tumezungumza *total collection* kwenye *Urban Authorities* ambazo ziko *Registered* tuna *collect* sasa bilioni 13 ambazo ni karibu 13 milioni *dollars.* Mjia pekee wa *Addis Ababa collection* yao iko 17 milioni *dollar.* Sasa inatokana na nini, mpaka sasa hivi tunachofanya tuna *recover cost za operations,* hatufanyi *full cost recovery* yaani wananchi hawalipii ile *investment* iliyowekwa.

Sasa tutafika huko kwa sababu njia mojawapo ya kupunguza misuse ya maji ni kufanya maji yawe na thamani. Sasa *contradiction* nasema kwa sababu ukiangalia Waheshimiwa Wabunge wengi wanasema ankara za maji ziko juu jamani tuko pazuri. Bahati mbaya tu tulizoea vya bure. Lakini mimi wananchi wangu kwenye Jimbo nawambia Bwana bure alishafariki. Siku hizi cha bure hakipo. Sasa tujaribu kuwahamasisha wananchi waone maji yana thamani, nina hakika kwamba *conservation* ya maji na matumizi bora ya maji tutayafikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutafiti maeneo nina hakika Mheshimiwa Njelu Kasaka haya maeneo sita kwa mwaka uliopita au saba kwa mwaka ni maeneo ambayo labda nitasema kwa bahati mbaya lakini ni wananchi wale wale ni upande wa pili wa Jimbo langu. Kwa hiyo, nina hakika unaelewa ni upande wa Songwe.

Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah ndiye alikuwa msemaji wa mwisho kwa kuzungumza hapa Bungeni. *Be use water* nakubaliana naye. Tatizo mnalolipata sasa hivi Pangani, hilo tatizo pia liko Lipopo, liko Zambezi haya maji yanayokwenda Baharini. Ukianza kuyatumia sana huku upande wa juu ina maana ile *velocity* yake kuingia baharini inapungua. Kinachotokea nini maji ya baharini yanaanza kufuata mto kwa sababu ya *global warming* barafu huko kwenye *Ataktic* na sehemu nyingine *level* ya bahari inapanda.

Kwa hiyo, *level* ya bahari inapopanda mto unaonekana ndiyo njia ya kupumua. Kwa hiyo, ni mawazo mazuri sana ambayo ameyaeleza kwamba tujaribu tunapotumia maji tuyarudishe kwenye mto ili ile *volume* ya maji inayoingia baharini ibaki pale pale. Hiyo itapunguza maji kuingia kwenye nchi kavu. *Ideologist* hawatoshi hilo linaeleweka Mheshimiwa Mbunge kwa muda mrefu karibu 10 Serikali ilikuwa haiajiri watu.

Lakini sasa tumeanza kuajiri. *Water rates* ziko *cheap* nakubali tunaangalia uwezekano wa ku-*review* nia yetu yote ni kujaribu kupunguza matumizi ovyo ya maji. *Gang leaders* halipwi tunaelewa tatizo la Bonde la Pangani na Wizara inafanya uchunguzi nani anayesema ukweli kwenye vitabu inaonekana wanalipwa, upande wa pili hawa *gang leaders* wanalalamika hawalipwi. Kwa hiyo, tutafanya uchunguzi ili tujue nani anayesema ukweli. *River Basin Management* kuna *River Basin Management* zinakuwa *managed* vizuri, lakini kuna matatizo kwa baadhi ya *River Basin Management* na mojawapo ni hiyo Pangani kwa tatizo kama ulilolisema. Lakini Wizara tuko macho na tunajaribu kuchunguza tatizo liko wapi na njia ipi tuitumie ili kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kama nilivyoeleza tuna wachangiaji wengi wa maandishi ambao ninawaomba sana kwamba muda hautoshi nusu saa imekwisha. Lakini tutawapa majibu kwa kila mlichokiomba kwa maandishi na tutajitahidi ikiwezekana ili tuwape majibu hayo tukiwa hapa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, narudia kuunga mkono hoja hii na kusema kwamba nina hakika Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtutakuwa katika msingi ule ule ili tupewe ruhusa ya kwenda kufanya kazi na kutatua matatizo yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu tena nimalizie hoja yangu iliyoanza asubuhi. Nilikuwa namuuliza Mheshimiwa Gideon Cheyo kwamba alitumia mbinu gani juzi akapita salama, hakuniambia. Lakini nina hakika nitajitahidi kutoa majibu. Lakini sitaweza kujibu yote kama alivyosema mwenzangu. Lakini tutawaandikia na tutatekeleza yale ambayo tutakuwa tumeyaahidi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima nikiri sana kwamba michango hii iliyotolewa safari hii imetusaidia sana, imetuimarisha sana na uchambuzi wao nina hakika utatusaidia kusonga mbele katika kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, walioachangia kwa kuzungumza hapa Bungeni wako 15 na walioachangia kwa maandishi wako 84. Ni utaratibu lazima niwataje wote kwa kuwatambua kwa kuwapa heshima yao. Waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni ni Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha, Mheshimiwa Major Jesse Makundi, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah na Mheshimiwa Anthony Diallo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Major Jesse Makundi, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, Mheshimiwa Raynald Mrope. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mheshimiwa Juma Salim Kidunda, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Aziza Ali, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Sumri Mohamed, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Salim Omar Ali, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Robert Mashala, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Mudhihir Mohammed Mudhihir, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Awesu Aboud, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga na Mheshimiwa Dr. Laurence Gama,

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Iddi Simba, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Mohamed Missanga na Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe. *(Makofi)*

Kwa hakika kama mnavyoona orodha ni kubwa na wakubwa wote hawa wamesema maneno mengi sana. Ningetamani kama ningepata muda wa kutosha nikamjibu kila mmoja wenu hapa hapa lakini kwa bahati mbaya muda ni mdogo wala sitaweza kuyajibu hata nusu yake. Lakini kama nilivyosema tutawapelekeeni majibu kwa maandishi wote niliowataja hapa.

Nianze na la kwanza hili wamesemea Mheshimiwa Chiduo na Mheshimiwa Paul Kimiti. Nawaheshimu sana ni makaka zangu. Ni Mawaziri wa zamani jambo kubwa kidogo ambalo wanajua mamlaka yake si yangu ya muundo wa Wizara. Kwa mujibu wa Katiba Rais anaunda Wizara kwa jinsi anavyoona inafaa. Jana nimejaribu kulieleza lakini ningetaka kulieleza kwa namna nyingine tofauti kidogo. Kwamba kwa miaka mingi sekta ya mifugo imekuwa na matatizo sana nchini. Iliwahi kuwa na Wizara yake ikakwama, Mwalimu akaiondoa. Ikapelekwa Kilimo ikawa vurugu, ikapelekwa tena kwenye Kilimo na Ushirika ikawa matatizo zaidi. Nadhani katika jitihada za kusema tufanye nini kuhusu sekta ya Mifugo ndipo busara za Rais zikamtuma kwamba aiunganishe na Maji. Na kwa nini na Maji?

Kwa sababu moja ya matatizo makubwa sana wafugaji nchi hii ni Maji. Ndiyo wanazunguka nchi nzima moja ya tatizo linalowasumbua ni maji. Sasa sitaki kujipigia debe lakini nasema hebu tupeni nafasi ndani ya miaka mitano mpime hii kazi imekuwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni la magonjwa ya mifugo. Nimesikitika sana na kwa maelezo ya Mheshimiwa Nguli kwamba hakuona busara za kuanza kutekeleza Waraka wa Rais. Nimesikitika kwa sababu namheshimu sana rafiki yangu Mheshimiwa Nguli. Lakini nimesikitika kwa sababu inaonekana mkoa wako ni mmoja wa mikoa iliyoanza kutekeleza kazi hii. Isitoshe tarehe 29 Aprili, 2003 Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Singida ilifanya kikao na kuamua kuanza kutekeleza waraka na yale yote uliyokuwa unayasema vituo, barabara gani zimewekwa. Kwa mfano kwa Wilaya ya Singida ili kusafirisha mifugo hiyo kwa magari na treni wanatumia *Kindai Holding Ground* ambayo ni Sepuka, Ititi mpaka Singida Mjini. Kuna Mtinko, Ilongelo, Kinyanto mpaka Singida Mjini. Mimi naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Singida kwa kazi nzuri aliyoifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge Rais hakuamka tu asubuhi akaleta waraka. Yako matatizo ya msingi katika suala zima la magonjwa ya mifugo. Niwaambieni ili tuweze kuuza mazao ya mifugo nje hatu-*qualify* sisi kwa sababu ya magonjwa. Ukizungumza *SMD* tunayo, ukizungumza *CPD* tunayo. Hakuna ugonjwa ambao hatuna hapa. Wenzetu wanaotaka nyama iliyo na *quality* hawatakubali kula nyama ya namna hii. Sasa Waheshimiwa Wabunge lazima kwanza tunapozungumza juu ya *Export Market* tuzungumze juu ya kuondoa magonjwa ya mifugo. Njia moja ya kuondoa magonjwa ya mifugo ni kuweka utaratibu kama huu tulioueleza. Mimi nina hakika utaratibu huu ukifuatwa vizuri tutaweza sisi ndani ya miaka mitatu ijayo kufuta kabisa magonjwa na tutaweza kushiriki vizuri zaidi na kikamilifu zaidi katika soko la dunia la mazao ya mifugo. *(Makofi)*

Nitoe mfano wa Botswana. Botswana ni nchi ile ndogo ameeleza Mheshimiwa Simpasa ina watu 1.3 milioni ina ng'ombe 150,000 *export* zao kwa mifugo peke yake ni 2.5 milioni *dollars.* Watanzania walioko pale ni familia laki moja na nusu ni asilimia kumi ya watu wa Botswana. Nusu ya wale ni wataalamu wa mifugo waliokuwa *SUA* na waliokuwa *Tanganyika Packer's.* Ndiyo. Lakini kikubwa katika ile nidhamu katika suala zima la mifugo, nchi nzima imewekwa senyenge kuzuia mifugo isitembee ovyo. Sasa lazima tufike mahali tuzuie mifugo katika nchi yetu isitembee ovyo. Niseme moja ya magonjwa yanayotusumbua sana ni magonjwa ya ndigana magonjwa yanayoletwa na kupe. Iko sheria tunaileta Bungeni mwezi Oktoba. Mkoloni aliweka sheria kwamba usipoogesha ng'ombe ulikuwa unalipa nadhani senti 50/= hivi. Lakini wakati ule ile senti 50/= ilikuwa kubwa sana. Zimbabwe leo wanaitekeleza ile usipoogesha ng'ombe unalipa pura nadhani kama 100 hivi. Sisi hapa wala hatusumbuki, tuna majosho zaidi ya 2,300 yanayofanya kazi ni 476. Yasiyofanya kazi ni 1,574. Sasa tusipoanza kuchukua hatua zetu *Are we serious?* Nawaombeni wenzetu mtuunge mkono katika hili ili taratibu hizo waraka huo wa Rais utekelezwe na kila Wilaya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nimewaelewa sana Waheshimiwa Wabunge kwa kutusikitikia juu ya Bajeti ya Wizara. Nashukuru sana kwamba Waziri wa fedha kama mlivyosema amekuwepo muda wote humu ndani. Lakini kwanza nakubaliana na pendekezo lazima tuendelee kufikiri. Ingawa nilikuwa najiuliza wakati nilikuwa nimekaa hapa, nikasema nimewasikilizeni kwenye debate sasa sijasikia hata mmoja akisema toka kwenye Wizara fulani. Kwa mfano barabara wametoa shilingi 126 bilioni, sijasikia hata mmoja akisema punguza pale peleka kwenye Maji na Mifugo, sijasikia hata mmoja. Wala kutoa kwenye Wizara nyingine yoyote. Kwa sababu kimsingi kila Wizara ina matatizo. Kila Wizara ina matatizo. Nilisema tutakuwa tunagawana sungura.

Niseme siku ile anamalizia hotuba yake Mheshimiwa Basil Mramba alisema tuimbe wimbo: "Mkapa mpeni raha", hakumalizia maelezo. Leo duniani tunakopesheka, tuna heshima kubwa sana kwa sababu ya sera ambazo zimesimamiwa na Rais wetu. Mimi nataka nikiri tatizo la Wizara yangu mara nyingine si pesa. Benki ya Dunia inatuambia tatizo letu si pesa tatizo ni *capacity* ya kutumia zile pesa.

**MBUNGE FULANI:** Rudia

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Ndiyo!! *Capacity* yetu ya kutumia zile pesa. Tulikuwa tumeanza na Wilaya 12 tumewa-*challenge World Bank* wakatuambia tunawapeni Wilaya 38 mtekeleze mkimaliza mwaka 2005 tunawapeni nyingine 38. Sasa ndio tumeanza nimezitaja leo hizo Wilaya 38. Lakini

Waheshimiwa Wabunge tusaidiane. Ukweli ni kwamba kule Wilayani kama Mbunge haupo ukapigia hili suala kelele ukalifuatilia hapa na pale zile fedha zinakaa pale hakuna kinachoendelea. *(Makofi)*

Lakini la pili, liko tatizo la Madiwani. Wewe haupo ataangalia ni mradi gani wa kupeleka ambao una maslahi yake badala ya kuangalia maslahi ya Wilaya kwa pamoja. Tatu, wataalamu wakipata miradi kama hii wanajua ndio wakati wa posho kwa hiyo hana haraka nao. Lakini ninyi Waheshimiwa Wabunge mna haraka kwa sababu mnataka mwaka 2005 muwe na agenda ya kusema nimefanya hiki, nimefanya hiki. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge tukisimamia hili suala la miradi hii ambayo tunayo katika Wilaya zetu, tukasimamia kwenye vikao tukawasukuma wataalam kila mmoja mwaka 2005 atakuja hapa anacheka kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Degera amejaribu kujibu Naibu Waziri suala la Mwisanga. Nataka ku-*declare interest* Warangi wakwe zangu. Lakini katika hili nataka muelewe busara zetu na sisi. Tulipowapeleekeni mradi wa *World Bank* tuliwapeni nafasi ya kuamua vipaumbele vyenu ni nini, hamkuweka Mwisanga. Una pesa zile fedha za *World Bank* nitaeleza sasa hivi masharti yake unaweza mpaka ukifika 10 bilioni kwenye Kijiji kimoja hawana mgogoro. Ninyi katika *priority* hamkuweka mmechagua Vijiji 10 na Mji wa Kondoa. Kwa hiyo, nauliza mngekuwa na *priority* nao kwa nini hamkuupangia pesa, kwa nini nimeshindwa. Naomba Waheshimiwa Wabunge tuelewane. Kuna matatizo hapa ya msingi ya sera kwamba Serikali ilikuwa inaanzisha miradi halafu Serikali ile ile inaendelea kuendesha ile miradi. Ikiiendesha miradi ile maana yake uwezo wake wa kuanza miradi katika maeneo mapya unakuwa mgumu. Nitawapeni ushahidi tunasimamia sasa hivi miradi mitano. Handeni *Trans Mail,* Maswa, Makondeko, Mgango Kiabakari, na Waging'ombe. Bajeti yangu ya Maji Vijijini ni shilingi 2.07 bilioni, Bajeti ya miradi hii ni shilingi 1.4 bilioni. Sasa nguvu za kuniwezesha kuanza miradi huko Kigoma, Mtwara, Nzega mnaitoa wapi kama nguvu yangu inabidi kuendesha miradi ambayo tayari Serikali imekwishaigharamia. Na ndiyo maana tunapoanzisha mamlaka tunazipa ile *capital* wakishaanza kujitegemea unapata nguvu nyingine ya kwenda mahali pengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Degera tutajitahidi kuangalia nini tunaweza kufanya lakini ningewasihi pia na nyinyi muangalie nini mnaweza kufanya. Lakini tuelewane kwamba jamani matatizo nchini ni makubwa sana ni asilimia 53 tu ndio inayopata vijijini ni asilimia 73 tu ndio wanapata maji mijini bado tatizo ni kubwa sana.

Sasa nije kwa maswali matatu. Hapana kwanza nirudie ule mradi wa *World Bank.* Mradi wa *World Bank* tunakwenda kwa Wilaya 38.

**WABUNGE FUANI:** Taja Wilaya ?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Naam !! Wilaya zinatakiwa kuchangia asilimia 5 tu na Halmashauri asilimia 5 basi. Nyingine yote unayokatwa inatoka Benki ya Dunia. Lakini uamuzi wa mradi gani ni wa kwenu. Mnaambiwa chagueni vijiji 10 tafuteni *priority* yenu ni kitu gani, leteni ile miradi, kaeni ninyi muamue hata mkandarasi mnamchagua nyinyi. Hata Mkandarasi mnamsimamia ninyi pale mlipo. Sasa nasema Waheshimiwa Wabunge tafadhali shikilieni hii miradi wale mlioipata na wengine wale ambao hawajapata watapata kwa haraka zaidi kadri tunavyotumia hizi fedha za *World Bank* vizuri zaidi. Kwa hiyo, narudia hoja yangu kwamba tatizo la pesa ndiyo, lakini tuna tatizo pia la kutotumia vya kutosha fedha za wafadhili ambao tunapata sasa kutokana na hali yetu ya uchumi kuwa nzuri. Lakini pendekezo la njia bora za kupata fedha za ndani niko tayari kulipokea tushauriane tuone tunafanya nini.

Mheshimiwa Paul P. Kimiti amelisemea jambo hili kwa uchungu mkubwa sana. Tumewahi kuonana mara kadhaa akifuatilia na mimi nakubali ni tatizo ambalo halitokani na Sumbawanga wala na sisi Serikali. Fedha za kuendeleza Mji wa Sumbawanga zilikuwa zinatoka *ADB. ADB* kama mnavyojua kwa mwaka mzima wamekuwa wanapigana kule Cote D Void, nchi ile inapigana. Imewachukua mwaka mmoja kutofanya kazi hatimaye *ADB* imeamua kuhamia Tunisia. Sasa tunategemea baada ya kuhamia Tunisia mradi huu pamoja na wa Shinyanga na wa Lindi utarejeshwa ili uweze kuendelea. Lakini haikuwa makusudi ya Serikali, tutaufuatilia kwa karibu sana kuhakikisha kwamba kama tulivyoahidi Sumbawanga tatizo lao linashughulikiwa. *(Makofi)*

Rafiki yangu Jesse Makundi *Kili Water.* Amelisemea sana hapa Bungeni katika maswali kadhaa. Namheshimu kama Mbunge ana maoni lazima nimsikilize, ametumwa na watu. Lakini nataka kusema hivi

mkishakubaliana sera za msingi ni lazima zile sera zifuatwe. Haiwezekani watu wa Mwika wakakataa kuchangia maji wakategemea tutawaondoa *Kili Water.* Sasa viongozi wa Wilaya na Mkoa wanafanya kazi kubwa na mimi napenda kumpongeza Mkuu wa Mkoa na Wilaya Moshi kwa kazi nzuri sana waliyoifanya. Lakini madhari umelisemea sana na kwa uchungu sana ukataka na *TV* kuona ili wapate ujumbe. Tumekubaliana na Mbunge wa Rombo ambaye pia ni Waziri wa Fedha, tutakwenda wote huko kwenu tukaangalie maana yake bomba liko Rombo na Mwika. Ila nakuja kwa masharti usitegemee kwamba tutabadilisha msimamo wa kuchangia. Ni lazima wachangie ndipo mradi uendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, tatizo la Sinya. Wale wananchi wako wanakubali kuwa tatizo lipo, ingawa tumejitahidi sana kuhudumia Moshi Vijijini. Tumetoa fedha kwa Umbwe, Uchira lakini tatizo la Sinya tutayatazama. Najua kuna *frustration* ya wananchi walichanga fedha zao zikaishia huko Wilayani hazikuwepo huko Wilayani, lakini tutajitahidi kulifuatilia ili kwa pamoja tuone tunaweza kukusaidiaje juu ya tatizo la Sinya. Hiyo nakuahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Kibaha. Kwanza ningependa kusahihisha kauli iliyotolewa kwenye magazeti juzi kwamba Kibaha sasa itakuwa na Mamlaka yake ya Maji tofauti. Hapana, hata kama imeundiwa Mji lakini leseni ile ya *City Water* ni maeneo yote yale yaliyokuwa yanamilikiwa na *DAWASA.* Kwa hiyo bado nafikiri mtabaki chini ya utaratibu wa *City Water.* Mimi nafikiri mngefurahi kwa sababu katika *package* ile ya Benki ya Dunia na ninyi Kibaha mpo. Lakini nikiri kwamba Kibaha kumekumbwa na matatizo kidogo ya muda mrefu lakini tunayashughulikia tumechelewa kidogo kumalizia mkataba wetu na *City Water* kwa mambo madogo madogo ya kisheria ambayo tunataka tuhakikishe tumejitosheleza kabla mambo hayajaanza. Kwa hiyo, tunaomba tupeni muda, wananchi wanaweza wakapata matatizo kidogo lakini nia yetu ni kuhakikisha kwamba tunayaondoa haya matatizo na nina hakika tatizo la Kibaha litakwisha maana Mheshimiwa Mbunge Msabaha alikuwa analalamika sana na kwamba hapati usingizi kwa sababu ya simu nyingi za wananchi. *(Makofi)*

Tatizo la Mheshimiwa Njelu tulikuahidi tutatekeleza, nadhani hakuna tatizo. Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha. Kwanza mimi nakushukuru sana kwa kutuunga mkono huko ni ukomavu wa hali ya juu sana. Nakiri kwamba hatukuweza kukutana si kwa nia mbaya, tutakunywa chai wakati wowote, usiwe na matatizo hata kidogo si kwa nia mbaya. Lakini sikubaliani na hotuba yako yote. Na hasa sikubaliani na wewe pale unapotaka kuiba sera za CCM ukatanguliza mambo ya chama chako, mbele tupo wenyewe. Alisema Mheshimiwa Mwadini kwamba Chama cha Upinzani ndicho kilichoshauri kwamba bwawa katika Mto Ruvu lijengwe ili kuwe na uhakika wa maji katika mji wa Dar es Salaam. Wakati sera zenyewe zinatungwa hawajazaliwa, Ndiyo!! Ndiyo!! Suala la bwawa hili sizungumzii mimi wamezungumza akina Mzee Al Noor Kassum akiwa Mawaziri wa Maji. Sasa hata wenzetu hawa wanajua kwa mpango utakaotekelezwa pale Dar es Salaam kwa dola za Kimarekani 164. 6 milioni tatizo la maji Dar es Salaam litakuwa historia. Sasa wangetaka wao kukimbia mbele kwamba ni sera za Wapinzani. Hapana bwana ni sera za CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hoja ni nyingi, nimezipokea, nimezikubali tutawaandikia, tutatekeleza bila matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 49 Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo**

Kif. 1001 - *Administration and General.*............Shs.843,518,300/=

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Natumia kifungu 1001 - Programu ya 10. Waziri asiwe na wasi wasi sina tatizo na shilingi katika mshahara wake. Lakini kwa kuwa ni swali ambalo limekaa muda mrefu nilitaka tu anihakikishie miaka karibu 7 iliyopita nilikuwa naomba *Water Right* katika Wilaya ya Karatu ziwe *reviewed* kwa sababu *Water Right* karibu zote zinamilikiwa na wenye mashamba makubwa.

Wakati huo hapakuwa na vijiji katika eneo hilo na tangu wakati huo vijiji vingi vimejengwa chini ya maeneo hayo ambapo kuna mashamba na wananchi hao sasa hawana maji na hawawezi kuyapata kwa sababu maji yote ya mito yanamilikiwa na wenye mashamba. Miaka 7 iliyopita niliahidiwa kwamba *Water Right* hizo zitakuwa *reviewed* na Serikali. Sasa nilitaka kuwa na uhakika tu Mheshimiwa Waziri anihakikishie je kazi hiyo sasa itafanywa lini ikiwa ni pamoja na kuoanisha *review* hiyo na Sheria za Maji ambazo pia zina masharti magumu kwa wananchi walioko katika upande wa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka ufafanuzi huo tu.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu hoja ya Mheshimiwa Slaa kama ifuatavyo:-

Kama tulivyosema katika sera maji ni rasilimali ya Taifa. Lakini upo utaratibu uliowekwa kisheria kwamba wakati unapofika muafaka jambo lile linatazamwa kwa mujibu wa sheria kila upande unajieleza halafu wanaangalia njia bora na ya uhakika zaidi ya kugawa maji yale. Tulishamwahidi Mheshimiwa Slaa kwamba linashughulikiwa. Ningependa atuamini kwamba linashughulikiwa pamoja na sheria hizo huko Morogoro.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa nilikuwa na mawazo asubuhi ya kuondoa shilingi katika mshahara wa Waziri lakini sasa nimefuta wazo hilo kwa sababu ya majibu yake mazuri. Lakini nilikuwa nataka ufafanuzi kuhusu:-

(a) Kwa kuwa ahadi hii ya Singa/Kibosho imekuwa ni ya muda mrefu sana na leo kwa kweli Waziri ameniahidi nashukuru. Kidogo angetupa matumaini ili nikienda huko nijue kabisa kwamba ni namna gani nitawaeleza wale wananchi.

(b) Kulikuwa na ahadi ya Rais kuhusu *Lower Moshi Irrigation.* Alivyokuja Moshi na hata nilimpokea karibu nipate matatizo kwenye chama changu ilionekana kwenye magazeti. Sasa Rais aliahidi kuhusu Maji ya *Lower Moshi Irrigation.* Je, Waziri anayo ya kusema kuhusu ahadi hiyo? Ahsante.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hili la *Lower Moshi.* Ni tatizo ambalo tunalifahamu. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Ngawaiya alikwenda kumpokea Rais, alikuwa anatekeleza wajibu wake sioni kwa nini walimzomea. Lakini ningependa kumhakikishia kwamba ni jambo ambalo tunalishughulikia. Tulishatoa uamuzi kule mwanzo, uamuzi ule ukalalamikiwa. Tunautazama tena uamuzi ule kama inawezekana kuubadilisha. Kama haiwezekani nitaufafanua na kuueleza kwa nini tumefikia uamuzi ule. Kwa tatizo la Singa mradi ule ni wa shilingi 140 milioni. Siwezi kumwambia kama sasa hivi naweza kumpa shilingi 140 milioni zote. Lakini namwambia tatizo lake nimelisikia na nitaangalia cha kufanya. Ningemwomba aniamini. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*....................Shs. 324,788,900/=
Kif. 1003 - *Policy Planning* .............................Shs. 580,477,800/=
Kif. 1004 - *Livestock Research & Training Institutes* ....................Shs. 2,385,044,900/=
Kif. 2001 - *Water Resource Assessement & Exploration* Shs. ...............................1,072,408,700/=
Kif. 2002 - *Central Stores* .....................Shs.271,031,700/=
Kif. 2003 - *Water Laboratory* ...................Shs. 244,543,500/=
Kif. 3001 - *Urban Water Supply and Sewerage* ............ Shs. 2,832,259,300/=
Kif. 3002 - *Central Water Board* Shs. 224,285,500/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 - *Rural Water Supply* .................. Shs. 2,478,577,200/=

**MHE. DR. THADEUS LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja tu la ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongelea sub vote 4001 kifungu kidogo 270100.Katika kuchangia kwa maandishi nimeelezea kama kuna miradi iliyoanzwa kutekelezwa na *DANIDA* huko nyuma katika Kata ya Chiwanda, Mtipwili na Ngumbo haikukamilika.Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameelezea kuwa kuna mpango wa kuikamilisha miradi iliyoanza na haikumalizika. Sasa naomba kufahamu hiyo miradi ya Kata hizi tatu bado haikukamilika. Je, ipo katika miradi hiyo 796 iliyoorodheshwa na Mheshimiwa Waziri na lini itaanza kufanyika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri je, miradi hiyo mojawapi ipo?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumjibu Mheshimiwa Dr. Luoga kwamba tulitoa kitabu asubuhi kinachoonyesha miradi 794 ambayo haijakamilika. Na tukasema tunahitaji shilingi 43 bilioni kuitekeleza. Sasa ningemwomba yeye atazame kama miradi hiyo haipo, kama alivyosema Naibu Waziri wakati wa ku wind-up tunaomba atuletee ili tuingize katika orodha ya miradi ambayo ni kiporo. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 - *Water Resource Institute*.............Shs. 407,404,300/=
Kif. 6001 - *Drilling*........................................Shs. 105,001,200/=
Kif. 7001 - *Veterinary Service*......................Shs.1,750,273,700/=
Kif. 8001 - *Animal Production*....................Shs.1,908,526,400/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 49 Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo**

Kif. 1001 - *Administration and General*......Shs. 8,000,000/=
Kif. 1003 - *Policy Planning*..........................Shs. 2,976,772,000/=
Kif. 1004 - *Livestock Research & Training Institute* .........................................Shs. 127,600,000/=

Kif. 2001 - *Water Resource Assessement and Exploration* .......................Sh. 825,000,000/=
Kif. 2003 - *Water Laboratory*.....................Sh.1,424,000,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3001 - *Urban Water Supply and Sewerage* Sh.18,419,000/=

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho 3001, napenda nimkumbushe tu ndugu yangu kwamba aliahidi kushughulikia maji ya Mji wa Kisarawe mwaka jana. Kwa bahati mbaya katika Ibara ya 56 ya hotuba yake inaonyesha kwamba maji yale yameshughulikiwa, lakini napenda nimwambie kwamba taarifa alizonazo si sahihi na ninamualika yeye na mimi twende Kisarawe ili akaone mwenyewe halafu maji yale yaweze kushughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, aliahidi kutafuta fedha, akijibu swali langu Namba 176 mwaka 2001 juu ya kushughulikia mabwawa ya Titu, Gumba na Bwawa la Kitanga kule Wilaya ya Kibaha, lakini mpaka sasa hivi bado hayajashughulikiwa. Naomba nipate majibu. Je, tumefikia wapi katika utekelezaji wa mabwawa hayo? Ahsante.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mzee wangu, Mheshimiwa Janguo kama ifuatavyo: Ahadi zangu zote huwa najitahidi kutekeleza, lakini nafikiri kuna tatizo la watumishi kati ya ofisi yake na Wizarani. Napenda kumwahidi kwamba nitafuatilia ili ahadi zile nilizoahidi kutekeleza tuzitekeleze.

Kif. 3002 - *Central Water Board*....... Sh. 36,000,000/=

(*Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitihwa na Kamati Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 4001- *Rural Waster Supply* ........ Sh.19,999,376,000/=

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu hicho 4001 *Project Number 3223, Borehole Drilling and Dams Construction.* Nilipokuwa nachangia katika hoja ya Waziri nilizungumzia kwamba bwawa la Mwisanga ni bwawa ambalo limejengwa, lakini halijakamilika.

Sasa, inaelekea kwamba wataalam labda hawakumweleza Waziri vizuri! Katika majibu yake amesema huu mradi umekwishakamilika. Kwa hiyo, anaukabidhi. Si kweli kwamba bwawa hili limekamilika, halijakamilika!

Pia, katika maelezo yake amesema kwamba, tungeweza kupendekeza kuwekwa katika mradi huu wa *World Bank,* lakini hatungeweza kupendekeza mradi huo kwa sababu ulikuwa unatekelezwa na Wizara. Naomba Waziri anieleweshe.

Je, ni kweli mradi huu umefutwa kwenye utekelezaji katika ngazi ya Wizara na sababu ni zipi? Pili, ni mbadala gani amependekeza ili Wananchi hawa waweze kupata maji? Naomba maelezo.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurudia maelezo yangu. Sikusema kwamba mradi wa Mwisanga ulikamilika na Naibu Waziri alieleza vizuri hapa kwamba ilikuwa imebaki kazi ya chujio na kuunganisha mabomba yale kutoka kwenye bwawa kwenda Ntomoko, ilikuwa haijakamilika.

Nilichosema ni kwamba, tulikuwa na matatizo ya fedha, lakini nilikuwepo tatizo la pili kubwa zaidi nalo ni kwamba, kulikuwa hakujaundwa chombo cha kuendeleza bwawa hilo litakapokuwa limekamilika. Wamechaguana sasa wanaweza kuwa ni chombo cha kuendesha bwawa hilo. Wakati ule bado wangeweza wao kuweka kwenye mradi wa Benki ya Dunia, lakini kwa kuwa hawakuwekwa ndiyo maana nikasema: "Tutaangalia cha kufanya katika mwaka ujao wa Bajeti."

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Waziri kwa maelezo yake ambayo ametoa. Natoa ombi kwamba maadam mwaka huu mradi huu hakuutaja, naomba mwakani autekeleze, naomba sana kwa kweli.

Lakini vile vile, nimejaribu kuangalia maelezo aliyotoa Mheshimiwa Waziri kwa agizo Namba 2 ya iliyokuwa Kamati ya Kisekta ya Uzalishaji Mali, alisema na aliahidi mwezi Juni, kwamba ametenga Shilingi milioni 275 kwa ajili ya kukamilisha miradi ya zamani ya uvunaji maji ikiwemo na bwawa la Misanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashangaa sana Waziri hapa amebadilika kwamba hana pesa za kunipa! Nafikiri aende akaangalie agizo hilo namba mbili na jibu lake, maelezo ametoa mwenyewe. Naomba aangalie, lakini pili naomba mwakani atengee mradi fedha huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyomuahidi, kwenye bajeti yangu mwaka kesho nitaiweka, namuahidi hivyo. *(Makofi)*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 5001- *Water DResources Institute*........... Sh. 55,000,000/=
Kif. 6001- *Drilling* .........................................Sh. 280,000,000/=
Kif. 7001- *Veterinary Services* ....................Sh.2,427,448,000/=
Kif. 8001 - Animal Production ....................Sh.4,176,000,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Bila Mabadiliko Yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi ya Bunge Zima imepitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ya mwaka 2003/2004 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Kwa hiyo, naomba sasa Bunge likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii yamepitishwa rasmi, baada ya hapo tumefika mwisho wa shughuli zilizokuwepo kwa leo. Sasa naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.10 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne Tarehe 22 Julai, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*